

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi – Tarehe 10 Februari, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. *(Makofi)*

Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na 2014/2015.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Serikali kuhusu majibu ya Serikali juu ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa Mwaka wa Fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2015.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka wa Fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual Report and Audited Accounts of Mzumbe University for the Financial Year ended 30th June, 2015).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu cha Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 *(The Annual Report and Audited Accounts of Ardhi University for the Financial Year 2014/2015).*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 *(The Annual Report and Audited Accounts of Road Fund Board for the Financial Year 2012/2013)*

MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa Kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MHE. CAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMIS – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 105

Ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Nyamisati

MHE. ALLY S. UGANDO aliuliza:-

Katika kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kwa changarawe barabara ya Kibiti – Nyamisati.

(a) Je, ni sababu zipi zilizochelewesha kukamilika kwa ahadi hiyo?

(b) Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuchelewa kwa matengenezo ya barabara ya Kibiti – Nyamisati kwa kiwango cha changarawe ni upatikanaji wa fedha. Tathmini iliyofanyika imebainisha kwamba barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 40.8 inahitaji shilingi bilioni 1.2 ili kufanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe. Hata hivyo, ili kuifanya barabara hiyo angalau iweze kupitika Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016 iliitengea barabara hiyo shilingi milioni 45.79 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya kilometa 38.31 na katika mwaka wa fedha 2016/2017 shilingi milioni 24 zilitumika kwa marekebisho ya sehemu korofi yenye urefu wa kilometa mbili na matengenezo ya kawaida ya kilometa 15.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Serikali itajitahidi kutenga fedha za matengenezo kwa awamu ndani ya kipindi hiki cha utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipande cha kilometa 32.8 kilichobaki baada ya hapo awali kufanyika matengenezo ya kilometa nane kwa kiwango cha changarawe kutoka Kibiti mpaka Ruaruke yaliyofanywa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani.

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nianze kusema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Waziri huyu ni mchapakazi, kweli tarehe 5 Januari, ni Waziri wa kwanza aliyefika maeneo ya Delta na nilifanya naye kazi na nikaonesha kweli kauli ya hapa kazi inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize maswali yangu mawili; moja, je, kutokana na barabara hii kwamba kwa sasa ina maeneo mawili ya daraja hayapitiki, je, Serikali haioni kwamba ina kila sababu ya kukarabati madaraja hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Barabara ya kutoka Muhoro kwenda Mbwela ina matatizo makubwa hasa kwenye Daraja la Mbuchi, je, Serikali itatusaidiaje katika hilo la Mbuchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kupokea shukrani zake ndugu yangu Mheshimiwa Ungando, naomba nikiri, kweli nilikuwepo kule na tulitembelea visiwa 40 vya Deltakatika Jimbo lile la Kibiti. Barabara ya kutoka hapa Bunju mpaka Nyamisati kule ndani kwa kweli ina changamoto kubwa sana naomba tulipokee jambo hili kwa sababu katika programu yetu ya uondoaji wa vikwazo tutajitahidi ofisi yetu tufanye kila liwezekanalo kwa sababu tukiwasaidia wananchi wa eneo lile tutakuwa hata tumewasaidia wananchi wa Mafia kwa sababu wanaposafiri kutoka Nyamisati kwenda Mafia lazima watumie barabara ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika suala zima la Daraja la Mbuchi, na kwa sababu tulipita kule na vilevile tunajua kuwa tuna harakati ofisi yetu kutengeneza Daraja la Mbwela, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kuhakikisha mambo haya yote ofisi yetu inayashughulikia na Mheshimiwa Ungando amini Serikali yako tutakupa ushirikiano kwa sababu jimbo lako ni miongoni mwa majimbo yenye changamoto kubwa.

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Barabara ya Tanga - Pangani - Bagamoyo ni barabara ambayo imekuwa ikitolewa ahadi kila chaguzi kuu zinapofika na Uchaguzi Mkuu uliopita pia ahadi hiyo ilitolewa ya kwamba itaanza kutengenezwa na tayari tunaambiwa upembuzi yakinifu umekwishafanyika, sasa je, ni lini utengenezaji wa barabara hiyo utaanza ikiwa tayari upembuzi yakinifu umekwishafanyika? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii nimepita mara kadhaa na juzijuzi nilivyokuwa natembelea Mkoa wa Tanga, ni miongoni mwa barabara niliyoipita kutoka Bagamoyo mpaka pale Pangani na kikubwa zaidi katika kufika pale nilikuta *reference* ya Waziri wa Miundombinu aliyekuwa akipita pale na kutoa ahadi hiyo ya ujenzi wa barabara hiyo lakini ikiwa sambamba na ujenzi wa daraja lile la pale Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu ni *commitment* ya Serikali na kipindi cha sasa kwa sababu ujenzi wa barabara ya lami lazima kwanza upembuzi yakinifu ufanyike na jambo hilo limekamilika, ninaamini suala la barabara hii kwa sababu ni barabara ya kimkakati, kwamba hata kwenda Mombasa ni barabara ya *shortcut* naamini Serikali hii itafanya kila liwezekanalo ujenzi wa barabara hii uweze kukamilika.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la dogo nyongeza. Barabara ya kutoka Mkuranga Mjini mpaka Kisiju Pwani ni miongoni mwa barabara ambayo zimekuwa zikiahidiwa pia kuwekwa lami na Awamu ya Nne na hata Awamu hii ya Tano. Barabara hii inapita katika Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Mkuranga lakini pia inapita katika Hospitali yetu Kuu ya Wilaya ya Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itatusaidia kuhakikisha barabara hii inawekwa lami kutoka Mkuranga Mjini kupita Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Hospitali ya Wilaya mpaka Kisiju Pwani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke kumbukumbu sawa, kwanza Mheshimiwa Ulega juzi kwa uchapakazi wake mzuri juzi alikuja ofisini kwetu kwa ajili ya kuhakikisha suala zima la miundombinu ya barabara katika jimbo lake na hii ni miongoni mwa barabara ambayo tulikuwa tukijadili na Katibu Mkuu wangu pale jinsi gani tutafanya, kwa sababu yale ni Makao Makuu ya Halmashauri na kila Makao Makuu ya Halmashauri lazima angalau barabara ya lami iweze kufikika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tutaangalia jinsi gani tutafanya lakini nikijua wazi barabara ile ambayo inaenda mpaka Kisiju Pwani ni jambo la mkakati mkubwa sana na kuna barabara nyingine kutoka Kimanzichana inapita katikati kule mpaka inakuja maeneo ya Msanga katika Jimbo la Kisarawe, hizi zote ni barabara za kimkakati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Mkoa wa Pwani unafunguka, lengo kubwa ni kwamba katika uchumi unaofunguka wa viwanda sasa wananchi waweze kushiriki vizuri katika mchakato wa viwanda.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ulega naomba nikuahidi tutakupa ushirikiano wa kutosha kujenga miundombinu yetu ya barabara za lami katika maeneo yetu.

Na. 106

Ahadi ya Kuboresha Maisha ya Wavuvi na Wakulima Nchini

MHE. QAMBALO W. QULWI (K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO) aliuliza:-

Wilaya ya Karatu inapakana na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro ambapo watalii wengi hutembelea hifadhi na kufanya Wilaya hii kupata fursa ya kujengwa hoteli za kitalii, pamoja na hoteli hizo kujengwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri hiyo hainufaiki na uwekezaji huo.

(a) Je, Halmashauri hiyo hairuhusiwi kutoza *hotel levy*?

(b) Je, nini mkakati wa Serikali kuitangaza Wilaya hii kutokana na uwekezaji wa hoteli nyingi, nzuri na za kisasa zilizopo katika Wilaya hii?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Hoteli Halmashauri hairuhusiwi kukusanya kodi katika hoteli za kitalii, hata hivyo Halmashauri zinaruhusiwa kwa mujibu wa kifungu cha 26(3) cha sheria hiyo kukusanya ushuru wa hoteli katika nyumba za kulala wageni (*guest houses*) zilizopo ndani ya Halmashauri. Vilevile Halmashauri zinaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura Na. 290 kifungu cha 6(u) kukusanya ushuru wa huduma (*service levy*) katika hoteli za kitalii zinazoendesha shughuli zake ndani ya Halmashauri kwa kiwango kisichoziidi asilimia 0.3 ya mapato ghafi ya taasisi husika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ipo katika hatua za mwisho za utengenezaji wa tovuti (*website*) yake ili kutangaza vivutio mbalimbali vilivyopo kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kutangaza vivutio vyote vilivyopo vya kitalii hapa nchini kupitia makongamano na shughuli mbalimbali za Kitaifa yakiwemo maadhimisho ya Nanenae na Sabasaba ambayo hufanyika mara kwa mara kila mwaka ili kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo huko Karatu.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fursa kubwa kwa Halmashauri hasa kama ile ya Karatu yenye vivutio vingi vya kitalii na hizi hoteli za kitalii hasa katika kipindi hiki ambacho Halmashauri zetu nyingi zinachechemea katika eneo la mapato ya ndani.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, huoni sasa umefika wakati wa kubadilisha sheria hiyo ili kodi hiyo ya *hotel levy* ikusanywe na Halmashauri zetu ili iweze kuchangia katika eneo lile la mapato ya ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika swali la msingi uliulizwa suala la Serikali inamkakati gani, lakini majibu bado yamerudi kwa Halmashauri ya Karatu kujitangaza pamoja na kwamba kuna kipengele kidogo cha Serikali kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu nyingi hazina mapato ya kutosha ya ndani, je, Mheshimiwa Waziri tunachouliza, ni mkakati wa Serikali wa kutangaza hoteli zile za kisasa ili wale wageni badala ya kulala hata Nairobi waje Karatu ili waondokee pale kwenda Ngorongoro na Manyara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nadhani yote ni mchakato huu wote mpana kwa sisi Waheshimiwa Wabunge kama tukiona kuna haja ya kubadilisha sheria basi nadhani katika mawazo ya pamoja tutafanya hilo kwa pamoja kwa lengo la Halmashauri zetu, lakini hilo ni takwa la kisheria, kwa hiyo, ni sisi wenyewe kufanya maamuzi katika hilo na mchakato huo ukianza inawezekana kila mtu kutakuwa na michango mbalimbali kama ya wadau nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la utangazaji, ni kweli nimezungumza kwamba *website* ya Karatu lakini kuna mipango mbalimbali ya Serikali na mpango mkubwa sasa hivi hata ukipitia shirika letu la ndege katika suala zima ambalo wenzetu wa Maliasili na Utalii mara nyingi sana wameamua katika shirika letu la ndege liwe miongoni mwa mojawapo kutangaza vivutio mbalimbali vya kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango wa kutangaza vitu mbalimbali vya kitalii hapa kama Serikali ina mipango mipana sana kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na hilo naomba niseme kwa suala la Karatu tutalipa kama *special preference* kwa ajili eneo lile lina hoteli nyingi zaidi lakini ni eneo la kimkakati mtu akifika pale anapata faraja anakuwa na sehemu nzuri ya kulala, hana mashaka ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naamini Serikali yetu kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii itaongeza upana wake wa utangazaji wa vivutio vyetu vya utalii, lengo kubwa tuweze kukuza uchumi wa nchi yetu kwa sababu tunategemea kwamba kwa fursa tulizonazo za vyanzo vya kitalii tukitangaza vizuri tutakwenda mbele zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba niungane na hoja yako, kama Serikali tutafanya mpango mpana kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri katika nchi yetu. (Makofi)

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, pengine Waziri wa Maliasili na Utalii au Waziri; katika Wilaya ya Serengeti ndani ya mbuga yetu ya wanyama ya Serengeti kuna mahoteli mengi na makampuni mengi ambayo kisheria wanatakiwa kulipa *service levy*, lakini kwa muda mrefu walikuwa mahakamani wakikataa na kupinga kulipa ushuru wa *service levy*. Sasa Serikali imewashinda, tumewashinda yale makampuni lakini mpaka sasa yale makampuni yanagoma kulipa ushuru wa *service levy*.

Je, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii inaweza kutusaidiaje sisi Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ili waweze kulipa *arrears*?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapo siku za nyuma tumekuwa na hiyo changamoto ya *hotels* kutofuata utaratibu ambao tulikuwa tumeshauweka na kwa kweli ni kwa mujibu wa sheria kwamba, walipaswa kulipa zile kodi mbalimbali kwa utaratibu ambao Mheshimiwa Mbunge anauzungumzia lakini ni kweli suala hili lilifika mahakamani na hukumu ilitolewa na mahakama sasa kwa bahati mbaya utekelezaji wa hukumu haukuweza kuendelea kwa sababu tulikuwa na changamoto ya kutokuwa na bodi ambayo kwa mujibu wa sheria ndiyo inayopaswa kufanya maamuzi na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa kwa ujumla kwamba tayari bodi imekwishaundwa, Mheshimiwa Rais alishateua Mwenyekiti wa Bodi na bodi imekamilika iko tayari na kwamba hivi karibuni suala hilo litapatiwa ufumbuzi na majibu yatapatikana na bila shaka hakuna mashaka tutakwenda kutekeleza ile hukumu kama ilivyotolewa na mahakama.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliouliza swali hilo hilo la *0.3 percent service levy*. Naomba kuuliza, je, Serikali itakuwa tayari pamoja na hiyo bodi mpya kuundwa, tunashukuru imeundwa kuwanyima leseni hoteli zote za kitalii ambazo zinafanya biashara ndani ya maeneo yetu ya halmashauri zote nchini ambao hawajalipa *arrears* za nyuma na kila mwaka kabla hawajapatiwa leseni mpya kama ilivyokuwa kwenye kodi nyingine, wasipewe leseni kabla ya kuhakikisha kwamba kodi zote za halmashauri zetu zimelipwa? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na kila jambo ambalo ni kubwa linagusa maslahi ya wananchi, linagusa maslahi ya Taifa ni vizuri tukaliacha likaenda kwa kufuata taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa tumesema kwamba madamu bodi imeshaundwa, tunakwenda kupitia hukumu lakini pia kwa kuzingatia Sheria zilizopo tunaenda kuangalia namna ambavyo maslahi ya Taifa yanazingatiwa. Ikiwa kutakuwa kuna mapungufu kwenye Sheria basi tunaweza kulazimika kufanya maerekebisho ya Sheria lakini kama Sheria iko vizuri basi tutatekeleza Sheria jinsi inavyosema ili mradi tu mwisho wa siku maslahi na maslahi ya jamii yaweze kulindwa.

MWENYEKITI: Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na.107

Ahadi ya Kuboresha Maisha ya Wavuvi na Wakulima Nchini

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Katika kampeni zake za kutafuta Urais, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli aliwaahidi wananchi wakulima na wavuvi kuboresha maisha yao, ikiwa ni pamoja na kununua mazao na kusaidia vifaa vya uvuvi kwa bei nafuu na mikopo kwa wavuvi.

(a) Je, katika bajeti ya mwaka huu azima hii imezingatiwa?

(b) Je, ni fedha kiasi gani itatengwa kwa ajili ya kununulia mazao?

(c) Je, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya mkopo kwa wananchi wanaojishughulisha na uvuvi hasa wale wa mwambao wa Ziwa Tanganyika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendeleza jitihada zake za kuwajengea mazingira mazuri wakulima na wavuvi na kuhakikisha gharama kubwa za pembejeo na vyombo vya uvuvi zinapungua ili waweze kuzipata kwa bei nafuu kwa kutenga kiasi cha milioni 100 kwa ajili ya ruzuku ya zana za uvuvi, na jumla ya shilingi bilioni 26.99 kwa ajili ya ununuzi wa mazao katika bajeti ya Wizara ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) umetengewa shilingi bilioni 15, Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko shilingi bilioni 8.95. Aidha, ili kuongeza uwezo wa hifadhi kwa ajili ya kuwezesha kutunza mazao mengi zaidi, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula unaendelea kukamilisha ujenzi wa ghala la Mbozi lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000. Wakala pia unaongeza uwezo wa kuhifadhi kutoka tani 246,000 hadi tani 496,000 kwa kujenga vihenge na maghala katika kanda za Arusha, Shinyanga, Dodoma, Makambako, Songea na Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikopeshi wavuvi bali inaweka mazingira wezeshi kwa wavuvi kupata mikopo yenye riba nafuu. Aidha, Serikali kupitia Benki ya Rasilimali (TIB) imeweka Dirisha la Kilimo Kwanza kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima na wavuvi. Pia Serikali imeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ambayo baadhi ya majukumu yake ni kuwapatia wakulima na wavuvi mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kutoa ruzuku kwa wavuvi kwa utaratibu wa Serikali kuchangia asilimia 40 na wavuvi kuchangia asilimia 60 ya gharama. Ruzuku hiyo itatolewa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Vikundi vya wavuvi vinavyomiliki vyombo vya uvuvi vilivyosajiliwa kisheria ambavyo vinalenga kuvua kwenye maji ya kina kirefu;

(ii) Vikundi kuthibitisha uwezo wa kulipa asilimia 60 ya gharama ya vyombo na zana zilizozombwa; na

(iii) Maombi husika yanatakiwa yapitishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuhimiza vikundi vya uvuvi vilivyo katika majimbo yao vilivyokidhi vigezo kukamilisha taratibu za kuchukua *engine* hizo. Aidha, vikundi vingine vinashauriwa kutuma maombi kupitia Halmashauri zao na kuwasilisha Wizarani ili viweze kupata *engine* za uvuvi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mheshimiwa Desderius John Mipata swali la nyongeza.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, nina swali moja la nyongeza. Kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwamba wako mbioni kujenga ghala mjini Sumbawanga lakini ameonyesha na sehemu mbalimbali ambazo ni *centre*, ni sehemu za mijini mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kwa upande wa Sumbawanga ambako barabara sasa inaimarika an kutokana na hali ya hewa nzuri, maeneo ya uzalishaji zaidi yako Wilayani.

Je Serikali haioni kwamba iweke mkazo katika kujenga maghala katika maeneo ya uzalishaji kama vile Nkasi, Sumbawanga Vijijini, Kalambo, Matei kule maana yake kuna barabara za lami ili iweze kupunguza pia hasara ya kwenda kuyafuata mazao hayo na kuleta Sumbawanga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba mara nyingine kumekuwa na changamoto ya kuweka huduma ya maghala kwenye maeneo ambayo hakuna uzalishaji, lakini kwa sasa kwa sababu bado hatuna maghala mengi, Wizaru inaweka maghala kwenye maeneo ambayo yako katikati katika maeneo ambayo ni rahisi kuweza kupata mazao kutoka kwenye Wilaya mbalimbali. Lakini kadri uwezo utakavyoongezeka, nia ni kujenga katika Wilaya zote tuwe na maghala ya kuweza kuhifadhi chakula.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe halafu Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kimsingi swali langu linafanana na swali namba 107 linakwenda Wizaru ya Kilimo. Kimsingi ninataka kufahamu, tukiwa tunaelekea kwenye uuzaji wa korosho msimu uliopita tumeshuhudia Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Mtwara (MAMKU) viongozi wake, watendaji wakuu wakishikiliwa kwa ajili ya uchunguzi kutokana na ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili pia limejitokeza katika vyama vikuu vya TANECU, Lindi Mwambao, Ilulu pamoja na Chama Kikuu cha Mkoa wa Pwani. Tumeona Mheshimiwa Waziri Mkuu akichukua hatua kwa viongozi hawa wa Chama Kikuu cha MAMCU sasa tunataka kufahamu kutoka kwa Waziri amejipangaje na yeye kuwachukulia hatua viongozi wa vyama vikuu nilivyovitaja kwa sababu ya kudhulumu na matumizi mabaya ya pesa za wakulima za korosho katika Mikoa ya Mtwara, Lindi pamoja na Pwani? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama alivyosema katika msimu uliopita wa korosho kumekuwepo na changamoto nyingi sana kuhusu malipo kwa wakulima wa korosho na ndiyo maana Waziri Mkuu alichukua hatua ya kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake kwa watu wa MAMCU, lakini vilevile mtunza ghala wa Chama cha Msingi cha Ushirika ambapo korosho ziliweza kupungua bei na tunavyozungumza tayari wahusika wamefunguliwa kesi ya kuhujumu uchumi na kesi inaendelea mahakamani, lakini vilevile tunawahakikishia wakulima wale ambao wamepata changamoto hiyo ya fedha zao kutolipwa kwa kiwango ambacho kilitarajiwa kwamba Chama cha Ushirika ambacho kilisababisha korosho zile ziweze kuingia kwenye sales catalogue wao watalazimika kurudisha ile tofauti ili mkulima asije akapata tatizo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunafahamu kwamba changamoto iliyotokea Mtwara lakini vilevile Nanyumbu tunafahamu vilevile imetokea Mkoa wa Pwani kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inachunguza changamoto hizo, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kashafanya uchunguzi huo na tumepata repoti. Lakini vilevile Waziri Mkuu mwenyewe aliagiza ufanyike uchunguzi wa kina na repoti iko tayari Serikali inapitia taarifa zile ili wale wote ambao wamehusika wakiwemo viongozi na watumishi wa MAMCU, TANECU na vya vingine vya ushirika kama KORECU ambao watakuwa wamehusika watachukuliwa hatua za kisheria. Cha maana zaidi, wakulima wale ambao hawakupata malipo stahiki kwa sababu ya vurugu au uzembe wa watumishi wa Vyama Vikuu au Vyama vya Msingi tunawahakikishia kwamba fedha zao zitalipwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ina upungufu mkubwa sana wa chakula pamoja na Wilaya za Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida; na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna Halmashauri za Wilaya 55 ambazo zina upungufu mkubwa sana wa chakula na Serikali ina chakula cha kutosha kwenye maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Serikali itaanza kusambaza chakula cha bei nafuu kwasababu hivi sasa debe la mahindi ni shilingi 20,000 na mfuko wa sembe ni shilingi 40,000 ni lini Serikali itaanza kusambaza chakula cha bei nafuu Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa pamoja na hizi Halmashauri 55?

MWENYEKITI: Mheshimiwa naibu waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyokumbuka tulishakuja kwenye Bunge hili mapema kueleza na kutoa taarifa ya tathmini ya kina ambayo Wizara imefanya kuhusiana na usalama wa chakula na katika taarifa ile kama mlivyosikia Waheshimiwa Wabunge tuliweza kuainisha maeneo ambayo yana upungufu mkubwa, lakini vilevile katika taarifa ile tulieleza kwamba Serikali imejidhatiti vilivyo kuhakikisha kwamba upungufu ambao unaelekea kutokea kati ya mwezi Januari na Aprili kwamba utashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea ili kuhakikisha maeneo yale ambayo yana upungufu kwamba wananchi wanapata chakula cha bei, nafuu kwa hiyo, naomba uvute subira taratibu zinaendelea.

MWENYEKITI: tunaendela, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Abdallah Khamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga aulize swali lake.

Na. 108

Wanunuzi wa Korosho Kutolipa Wakulima kwa Wakati

MHE. ABDALLAH H. ULEGA aliuliza:-

Je, ni hatua gani madhubuti Serikali itachukua kwa kampuni zinazoshinda *tender* (zabuni) za ununuzi wa korosho lakini haziwalipi wakulima kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya masuala ya msingi katika miongozo ambayo hutolewa na Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania ni kuwataka wanunuzi wa korosho kulipia kwa wakati korosho wanazoshinda kwenye mnada. Hata hivyo, baadhi ya wanunuzi hukiuka masharti hayo kwa visingizio mbalimbali ikiwemo kushuka kwa ubora wa korosho tofauti na ule uliopo kwenye *sales catalogue* na kushuka kwa bei ya korosho katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Korosho imekuwa ikihimiza wanunuzi kufuata sheria, kanuni za taratibu zilizowekwa na mamlaka husika.

Aidha, Serikali kupitia Sheria ya Korosho Namba 18 ya mwaka 2009 kifungu cha 17 na kanuni za mwaka 2010 kanuni ya 33, itafungia kampuni yoyote ambayo inafanya biashara ya korosho nchini endapo itakiuka sheria na kanuni ikiwemo ya kutowalipa wakulima kwa wakati ili kubaki na makampuni yanayotii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Korosho imefanya maboresho na kutoa mwongozo ulioanza kutumika msimu wa mwaka 2016/2017 kwa kila mnunuzi kuweka dhamana ya fedha taslimu au hundi ya benki kulingana na kiasi cha korosho alizonunua kama dhamana itakayotumika kuwalipa wakulima endapo mnunuzi akishindwa kuwalipa wakulima. Kiwango cha chini ni kununua tani 50, mnunuzi akinunua kati ya tani 50 na 100 atalazimika kulipa shilingi milioni 50 kama dhamana. Kati ya tani 101 na tani 1000 dhamana yake ni shilingi milioni 100 na zaidi ya tani 1001 dhamana yake ni shilingi milioni 300. Dhamana hiyo huchukuliwa mara baada ya Bodi ya Korosho na wahusika wote vikiwemo Vyama vya Ushirika kujiridhisha kuwa mnunuzi alikiuka taratibu na pia adhabu nyingine zinaweza kuchukuliwa dhidi ya kampuni husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Ulega swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kwa namna ya kipekee kabisa wakati nikijielekeza kuuliza swali hilo niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayofanya ya kuwalinda wakulima wetu na wananchi wetu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hiyo pia nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa *Engineer Evarist Ndikiro* kwa kazi nzuri aliyofanya mwaka wa jana wa kuyalazimisha Makapuni mawili ya *Alpha Choice* na *Kaisari* ambayo yaligoma kuwalipa kwa wakati wakulima wa korosho wa vijiji vya Msonga, Kalole, Mkuranga mjini na Kimanzichana Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri anaeleza kwamba wanapochelewesha...

MWENYEKITI: Naomba ufupishe swali Mheshimiwa Ulega.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Ahsante sana. Wanapochelewesha kulipa malipo ya wakulima wa korosho huchelewa. Je, Serikali ipo tayari sasa kuhakikisha inawasimamia ipasavyo na madhubuti

kabisa wanunuzi hao ili wawe wanaondoa mazao yao katika maghala yetu mapema iwezekanavyo ili mzigo mwingine wa wakulima uingie kwa wakati na waweze kupata pesa za kuinua maisha yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona zao la korosho kama mfano wa namna ambavyo tunaweza tukafanya kilimo chetu kifanikiwe. Mafanikio makubwa na ya kihistoria ambayo yamepatikana katika korosho katika msimu uliopita ni kielelezo tosha cha namna Serikali ya Awamu ya Tano inavyotaka kushughulikia changamoto za kilimo. Kwa hiyo, hatutakubali mtu yoyote aje avuruge mafanikio yetu na ndiyo maana hizo kanuni zimeweka wazi kama unaenda ku-*bid* kununua korosho ni lazima kuweka dhamana. Hiyo inatusaidia kuwashughulikia wanunuzi wababaishaji ambao wanaenda ku-*bid* lakini baadaye korosho zinahifadhiwa halafu baadae wanakuja kulalamika kwamba zimepoteza sifa.

Kwa hiyo, kwa sasa haiwezekani tena na niwahakikishie tu wakulima na Waheshimiwa Wabunge kwamba mtu yeyote ambaye ameshinda *tender* ya kununua korosho atalazimika kulipia na haiwezekani baadaye akaja kuleta malalamiko mengine, kwa hiyo, hilo halitatokea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Zakaria Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Tatizo hili la wazabuni kushinda *tender* na baadae kuchelewesha huduma kwa Watanzania kwa muda uliokusudiwa imekuwa tatizo kubwa katika nchi yetu. Mifano ya wazi zipo katika Halmashauri za Wilaya ya Mbulu kwa miradi ya maji na miradi ya afya. Mifano hiyo ni kama ambavyo kupewa *tender* makampuni ambayo hayana uwezo na hatimaye baadaye kuchelewesha huduma hizi.

Je, Serikali yetu sasa kutokana na hali hii ambapo tenda hutolewa na wataalam ndani ya Halmashauri, inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma kwa wakati uliokusudiwa kutokana na muda wa mikataba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nilichozungumzia kwenye korosho ni zile taratibu ambazo tumeweka kwa ajili ya korosho, lakini ukweli wa mambo, kuna utaratibu wa kawaida wa kisheria kuhusiana na mambo ya *tender*. Sheria yetu ya manunuzi inaweka wazi namna *tender* inavyotakiwa kuendeshwa, lakini vilevile inaweka masharti kuhusiana na utekelezaji wa miradi kwa yule ambaye ameshinda *tender* na kwa vyovyote vile hairuhusiwi kisheria mtu ambaye ameshinda kutelekeza ile kazi kama kuna mapungufu ambayo yametokea ni vizuri kuangalia katika kesi zenyewe ili wale ambao wamehusika waweze kuchukuliwa hatua za sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Moja ya sababu zinazofanya ucheleweshwaji wa malipo ya korosho ni pamoja na tamko la Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, alitamka kwamba korosho zote za Mkoa wa Lindi na Mtwara zipitie Bandari ya Mtwara kitendo ambacho bandari ya Mtwara ilishindwa kusafirisha korosho hizo kwa wakati na wanunuzi wakaacha kulipa kwa sababu korosho zao mpaka ziingie kwenye maji ndipo waendeleo kufanya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, sababu ya pili; ni kwamba hata hayo makampuni mnayosema kwamba mnayadhibiti pale ambapo yanakuwa yanachelewesha kulipia lakini bado kuna mtindo wa hayo makampuni kubadilisha majina. Unalifutia jina kampuni hili, mwenye kampuni ni yule yule anatengeneza kampuni nyingine...

MWENYEKITI: Swali la nyongeza Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Je, Serikali inatoa kauli gani namna ya kukabiliana na matatizo hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama alivyosema kwamba kitendo cha kuelekeza korosho ipelekwe nje kupitia Bandari ya Mtwara ilikuwa ni moja kati ya sababu ambazo zilipelekea ucheleweshwaji wa malipo na kuvuruga kwa kiasi fulani soko la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Serikali kwa ujumla walifanya hivyo kwa nia njema. Tilitaka vilevile kujenga Bandari ya Mtwara kama moja kati ya bandari zetu, kwa hiyo, ilikuwa ni kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hata ilipotoka changamoto ile ya mizigo kurundikana bandarini, Serikali ilikuwa rahisi kuchukua hatua na kuruhusu ipitie Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, baadae tatizo hilo liliisha.

Kuhusu hili la makampuni kutumia majina mbalimbali, ni tatizo kubwa, tunatambua kwamba unakuta mtu mmoja au watu wale wale wanakuwa na kampuni zaidi ya kumi, wana-*bid* katika soko lile lile. Lakini nikueleze tu kati ya mabadiliko makubwa ambayo tumefanya ni hilo la kuleta kanuni na utaratibu ambao ni lazima kuweka *security bid* ili baadaye ukishashinda *tender* baadaye huwezi kukimbia na kusema kwamba sitakuja kuchukua korosho. Kwa sasa ni lazima uchukue kwa sababu usipochukua, fedha zako tayari ulishaziacha na Serikali itawalipa wakulima.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma Mbunge wa Bububu sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Khadija Nassir kwa niaba yake.

Na.109

Ongezeko la Matukio ya Uhalifu Zanzibar

MHE. KHADIJA NASSIR ALI (K.n.y MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA) aliuliza:-

Zanzibar kumekuwa na matukio ya uhalifu yanayojitokeza mara kwa mara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia vitendo vya uhalifu visijitokeze Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu kamaifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mipango ya muda mfupi, kati na mrefu wa kukabiliana na wahalifu na uhalifu ndani ya mipaka ya nchi yetu. Mikakati iliyopo ni pamoja na:-

(i) Kuwajengea uwezo wa utendaji kazi askari wote ili wawe na uwezo wa kubaini, kupeleleza na kufuatilia mitandao ya kiuhalifu hapa nchini.

(ii) Kufanya misako na doria za miguu, pikipiki na magari ili kubaini na kuzuia hali zozote za kihalifu zinazoweza kujitokeza.

(iii) Kuimarisha ulinzi maeneo ya mipaka yote ikiwemo ya maji ili kuzuia uhalifu.

(iv) Kuimarisha kikosi cha kuzuia na kupambana na madawa ya kulevya cha polisi sambamba na madawati ya Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya.

(v) Kuimarisha ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na taasisi nyingine nchini hasa vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yakifanyika haya pamoja na mambo mengine vitendo vya uhalifu na wahalifu vitapungua nchini ikiwemo na Zanzibar.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija Nassir, swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nina swali moja la nyongeza.

Kwa vile hali ya kiusalama sasa Zanzibar ni shwari na naomba niendeleo kuipongeza Serikali kwa hilo, je, Serikali ina mpango gani wa kuzidi kuimarisha hali hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunashukuru Mheshimiwa Khadija Nassir kwa kuona jitihada na mafanikio makubwa ya hali ya kuimarisha usalama sio tu kwa Zanzibar lakini Tanzania nzima na tunaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla waendeleo kutoa ushirikiano wao kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili hali hiyo iweze kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi tutaendelea kuhakikisha kwamba hali hii inadumu kwa kuhakikisha kwamba tunaimarisha vitendea kazi na uwezo kwa maana ya uwezo wa kiutendaji wa vyombo hivi vya ulinzi tukitarajia kabisa ushirikiano kati ya wananchi na vyombo hivyo utaongezeka ili kuweza kupata taarifa za kiintelejensia kabla ya kuanza kufanya kazi za kuweza kuwakamata wahalifu ambao wamekuwa wakisumbua Taifa letu kwa kiwango fulani katika nchi yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Shangazi *and then* Mheshimiwa Salma Mwasa.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa vitendo hivi vya uhalifu vipo nchi nzima na kule Jimboni Mlalo mwezi wa nane/tisa vikundi vya ugaidi vimeua watu wawili na kuchoma mabweni ya Chuo Kikuu cha SEKOMU.

Je, ni lini Serikali itaimarisha ulinzi katika maeneo ya Jimbo la Lushoto ikiwa ni pamoja na kujenga seliya kuwekea silaha katika Kituo cha Mlalo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuna kazi kubwa imefanyika ya kuweza kupambana na ujambazi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Tanga. Kimsingi nchi yetu haina ugaidi, tunasema tunavimelea vya ugaidi. Kwa hiyo, kilichofanyika Tanga na ninyi ni mashahidi katika maeneo ya Amboni na kwingineko ni kazi kubwa sana ambayo imefanyika kwa mafanikio makubwa na hakika kwamba mafanikio yale ndiyo ambayo yamesababisha mpaka sasa hivi Mkoa wa Tanga kwa ujumla wake ikiwemo Lushoto kuendelea kuwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa suala la uhalifu ni suala ambalo linaendelea kuwepo, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaimarisha kazi hiyo ifanyike zaidi na zaidi ili kutokomeza kabisa uhalifu katika maeneo ambayo yamesalia katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salma Mwasa.

MHE. SALMA M. MWASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kumekuwa na utaratibu wa vituo vya polisi vidogo (*police post*) hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam kufungwa saa kumi na mbili hii inasababisha matukio mengi ya uhalifu hasa yanatokea usiku. Je, Serikali haioni

inahatarisha usalama wa wananchi hasa Mkoa wa Dar es Salaam wenye wakazi zaidi ya milioni tano? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa PGO kuna vituo vya polisi vya aina tatu; kuna *Class A*, *Class B* na *Class C*. Kwa hiyo, vituo vya *Class C* kwa kawaida havifunguliwi zaidi ya saa 12. Sasa sina hakika Mheshimiwa Mbunge kituo ambacho anakizungumzia ni kituo kiko katika class gani labda pengine baada ya hapo tuone kama kitakuwa kipo katika nje ya class ambayo inapaswa kifungwe zaidi ya hapo na kinafungwa basi tutachukua hatua tuone nini kinafanyika tufanye uchunguzi tujue tatizo ni nini. Lakini nadhani kulijibu moja kwa moja swali lako kwasababu hajaainisha kituo chenyewe ni kituo gani kwa wakati huu itakuwa ni vigumu.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ally Saleh.

Na. 110

Ushiriki wa Zanzibar Katika Taasisi ya Arusha AICC

MHE. ALLY SALEH ALLY (k.n.y. MHE. HAJI KHATIB KAI) aliuliza:-

Arusha International Conference Center ni miongoni mwa taasisi ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo mwaka 1977, hivyo hii inaonyesha kwamba taasisi hiyo ina sura ya Muungano.

Je, ni kwa nini taasisi hii haionyeshi ushiriki wa Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), kilianza shughuli zake rasmi tarehe 1 Julai, 1978 kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya awali ya Afrika Mashariki mwaka 1977. Kituo hicho kilianzishwa kwa kuzingatia Sheria mama ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 kwa kupitia *establishment order* iliyotolewa kupitia *notice* ya Serikali Na. 115 ya tarehe 25 Agosti, 1978.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hicho pamoja na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere vimemilikishwa kupitia Notisi ya Serikali Na. 84 ya tarehe 4 Aprili, 2014, ambapo vituo vyote vipo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kituo kilianza shughuli zake kikiwa na madhumuni makubwa mawili ambayo ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba na ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimuundo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Wajumbe wa Bodi huteuliwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa kutambua umuhimu wa ushiriki wa Zanzibar katika uendeshaji wa kituo kama taasisi ya Muungano, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki huwa wakati wote anamteua Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kutoka Zanzibar ili kuhakikisha ushiriki wao katika kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kinafanya kazi chini ya Bodi ya Wakurugenzi na shughuli za uendeshaji za kila siku zinasimamiwa na Mkurugenzi Mwendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pale inapotokea fursa ya ajira katika nafasi za utendaji, nafasi hutolewa kwa ushindani na hutangazwa kupitia magazetini ambapo pande zote mbili za muungano huchangamkia nafasi hizo na washindi hupatikana kulingana na uwezo wao katika nafasi walizoomba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh swali la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hiki ni kituo cha pamoja au cha ubia kama ambavyo ingepaswa kuonekana wazi wazi katika taasisi mbalimbali za Muungano. Swali langu linakuja, je, Naibu Waziri anaweza kutuambia pamoja na kueleza kwamba nafasi za ushindani kuna Wazanzibari wangapi walioajiriwa katika taasisi hiyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vituo hivi ni pamoja na kufanya biashara na biashara huwa na faida na hasara. Je, Zanzibar imewahi kupata mgao wake wa faida japo nyama ya sungura ya 4.5%? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba kuna Wazanzibari wangapi wameajiriwa katika kituo hicho nimekwisha sema kwamba kwa uelewa wangu mpaka sasa hivi sijaona kama kuna Mzanzibari ambaye amejiriwa maana yake nimesema kwamba ajira zinatolewa na watu wanatakiwa kuchangamkia fursa hizo na kama wana uwezo na *capacity* na wanaofanyiwa *interview* wakishinda basi wataajiriwa.

Lakini pia tunawahamasisha zinapotokea fursa na nafasi zinapotangazwa basi watu kutoka Zanzibar waombe nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza kwamba kituo kinafanya biashara, je, Zanzibar imepata gawio kiasi gani katika miaka yote hiyo. Kama anavyofahamu kwamba kama hii ni taasisi ya Muungano tunajua kwamba gawio huwa linakwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa hiyo, kutokana na huo Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ujumla wake wanapata lile gawio kutokana na Sheria inavyotutaka. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Karibu Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, naomba kuongezea na hasa kile kipengele cha pili kuhusu gawio. AICC haijawahi kupata gawio na hivi sasa *Joint Finance Commission* na Ofisi ya Msajili wa Hazina wameunda kikosi kazi ambacho kitachambua na kukisaidia kile kituo ili kiweze kupata faida na kuleta gawio Serikalini kuanzia mwaka ujao wa fedha. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa suala hili linahusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, nilitaka kujua je, wastaafu wa Afrika Mashariki wa nchi nyingine walishalipwa lakini Tanzania imekuwa inasuasua na kuna sintofahamu wakati ambapo wengine wanasema wameshalipwa, bado tunatambua kuna wastaafu wengi wa Tanzania hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tamko la Serikali, je, wastaafu hao ni kweli wamelipwa wote na kama bado kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wastaafu wao au warithi wao wanapata fedha zao? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu hao wamelipwa na kama kuna madai zaidi wayawasilishe Serikalini tutayashughulikia kwa mujibu wa taratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa majengo haya ya *Arusha International Conference Center (AICC)* yalikuwa yakitumiwa na Mahakama ya Kimataifa (*ICTR*) na kwa hivi sasa Mahakama hii ina majengo yake na imehama katika majengo haya ya *AICC*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba heshima iliyokuwepo kwa majengo haya inaendelea kuwepo kwasababu hivi sasa wapangaji wakubwa hao wamekwishahama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Amina Mollel kwa swali lake la nyongeza kwamba Serikali tutahakikisha majengo haya yanasimamiwa vizuri na kuhakikisha hayaharibiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jana Mheshimiwa Amina Mollel ulisikiliza vizuri kwenye taarifa ya Kamati ya Uwekezaji ya Mashirika ya Umma jana kituo kinafanya kila inachoweza kuhakikisha kinapata watu ambao wanaweza kuja kupanga katika ofisi zile na sisi kama Wizara tutahakikisha tunafuatilia hilo ili kuhakikisha majengo hayaharibiki na yanabaki katika kiwango kinachotakiwa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza sasa aulize swali lake.

Na. 111

Utekelezaji wa REA III

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Jimbo la Muheza lina kata 37 na vijiji 135, katika Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Mradi wa *REA* ni vijiji vichache tu vilipata umeme.

Je, utekelezaji wa *REA III* ni vijiji vingapi vinategemea kupata umeme ili wananchi wa maeneo haya waweze kujiandaa katika kujiendeleza kiuchumi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vijiji 37 ambavyo havijapatiwa umeme katika Jimbo la Muheza na vitongoji 137 vinatarajiwa kupatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu utakaoanza mwezi Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini kwa nchi nzima unategemewa kufanya katika vipengele vitatu unaojumuisha *densification*, *grid extension*, pamoja na *off-grid renewable*. *REA* Awamu ya Tatu kwa ujumla wake katika nchi nzima ikiwa ni pamoja na Jimbo la Muheza itaanza mwezi Machi 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mradi huu katika Jimbo la Muheza utajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilometa 50; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 82; ufungaji wa transfoma 41; pamoja na kuwanganishia umeme wateja 1025. Mradi huu utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 3.94.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Adadi swali la nyongeza.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili. Kwanza ningependa kuipongeza Wizara hiyo kwa sababu Waziri wake Profesa Muhongo alifika kwenye baadhi ya kata za Jimbo la Muheza ambalo liko jirani na *power station* ya Hale na akasikiliza kilio cha Wana-Muheza kwenye Kata hizo za Kwafungo, Songa, Bwembwera na Makole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu la kwanza ni hili, REA Awamu ya Pili na ya Kwanza iliweka mkandarasi, na mkandarasi yule alikuwa hatimizi wajibu wake kwa wakati, kwa sababu alikuwa ana kazi nyingi sana. Sasa Serikali itawahakikishiaje wanamuheza kwamba REA hii Awamu ya Tatu itakapoanza mkandarasi ambaye atateuliwa atadhibitiwa na atafanya kazi hizo kwa wakati? (Makofi)

Swali langu la pili, ni kwamba REA Awamu ya Pili na ya Kwanza ilipitisha nguzo kwenye baadhi ya vijiji na vitongoji lakini vitongoji na vijiji vile havikupata umeme. Sasa kwenye hii Awamu ya Tatu vijiji ambavyo vilipitiwa na nguzo tu bila kupata umeme, vitongoji na vijiji vile Serikali inasemaje kuhakikisha kwamba vijiji hivyo na vitongoji hivyo na vyenyewe vinapata umeme badala ya kuona nguzo tu zimepita mbele yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Adadi Rajab anavyofatilia kwa kina sana kupatikana umeme katika katika Jimbo la Muheza. Nimpongeze sana tulipata orodha yako ya tarafa zako nne ikiwemo Tarafa ya Amani, Ngomeni, Bwembwera pamoja na Muheza yenyewe, kwa hiyo tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kumaliza kazi kwa haraka, katika utekelezaji wa REA Awamu ya Tatu tumefanya maboresho katika usimamizi. Maboresho ya kwanza ni pamoja na kuweka msimamizi yaani *supervisingengineer* ambaye kazi yake ni kumsimamia mkandarasi ili amalize kazi haraka, hiyo ni kazi ya kwanza. Pili, tumeweka kila ofisi ya Wilaya kwa wasimamizi wa TANESCO, tumeteua Meneja Maalum atakayesimamia miradi ya REA yaani yeye akilala, akiamka anakumbuka REA, kwa hiyo tunaamini kwamba atamaliza kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ni muhimu sana kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tumeweka sasa kila mkandarasi akiingia *site* lazima kwanza amshirikishe Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo mtatusaidia sana kwenye usimamizi wa jambo hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Adadi Rajab tuna hakika kwamba itakwenda kwa kasi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vitongoji, kwanza kama nilivyompongeza, tunajua vitongoji vyake 137 Mheshimiwa Mbunge Adadi Rajab vingi havijapata umeme, kama ambavyo nilikueleza, tunajua vitongoji vyetu tumeweka *densification*, mradi wa *densification* unaenda kwenye vitongoji vyote nchi nzima. Hivi sasa ninavyoongea katika Mkoa wa Tanga mkandarasi ameshaingia.

Kwa hiyo, nikuhakikishie vitongoji vyako vyote ambavyo Mheshimiwa Mbunge unavifatilia sana ikiwemo Kitongoji cha Mambo leo, Mbwembeza, Msongambebe, Mto wa Mbuji, Kwambambere pamoja na kwa Mpota na Maramba vyote vitapata umeme. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana hili swali lina watu wengi kweli jamani sasa...

MBUNGE FULANI: Huku nyuma huku.

MWENYEKITI: Ni kazi. Haya Mheshimiwa wako watatu hapo sasa ni hatari, yule wa pili pale, baada ya Mheshimiwa Flatei nyuma yake.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi kuna vijiji vya Mbugani, Agondi, Mabondeni, Kitopeni, Ipande, Muhanga, Damwelu, Kitalaka, Kaskazi Stesheni, Kintanura, Lungwa na Kalangali havina umeme. Je, Serikali inaweza kutoa tamko kwamba REA Awamu ya Tatu wananchi wa vijiji hivi watafikiwa na umeme?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa, nakupongeza sana juzi uliniletea orodha ya vijiji vyako vyote, kwa hiyo vijiji vyako vyote Mheshimiwa Mbunge ulivyotaja katika Awamu ya Tatu vyote vitapitiwa na umeme, na nikuhakikishie kwamba kufikia mwezi Machi kama ambavyo tumeeleza, vijiji vyote kwa nchi nzima wakandarasi watakuwa *sife* ikiwa ni pamoja na Jimbo lako la Manyoni Magharibi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Maftaha!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa si ulinitaja?

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa kwamba Serikali iliweka mkakati wa kuhakikisha ya kwamba maeneo yote ambayo limepita bomba la gesi kitaalam wanaita mkuza wa gesi, kwamba vijiji vile na mitaa ile itakuwa imepatiwa umeme kupitia REA Awamu ya Kwanza, Pili na ya Tatu. Lakini mpaka sasa hivi ninavyozungumza maeneo mengi ya vijiji na vitongoji vya Mtwara Mjini na Lindi kwa mfano Dimbozi, Mbawala Chini, Mkunjanguo na Naulongo kule kote bado hakujapelekwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ukoje kuhakikisha kwamba wanamaliza tatizo hili katika ule mkuza wa gesi kwamba wapate umeme wale wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi tafadhali!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Maftaha kwamba tunapotekeleza Mradi wa REA Awamu ya Tatu, awali ya yote tunaanzia kwenye vijiji ambavyo viko kwenye mkuza wa bomba la gesi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Maftaha na niombe tu kwamba tutakapomaliza Bunge kama una fursa basi tutapanga siku tupitie kijiji hadi kijiji ili kuhakikisha wananchi wako wanapata umeme. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa naona hili swali lina watu wengi jamani bora tuendelee tu sasa. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Jamal Kassim Ali sasa aulize swali lake.

Na. 112

Mchango wa DSE na CMSA kwa Wazawa

MHE. JAMAL KASSIM ALI aliuliza:-

Je, *Dar es Salaam Stock Exchange Market (DSE)* na *Capital Markets and Securities Authority (CMSA)* mpaka sasa zimetoa mchango gani kwa wafanyabiashara wazalendo?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu Soko la Mitaji (*Capital Market*) linahudumiwa na taasisi mbili ambazo ni: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ambaye ni msimamizi wa soko (*regulator*) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ambaye ni mwendeshaaji (*operator*) kwa kuuza hisa na dhamana kwa taasisi na watu binafsi kwa niaba ya makampuni ambayo yanayohitaji kuongeza mitaji baada ya kupata kibali kutoka CMSA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kampuni zilizoordhesha hisa zao katika Soko la Hisa, baada ya kubinafsishwa ni pamoja na TBL, TOLGases, TCC, Swissport, Tanga Cement, Twiga Cement na NMB Bank. Makampuni haya yamekuwa yakitoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi ikiwemo ajira, gawio kwa Serikali na wanahisa, lakini pia ni miongoni mwa walipa kodi wakubwa. Kwa mfano mwaka 2015 NMB iliweza kutoa gawio la shilingi bilioni 16.5 na TCC gawio la shilingi bilioni 1.4 kwa hisa zinazimilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanahisa wengineyo walipata gawio la shilingi bilioni 35.4 kutoka NMB na shilingi bilioni 58.6 kutoka TCC. Mapato yanayotokana na kodi pamoja na gawio, vinatumiwa katika kutoa huduma mbalimbali ambazo jamii ikijumuisha wafanyabiashara wadogo ambao wananufaika nazo. Vilevile Serikali imekuwa ikitumia masoko ya mitaji kama chanzo cha upatikanaji wa fedha za bajeti kwa miradi ya maendeleo, kwa kutoa hatifungani za Serikali (*treasury bonds*). Miradi inayotekelezwa na fedha hizi pamoja na mambo mengine imekuwa ikitoa ajira na fursa za kibiashara kwa wafanyabiashara wazalendo wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mchango mkubwa wa makampuni madogo katika kukuza uchumi wa nchi, mwaka 2013 Soko la Hisa Dar es Salaam lilianzisha dirisha la makampuni madogo na ya kati (*enterprises growth market*) kwa lengo la kutoa nafasi kwa makampuni za wazawa zilizokidhi vigezo vya dirisha kuu la soko (*main investment market*) kuweza kutumia soko la hisa katika kupata mitaji na kuorodheshwa kupitia soko la hisa. Dirisha hili linatoa fursa kwa makampuni madogo na yanayoanza kulitumia soko kikamilifu kupata mitaji kutoka kwa umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii Watanzania wengi wananufaika na uwepo wa soko la hisa na kushiriki moja kwa moja katika umiliki wa uchumi wa nchi. Baadhi ya wanufaika na dirisha hili dogo ni pamoja na Mwalimu Commercial Bank, Swala Oil and Gas Tanzania, Maendeleo Bank PLC, Yetu Microfinance na Mkombozi Commercial Bank. Makampuni haya mpaka sasa yana jumla ya mitaji isiyopungua bilioni 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi na hasa wafanyabiashara wazawa kutumia fursa hii ya dirisha dogo kwa ajili ya kujiongeza mtaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jamal swali la nyongeza.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wafanyabiashara wengi wetu ni wadogo na wa kati na wengi wao wanakabiliwa na changamoto kubwa ya mitaji. Je, Serikali ina mkakati gani ya kuhakikisha taarifa ya fursa hii inawafikia?

Lakini pia katika mwaka uliopita *trend* ya mauzo ya hisa katika soko letu la hisa la Dar es Salaam linaonyesha kushuka, na *share* nyingi ambazo zilizokuwa *traded* pia *price* zake zimeshuka. Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kutatua changamoto hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha majibu kwa ufupi tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa maana ya mkakati, kikubwa ni elimu kwa umma. Kwa kweli soko hili watu wengi hawalielewi, na tumeendelea kusisitiza kwamba *Capital Market and Securities Authority* na DSE wenyewe waongeze jitihada katika kutoa elimu kwa umma. Lakini pia nitumie nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema katika jibu langu la msingi nao pia wachangie kutoa elimu, kwa kweli kuna fursa kubwa

katika kuiongezea mitaji makampuni mbalimbali kwa wananchi wetu kununua hisa katika makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *trend* inashuka lakini kilicho kikubwa kama nilivyosema ni kwa sababu ya uelewa mdogo na kwa hiyo, Serikali inafanya jitihada kupitia taasisi hizi kuongeza elimu kwa umma na fursa hizi zitaongezeka katika siku zijazo ndio matumaini ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa hapo karibu na Mheshimiwa Selasini, halafu Mheshimiwa Frank George Mwakajoka.

MHE. FRANK MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio mimi, naitwa Frank George Mwakajoka. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa kipindi hiki cha miaka miwili kumekuwa na tatizo kubwa sana la malalamiko ya wafanyabiashara katika nchi hii na wafanyabiashara wengi sana wamekuwa wakifunga biashara zao, wafanyabiashara wa maduka pamoja wafanyabiashara wa hoteli, lakini pia wawekezaji wa kutoka nje, wamekuwa wakifunga shughuli zao na kuondoka.

Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia malalamiko ya wafanyabiashara kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanaendelea kuwekeza katika nchi yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango majibu kwa ufupi tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba katika biashara yoyote ile kuna kupanda na kushuka. Kwa hiyo pamoja na kuwa tumeona kwamba baadhi ya biashara zimefungwa lakini ni ukweli pia kwamba baadhi ya biashara nyingine zimechipuka, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili mkakati wa Serikali ni kuendelea kuzungumza na wafanyabiashara ili kuelewa changamoto ambazo zinawakabili, na zile ambazo zinahusu Serikali tutazitatua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa mwisho kabisa hapo. Mheshimiwa Shally.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa Waziri ametueleza kwamba shida kwenye kuwekeza hisa iko kwenye elimu kwa umma; na kwa kuwa ametutajia kwamba wanaonufaika na lile dirisha dogo zaidi ni makampuni. Nilikuwa naomba kuuliza kwa kuwa wengi wa wajasiriamali ni wadogo wadogo wakiwepo wale wamama wa Kilimanjaro na mpaka sasa elimu ya hisa inatoka tu labda kutokea Benki ya CRDB kupitia matawi yake, ni lini sasa mabanki mengine yaliyotajwa pamoja na TOL, TCC, NMB watatoka elimu ya hisa kupitia matawi yao yaliyo huko mikoani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango majibu kwa ufupi tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sikusikia vizuri jina la Mheshimiwa Mbunge aliyetuliza swali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally Raymond.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza haya mashirika na taasisi ambazo nimezitaja, linalonufaika na dirisha dogo, mashirika haya, hisa zao zile wao ndio wanapopata faida wanawagawia wanahisa wao. Kwa hiyo, wananchi wadogo wadogo wananufaika kupitia hizo taasisi ambazo zinanufaika na hilo dirisha dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa swali dogo la pili nitumie nafasi hii kuyashauri mashirika yote yanayohusika na benki hizi kuongeza elimu katika matawi mbalimbali ili wananchi waweze kupata elimu na kunufaika na hilo dirisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Haya sasa Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini aulize swali lake.

Na. 113

Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Moshi

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL aliuliza:-

Uwanja wa ndege wa Moshi ni muhimu sana kwa kukuza masuala ya utalii kwani unatumiwa na watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro lakini uwanja huo unahitaji kufanyiwa ukarabati ili uweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Je, ni lini Serikali itaufanyia ukarabati uwanja huo ili uweze kufanya kazi yake kwa ufanisi hasa kuendeleza sekta ya utalii na uchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kiwanja cha ndege cha Moshi kwa sekta ya usafiri wa anga na mchango wake katika uendelezaji wa sekta ya utalii na uchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu huo wa kiwanja cha ndege cha Moshi, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hicho kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kazi hii ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inahusisha pia viwanja vya ndege vya Iringa, Njombe, Songea, Lindi, Kilwa Masoko, Tanga, Lake Manyara, Singida, Musoma na kiwanja kipya katika Mkoa wa Simiyu na inatarajiwa kukamilika ifikapo Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ifikapo Machi, 2017 Serikali itaendelea na hatua inayofuata ya kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja hicho.

Aidha, mamlaka ya viwanja vya ndege imekuwa ikifanya matengenezo ya miundombinu ya kiwanja mara kwa mara ili kiweze kutoa huduma katika kipindi chote cha mwaka. Vilevile katika mwaka 2016/2017, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetenga shilingi milioni 350 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Raphael Japhael swali la nyongeza.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, uwanja wa ndege wa Moshi umeharibika sana na ni uwanja wa muda mrefu sana tangu wakati wa Muingereza; na ni uwanja muhimu sana na wenye faida sana kiuchumi hasa utalii, kama ilivyoonekana hapa. Na unawezekana kujiendesha wenyewe na ukaleta faida wala hautategemea viwanja vingine kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, nilikuwa naomba *time frame*, je, ni lini Serikali sasa itapeleka hata hizi milioni 350 angalao basi kufanya huo ukarabati ili uwanja huo uweze kutumika? Kwa sababu hii inaonekana inaweza ikawa ni ahadi ya kibajeti, lakini fedha hii isiende kwa wakati; na labda bajeti iishe ikiwa haijapatikana. Naomba nipate uhakika ni lini fedha hii itaenda ili uwanja huo uweze kutumika na uweze kujengewa uzio wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kulikuwa na mpango wa Serikali wa kuwa na chuo cha mambo ya anga (*school of aviation*). Naomba kujua kutoka Serikalini, ni lini chuo hicho kitaanza ili kuweza kusaidia watu wetu kupata utaalum wa mambo ya anga katika nchi hii? Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo shilingi milioni 350 naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kilimanjaro kwamba zitatumika katika mwaka huu wa fedha; na taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya hiyo kazi zimeshaanza. Kusema lini, kwa maana ya tarehe naomba unipe subira, wakati hiizi taratibu zitakapokamilika ndipo tutakapojua. Lakini kikubwa ni kwamba fedha hizi kwa vyovyote vile lazima zitatumika katika mwaka huu wa fedha kabla haujaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule ya *aviation*, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mipango hiyo katika viwanja vingi na hizi zote zinaunganika. Kwa sababu katika masuala ya kufundisha, kwa mfano wenzetu marubani wanahitaji kutumia viwanja vingi na kimoja kati ya viwanja hivi ni hiki cha Moshi. Tuna shule, *NIT* wameanzisha kwa ajili ya kufundisha marubani na ndege zitakuwa zinatumia viwanja hivyo vyote ambavyo viliainishwa toka mwanzo kama sehemu ya *aviation school*.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile muda umekwenda itabidi sasa tuchukue swali moja la msingi na muuliza swali tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel ambaye atauliziwa kwa niaba na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

Na. 114

Barabara ya Kijiji cha Nondwa Wilaya ya Bahi Kuchukuliwa na TANROADS

MHE. DANIEL E. MTUKA (K.n.y. OMARY A. BADWEL) aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne aliahidi barabara ya kijiji cha Nondwa - Sanza, Wilaya ya Bahi itachukuliwa na TANROADS Mkoa wa Dodoma, hata hivyo ahadi ya Mheshimiwa Rais haijatejelezwa mpaka sasa.

Kwa kuwa kipande hicho kinahusisha TANROADS Dodoma na Singida. Je, Serikali ipo tayari kuiagiza TANROADS Dodoma na TANROADS Singida kukiingiza kipande hicho cha barabara katika mpango wa matengenezo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Chidilo - Zegere hadi Nondwa yenye urefu wa kilometa 31 ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi. Barabara hii inaungana na barabara ya Mkoa ya Igongo, ambapo ni mpakani mwa Dodoma na Singida kuelekea Chipanga - Chidilo hadi Bihawana *Junction*, yenye urefu wa kilometa 69 ambayo mwaka 2010 ilipandishwa hadhi kutoka barabara ya Wilaya na kuwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa hadi sasa maombi ya kupandisha hadhi barabara ya Chidilo - Zegere hadi Nondwa hayajawasilishwa rasmi Wizarani kwangu. Ili Wizaru yangu iweze kuyafanyia kazi maombi ya kuipandisha hadhi barabara hii kuwa barabara ya Mkoa, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge afuate utaratibu uliobainishwa kwenye Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009 kwa kupitisha maombi hayo kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuunganisha mikoa miwili ni jambo kubwa sana; na kwa kuwa barabara ya Manyoni - Sanza pamoja na ile ya Chali - Igongo zote zina hadhi ya TANROADS, na tatizo kubwa ni Daraja la Mto Sanza; daraja hili muda mrefu limekuwa ni wimbo. Je, ni lini Serikali itanza ujenzi wa daraja hili ili sasa kuunganisha mikoa miwili?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kufuatilia suala hili, kwa sababu sio mara ya kwanza kulisema hapa. Amemuona Waziri wangu kwa ajili ya utekelezaji wa suala hili. Utakumbuka tulikuambia na ninaomba kupitia nafasi hii wananchi wako wajue kwamba daraja hili ni kipaumbele katika Wizara yetu katika bajeti itakayofuata, labda kama vyanzo vya fedha mtavipunguza, lakini kama hamtavipunguza tuna uhakika tutapata fedha za kutosha kwenye bajeti ya Wizara kuhakikisha na Daraja hili la Mto Sanza tunaliingiza kwenye bajeti.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, sasa ninamkaribisha Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 115

Athari za Bidhaa Feki kwa Wananchi

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza:-

Kumekuwa na bidhaa *fake* katika nchi yetu na zinagundulika zikiwa zimeingia nchini.

Je, Serikali haioni kuwa kugundua bidhaa hizo zikiwa ndani ya nchi zinakuwa tayari zimewaathiri wananchi?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kugunduliwa kwa bidhaa *fake* au bandia zikiwa ndani ya nchi zinakuwa tayari zimewaathiri wananchi. Ili kukabiliana na tatizo la bidhaa hizo kuingia nchini na kuleta madhara kwa watumiaji Serikali kupitia Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission*) kwa kushirikiana na wamiliki wa nembo za bidhaa mbalimbali imekuwa ikitekeleza mikakati ya kuhakikisha bidhaa *fake* haziingii nchini.

Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuwafahamisha wananchi madhara ya bidhaa bandia kiafya, kiuchumi na kimazingira na jinsi ya kutambua bidhaa bandia. Elimu hiyo hutolewa kupitia warsha, makongamano, maonesho ya biashara, vyombo vya habari kama radio, luinga, mitandao ya *computer* na magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika njia za kuingizia bidhaa, ikiwemo Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Viwanja vya Ndege vya JK Nyerere, KIA na mipaka inayopitisha bidhaa kutoka nje ya nchi kwa wingi. Pia, kaguzi za kushitukiza hufanyika katika maduka na maghala yanayohisiwa kuhifadhi na kuuza bidhaa bandia kinyume na Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 na marekebisho yake ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inadhhibiti uingizaji wa bidhaa bandia nchini kwa kuimarisha ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi kabla ya kuingizwa nchini (*Pre Shipment Verification of Conformity Standard*). Kuendelea kuajiri wataalam zaidi na kufungua vituo vya ukaguzi wa ubora wa bidhaa katika mipaka zinapoingilia bidhaa kutoka nchi nyingine. Mipango hiyo inahusu mipaka ya Horohoro, Holili, Namanga, Sirari, Mutukula, Kabanga, Rusumo, Tunduma na Kasumulo. Aidha, *Fair Competition Commission* hushirikiana na taasisi za Serikali hususan Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*), *TBS*, Jeshi la Polisi, Serikali za Mitaa na wananchi wenye mapenzi mema ili kufanikisha ukaguzi na utekelezaji wa bidhaa bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuwachukulia hatua wale wote watakaohusika na uingizaji wa bidhaa bandia, ikiwa ni pamoja na kuteketeza bidhaa hizo au kuzirejesha zilikutoka.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa bidhaa nyingi zinazoonekana nchini kuwa ni feki kwa asilimia kubwa zinatoka nchi ya China na kupitia Bandari ya Dar es Salaam; mpaka sasa Serikali imewachukulia hatua gani *TBS, FCC*, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama vinavyosababisha bidhaa hizi kupita na baadaye kuwaathiri wananchi wasiojua chochote kinachoendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hivi karibuni Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano alitangaza kuzima simu ambazo zilionekana ni *fake*, wakati zinaingia nchini zililipa kodi na zikaonekana ni sahihi mpaka kuingizwa kwenye maduka na baadaye wananchi wakazinunua. Lakini baadae Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi ikaona hazifai na zikazimwa, badala yake wananchi ndio wakapata gharama ya kuingia tena kununua simu nyingine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia au kuwalipa gharama wananchi kwa kuwa uzembe huu ulifanyika na Serikali yenyewe ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida, na nianze na hili la pili ambalo ni rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya mambo yanayotusaidia ni Wanasayansi wa Wizara ya Mawasiliano kwa kugundua njia rahisi ya kuweza kugundua kitu feki. Kwa kufanya hivyo wametusaidia kwa sababu simu zile zina madhara. Bidhaa imeingia, umeinunua, umelipa kodi; si busara kukuacha uendelee kuitumia ikuumize kwa sababu ulilipa kodi; nichukue fursa hii kuwashukuru wataalamu wetu waliogundua njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawasaidiaje; tunalenga kutengeneza kiwanda cha kutengeneza simu ambazo zitawafaa wale wananchi ambao wanashawishika kununua simu za bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba (a) hatua gani tumechukua kwa *TBS* na *FCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa bandia zinaingiaje nchini, tuna matatizo. Mipaka yetu ni *porous*, lakini katika jibu langu la msingi nimesema kuna wananchi wema wanatusaidia. Kwa hiyo, nchi yetu kwa sababu mpaka ni mkubwa na ni *porous*, kuna wimbi kubwa la bidhaa zinazolingia humu kimagendo na ndiyo maana kikwazo kimojawapo cha kufufua baadhi ya viwanda, hasa vya nguo ni kwa sababu, kuna bidhaa zinaingia kimagendo kutoka nchi jirani na kutoka hizo nchi zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba bidhaa yote bandia inatika China, sina uhakika wa suala hilo.

Na. 116

Kuendeleza Eneo la EPZ Wilaya ya Kilolo

MHE. VENANCE M. MWAMOTO aliuliza:-

Mkoa wa Iringa ulitenga eneo la EPZ katika Wilaya ya Kilolo. Je, ni lini eneo hilo litaanza kuendelezwa na ni nini faida ya EPZ?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maagizo ya Serikali kwa mikoa yote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji kwa mfumo wa EPZ na SEZ. Baada ya Serikali katika ngazi ya Mikoa na Wilaya kutenga maeneo hayo inatoa taarifa kwa Mamlaka ya EPZ, ili maeneo hayo yaweze kutangazwa kama maeneo huru ya uwekezaji nchini chini ya Mamlaka ya EPZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mamlaka ya EPZ haijakabidhiwa eneo lililotengwa kwa ajili ya uzalishaji katika Wilaya ya Kilolo kama ilivyobainishwa. Hii inazingatia kuwa tangu kufutwa kwa umiliki wa kwanza wa shamba hilo, kupitia Tangazo la Serikali Namba 130 la tarehe 17 Februari, 2012 taratibu za kulitangaza kama EPZ zilikuwa hazijakamilika. Hata hivyo, Halmashauri imeanza hatua ya awali ili iweze kukamilisha taratibu za kukabidhi eneo la Ruhundamatwe lililotengwa kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda. Michoro (*master plan*) ya eneo husika imekamilika na kazi inayoendelea sasa ni kupima eneo husika. Kazi hiyo ikikamilika Halmashauri hiyo itakabidhi rasmi eneo husika kwa Mamlaka ya EPZ kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji chini ya Mamlaka ya EPZ una faida zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kukuza mauzo nje ya nchi hivyo, kuongeza mapato ya fedha za kigeni; pili, kukuza sekta ya viwanda; tatu, kuongeza ajira na kufundisha stadi za uzalishaji viwandani; nne, kuendeleza uhawilishaji wa teknolojia ya viwanda; tano, kuhamasisha isindikaji wa mazao yetu na uchakataji wa malighafi ili kuongeza thamani; na ksita, uchangia katika kuongeza kipato kwa wananchi, hivyo kupunguza umaskini.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa naamini kabisa wapo watu kutoka EPZ ambao walikuwa wanafuatilia jambo hili na kwa mara ya mwisho shamba hili lilifutwa miaka mitano iliyopita, kwa hiyo jambo hili lilikufa. Lakini kutokana na jitihada za Mkuu wetu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi limefufuliwa.

Sasa Mheshimiwa huoni kuna haja sasa ya wewe mwenyewe kufika na kujionea; kwasababu, katika Mkoa wa Iringa sehemu pekee ambayo tumeitenga ni sehemu ambayo wananchi waliitoa au tulinyang'anya mashamba kutoka kwa watu wengine ambao kwa muda mrefu wamekuwa hawayatumii. Sasa huoni kuna haja yaw ewe Mheshimiwa Waziri, na kwa kuwa, umesoma Tosa Maganga, ukafika ukaona hili jambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, kiashiria kimojawapo cha ujio wa viwanda ni pamoja na EPZ na mambo mengine, na ili viwanda viendeleo, ili upate viwanda ambavyo unaimba kila siku na kuvizungumzia vizuri unahitaji uwe na miundombinu ya barabara, maji na umeme; na ukichukulia kwamba katika Mkoa wa Iringa sehemu pekee ni Kilolo ambayo ina sifa hizo, lakini haina miundombinu ya barabara, maji wala haina umeme wa kutosha.

Sasa je, huoni kuna haja ya wewe na Mawaziri wenzio mkakaa mkaangalia uwezekano wa kuboresha miundombinu, hasa katika Wilaya ya Kilolo katika barabara za Rang'ang'ange, Kidabaga, Mwatasi na sehemu nyingine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi tu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari na nilishazungumza hata Mheshimiwa Ritta, kuna viwanda vya maji vinatengenezwa. Niko tayari sana, nakwenda, na nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba, inatengenezwa *master plan* ambayo itaonesha miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. Miundombinu wezeshi na saidizi ndio inawahusu Mawaziri wengine. Ngoja mimi nisafishe njia, Mawaziri wengine watakuja, nakwenda Kilolo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tunaanza na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 117

Matumizi ya Lugha ya Kiingereza

MHE. SOPHIA M. SIMBA aliuliza:-

Lugha ya Kiingereza ina umuhimu mkubwa katika majadiliano na wenzetu wa nchi nyingine na pia hutumika kufundishia katika shule zetu kuanzia sekondari hadi vyuo vikuu, lakini lugha hii imekuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi katika masomo yao.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufundisha lugha ya kiingereza kuanzia shule za awali na kuendelea ili Watanzania wawe na lugha ya pili inayotumiwa na watu wote?

(b) Je, Serikali haioni kuwa wananchi wengi wanapenda kuongea kiingereza hivyo ione namna ya kuwawezesha?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mattayo Simba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mfumo wa elimu wa Tanzania zipo shule za msingi za Serikali zipatazo 11 na zisizo za Serikali zinazotumia lugha ya kiingereza kuanzia darasa la awali ambapo lugha ya kiswahili hutumika kama somo. Vilevile sehemu kubwa ya shule za msingi za Serikali hutumia lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia tangu awali na lugha ya kiingereza kama somo kuanzia darasa la tatu na kuendelea. Aidha, lugha ya kiingereza ni lugha inayotumika kufundishia shule za sekondari na vyuo vikuu kwa masomo yote isipokuwa komo la kiswahili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inathamini mchango wa matumizi ya lugha ya kiingereza kwani hutumiwa na wananchi kama lugha ya pili katika kupata maarifa na ujuzi katika nyanja za uchumi, siasa, utamaduni, sayansi na teknolojia. Katika kuimarisha matumizi ya lugha ya kiingereza kwa walimu, kati ya mwaka 2014 hadi 2016 Serikali iliendesha mafunzo ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiingereza kwa walimu wapato 14,054 kupitia mpango wa *Student Teacher Enrichment Programme (STEP)*. Pia kati ya mwaka 2015 hadi 2017 iliendesha mafunzo ya mitaala mipya kwa walimu wapato 82,186 ili kumudu stadi za ufundishaji wa masomo yote ikiwemo kiingereza. Aidha, kwa watu wazima wanaopenda kujifunza lugha ya kiingereza zipo taasisi ambazo hutoa mafunzo ya muda mfupi (*short courses*).

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi alivyojibu kwa umakini sana na hususani pale alipozungumzia kwamba walimu wanapata mafunzo zaidi, *refresher course* ambazo kwa kweli wengi wanazihitaji. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiuliza Serikali je, haioni kwamba kuanza kutumia kiingereza kama lugha ya kufundishia kuanzia masomo ya sekondari inasababisha kuleta ugumu sana kwa wanafunzi na matokeo yake wanakuwa wanakariri hasa katika masomo ya sayansi na teknolojia, kitu ambacho kinapelekea wasifanye vizuri sana katika masomo hayo wakati wa mitihani yao, na wale ambao wapo kwenye shule za *private* wanafanya vizuri zaidi? Sisemi shule zote, lakini hii ni sababu mojawapo ya shule za sekondari za *private* kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kipekee kabisa kuhakikisha kiingereza kinatiliwa mkazo kwa sababu kwenye soko la ajira mara nyingi unaona inatokea kwamba *interview* zinafanywa kwa kiingereza. Hata mashirika mengine ya umma wakienda vijana *interview* unawauliza mmefanyiwaje anasema ni kwa kiingereza. Isitoshe sisi tunawakaribisha wawekezaji lakini wale wawekezaji wanahitaji wale ambao wana lugha ya pili ambayo ni kiingereza ili ku-*communicate*. Je, Serikali haioni kwamba tunapoteza ajira nyingi kutokana na ukosefu wa kujiamini wa kuongea lugha ya kiingereza na matokeo yake uakuta hata kwenye *EPZ* wako

Wakenya, Waganda na Wazimbabwe wameajiriwa na mashirika haya ya uwekezaji. Naomba anijibu hilo tunafanya nini, ajira zinapotea. Ahsante sana (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sophia, majibu tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda ifahamike lugha ya kiswahili ni lugha ambayo ni lugha ya taifa, na ni lugha ambayo inafahamika na wananchi wengi toka wakiwa wadogo. Mwanafunzi anapofundishwa lugha ambayo ameozea na amezaliwa nayo ni rahisi zaidi kupokea mitaala anayowekewa kuliko pale ambapo unamfundishia lugha mpya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo tunasema kwamba, sisi kwa kuzingatia kwamba kiswahili ndiyo lugha yetu ya msingi tunasema kwamba mtoto aanze kufundishwa kwa lugha hiyo, lakini mara anapofika darasa la tatu dozi ya kiingereza inaanza kuongezeka kama nilivyosema mpaka kufikia vyuo vikuu. Kwa siku za nyuma kulikuwa na upungufu zaidi kwa sababu unakuta kwamba walimu walikuwa wanaweza kufundisha somo la Kiingereza hata kama alikuwa hana ufaulu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile unakuta mwalimu mmoja alikuwa anafundisha masomo mengi. Kadiri tunavyoenda na kuimarisha sifa za walimu na kuongeza idadi ya walimu kutakuwa na *specialization* kiasi kwamba sasa mwalimu atakuwa anafundisha somo husika na somo alilofaulu na hivyo kiingereza kitazidi kuimarika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa suala la kukosa ajira nipende tu kusema ukweli kwamba kiingereza kimekuwa kikiendelea kuzingatiwa; na niseme tu kwamba kwetu Watanzania yawezekana pengine unyanyapaji wetu nao unachangia katika kuwafanya watoto waogope somo la kiingereza; na kila wakati kutokujiamini na kutokuzungumza kiingereza kwa hofu kwamba nitaambiwa sijui kiingereza. Mimi nasema kwamba kiingereza ni lugha sawa na lugha nyingine, mtu zungumza bila uoga sawa na ambavyo wengine wanaweza kujaribu kuzungumza kiswahili bila uoga na watu tunaelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, serikali itaendelea kuweka mikakati ya kuboresha somo la kiingereza katika shule na kuongeza mijadala katika shule au midahalo, lakini vilevile kupata hata wataalam mbalimbali wanaopenda kuja kujitolea katika nchi yetu kutoka nchi mbalimbali.

Kwa hiyo, niwaombe wote tushikamane kuona kwamba lugha hii ya pili ambayo itatusaidia zaidi katika masuala ya mawasiliano hasa ya kibiashara ili nayo iweze kupata nguvu sawa na ambavyo tunasisitiza katika lugha yetu nzuri lugha ya kiswahili, lugha ambayo ni ya upendo na upole. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali kadhalika tunasema kwamba bado lazima tuongeze jitihada hata katika lugha za alama kwa sababu huyu mwanafunzi si kiingereza peke yake, ni pamoja na lugha ya alama...

MWENYEKITI: Mheshimiwa inatosha hiyo ahsante tumeelewa. Ahsante sana, *it's true* tunakubaliana na wewe. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Leonidas Gama, Mbunge wa Songea Mjini aweze kuuliza swali lake sasa.

Na. 118

Kukosekana kwa Dawa za Shinikizo la Damu Kwenye Zahanati Zetu Vijijini

MHE. LEONIDAS T. GAMA aliuliza:-

Zahanati zetu zilizopo vijijini ambako ndiko walipo wazee walio wengi wakiwemo wastaafu ambao mara kwa mara hukabiliwa na magonjwa yanayotokana na utu uzima ikiwemo shinikizo la damu zinazokabiliwa na ukosefu wa dawa za magonjwa hayo na inasemekana pia zahanati hazitakiwi kuwa na dawa za shinikizo la damu hivyo wazee kutakiwa kwenda ngazi za vituo vya afya

na au hospitali hali inayopelekea wazee hao kupewa dawa za kukojoa tu (*Lasix*) badala ya dawa za shinikizo la damu kwa ajili ya matibabu.

(a) Je, Serikali haijui kuwa wazee wengi wanaosumbuliwa na magonjwa hayo wanaishi vijijini ambako kuna zahanati pekee na siyo hospitali?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha dawa za aina mbalimbali za shinikizo la damu zinazowekwa katika zahanati zetu zilizoko vijijini ambako ndiko wazee wengi walipo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa wazee wengi sehemu za vijijini ambao wanasumbuliwa na magonjwa mbalimbali ya utu uzima ikiwemo shinikizo la damu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imeboresha mgao wa fedha utakaowezesha upatikanaji wa dawa zikiwemo za shinikizo la damu katika ngazi zote za kutolea huduma za afya kuanzia hospitali hadi vituo vya afya na zahanati kulingana na miongozo iliyopo ya utoaji huduma za afya nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inao mwongozo wa utoaji tiba za dawa unaojulikana kama *Standard Treatment Guideline* ya mwaka 2014 ambao umeambatanishwa na orodha ya taifa ya dawa muhimu (*National Essential Medicines List of Tanzania*). Orodha hiyo imebainisha dawa mbalimbali ambazo zinatumiwa katika ngazi mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya, ikiwemo vituo vya afya na zahanati. Dawa za shinikizo la damu zilizopo kwenye orodha hiyo ni kama *Propranolol, Methyldopa, Frusemide, Hydrochlorthiazide* na *Bendrofluazide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vituo vya kutolea huduma za afya vinayo mamlaka ya kuagiza dawa nyingine za kutibu shinikizo la damu nje ya hizi tulizotaja hapo juu kulingana na uwezo na kiwango cha elimu cha wataalam waliopo kwenye kituo husika. Hii ina maana kuwa Wizara hauizuii kituo chochote kuagiza dawa mahali popote za kutibu shinikizo la damu ikiwa kituo husika kitaona kina uwezo wa kufanya hivyo kwa kutoa huduma kwa viwango vinavyostahili. Sanjari na hilo, kulingana na mfumo uliopo wa ugavi na usambazaji wa dawa za Serikali, ni jukumu la watendaji wa vituo husika kuainisha mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuagiza mahitaji yao kutoka Bohari ya Dawa (MSD) kwa kutumia fomu maalum ya taarifa na maombi (*Report and Request – R&R*).

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunajua kwamba tutakuwa wazee, hawa wazee hivi sasa wanateseka sana, hali zao za maisha ni ngumu, uwezo wao wa kupata huduma za dawa ni mdogo. Sasa nilitaka nijue katika mpango wetu tumepanga mpango wa kuhakikisha wazee hawa wanatibiwa bure. Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa kuwatibu bure wazee ili angalau waondokane na matatizo waliyonayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tulizungumza sana juu ya suala la wazee kupata pensheni ili ziwawezeshe kupata huduma muhimu. Mpango huu tumezungumza lakini hatujapata mwelekeo wa nini tunafanya kwa wazee ili waweze kupata pensheni zao. Sasa naomba nipate uhakika Serikali ina mpango gani na imejipangaje, lini tutaanza utaratibu wa kuwapa pensheni wazee ili waweze kujipatia huduma muhimu kama za matibabu, elimu na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza, kwamba ni lini Serikali itaanza kutoa huduma bure za afya kwa wazee, jibu letu ni rahisi tu kwamba tayari Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 inatoa msamaha wa matibabu kwa wazee wote wenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea wasiojiweza; napigia

mstari neno wasiojiweza. Kwa hivyo, taratibu za kuwahudumia wazee wasiojiweza zipo na zimewekwa wazi na Sera ya Afya ya Taifa lakini pia na miongozo mbalimbali ya kutoa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakoelekea mkakati wetu kama Serikali ni kutafuta namna bora zaidi ya kuzihamasisha na kuziwezesha Halmashauri zetu nchini kuwakatia kadi za CHF wazee wote ambao wanakidhi vigezo hivyo. Tayari Waziri wa Afya mwezi wa 12 alitoa agizo hilo kwenye Halmashauri zote nchini na kuna baadhi ya Halmashauri zimeanza utekelezaji wa agizo hilo na ninaamini wazee wanafaidika na mpango huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pensheni kwa wazee; Serikali inatambua mchango mkubwa uliotolewa na wazee wetu kwenye ujenzi wa Taifa hili, na ndiyo maana tunaweka mikakati mbalimbali ya kuwahudumia wazee wetu hususani katika kipindi ambapo wame-*retire* na hawawezi kuendelea kufanya kazi za nguvu za kuzalisha na kukuza kipato chao. Na kwa msingi huo ndiyo maana tumeanza mchakato wa kutengeneza mkakati ambao utatuwezesha kuwahudumia wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza tuliyoifanya ni kutazama takwimu za sensa na kuona kama tutakuwa na uwezo wa kuwa hudumia na kwamba tutakuwa tunabeba mzigo kiasi gani wa wazee ili tuweze kufikiria kama ni kitu tunachoweza kukitekeleza na pengine kukiingiza kwenye bajeti. Kwa sasa kamati ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge inaendelea kutekeleza utaratibu mbalimbali wa kupitia takwimu hizo na kufanya tathmini na baadaye mchakato wa ndani ya Serikali utakapokamilika tutafanya utekelezaji wa mpango huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge wote tuliopo hapa na wananchi wote wakazi wa Dodoma kushiriki kwenye mazoezi ambayo yataongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho asubuhi saa 12 kuanzia kwenye viwanja vya Bunge tutatembea kilometa 5.2 tukiongozwa na Waziri Mkuu wetu mpaka kwenye viwanja vya Jamhuri. Hii itatusaidia kuondokana na changamoto za kutumia sana dawa za shinikizo la damu, lakini pia dawa za kisukari kwa sababu tutakuwa na afya bora. Nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tumemaliza maswali yetu kwa siku ya leo na hapa nina matangazo machache tu.

Tangazo la kwanza ni wageni ambao tunao hapa Bungeni asubuhi hii ya leo. Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni ambao baadhi yao ni wanafunzi wakiwemo wanachuo wa UDOM kutoka Tabora waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, wageni wetu karibuni sana na wanafunzi karibuni mje kujifunza. (Makofi)

Tangazo lingine linatoka Wizara ya Afya, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wanapenda kuwakaribisha Wabunge wote kushiriki katika matembezi ya kilometa tano ikiwa ni sehemu ya kutii agizo la mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kusisitiza wananchi kufanya mazoezi mara kwa mara ili kujilinda na kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukizwa kama vile shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na saratani.

Matembezi hayo yatafanyika siku ya Jumamosi tarehe 11 Februari, 2017 yaani kesho kuanzia saa 12 asubuhi na yataanza viwanja vya Bunge hadi uwanja wa Jamhuri na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake Tanzania Mheshimiwa Margaret Sitta, anawatangazia Wabunge wote wanawake kuwa leo tarehe 10 Februari, 2017 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi wa *dispensary* uliopo jengo la *Utawala Annex*, na semina hiyo itafanyika mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge za leo mchana saa saba.

Hayo ndio matangazo yetu, katibu!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Haya leo nitachukua mwongozo mmoja huku na mmoja huku, tunaendelea, Mheshimiwa Mtulia na Mheshimiwa pale...

MHE. MWITA M. WAITARA: Wawili, wawili, siku muhimu hii!

MHE. JOSEPH O. HAULE: Mwongozo wa Spika.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MBUNGE FULANI: Chukua yote kama wenzako wanavyofanyaga.

MWENYEKITI: Ah! msinifundishe subirini basi, tuanze na wewe.

MHE. JOSEPH O. HAULE: Tumalize vizuri Bunge leo, *it's very important*.

MWENYEKITI: Tunaanza na Mheshimiwa pale.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68 sitaisoma, mwongozo wangu unahusiana na jambo la kuichangia timu ya *Serengeti Boys* ambao walitutebelea jana wanakwenda kushiriki kwenye mashindano ya *under seventeen*. Nilikuwa najaribu kupiga mahesabu na nikaona kwamba maana bado kuna *confusion* kama tunachanga shilingi 20,000 au posho ya siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kwa sababu ya hali halisi nikajielekeza kwamba tunachanga shilingi 20,000 na nilipopiga hesabu za haraka inaonekana tunaweza tukapata kama milioni saba au nane. Na ukiangalia kwenye bajeti kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari ya *TFF* maandalizi ya kufanikisha ushiriki wa timu hii yanahitaji kiasi kisichopungua shilingi bilioni moja. Sasa nikawa najjuliza shilingi milioni saba ni nini katika shilingi bilioni moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa, naomba tusikilizane Waheshimiwa Wabunge; nilikuwa na wazo kwamba Wabunge wapenzi wa Simba na Yanga wacheze mechi na kile kitakachopatikana tuweze kuichangia *Serengeti Boys*; kwa sababu nakumbuka wakati wa maafa ya Kagera tulipata zaidi ya shilingi milioni 180. Lakini sambamba na hilo hicho kitakachopatikana kwanza kiwe na usimamizi ulio madhubuti kwa sababu jana mmeona *reluctance* ya Wabunge hapa katika kuchangia ni kutokana kutokuwa na imani na *TFF*. Wabunge ni wepesi sana katika kuchangia shughuli mbalimbali, lakini jana walikuwa *reluctant* kama *indicator* ya kutokuwa na imani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Wabunge pia walikwenda kushiriki mashindano Mombasa katika hali ambayo haielezeki ugumu wake mimi nilikuwa ni mmoja wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa *spirit* hiyo hiyo baada ya mechi ya Simba na Yanga kama itaafikiwa kile kitakachopatikana *partly* kiende kwa *Serengeti Boys* na *partly* kikapunguze maumivu ya wale waliokuwa wameenda Mombasa ili kuonesha *solidarity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Bobali, haya wote! Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Mtulia, Maji Marefu na Mheshimiwa Waitara.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaniruka vipi mimi?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. JOSEPH O.MBILINYI: *It's very important.*

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7)...

MWENYEKITI: Tafadhali naomba mtoe kwa ufupi jamani, ieleweke, kwa sababu ni wengi mnataka miongozo.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaisoma pamoja na Kanuni ya 46(1) kuhusu namna ya kujibu maswali Bungeni.

Leo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wakati anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi alisema kwamba Tanzania hakuna ugaidi. Lakini hivi karibuni katika mkutano huu huu Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba alilithibitisha Bunge hili kwamba Tanzania kuna ugaidi na akahoji. Tunahitaji viashiria vya namna gani tuthibitisha kwamba nchi hii ina ugaidi? Akatolea mfano kushambuliwa kwa Ubalozi wa Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba mwongozo wako, wapo watu wako ndani sasa mwaka wa nne. Yanapokuja majibu kwamba huyu anasema kuna ugaidi, huyu anasema hakuna ugaidi mnatuchanganya, kuna watu wako ndani huu mwaka wa nne. Naomba mwongozo wako, Serikali itoe *definition*, maana halisi ya nini maana ya ugaidi, watu wanateseka, wako magerezani, Naibu Waziri anasema hakuna ugaidi, Waziri anasema kuna ugaidi, tunahitaji tafsiri halisi ya nini maana ya ugaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini mimi mwongozo wangu tayari Mheshimiwa Chumi ameshaumaliza, kwa hiyo, sina cha nyongeza. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa humu Bungeni tukajadiliana vizuri na kwa mara ya kwanza tukashikamana kwa maana ya kujenga hadhi na heshima ya Bunge hili tukapitisha maazimio manne muhimu sana. Lakini leo asubuhi nimetumiwa *clip* mbalimbali na wananchi wa kawaida kabisa, wanahoji namna ambavyo hadhi ya Bunge tuna namna ya kujipanga ili tuheshimiane humu ndani, mjadala umefanyika kwa asilimia 100 maazimio yaliungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye gazeti la leo la Habari Leo, ukurasa wa 25 imeandikwa habari na mwandishi Halima Mlacha akiwa hapa Dodoma, lakini nimesikia *clip* ya redio ikimnukuu na kum-*quote* Katibu wa Bunge hili, Mheshimiwa Dkt. Kashililah ambaye yuko humu ndani akisema, ntachukua tu maeneo machache, naomba ninukuu, kwamba; "Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah amebainisha kuwa maazimio yaliyopitishwa na Bunge dhidi ya viongozi hao hayakufuata utaratibu na kanuni za Bunge hili."

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea; "Akizungumza na baadhi ya waandishi wa habari katika viwanja vya Bunge Mjini Dodoma jana, Dkt. Kashililah pamoja na kukataa kuzungumza kama ofisi yake akitekeleza maazimio hayo, kama itatekeleza au la, kwa sababu imesema haikufuata utaratibu, alisisitiza kuwa maazimio hayo yalipitishwa kimakosa kwa kuwa hayakufuata taratibu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama nikaona kwamba kumbe tunadhani kwamba wanaolihalilisha Bunge wako nje ya Bunge kumbe tunao humu ndani, na hii ni hatari sana, tulikubaliana humu. Sasa nataka niombe mwongozo wako kwamba kama Mwenyekiti, ambaye ni mtu ambaye kweli tunamuamini sana tunamheshimu sana Mheshimiwa Andrew Chenge, ambaye hata wewe wakati mwingine tunafanya *consultation* kupata namna ya kwenda mbele kwa maana ya kwa maslahi mapana ya nchi hii, na Makatibu wako hapo mbele, na Katibu wa Bunge yuko

Bungeni, kitendo cha kwenda kuandika maneno haya kwenye magazeti ni kulidhalilisha Bunge na kutuhujumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ni *attempt* ya Bunge. Tulitarajia kama kuna hoja alikuwa nayo angepenyeza kwa utaratibu wa kawaida kushauri kiti hapo vizuri. Lakini siamini na sishawishiki kwamba inawezekana Mheshimiwa Chenge kwa umahiri wake, na miona alivyoongoza kikao kwa kutoa maelekezo na ushauri na wote Waheshimiwa Mawaziri mpaka AG alikuwepo humu ndani, tulikubaliana kwamba maazimio yaende, kama kuna hoja itarudishwa humu ndani tutajadili kama ni kubadilisha Bunge libadilike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe mwongozo wako, kwamba haya matendo yanayoendelea sasa, kama nilivyosema, naomba nirudie, ni majaribu makubwa katika Bunge hili. Wananchi wa kawaida wanahoji, inawezekana tunajadili jana, juzi tulikuwa hapa halafu Katibu ambaye kimsingi kama ni kuandika barua kwenda kwa wahusika ataandika yeye kama Mtendaji Mkuu wa Bunge hili, kama ni utaratibu mwingine wa kawaida hatukuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ili jambo hili tujue namna ya kwenda mbele. Ahsante. (Makofi)

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kuniona. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Ninaomba mwongozo wako, nimeshtushwa sana wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani akijibu swali namba 109. Swali namba 109 linafanana kabisa na swali namba 4 lililojibiwa hapa tarehe 31 Januari, ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ally Saleh kwa niaba ya Mheshimiwa Muhammed Amour.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya tarehe 31, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alisema kwamba Wizara yake haina taarifa na haya matukio ya uhalifu ya mara kwa mara yanayotokea Zanzibar. Lakini leo akijibu swali namba 109 amesema kwamba ni kweli matokeo haya ya uhalifu yanatokea mara kwa mara Zanzibar na hivyo Wizara inajipanga kuhakikisha kwamba Jeshi litakuwa na uwezo wa kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, majibu yapi ndiyo yana makosa, yale ya tarehe 31 au haya? Ili kwa mwongozo wako sasa uielekeze Wizara hii irudie swali moja ambalo majibu yake yatakuwa sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa George.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti *I am not George, I am Joseph, ahsante. George Mkuchika is over there.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niko kwenye kanuni ya 68(7), jambo lililotokea mapema. Jambo lililotokea mapema na linaloendelea ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wanajadili na pia Taifa limeshtuka. Wabunge wanajadili na Taifa limeshtuka Serikali imetangaza kuzuia *online tv*. Maamuzi kama haya yanazidi kuliingiza Taifa hili gizani. Tunakuwa *North Korea* kwa *speed* ya ajabu sana na tunajitengeneza kuwa *a pariahstate*, tunaonekana wa ajabu kwenye *international community* kwa maamuzi kama haya. Wananchi wana haki ya kupata habari za upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano jana Askofu Gwajima na mfanyabiashara Manji walipata nafasi ya kujibu haraka sana tuhuma dhidi yao zilizotangazwa kwenye *tv* pendwa za Serikali, lakini wao wasingeweza kupata nafasi ya *live* kama kusingekuwa na *online tv* wakaweza kujitetea kwa haraka sana. Sasa wananchi pia sasa wamekuwa wakitegemea *online tv* kupata habari za Bunge, kwa hiyo ni wazi suala la kuzuia kwa namna yoyote *online tv* ni mwendelezo wa kuzuia wananchi kupata habari za Bunge, na ni mwendelezo wa kuliweka Taifa gizani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka mwongozo wako, kwa nini *online broadcasting* isiendelee mpaka pale hicho kinachodaiwa sheria itakapotungwa kwa sababu kuwepo kwake hakuvunji sheria zozote? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Tumemaliza miongozo eeh. Haya, ahsanteni sana kwa miongozo yenu. Nimepokea miongozo yenu, nimepokea miongozo mitano hapa, mwongozo wa kwanza kuhusu *Serengeti Boys*, wa pili kuhusu namna ya kujibu maswali hapa Bungeni, ametajwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri wa Katiba na Sheria, pia Mheshimiwa Waitara hapa amezungumzia kuhusu Bunge lililopoitisha maazimio hapa sina haja ya kurudia yote, na namna ambavyo amemnukuu Katibu wetu wa Bunge, Dkt. Kashilillah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la nne linahusiana pia na swali namba 109 kufanana na swali lingine ambalo limetajwa hapo kuhusu Wizara hii sasa ametaka jibu lipi ni sahihi kati ya hayo na lipi lina makosa.

Mwisho Mheshimiwa Joseph anazungumzia suala linaloendelea kuhusu *online tv*. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(10) nimepokea miongozo yote na tutaifanyia kazi baadaye, tuendeleee. Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA –KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*]

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

MWENYEKITI: Haya, muswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza kwa hiyo utakwenda kwenye Kamati inayohusika, tuendeleee. Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo
na**

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya
Bunge
na**

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

MWENYEKITI: Tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, karibu Mwenyekiti. (Makofi)

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na kamati katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017. Aidha, taarifa hii imeainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo mbalimbali zilizowasilishwa tarehe 01 Novemba, 2016 katika Mkutano wa Tano wa Bunge, pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu sheria ndogo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii vilevile inafafanua kuhusu taratibu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati sanjari na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu namna bora ambavyo Bunge linaweza kuisimamia Serikali katika mchakato wa utungaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo miongoni mwa mambo mengine ni kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni na Serikali ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi. Malengo ya masharti haya ya kanuni ni kulipatia Bunge mamlaka ya udhibiti wa utungaji wa sheria ndogo kwa vyombo vingine ambayo Bunge limekasimu kwake kwa mujibu wa Ibara ya 97(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (*The Parliamentary Control Over Delegated Legislation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Namba Moja (*The Interpretation of Laws Act, Cap. 1, Revised Laws of 2002*) inaweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nguvu ya udhibiti wa sheria ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa sheria ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kwa niaba ya wananchi kinachoishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti huu wa Bunge pia ni kwa sababu sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania. Shughuli hizo ni pamoja na zifuatazo; kilimo cha mazao ya biashara na chakula, ufugaji na minada ya mifugo, uvuvi, biashara za mama lishe, biashara za usafiri ikiwemo bodaboda, uchimbaji wa madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia zinazotumika kutekeleza majukumu ya Kamati ni kuwa baada ya sheria ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, sheria hiyo inatakiwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 38(1) cha tafsiri ya sheria kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita ya Vikao vya Bunge vya Mkutano husika. Aidha, matakwa ya sheria yanapewa pia nguvu kupitia Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayosomeka kama ifuatavyo, nanukuu; "37.- (2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri na kugawiwa kwa Wabunge."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua hiyo, Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa sheria ndogo yoyote iliyowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, sheria ndogo ambazo hutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni ni zifuatazo:-

Moja, *Orders* (Amri); mbili, *Proclamations* (Matamko); tatu, *Rules* (Kanuni); nne, *Rules of Court* (Kanuni za Mahakama); tano, *Regulations* (Kanuni za Mawaziri na Mamlaka nyingine); sita, *Notices* (Ilani/Taarifa); saba, *By-laws* (Sheria Ndogo za Halmashauri) na nane, *Instruments* (Hati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo ambazo hutungwa na vyombo mbalimbali vya Serikali ambavyo Bunge limekasimu kwake madaraka ya kutunga sheria ni nyingi. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(8) ya Kanuni za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza majukumu yake kwa kufanya mambo yote yaliyoainishwa katika ibara ya 1.3.4 ya taarifa hii ambayo naomba Waheshimiwa Wabunge waipitie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara namba 1.3.5 ya taarifa ya Kamati kuna kielelezo kinachoonesa kwa muhtasari tu na katika lugha ya picha hatua za utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika mchakato wa udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo zinazowasilishwa Bungeni na Serikali baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizofanywa na Kamati kati ya Januari, 2016 na Januari, 2017 ni pamoja na uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilisha katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na

Mkutano wa Nne wa Bunge. Katika Mkutano wa Pili, wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge lako, Serikali iliwasilisha Bungeni Sheria Ndogo mbalimbali. Kati ya sheria ndogo zilizowasilishwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo 180.

Aidha, Kamati ilipokea maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa kwa namna moja au nyingine na Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati. Wadau ambao walifika na kutoa maoni yao ni pamoja na makundi yafuatayo; vyama vya wakulima, ushirika na masoko, asasi za kiraia, vyama vya wafanyakazi, wasanii wa muziki, filamu na sanaa za maonesho, makampuni binafsi na vyama vya kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo pia ni Kamati ya sekta mtambuka, Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari au masharti yake kuhitaji ufafanuzi wa kina kuhusu maudhui yake, ziligusa Wizara zote isipokuwa zifuatazo:-

- (i) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa,
- (ii) Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
- (iii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,
- (iv) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
- (v) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasiliswa katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge, Kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na zifuatazo ni baadhi tu ya dosari hizo:-

(i) Sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama inayoidhinisha sheria ndogo husika kutungwa;

(ii) Sheria ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia, yaani kuwa na *unreasonable provisions*;

(iii) Sheria ndogo kuwa na makosa ya kiuandishi na kiuchapaji; na

(iv) Sheria ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika mchakato wa utungaji wa Sheria ndogo ambazo zinachangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika Sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Uchache wa Wanasheria wenye taaluma ya Uandishi wa Sheria katika Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uhaba wa wataalam hao unasababisha Sheria Ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa sababu naye si tu kwamba ana wataalam wachache, lakini pia ana kazi nyingi.

(ii) Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno (*copy and paste*) bila kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili Sheria Ndogo zisizoendana na uhalisia wa sababu na madhumuni ya kutungwa kwake.

(iii) Baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa Mamlaka waliyopewa na Bunge ya kutunga Sheria Ndogo kuweka masharti ambayo ama yalikataliwa au kupingwa na Kamati za Kudumu za Bunge wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria inayotoa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo husika (*Principal Act*). Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa na jukumu kubwa la kushughulikia dosari za masharti yaliyomo ndani ya Sheria Ndogo ambayo yangeweza kupatiwa uhalali kwa kuyaweka masharti hayo katika sheria mama.

(iv) Baadhi ya Wizara kutoshirikisha kikamilifu wadau wanaoguswa na masharti ya Sheria Ndogo na hivyo kusababisha kuwepo kwa vifungu ambavyo vina dosari au utekelezaji wake kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria Ndogo zote zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari, Kamati ilitoa maoni, na mapendekezo ili Serikali iyafanyie kazi. Aidha, itakumbukwa kuwa katika taarifa ya kwanza ya Kamati hii kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo kuhusu iliyowasilishwa Bungeni tarehe 10 Novemba, 2016, Bunge lilipitisha azimio la kuyakubali maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa sehemu kubwa, Serikali imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ingawa kiwango cha utekelezaji wa maoni na mapendekezo hayo unatofautiana kati ya Wizara moja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao na Misitu iliyotungwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ya mwaka 2015, iliyotungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kiliweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi 100,000 kutokana na makosa yaliyoainishwa. Hata hivyo, adhabu ya kifungu hicho ilikuwa kinyume na masharti ya kifungu cha 67 cha sheria mama, Sura ya 290 ambacho kinazitaka Halmashauri zinapotunga Sheria Ndogo yoyote chini ya sheria hii kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi 50,000. Hivyo basi, Kamati iliishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hiyo ili kuondoa dosari iliyobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitekeleza maoni na ushauri wa Kamati na Halmashauri husika imefanya marekebisho katika Sheria Ndogo hiyo kwa kuweka faini isiyozidi shilingi 50,000 kama yalivyo matakwa ya sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilibaini kuwa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo za baadhi ya Halmashauri zinatokana na changamoto mbalimbali katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo ikiwemo ya wanasheria kutokuwa na elimu stahiki ya uandishi wa sheria kama ilivyoelezwa awali. Kwa sababu hiyo, Kamati iliishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuandaa programu ya mafunzo ya mara kwa mara kwa wanasheria wa ofisi hiyo, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Halmashauri zinatunga Sheria Ndogo ambazo zina viwango vya faini vikubwa kuliko vilivyowekwa na sheria mama kutokana na hisia kwamba, Sheria za Serikali za Mitaa zilizotungwa na Bunge hili zinaweka kiwango kidogo cha adhabu ya faini ukilinganisha na uzito wa baadhi ya makosa yanayoweza kutendwa na kushughulikiwa na mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kamati, hisia hizi kamwe haziwezi kuhalalisha Halmashauri hizo kutunga Sheria Ndogo zinazoweka adhabu kubwa kinyume na masharti yaliyomo katika sheria mama. Hivyo basi, Kamati iliishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kufanya marekebisho ya viwango vya faini na adhabu vilivyopitwa na wakati kwa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mama husika, iwapo itaona kuna ulazima wa kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni Sheria Ndogo inayoitwa *The Petroleum Bulk Procurement Regulations, 2015* ambayo imo katika Tangazo la Serikali Na. 508 la tarehe 6 Novemba, 2015 iliyotungwa chini ya vifungu vya 168 na 258 vya Sheria ya Petroli. Sheria Ndogo hii imetungwa na Waziri wa Nishati na Madini kwa lengo kuanzisha mfumo wa uagizaji wa pamoja (*bulk procurement system*) wa bidhaa za petroli hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hoja nyingine, Kamati ilibaini kuwa kanuni ya 15(7) ya Sheria Ndogo hiyo inaweka masharti kwamba Waziri anaweza kuzuia bidhaa za petroli zinazosafirishwa kwenda nchi za jirani kupitia Tanzania (*transit petroleum products*) ili zitumike hapa

nchini katika mazingira ya dharura atakayotangaza. Kanuni hiyo inasomeka kama ifuatavyo; *"Under emergency conditions declared by the Minister, transit petroleum products may be localized."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kamati, masharti ya kanuni hiyo yamempa Waziri wa Nishati na Madini mamlaka ambayo endapo yatatumika isivyopasa yanaweza kuhatarisha mahusiano ya kibiashara na kisiasa na nchi za jirani husika. Bila kuathiri masharti ambayo yanapatikana katika sheria mama, Kamati ilishauri kwamba kanuni hiyo irekebishwe kwa kufafanua masharti na maana halisi iliyopo katika kifungu cha 253 cha sheria mama ili kuendana na dhamira ya Bunge wakati inatunga sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilipendekeza kuwa kanuni hiyo iweke masharti ambayo mwenye leseni ya kusafirisha mafuta hayo pamoja na mpokeaji wa mzigo huo katika nchi jirani wawe na haki ya kupewa taarifa kuhusu hatua inayokusudiwa kuchukuliwa na Waziri kuhusiana na bidhaa hiyo. Kamati ilipendekeza kuwa kanuni hiyo iandikwe kama ifuatavyo; *"Under emergency conditions provided for under section 253 of the Act, The Minister may localize transit petroleum products after notice has been given to the licensee and to the consignee."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Nishati na Madini aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa maoni na mapendekezo ya Kamati tarehe 26 Januari 2017, ambapo pamoja na masuala mengine, alibainisha kuwa Wizara yake imefanya mapitio ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na kupendekeza rasimu mpya ya kanuni hizo ikiwemo kanuni ya 15(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na majibu hayo kwa sababu Wizara haikuonesha jitihada za haraka za kufanya marekebisho yaliyopendekezwa tangu kuibuliwa kwa hoja hiyo katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Februari, 2016 wakati kuna Sheria Ndogo nyingine zilizotungwa na Wizara hiyo hiyo Septemba, 2016 na tayari zilikuwa zimefanyiwa marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilichambua Sheria Ndogo inayoitwa *The Drugs Control And Enforcement General Regulations, 2016* ambayo imo katika Tangazo la Serikali Na. 173 la tarehe 10 Mei, 2016 iliyotungwa chini ya kifungu cha 67 cha Sheria ya Udhidhi wa Dawa za Kulevya (*The Drugs Control and Enforcement Act, CAP. 95*) ya sheria za nchi yetu. Sheria hii inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Dosari zilizoibuliwa na Kamati kuhusiana na Sheria ndogo hiyo zipo kwenye ibara namba 2.3.14 hadi ibara namba 2.3.18 ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 20 Januari, 2017, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Walemavu aliwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Sheria Ndogo hiyo, ambapo pamoja na masuala mengine alibainisha kuwa ofisi yake imefanya marekebisho katika kanuni tajwa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Marekebisho hayo yatawasilishwa Bungeni baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata fursa ya kuchambua Sheria Ndogo mbalimbali zinazohusiana na masuala ya watoto kutokana na Sheria ya Mtoto, Sura Namba 13 ya mwaka 2009. Moja kati ya Sheria Ndogo hizo ni Kanuni za Ajira za Watoto za mwaka 2012, tangazo la Serikali Namba 168 la tarehe 13 Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo hiyo inaweka masharti kuhusu haki ya mtoto kufanya kazi, makatazo na mazingira ambayo mtoto hapaswi kufanya kazi, haki za mtoto anayefanya kazi pamoja na taratibu za ufuatiliaji ustawi wa mtoto ambaye anafanya kazi. Dosari zilizoibuliwa na Kamati kuhusu Sheria ndogo hiyo zimeainishwa kuanzia ibara namba 2.3.21 hadi ibara namba 2.3.24 ya Taarifa ya Kamati

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 18 Januari, 2017, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aliwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ambapo pamoja na masuala mengine, alibainisha kuwa Wizara yake imefanya marekebisho katika kanuni zote zilizobainika kuwa na dosari kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge. Sheria Ndogo zilizowasilishwa mezani na Serikali katika mkutano wa tano zimeorodheshwa katika ibara ya 2.4.1 ya taarifa ya Kamati. Kwa kuzingatia hilo, uchambuzi uliofanywa ulilenga kujiridhisha kuwa Sheria Ndogo hizo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba na sheria nyingine za nchi mbalimbali ikiwa pamoja na kwenda kinyume na sheria mama na sheria nyingine. Dosari hizo mtaziona katika ibara ya 2.4.4 mpaka ibara ya 2.4.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu ya muda, nijielekeze tu katika mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati yapo katika taarifa hii Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kuyasoma. Ipo kazi ya ziara ambazo zimefanywa lakini kubwa ambalo tunataka tuliseme ni kwamba sheria hizi, hasa yale ambayo yanatokana na maamuzi ya Serikali tunataka tuwasaidie. Mkutano wa wadau ambapo tunatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupunguza na kuondoa kero kwa wakulima wa mazao mbalimbali zinazotokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazowekwa na sheria tofauti mtaona mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yapo mapendekezo ya jumla ambayo ndiyo msingi wa hoja hii. Katika upande wa uandishi wa Sheria Ndogo, Kamati imependekeza na kushauri Serikali za mitaa ziachane na mtindo wa kunakili Sheria Ndogo kutoka katika mamlaka nyingine na kutunga Sheria Ndogo kulingana na mazingira halisi. Makosa kuhusu uchapishaji, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Bungeni tangu Mkutano wa Pili hadi sasa ambapo imebainika kuwa kuna makosa ya kiuandishi na kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuandaa programu endelevu ya mafunzo kwa wanasheria wa Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kujijengea uwezo wa uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utungaji wa Sheria ndogo, mchakato wake; Kamati inashauri Mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaotungwa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maboresho; Kamati inashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianze kutumia mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa upitishaji wa Sheria Ndogo katika hatua mbalimbali (*The By-Laws database*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali na vyombo vyake kuchukua hatua za haraka katika kuzifanyia marekebisha Sheria Ndogo zote zenye dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ikichukuliwa na Serikali haraka, itaiwezesha Serikali kulifanyia kazi tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu kupunguza kodi, tozo na ada katika mazao mbalimbali. Kupunguza kodi, tozo na ada zinazohusiana na masuala ya maliasili na misitu. Lakini pia tunapendekiza tuzingatie matakwa ya sheria kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria cha kuwasilisha kwa wakati kanuni zinazochapishwa au zinazotungwa na mamlaka mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 3.2.2 tunatoa mapendekezo ya Kamati kuhusiana na kazi iliyofanywa kwa Sheria ndogo zilizowasilishwa katika mkutano wa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kwa kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu, Mkutano wa Nne na Mkutano wa Tano wa Bunge lako tukufu na hatimaye kufanikisha ukamilishaji wa taarifa hii. Wajumbe hao mtawaona katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa namshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, ninawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima ningependa kuwatambua lakini kwasababu a muda sitaweza kuwataja wote lakini tunawatambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali.

Vilevile niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao na wale ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi. Ushiriki wao katika vikao vya Kamati pamoja na maoni waliyowasilisha umesaidia sana kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo na uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO PAMOJA NA MAONI NA MAPENDEKEZO YALIYOMO KWENYE TAARIFA HIYO – KAMA ILIVYOWALISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 MAELEZO YA AWALI

- 1.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.
- 1.1.2 Aidha, Taarifa hii imeainisha matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa tarehe 1 Novemba, 2016 katika Mkutano wa Tano wa Bunge pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo hizo.
- 1.1.3 **Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii vilevile inafafanua kuhusu njia mbalimbali zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati sanjari na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu namna bora ambavyo Bunge linaweza kuisimamia Serikali katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

1.2 MAJUKUMU YA KAMATI NA MSINGI WA UTEKELEZAJI WAKE

- 1.2.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo ni kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Malengo ya masharti haya ya kikanuni ni kulipatia Bunge Mamlaka ya Udhhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo kwa vyombo vingine *(Parliamentary Control Over Subsidiary*

Legislation) ambayo Bunge limekasimu kwake kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

- 1.2.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002) inaweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nguvu ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoishauri na kuisimamia Serikali. Udhibiti huu wa Bunge pia ni kwa sababu Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania. Shughuli hizo ni pamoja na zifuatazo:-
- Kilimo cha mazao ya biashara na chakula
 - Ufugaji
 - Uvuvi
 - Biashara za mama lishe
 - Biashara ya usafiri wa "bodaboda"
 - Uchimbaji wa madini


1.3 NJIA ZINAZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA KAMATI

- 1.3.1 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria hiyo inatakiwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1), kuwasilishwa Bungeni (*laid before the National Assembly*) ndani ya siku sita (6) ya Vikao vya Bunge (*six sitting days*) vya Mkutano husika. Aidha, matakwa haya ya Sheria yanapewa pia nguvu kupitia Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayosomeka kama ifuatavyo:-
- "37.- (2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri ..."*
- 1.3.2 Baada ya hatua hiyo, Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo yeyote iliyowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.
- 1.3.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo ambazo hutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni ni hizi zifuatazo:-
- Orders (Amri)
 - Proclamations (Matamko)
 - Rules (Kanuni)
 - Rules of Court (Kanuni za Mahakama)
 - Regulations (Kanuni za Mawaziri na Mamlaka nyingine)
 - Notices (Taarifa/Ilani)
 - By - Laws (Sheria Ndogo za Halmashauri)
 - Instruments (Hati Idhini)
- 1.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo ambazo hutungwa na vyombo mbalimbali vya Serikali ambavyo Bunge limekasimu kwake madaraka ya kutunga Sheria ni nyingi. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-
- Kuandaa Orodha ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika kila Mkutano wa Bunge;
 - Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa;

- c) Kufanya Mikutano ya Kusikiliza Maoni ya Wadau (Public Hearing) kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa;
- d) Kuandaa Jedwali la Uchambuzi wa Kamati (Matrix) linalobainisha matokeo ya Uchambuzi wa Kamati na kuliwasilisha Serikalini ili iandae majibu ya hoja zilizobuliwa kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni;
- e) Kukutana na Wizara husika (relevant Ministries) ili kupokea majibu ya Serikali kutokana na Uchambuzi wa Kamati;
- f) Kuwasilisha Bungeni Taarifa Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati na kutoa maoni na mapendekezo ili Bunge liridhie kwa Azimio la Bunge (*Parliamentary Resolution*) kwa ajili ya Utekelezaji wa Serikali;
- g) Kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali itokanayo na Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo;
- h) Kufanya ziara, mafunzo na semina kuhusiana na Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo na namna ya uchambuzi wa Sheria Ndogo

1.3.5 **Mheshimiwa Spika**, kielelezo kinachofuata kinaonyesha kwa muhtsari na katika lugha ya picha hatua za utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika Mchakato wa Udhhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

MCHAKATO WA UDHIBITI WA KIBUNGE WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI (THE PROCESS OF PARLIAMENTARY CONTROL OVER SUBSIDIARY LEGISLATION)



SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA KAMATI KATI YA JANUARI, 2016 NA JANUARI, 2017

2.1 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHA KATIKA MKUTANO WA PILI, MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE

2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa hapo juu, Serikali iliwasilisha Bungeni Sheria Ndogo mbalimbali. Kati ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo mia moja themanini (180). Aidha, Kamati ilipokea maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa kwa namna moja au nyingine na Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati. Wadau ambao walifika na kutoa maoni yao ni pamoja na makundi yafuatayo:-

- a) Vyama vya Wakulima, Ushirika na Masoko
- b) Asasi za Kiraia
- c) Vyama vya Wafanyakazi
- d) Wasanii wa Muziki, Filamu na Sanaa za Maonyesho
- e) Makampuni binafsi
- f) Vyama vya Kitaaluma

2.1.2 **Mheshimiwa Spika**, aidha, kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo ni Kamati ya Sekta Mtambuka, Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari au masharti yake kuhitaji ufafanuzi wa kina kuhusu maudhui yake, ziligusa Wizara zote isipokuwa zifuatazo:-

- a) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
- b) Wizara ya Maji na Umwagiliaji
- c) Wizara Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa,
- d) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
- e) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
- f)

2.2 MATOKEO YA UCHAMBUZI SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISWA KATIKA MKUTANO WA PILI, MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE

2.2.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa hapo juu, Kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na zifuatazo ni baadhi yake:-

- a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama inayoidhinisha Sheria Ndogo husika kutungwa;
- b) Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (*unreasonable provisions*);
- c) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiandishi na kiuchapaji; na
- d) Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu.

2.2.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo ambazo zinachangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo zilifanyiwa uchambuzi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Uchache wa wanasheria wenye taaluma ya uandishi wa sheria (*legislative drafters*) katika Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uhaba wa wataalamu hao unasababisha Sheria Ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali zikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (*Chief Parliamentary Draftsman*) kwa sababu naye siyo tu kwamba ana wataalam wachache, lakini pia ana kazi nyingi.

- b) Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno (*copying and pasting*) bila kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili Sheria Ndogo zisizoendana na uhalisia wa sababu na madhumuni ya kutungwa kwake.
- c) Baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa mamlaka waliyopewa na Bunge ya kutunga Sheria Ndogo kuweka masharti ambayo aidha yalikataliwa au kupingwa na Kamati za Kudumu za Bunge wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria inayotoa madaraka (*Principal Act*). Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa na jukumu kubwa la kushughulikia dosari za masharti yaliyomo ndani ya Sheria Ndogo ambayo yangeweza kupatiwa uhalali kwa kuyaweka masharti hayo katika Sheria Mama.
- d) Baadhi ya Wizara kutoshirikisha kikamilifu wadau wanaoguswa na masharti ya Sheria Ndogo na hivyo kusababisha kuwepo kwa vifungu ambavyo vina dosari au utekelezaji wake kuwa na changamoto.

2.2.3 **Mheshimiwa Spika**, katika Sheria Ndogo zote zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari, Kamati ilitoa maoni, na mapendekezo ili Serikali iyafanyie kazi. Aidha, itakumbukwa kuwa katika Taarifa ya Kwanza ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo iliyowasilishwa Bungeni tarehe 10 Novemba, 2016, Bunge lilipitisha azimio la kuyakubali maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

2.3 UTEKELEZAJI WA MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI, MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE

2.3.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa sehemu kubwa, Serikali imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ingawa kiwango cha utekelezaji wa maoni na mapendekezo hayo unatofautiana kati ya Wizara moja na Wizara nyingine.

2.3.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Mimitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ya Mwaka, 2015 iliyotungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290), Kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kiliweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki moja (100,000/=) kutokana na makosa yaliyocainishwa. Hata hivyo, adhabu ya kifungu hicho ilikuwa kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 67 cha Sheria Mama (Sura ya 290) ambacho kinazitaka Halmashauri zinapotunga Sheria Ndogo yoyote chini ya Sheria hiyo kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=). Hivyo basi, Kamati ilishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hiyo ili kuondoa dosari iliyobainika.

2.3.3 **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ilitekeleza maoni na ushauri wa Kamati na Halmashauri

husika imefanya marekebisho katika Sheria Ndogo hiyo kwa kuweka faini isiyoziidi shilingi elfu hamsini (50,000) kama inavyotajwa katika Sheria Mama.

- 2.3.4 **Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilibaini kuwa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo za baadhi ya Halmashauri zinatokana na changamoto mbalimbali katika Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo ikiwemo ya Wanasheria kutokuwa na elimu stahiki ya Uandishi wa Sheria kama ilivyoielezwa awali. Kwa sababu hiyo, Kamati iliishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuandaa programu ya mafunzo ya mara kwa mara kwa Wanasheria wa Ofisi hiyo, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo kwa ufanisi zaidi.
- 2.3.5 **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa programu ya mafunzo ya siku tatu (3) kwa Wanasheria wa Tawala za Mikoa na wa Mamlaka za Serikali Mitaa iliyofanyika katika Chuo cha Mipango, Dodoma kati ya tarehe 25 - 27 Januari, 2017 ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo zinazokidhi mataakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kamati iliishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhakikisha kuwa, mafunzo kama hayo yawe endelevu ili kuwajengea uwezo wanasheria hao ili pia wawaelimisha Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri kuhusu nafasi yao katika Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo.
- 2.3.6 **Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Halmashauri zinatunga Sheria Ndogo ambazo zina viwango vya faini vikubwa kuliko vilivyowekwa na Sheria Mama kutokana na hisia kwamba, Sheria za Serikali za Mitaa zilizotungwa na Bunge zinaweka kiwango kidogo cha adhabu ya faini ukilinganisha na ukubwa wa baadhi ya makosa yanayoweza kutendwa na kushughulikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- 2.3.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, hisia hizi kamwe haziwezi kuhalalisha Halmashauri hizo kutunga Sheria Ndogo zinazoweka adhabu kubwa kinyume na masharti yaliyomo katika Sheria Mama. Hivyo basi, Kamati iliishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kufanya marekebisho ya viwango vya faini na adhabu vilivyopitwa na wakati kwa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mama husika, iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.
- 2.3.8 **Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine ni Sheria Ndogo inayoitwa **The Petroleum (Bulk Procurement) Regulations, 2015** Tangazo la Serikali Na. 508 la tarehe 6 Novemba, 2015 iliyotungwa chini ya vifungu vya 168 na 258 vya Sheria ya Petroli (*The Petroleum Act No. 21 of 2015*). Sheria Ndogo hii imetungwa na Waziri wa Nishati na Madini kwa lengo kuanzisha Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja (*Bulk Procurement System*) wa bidhaa za petroli.
- 2.3.9 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hoja nyingine, Kamati ilibaini kuwa Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo hiyo inaweka masharti kwamba, Waziri anaweza kuzuia bidhaa za petroli zinazosafirishwa kwenda nchi za jirani kupitia Tanzania ili zitumike ndani ya nchi katika mazingira ya dharura atakayo yatangaza. Kanuni hiyo inasomeka kama ifuatavyo:-
"15.- (7) Under emergency conditions declared by the Minister, the transit petroleum products may be localized."

- 2.3.10 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti ya Kanuni hiyo yamempa Waziri wa Nishati na Madini mamlaka ambayo, endapo yatatumika isivyopasa, yanaweza kuhatarisha mahusiano ya kibiashara na kisiasa na nchi za jirani. Bila kuathiri masharti ambayo yanapatikana katika Sheria Mama, Kamati ilishauri kwamba Kanuni hiyo irekebishwe kwa kufafanua masharti na maana halisi inayopatikana katika Kifungu cha 253 cha Sheria Mama ili kuendana na dhamira ya Bunge wakati inatunga Sheria hiyo.
- 2.3.11 Aidha, Kamati ilipendekeza kuwa Kanuni hiyo iweke masharti ambapo mwenye leseni ya kusafirisha mafuta hayo pamoja na mpokeaji wa mafuta katika nchi husika watakuwa na haki ya kupewa taarifa kuhusu hatua inayokusudiwa kuchukuliwa na Waziri kuhusiana na bidhaa hiyo. Kamati ilipendekeza kuwa Kanuni hiyo iandikwe kama ifuatavyo:-
"15.- (7) Under emergency conditions provided for under Section 253 of the Act, the Minister may localize transit petroleum products after notice has been given to the licensee and the consignee."
- 2.3.12 **Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Nishati na Madini aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati tarehe 26 Januari, 2017 ambapo pamoja na masuala mengine, alibainisha kuwa Wizara yake imefanya mapitio ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na kupendekeza rasimu mpya ya Kanuni hizo ikiwemo Kanuni ya 15 (7). Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na majibu hayo kwa sababu Wizara haikuonesha jitihada za haraka za kufanya marekebisho yaliyopendekezwa tangu kuibuliwa kwa hoja hiyo katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Februari, 2016 wakati kuna Sheria Ndogo nyingine zilizotungwa na Wizara hiyo Septemba, 2016 na tayari zilikuwa zimefanyiwa marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
- 2.3.13 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua Sheria Ndogo inayoitwa **The Drugs Control And Enforcement (General) Regulations, 2016** Tangazo la Serikali Na. 173 la tarehe 10 Mei, 2016 iliyotungwa chini ya Kifungu cha 67 cha Sheria ya Udhubiti wa Dawa za Kulevya (*The Drugs Control and Enforcement Act, CAP. 95*). Sheria hii iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.
- 2.3.14 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hoja nyingine, Kamati ilibaini kuwa katika Kanuni ya 14 ya Sheria Ndogo hiyo ambayo inaweka masharti ya uratibu wa zoezi la kuharibu dawa za kulevya zilizokamatwa (*destruction of seized drugs*), Kanuni Ndogo ya 14 (1) imewataja watu ambao ni lazima wawepo wakati zoezi hilo linatekelezwa. Watu hao ni wafuatao:-
- a) Jaji au Hakimu
 - b) Mwakilishi wa Kamishna wa Dawa za Kulevya, Inspekta Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi wa Mashitaka, Mkemia Mkuu wa Serikali
 - c) Mwakilishi kutoka Baraza la Mazingira la Taifa na Usalama wa Taifa; na
 - d) Mtu mwingine yeyote ambaye Kamisha wa Madawa ya Kulevya atamteua.
- 2.3.15 Hata hivyo, Kanuni ya 14 (2) ya Sheria Ndogo hiyo inaweka masharti kwamba, Kamishna wa Dawa za Kulevya au Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru madawa ya kulevya yaliyokamatwa yaharibiwe bila kuwashirikisha watu wanaotajwa katika Kanuni ya 14 (1).

- 2.3.16 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti ya Kanuni hii yanakiuka misingi ya uandishi bora wa Sheria kwa kuwa kuna mkinzano wa masharti. Kanuni ya 14 (1) imetumia neno “shall” kuonesha ulazima wa kuwepo kwa watu waliotajwa wakati huo, Kanuni ya 14 (2) inatumia neno “may” kuonesha utashi anaoweza kutumia Kamishna kuamuru kuharibiwa kwa dawa za kulevya bila kuwepo watu waliotajwa katika Kanuni ya 14 (1).
- 2.3.17 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine Kamati iliona kwamba, matakwa ya Kanuni ya 14 (2) yanakinzana na Kanuni ya 14 (3) inayoweka masharti kwamba, wakati wa kuharibu dawa za kulevya, ulinzi wa afya, ulinzi wa mazingira na usalama unazingatiwa. Hivyo basi kukosekana kwa watu waliotajwa katika Kanuni ya 14 (1) kunaweza kuchangia ukiukwaji wa Kanuni ya 14 (3).
- 2.3.18 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kanuni ya 14 (5) na Kanuni ya 14 (7) zinaweka sharti kwa Jaji au Hakimu aliyeshuhudia kuharibiwa kwa madawa yaliyokamatwa kujiridhisha kwamba madawa yote yameharibiwa na hatimaye kujaza fomu ya kuthibitisha hilo. Hivyo basi, kutokuwepo kwa Jaji au Hakimu kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (2) kunaweza kusababisha zoezi hilo kutokamilika kisheria. Kwa kuzingatia dosari hizo zilizobainika, Kamati ilishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya marekebisho katika Kanuni ya 14 ya Sheria Ndogo hiyo ili kuondoa mkanganyiko unaojitokeza.
- 2.3.19 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 20 Januari, 2017, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) aliwasilisha Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambapo, pamoja na masuala mengine, alibainisha kuwa Ofisi yake imefanya marekebisho katika Kanuni tajwa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Marekebisho hayo yatawasilishwa Bungeni baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.
- 2.3.20 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kuchambua Sheria Ndogo mbalimbali zinazohusiana na masuala ya Watoto kutokana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009. Moja kati ya Sheria Ndogo hizo ni Kanuni za Ajira za Watoto za Mwaka 2012 Tangazo la Serikali Na. 168 la tarehe 13 Mei, 2016. Sheria Ndogo hiyo inaweka masharti kuhusu haki ya mtoto kufanya kazi, makatazo na mazingira ambayo mtoto hapaswi kufanya kazi, haki za mtoto anayefanya kazi pamoja na taratibu za ufuatiliaji ustawi wa mtoto ambaye anafanya kazi.
- 2.3.21 **Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini dosari kadhaa katika Sheria Ndogo hiyo na moja kati ya dosari hizo ni kwamba, Kanuni hazijataja Kifungu cha Sheria Mama kinachoipa madaraka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo.
- 2.3.22 Aidha, katika Kanuni ya 3 ambayo inatoa tafsiri, maneno “kazi za hatari” yametafsiriwa kumaanisha “kazi yoyote ambayo inamuweka mtoto katika hatari ya magonjwa ya kimwili au majeraha ya kiakili” wakati Sheria Mama inatoa tafsiri ya maneno “kazi hatarishi” kuwa ni “kazi yoyote inayomuweka mtoto katika hatari ya kupata madhara ya kimwili au kiakili”. Kwa maoni ya Kamati, tafsiri hizi mbili zinazungumzia kitu kinachofanana lakini zinatofautiana kimaudhui na kimantiki.
- 2.3.23 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri kuwa Kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho ili tafsiri inayotumika katika Sheria Mama itumike katika

Sheria Ndogo kwa lengo la kukidhi matakwa ya Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinachosema:-

“39.- (1) Words and expressions used in subsidiary legislation shall have the same respective meaning as in the written law under which the subsidiary legislation is made.”

2.3.24 **Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati ilibaini Kanuni ya 4 ya Sheria Ndogo hiyo inazungumzia umri wa chini wa kuajiriwa kuwa ni miaka kumi na nne (14). Hata hivyo, Kanuni ya 4 (2) inaweka masharti maalum ambapo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne anaweza kuajiriwa. Kamati ilishauri kwamba, Kanuni hiyo iandikwe upya kuondoa maneno “chini ya” ili kuepuka mazingira ambayo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne (14) anaweza kuajiriwa.

2.3.25 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 18 Januari, 2017, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aliwasilisha Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ambapo, pamoja na masuala mengine, alibainisha kuwa Wizara yake imefanya marekebisho katika Kanuni zote ambazo zilibainika kuwa na dosari kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

2.4 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TANO WA BUNGE

2.4.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Kikao cha Bunge cha tarehe 1 Novemba, 2016 Serikali iliwasilisha Mezani Sheria Ndogo mbalimbali kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Sheria Ndogo zilizowasilishwa ni zile zinazopatikana katika matoleo yafuatayo ya Gazeti la Serikali:-

- a) Toleo Na. 16 la Tarehe 15 Aprili, 2016
- b) Toleo Na. 17 la Tarehe 22 Aprili, 2016
- c) Toleo Na. 21 la Tarehe 20 Mei, 2016
- d) Toleo Na. 36 la Tarehe 36 Agosti, 2016
- e) Toleo Na. 37 la Tarehe 02 Septemba, 2016
- f) Toleo Na. 38 la Tarehe 09 Septemba, 2016
- g) Toleo Na. 40 la Tarehe 23 Septemba, 2016
- h) Toleo Na. 41 la Tarehe 30 Septemba, 2016
- i) Toleo Na. 42 la Tarehe 7 Oktoba, 2016
- j) Toleo Na. 43 la Tarehe 14 Oktoba, 2016

2.4.2 **Mheshimiwa Spika**, jumla ya Sheria Ndogo Sabini na Nne (74) zilichambuliwa na Kamati na kati ya hizo, Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari ni Kanuni zilizotungwa na Mawaziri (Rules and Regulations) kama ambavyo inaonekana katika Jedwali la Uchambuzi lililoambatishwa. Kanuni zinazotungwa na Mawaziri hutungwa kwa utaalum na mara nyingi uandishi wake unalenga kufafanua kwa kina masharti yanayotokana na Sheria Mama iliyotungwa na Bunge.

2.4.3 Kwa kuzingatia hilo, uchambuzi uliofanywa ulilenga kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo hizo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi ambapo Kamati ilibaini kuwepo na dosari zifuatazo katika Sheria Ndogo hizo:-

a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi

2.4.4 **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka masharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka

masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka au Sheria nyingine yoyote.¹ Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo (*Regulations*) zinakwenda kinyume na masharti hayo.

- 2.4.5 **Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, Sheria Ndogo inayoitwa **The Engineers Registration (Registration of Independent Consulting Engineers Rules, 2016)** Tangazo la Serikali Na. 265 la 2016 ambayo inaonyesha kuwa imetungwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wahandisi, Sura ya 63 (*The Engineers Registration Act, CAP 63*) lakini wakati huo huo ikitamka kwamba Mamlaka ya kutungwa kwake yametokana na Kanuni ya 40 (*Made Under Regulation 40*). Hata hivyo, ukisoma Kanuni iliyorejewa katika Sheria Ndogo hii inayoitwa *The Engineers Registration Regulations, 2009*, Kanuni ya 40 inazungumzia Usajili na Vigezo wanavyopaswa kuwa navyo Makandarasi Washauri Wakujitegemea na sio Kanuni inayotoa mamlaka ya uanzishaji wa Sheria Ndogo hii.
- 2.4.6 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo ilipaswa kunukuliwa kuwa inatokana na Kifungu cha 34 (i) cha Sheria Mama ambacho ndicho kinachotoa mamlaka ya uanzishwaji wa Kanuni husika. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-
- “34.-(i) With the consent of the Minister the Board may make by-laws for the better carrying, out of its objects and functions, and without prejudice to the generality of the preceding provisions, may make by-laws- prescribing rules for professional practice, conduct and ethics for engineers and consulting firms;”*
- 2.4.7 Aidha, kwa maoni ya Kamati, Kanuni moja haiwezi kutoa mamlaka ya uanzishaji wa Kanuni nyingine isipokuwa ni Sheria Mama tu yenye hayo mamlaka.
- 2.4.8 **Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine ni Sheria Ndogo inayoitwa **The Petroleum (Natural Gas Pricing) Regulations, 2016** Tangazo la Serikali Na. 285 la 2016 iliyotungwa na Waziri wa Nishati na Madini chini ya Kifungu cha 165 na 258 (1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392. Kanuni ya 33 ya Sheria Ndogo hii inaipa mamlaka Mamlaka ya udhibiti wa shughuli za petroli wa Mkondo Juu (PURA) kusimamia na kukagua bei ya gesi asilia katika mkondo wa chini (*down stream*). Mamlaka hayo ni kinyume na mamlaka ya PURA yaliyoainishwa katika Kifungu cha 11, 12 na 13 cha Sheria ya Petroli (Sheria Mama).
- 2.4.9 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kanuni hiyo inakiuka Kifungu cha 7(1)(b)(iv) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*The Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act, CAP 414*) pamoja na Kifungu cha 30, 163, 164 na 165 vya Sheria ya Petroli ambavyo vimeipa EWURA mamlaka ya kusimamia masuala ya bei za gesi asilia. Uwepo wa Kanuni ya 33 kuhusu majukumu ya PURA unakinzana na msingi wa matumizi ya Kanuni hii ambao umeainishwa chini ya Kanuni ya 2 kuhusu bidhaa za gesi asilia katika hatua ya udhibiti wa mkondo wa chini (*downstream*) ambayo kimsingi inatekelezwa na EWURA.
- b) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiuandishi na kiuchapaji**
- 2.4.10 **Mheshimiwa Spika**, makosa ya kiuandishi na kiuchapaji katika Sheria Ndogo yoyote yanaweza kusababisha athari kubwa kwa watumiaji

¹ Sura ya 1 Toleo la 2002

endapo masharti yatakayo andikwa au kuchapishwa yatakuwa si yale yaliyokusudiwa. Pia, dosari hizo zinaweza kusabisha mkanganyiko wa maana endapo Sheria fulani itahitaji kutafsiriwa na vyombo vya utoaji haki.

- 2.4.11 **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Kanuni zilizochambuliwa na Kamati, zilibainika kuwa na dosari za uandishi na uchapaji na hivyo kuwa na uwezekano wa kuathiri utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo endapo marekebisho hayatafanyika. Kwa mfano, katika Sheria Ndogo ya **The Public Service (Tanzania Foreign Service) Regulation, 2016** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Public Service Act (CAP 298)*, imebainika kuwa na makosa ya kiuandishi ambapo Jedwali la Tano la kanuni hizi halina kichwa cha habari kama ambavyo majedwali mengine yamezingatia takwa hilo, hali inayoleta changamoto ya usomaji wa sheria.
- 2.4.12 Aidha, Kamati imebaini dosari ya uandishi ya Kifungu kinachoanzisha Kanuni hii kwani imerejea Kifungu cha 35 (1) ambacho hakipo katika Sheria Mama, badala yake Sheria ilipaswa kurejea Kifungu cha 35A ambacho ndicho kinatoa mamlaka ya uanzishaji wa Sheria Ndogo hii.
- 2.4.13 **Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine ni Sheria Ndogo inayoitwa **Occupational Safety and Health (Vessel Under Pressure) Regulations, 2016** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *Occupational Safety and Health Act (CAP 297)*. Jedwali la pili la Sheria Ndogo hii limeanzishwa chini ya Kanuni ya 12 lakini uandishi wa Kanuni hiyo hauoneshi maneno ya uanzishwaji wa Jedwali hilo. Aidha, Jedwali la Nne na Tano la Sheria Ndogo hii yamebainika kuwa na makosa hayo hayo ya kiuandishi ambayo kimsingi yanaondoa muunganiko (*connectivity*) kati ya Kanuni husika na majedwali hayo hivyo kuleta changamoto ya usomaji hasa wakati wakufanya rejea.

c) Sheria Ndogo kukiuka misingi bora ya uandishi wa Sheria (drafting issues)

- 2.4.14 **Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi Kamati ilibaini kuwepo kwa baadhi ya Sheria Ndogo ambazo zimerejea kwa makosa vifungu vya Sheria Mama nyingine tofauti na vile vilivyopaswa kurejewa. Kwa mfano, Sheria Ndogo ya **The Capital Markets And Securities (Licensing) (Amendment) Regulation, 2016** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Capital Markets And Securities Act* imeandikwa kama Sura ya 70 badala Sura ya 79, kimsingi rejea ya Sura hiyo ya 70 ni Sheria nyingine ya *Medical Stores Department Act*. Kwa kurejea Sura ambayo si sahihi, kunaweza kuhesabika kwamba Kanuni hiyo inakosa Sheria inayotoa mamlaka ya kuanzishwa kwake.
- 2.4.15 **Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine wa Sheria iliyokiuka misingi bora ya uandishi wa Sheria ni **The Mental Health (General) Regulations, 2016** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Mental Health Act, CAP. 98*, ambapo maudhui ya Kanuni ya 20 yanajirudia/yanafanana na yale yanayopatikana katika Kanuni ya 28 ambayo inazungumzia utaratibu wa kufuata endapo mgonjwa wa akili atafariki.
- 2.4.16 **Mheshimiwa Spika**, uwepo wa Kanuni mbili zenye maudhui yanayojirudia (*duplication*) kunaleta changamoto ya kuwa na rejea ya pili isiyokuwa na ulazima wakuwepo.

d) Sheria Ndogo kukiuka misingi ya Haki za Binadamu

- 2.4.17 **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya Haki za Binadamu kwa mujibu wa Katiba na Mikataba ya Kimataifa ambayo imeridhiwa na nchi yetu. Bunge la Jamhuri ya Muungano lina wajibu wa kutunga Sheria ambazo zinazingatia misingi hiyo ili kuhakikisha kuwa, Haki za Binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa. Kila mamlaka ambayo imekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge, nayo inawajibika kuhakikisha kuwa inatunga Sheria Ndogo ambazo zinalinda na kuhifadhi haki hizo.
- 2.4.18 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa misingi ya Haki za Binadamu kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Bunge, Kamati imebaini kuwepo kwa Sheria Ndogo ambazo zina vifungu ambavyo vinaweza kutafsiriwa kuwa vinakiuka misingi ya Haki za Binadamu.
- 2.4.19 **Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi Kamati imebaini kuwepo kwa Sheria Ndogo ambazo zina vifungu ambavyo vinakiuka misingi ya Haki za Binadamu. Kwa mfano, Sheria Ndogo ya **The Mental Health (General) Regulations, 2016** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Mental Health Act, (Sura ya 98)*, katika Kanuni ya 20 ya Kanuni hizi inazungumzia utaratibu pale ambapo mtu mwenye ugonjwa wa akili atafariki akiwa katika kituo cha tiba ya afya ya akili, inatoa jukumu kwa Afisa msimamizi kutoa taarifa kwa Mganga Mkuu, Polisi pamoja na Hakimu aliyekaribu mwenye Mamlaka ya kusikiliza mashauri ya uchunguzi wa vifo.
- 2.4.20 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hii haijaweka sharti la utoaji wa taarifa za kifo kwa ndugu wa marehemu (mtu mwenye ugonjwa wa akili), kwani sharti la kuhusishwa ndugu limezungumzwa katika kanuni kadhaa kama vile kanuni ya 11, ambayo inatoa sharti la kumhusisha Ndugu wa Mgonjwa wa Akili pale anaporuhusiwa kutoka katika matibabu. Aidha, msingi wa kutoa taarifa kwa ndugu unatokana na takwa la Ibara ya 18(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotamka;
*18. Kila mtu,
(d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za Wananchi na pia kuhusu masuala mbalimbali kwa jamii.*
- 2.4.21 Vilevile kwa mujibu wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa (*Access to Information Act No. 6, 2016*) chini ya Kifungu cha 5(1) inatoa haki kwa mwananchi ya kupata Taarifa kutoka kwa mamlaka husika. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo;
5.- (1) Every person shall have the right of access to information which is under the control of the information holders.
- 2.4.22 **Mheshimiwa Spika**, ni vyema uandishi wa Sheria Ndogo ukazingatia misingi ya Haki za Binadamu iliyowekwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za nchi kwa lengo la upatikanaji wa haki za msingi kwa wananchi.
- 2.4.23 **Mheshimiwa Spika**, kuna haja ya uandishi wa Sheria Ndogo zinazohusu maisha ya kijamii kutambua uwepo wa wanajamii pamoja na haki zao katika utekelezaji wa Sheria hizo. Hii ni pamoja na haki ya kupata taarifa stahiki na kwa wakati.

2.5 ZIARA ZA KAZI

- 2.5.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilitembelea Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali tarehe 15 Machi, 2016 ambapo wajumbe walipata fursa ya kujionea maeneo mbalimbali ambayo Sheria Ndogo hupitia

katika hatua za uchapaji pamoja. Aidha Wajumbe walitumia fursa hiyo kutambua changamoto mbalimbali zinazoikabili Ofisi hiyo.

- 2.5.2 **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni muhimu katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa kuwa huchapisha Sheria Ndogo zote nchini na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Idara hii isipotekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hawezi kuwasilisha kwa wakati Sheria Ndogo kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsihi, Sura ya 1.
- 2.5.3 Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, Ofisi hiyo haikuwa ikiendeshwa kwa viwango vinavyokidhi mahitaji yaliyopo ili kuziwezesha Sheria Ndogo kuchapishwa kwa wakati. Dosari hii inatokana na ukweli kwamba, Ofisi hii ilikuwa ikitekeleza majukumu yake kwa vitendea kazi duni ukilinganisha na maendeleo ya teknolojia ya sasa na pia maslahi hafifu kwa watumishi ukilinganisha na ukubwa wa kazi zao. Kamati ilishauri kufanyika kwa maboresho ili kuondokana na changamoto hizo.
- 2.5.4 **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, tarehe 20 Januari, 2017 Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri (SBAU) aliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambapo pamoja na masuala mengine, alikiri kuwepo kwa mapungufu ya utendaji kazi katika Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Waziri wa Nchi aliieleza Kamati kuwa Ofisi yake imekusudia kuboresha utendaji wa Idara katika uendeshaji, kuwa na Mpango wa Biashara (*Business Plan*), kununua mitambo ya kisasa na kuboresha maslahi ya watumishi.

2.6 MIKUTANO NA WADAU WA MAZAO

- 2.6.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na wadau wa mazao mbalimbali katika jitihada za kuanza kuzishughulikia Sheria Ndogo zinazowagusa ili waweze kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo, changamoto wanazokabiliana nazo katika uzalishaji na uuzaji wa mazao hayo. Uamuzi huo wa wa Kamati ulilenga kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli katika kupunguza au kuondoa kero kwa wakulima wa mazao mbalimbali zitokanazo na tozo mbalimbali zinazowekwa na Sheria Ndogo tofauti. Katika kusikiliza maoni ya wadau hao, Kamati ilibaini kuwepo kwa mlolongo wa kodi, ada na tozo katika mazao mbalimbali ambao ni mzigo mkubwa kwa mkulima na hivyo kuathiri uzalishaji na kipato chake.
- 2.6.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, kodi, ada na tozo ambazo zinazungumziwa zinatokana na Sheria Ndogo mbalimbali zikiwemo Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) pamoja na Sheria Ndogo za zinazotungwa na Mawaziri na Mamlaka nyingine (*Regulations*) katika mazao tofauti. Kamati itaendelea kuzifanyia mapitio Sheria Ndogo hizo kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa madhumuni ya kupata njia bora ya kupunguza kero hizo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

3.1.1 Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo yaliyokasimiwa kwa Mawaziri na vyombo vingine vya Serikali kwa Sheria zilizotungwa na Bunge, si mamlaka Kamili (it is only delegated). Muda wowote Bunge linaweza kufanya mabadiliko ya Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge litaona ulazima wa kuifanyia marekebisho kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri Mawaziri na vyombo vyote vilivyokasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo ambazo Kamati imebaini kuwa na dosari wazifanye marekebisho yaliyopendekezwa haraka na kuyatangaza katika Gazeti la Serikali kabla ya Mkutano wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanatokana na Kamati kubaini kuwa majibu ambayo baadhi ya Mawaziri wamekuwa wakiwasilisha mbele ya Kamati, yamejaa ahadi za utekelezaji unaochukua muda mrefu wakati Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari bado zinaendelea kutumika na baadhi kuwa na madhara makubwa kwa wananchi kiuchumi na katika haki zao za msingi.

3.1.2 Uandishi wa Sheria Ndogo (*Drafting*)

KWA KUWA, imebainika kuwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno (*copying and pasting*) bila kufanya marekebisho ya msingi,

NA KWA KUWA, hali hiyo husababisha kunakili dosari za Sheria Ndogo hizo na wakati mwingine kutoendana na mazingira na mahitaji ya Mamlaka inayotunga Sheria Ndogo hiyo,

KWA HIYO BASI, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziachane na mtindo wa kunakili Sheria Ndogo kutoka katika Mamlaka nyingine na zitunge Sheria Ndogo kulingana na mazingira halisi ya mamlaka husika.

3.1.3 Makosa ya Kiuchapaji (*Typography*)

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na makosa mengi ya kiuchapaji na kiuchapaji, na baadhi kufanya rejea za vifungu katika majedwali kimakosa, zilikosewa kiasi cha

NA KWA KUWA, makosa hayo yanasabisha tafsiri ya masharti ya Sheria Ndogo hizo kuleta mkanganyiko au kupoteza maana iliyokusudiwa,

NA KWA KUWA, baadhi ya dosari zilizobainika zimetokana na kukosekana kwa Wanasheria wa kutosha na wenye taaluma ya uandishi wa sheria katika Ofisi hizo,

KWA HIYO BASI,

- a) Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Bungeni tangu Mkutano wa Pili hadi sasa ambazo zimebainika kuwa na makosa ya kiuchapaji na kiuchapaji ili kuondoa dosari hizo.
- b) Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuandaa program endelevu ya mafunzo kwa Wanasheria wa Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo ambazo

zinakidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

3.1.4 Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo

- a) **KWA KUWA**, ilibainika kwamba wakati wa mchakato wa utungaji wa baadhi ya Sheria Ndogo haukushirikisha wadau kikamilifu,

NA KWA KUWA, kutoshirikisha wadau kunaleta changamoto ya utekelezaji wa Sheria Ndogo husika miongoni mwa makundi husika yanayoguswa na Sheria hizo,

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote.

- b) **KWA KUWA**, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilikusudia, miongoni mwa mambo mengine, kuweka mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo katika hatua mbalimbali (*The By-Laws Database*),

NA KWA KUWA, uwepo wa mfumo huo ulilenga kurahisisha uhakiki wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuwa na Sheria zinazokidhi vigezo vinavyotakiwa kabla ya hatua ya uchapishwaji katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika,

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ianze kutumia mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa upitishaji wa Sheria Ndogo katika hatua mbalimbali (*The By – Laws Database*).

3.1.5 Marekebisho ya Mara kwa Mara ya Sheria Ndogo

Kamati inashauri Serikali na vyombo vyake kuchukua hatua za haraka katika kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari na ambazo zinalalamikiwa kuwa zinawakandamiza wananchi. Baada ya marekebisho hayo kufanyika, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria ili Kamati yangu ipate fursa ya kuzifanyia uchambuzi. Hatua hii itaiwezesha Serikali kulifanyia kazi tamko la Waziri Mkuu kuhusu kupunguza kodi, tozo na aa katika mazao mbalimbali; kupunguza kodi, tozo na ada zinazohusiana na masuala ya maliasili na utalii kama vile tozo za kitanda na Sheria Ndogo nyingine yoyote ambayo itaonekana ni kero kwa wananchi.

3.1.6 Uwasilishaji wa Sheria Ndogo Bungeni

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Kamati inaendelea kusesitiza na kuishauri Serikali kuhakikisha inawasilisha kwa wakati katika kila Mkutano wa Bunge, Sheria Ndogo zote zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita. Hatua hii italiwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikamilifu laini pia litaepusha mgogoro wa kiutendaji wa Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge linaweza kuazimia isitumike kwa kutowasilishwa Bungeni kwa wakati.

3.2 MAONI NA MAPENDEKEZO KWA SERIKALI KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TANO

- 3.2.1 **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yameandaliwa kwa muhtsari kuzingatia matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano wa Bunge na

yamefafanuliwa kwa kirefu katika Jedwali la uchambuzi ambalo limeambatishwa na Taarifa hii. Jedwali hilo limeanisha mapendekezo mahsusi kwa kila Sheria iliyobainika kuwa na dosari kama inavyoonekana kwenye kiambatisho hicho.

3.2.2 **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

a) Sheria Ndogo Zinazokiuka Matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

KWA KUWA, zipo Sheria Ndogo zinazokiuka masharti na matakwa ya Sheria Mama, Kwa mfano, *The Capital Market and Securities (Licensing (Amendments) Regulation, 2016*, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1,

NA KWA KUWA, Sheria Ndogo zinazokinzana na Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 zinahesabika kuwa ni batili (*void to the extent of inconsistency*);

KWA HIYO BASI, Sheria Ndogo zilizo orodheshwa katika Taarifa ya Kamati pamoja na Jedwali lililoambatishwa zirekebishwe na kisha ziwasilishwe Bungeni kupitia Gazeti la Serikali.

b) Pendekezo Kuhusu Dosari za Uandishi wa Sheria

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano Tano wa Bunge na kuchambuliwa na Kamati zimebainika kuwa na dosari za uandishi na uchapaji (*drafting errors*),

NA KWA KUWA, makosa hayo yanasababisha kupotea kwa maana iliyokusudiwa na Sheria Ndogo husika na kuweza kuathiri mantiki ya Sheria Mama inayokasimu utungwaji wa Sheria Ndogo hiyo,

KWA HIYO BASI, Sheria Ndogo zilizoainishwa katika Taarifa ya Kamati pamoja na Jedwali lililoambatishwa zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za uandishi kisha ziwasilishwe Bungeni kupitia Gazeti la Serikali.

c) Pendekezo Kuhusu Sheria Ndogo Zinazokiuka Misingi ya Haki za Binadamu

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano Tano wa Bunge na kuchambuliwa na Kamati zimebainika kuwa Kukiuka Misingi ya Haki za Binadamu,

NA KWA KUWA, dosari hizo zinasababisha ukiukwaji wa Misingi ya Katiba ya Nchi kwa kupokonya haki za msingi za wananchi,

KWA HIYO BASI, Sheria Ndogo zilizoainishwa katika Taarifa ya Kamati pamoja na Jedwali lililoambatishwa zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za ukiukwaji wa Misingi ya Haki za Binadamu kisha ziwasilishwe Bungeni kupitia Gazeti la Serikali.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 SHUKRANI

4.1.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa

taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana.

4.1.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano Tatu, Mkutano wa Nne na Mkutano wa Tano wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Andrew John Chenge (Mb)
2. Mhe. William Mganga Ngeleja (Mb)
3. Mhe. Abdallah Ally Mtolea (Mb)
4. Mhe. Halima James Mdee (Mb)
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka (Mb)
6. Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)
7. Mhe. Aida Joseph Khenani (Mb)
8. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)
9. Mhe. Esther Michael Mmasi (Mb)
10. Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb)
11. Mhe. Hassani Seleman Kaunje (Mb)
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis (Mb)
13. Mhe. Khamis Mtumwa Ali (Mb)
14. Mhe. Hassan Elias Massala (Mb)
15. Mhe. Leonidas Tutubert Gama (Mb)
16. Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)
17. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga (Mb)
18. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma (Mb)
19. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)
20. Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu (Mb)

4.1.3 **Mheshimiwa Spika**, Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Jenista J. Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. George Boniface Simbachawane (Mb)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)
2. Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb)
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
3. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo (Mb)
Waziri wa Nishati na Madini
4. Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb)
Waziri wa Katiba na Sheria
5. Mhe. Umy Ally Mwalimu (Mb)
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
6. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb)
Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

7. Mhe. Charles John Paul Mwijage (Mb)
Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji
 8. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb)
Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi
 9. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb)
Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee
 10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemami (Mb)
Naibu Waziri wa Nishati na Madini
 11. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb)
Naibu Waziri wa Fedha na Mipango
 12. Mhe. Mhandisi Edwin Amandus Ngonyani (Mb)
Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
- 4.1.4 Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali. Vilevile niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao na wale wote ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi (*submissions*). Ushiriki wao katika vikao vya Kamati pamoja na maoni waliyowasilisha yamekuwa na manufaa kwa Kamati katika utekelezaji bora wa shughuli zake.
- 4.1.5 **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.
- 4.1.6 **Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 HOJA

- 4.2.1 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hii.
- 4.2.2 **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge (Mb)

MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo

Februari, 2017

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea napenda tutambue uwepo wa wageni wa *Korogwe Girls* ambao wamekuja na walimu wao kumi. Karibuni sana wasichana wetu ambao ni akina mama wa baadae ili muweze kujifunza yanayoendelea hapa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa utunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

MHE. KAPT. (MST). GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE : Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kwamba endapo sitamaliza kusoma yote taarifa hii iingie rasmi katika *Hansard* kwamba ndiyo taarifa kamili ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi wote afya na uzima. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kuniamini na kunichagua kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na kwa ushirikiano wanaonipatia. Aidha, napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la uchaguzi la Newala Mjini kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano na msaada wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Majukumu hayo yalitekelezwa kuanzia kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017. Masharti ya Kanuni hii yanataka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge iwasilishe Bungeni taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli zake ili ziadiliwe na Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imeundwa chini ya Kanuni ya Bunge ikisomwa pamoja na fasili ya 1(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa fasili ya 4 (1) ya Nyongeza ya Nane, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika; na

(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Kamati haijaanza kutekeleza majukumu yake Wajumbe wa Kamati walipatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Mafunzo hayo yalikuwa na manufaa kwa Wajumbe kwa kuwa ilikuwa ni mwanzo wa Bunge jipya la Kumi na Moja, ambapo Wajumbe wengi wa Kamati walikuwa ni wapya. Mafunzo yalifanyika mwezi Januari na Februari Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitokeleza majukumu ya kikanuni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016.

Pili, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa dhidi ya Mheshimiwa Saeed Kubenea kuhusu kusema uongo Bungeni.

Tatu, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Hamad Masauni, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi dhidi ya Mheshimiwa Susan Lyimo kuhusu kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi dhidi ya Mheshimiwa Anatropia Theonest kuhusu kusema uongo Bungeni.

Tano, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu dhidi ya Mheshimiwa James Kinyasi Millya kuhusu kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya kusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani lililowasilishwa na Mheshimiwa James Millya.

Saba, kusikiliza shauri la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kuhusu kitendo cha kutoa ishara ya matusi Bungeni na nane, kutoa tafsiri kwa Spika kuhusu adhabu zitolewazwo kwa Waheshimiwa Wabunge waliosimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa mashauri yaliyoshughulikiwa na Kamati. Baada ya kuorodhesha shughuli zilizofanywa na Kamati, ni vema sasa kutoaufafanuzi wa shughuli hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016. Shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016 lilikuwa na makosa matatu ambayo ni:-

1. Kusimama na kuomba mwongozo kuhusiana na jambo ambalo limekwishatolewa uamuzi;
2. Kusimama na kuzungumza bila utaratibu; na
3. Kudharau mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shauri hili lililwahusu Waheshimiwa Wabunge tumewaorodhesha pale. Walikuwa Wabunge saba, nitawasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kusikiliza shauri hili iliwakuta na hatia Waheshimiwa Wabunge waliohusika. Wabunge waliokutwa na hatia kwa makosa yote ni Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Tundu Lissu na kupendekeza kuwa wasihudhurie vikao vya Mkutano wa Tatu vilivyokuwa vimebaki na vikao vyote vya Mkutano wa Nne.

Aidha, Kamati ilipendekeza kuwa Wabunge waliotiwa hatiani kwa baadhi ya makosa katika hayo matatu ambao ni Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Halima James Mdee wasihudhurie vikao vilivyokuwa vimebaki vya Mkutano wa Tatu. Vile vile Kamati ilipendekeza Mheshimiwa John Heche asihudhurie vikao kumi vya Mkutano wa Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya adhabu hizi yalizingatia namna kila Mbunge alivyoshiriki katika tukio hilo la uvunjifu wa Kanuni. Mapendekezo hayo yaliridhiwa na kuazimiwa na Bunge lako tukufu tarehe 30 Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusikiliza na kutoa mapendekezo kuhusu malalamiko ya Mheshimiwa Hussein Mwinyi. Katika Shauri hili Mheshimiwa Hussein Mwinyi alimlalamikia Mheshimiwa Saed Kubenea kwa kusema uongo dhidi ya Jeshi la Wananchi kuwa limeingia mkataba na kampuni ya *Henan Guiji Industry Investment Co. Ltd.* wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi. Mheshimiwa Kubenea alieleza kuwa Jeshi la Wananchi lilikabidhi kampuni hiyo eneo lake lililopo Kitalu Namba 1255 Masaki jijini Dar es salaam na ujenzi ukikamilika kampuni hiyo itaendesha eneo hilo kwa muda wa miaka 40 na baada ya hapo eneo litarudishwa Jeshini.

Aidha, aliongeza kuwa katika mkataba huo, kilikuwepo kipengele kwamba Mheshimiwa Waziri angejengewa nyumba katika Kitalu Namba 2435/5 eneo la Sea View Upanga Jijini Dar es Salaam. Baada ya kulifanyia kazi shauri hili Kamati ilibaini kuwa kauli za Mheshimiwa Kubenea hazikuwa na ukweli wowote. Hivyo Kamati ilipendekeza kuwa Mheshimiwa Kubenea achukuliwe

hatua kwa mujibu wa Kanuni. Spika alikubaliana na ushauri wa Kamati na Mheshimiwa Kubenea alisimamishwa kuhudhuria Vikao vitano vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Hamad Masauni. Katika shauri hili Mheshimiwa Hamad Masauni, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alimlalamikia Mheshimiwa Susan Lyimo kwa kauli aliyoitoa wakati akichangia hotuba ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii kwa kudai kuwa Serikali imenunua na kuingiza nchini magari ya washawasha 777 badala ya kununua CT-Scanner na MRI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililifanyia kazi shauri hili na kubaini kuwa maneno aliyoyasema Mheshimiwa Susan Lyimo hayakuwa na ukweli. Kamati ilipendekeza Mheshimiwa Susan Lyimo asimamishwe kuhudhuria Vikao vitano vya Bunge lililokuwa linaendelea na mapendekezo hayo yaliridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne. Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa William Lukuvi. Katika shauri hili Mheshimiwa Anatropia Theonest alilalamikiwa na Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu kauli aliyoitoa Bungeni kwamba Mheshimiwa William Lukuvi mnamo mwaka 2011 akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alihusika na uporaji wa viwanja vya waathirika wa mabondeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati inafanya uchunguzi wake, Mheshimiwa Anatropia bila kupoteza muda wa Kamati, alikiri mbele ya Kamati kuwa kauli yake haikuwa na ukweli. Katika mazingira hayo Kamati ilipendekeza Mheshimiwa Anatropia asimamishwe kuhudhuria vikao vitatu vya Bunge katika Mkutano uliokuwa unaendelea. Ushauri na mapendekezo haya yalikubaliwa. Kamati ilimpongeza na inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Anatropia Theonest kwa ushirikiano alioitoa kwa Kamati kwa kusema ukweli bila kupoteza muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Jenista Mhagama. Katika shauri hili Mheshimiwa James Millya wakati akichangia mjadala wa hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini alimtaja Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu kuwa ni shemeji wa mmoja wa mbia wa kampuni ya *Sky Associate* inayomiliki Mgodini wa *Tanzanite One*. Kampuni hiyo ilikuwa inadaiwa kunyanyasa wananchi wa Mererani Mkoani Arusha. Maelezo hayo yalilalamikiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kuwa ni ya uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichunguza malalamiko haya na kubaini kuwa kauli ya Mheshimiwa Millya haikuwa na ukweli na ilikiuka Kanuni ya Bunge, tumeitaja hapo. Hivyo Kamati ilipendekeza Mheshimiwa Millya asimamishwe kuhudhuria vikao vitano vya Bunge lililokuwa linaendelea. Mheshimiwa Spika alikubali mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la kusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani lililowasilishwa na Mhe James Millya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea kusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani. Kusudio hilo liliwasilishwa na Mheshimiwa James Millya ambaye katika kujenga hoja yake aliainisha sababu tano ambayo tumeorodhesha; kwamba Naibu Spika ameweka maslahi ya chama chake cha siasa mbele kuliko maslahi ya Bunge; kwamba Naibu Spika alitumia vibaya madaraka kwa kutothamini heshima wanayostahili wanawake wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Mheshimiwa Naibu Spika alimdhaliisha Mheshimiwa Selemani Bungala (Bwege) kwa kumuita Mheshimiwa Bwege aache ubwege.

Sita, kwamba Naibu Spika alivunja Katiba kwa kumzuia Mheshimiwa Joshua Nassari kutekeleza jukumu la kuishauri Serikali pale ambapo alikataa hoja ya Mheshimiwa Joshua Nassari ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura kuhusu kufukuzwa kwa wanafunzi wa diploma maalum wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Naibu Spika alitisha kikao cha Kamati ya Kanuni tarehe 26 Mei, 2016 ambacho kilibadili hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililifanyia kazi suala hili na kubaini, pamoja na mambo mengine kuwa orodha ya majina ya Wabunge iliyoambatanishwa kwamba ndiyo waleta hoja ya kumuondoa Naibu Spika madarakani, kwamba walikuwa wanaunga mkono hoja hiyo orodha hiyo haikuwa sahihi, ilikuwa fake. Orodha ya iliyoambatanishwa ilikuwa ni majina ya Wabunge wa UKAWA waliohudhuria kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 31 Mei, 2016. Kwa hiyo, zoezi la kuwaomba Wabunge wa kuunga mkono hoja halikufanyika.

Aidha, tarehe ya kusudio la kumwondoa Naibu Spika madarakani na tarehe ya mahudhurio ya kikao cha UKAWA zilitofautiana kwani orodha ya mahudhurio ni tarehe 31 Mei, 2016 na kusudio liliandaliwa tarehe 1 Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kubaini hayo ilijielekeza katika Kanuni ya 138(2) ambayo inaeleza utaratibu wa kumwondoa Naibu Spika maradakani. Sehemu ya Kanuni inaeleza ifuatavyo na ninanukuu; *"Endapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaridhika kuwa zipo tuhuma mahususi dhidi ya Naibu Spika zinazohusu uvunjaji wa Katiba, sheria au kanuni zinazoongoza shughuli za Bunge, basi Kamati hiyo itaidhinisha kuwa hoja hiyo ipelekwe Bungeni ili iamuliwe."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo hapo juu na ushahidi ulioletwa kama ilivyoelezwa hapo juu na kwa mujibu wa Kanuni hii, Kamati haikuridhika na ushahidi ulioletwa kuthibitisha hoja hiyo, hivyo, Kamati haikuridhia hoja hiyo na ndiyo maana haikuletwa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusikiliza na kutoa mapendekezo kuhusu shauri la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kuhusu kitendo cha kutoa ishara ya matusi Bungeni. Katika shauri hili Mheshimiwa Mbilinyi ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo alidaiwa kuwa tarehe 6 Juni, 2016 baada ya kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni, wakati akitoka nje ya Ukumbi wa Bunge alionesha ishara ya matusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati baada ya kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizi ilibaini kuwa kweli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alitenda kosa na pia Mheshimiwa Mbunge huyo alikiri mbele ya Kamati kufanya kosa hilo.

Kwa mazingira hayo Kamati ilimtia hatiani na kupendekeza asimamishwe kuhudhuria vikao kumi vya Mikutano ya Bunge na pendekezo hilo liliridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, Kamati kutakiwa kutoa tafsiri kuhusu Kanuni ya 75 kwa kuzingatia adhabu walizokuwa wamepewa baadhi ya Wabunge waliofanya fujo. Baada ya Kamati kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukulia kwa baadhi ya Wabunge waliokutwa na hatia ya kufanya vurugu siku tajwa hapo juu na Bunge kuazimia kulingana na mapendekezo ya Kamati, suala la matumizi ya Kanuni ya 75 sasa lilijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitoa tafsiri hiyo kwa Bunge kuwa, Kanuni ya 75 inahusu Mbunge aliyesimamishwa kwa mujibu wa Kanuni kutoka katika Bunge na kutoingia sehemu yoyote ya Ukumbi wa Bunge na maeneo mengine ya Bunge kwa muda wote atakaokuwa amesimamishwa. Aidha, Kanuni hiyo inaeleza kuwa Mbunge aliyesimamishwa atalipwa nusu mshahara na nusu posho zinazoambatana na mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa. Shauri linalowahusu Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Joshua Nassari. Katika shauri hili Mheshimiwa hawa walituhumiwa kudharau mamlaka ya Spika kwa kufanya fujo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Usikilizaji wa shauri hili haukukamilika kutokana na Mheshimiwa hawa kuwa na udhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Joshua Nassari alitoa taarifa kuwa alikuwa kwenye mitihani ya shahada ya pili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mheshimiwa Ester Bulaya alitoa taarifa kuwa anasafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

Kamati iliridhia maombi yao na kuamua kuwa shauri hili litasikilizwa wakati mwingine. Aidha, baadaye Mheshimiwa Ester Bulaya, alitwa na kufika mbele ya Kamati ambapo kabla shauri lake halijaanza kusikilizwa, Kamati iliahirisha usikilizwaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati kukutana na Kamati za Maadili za Bunge la Kenya na Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawakilishi. Kamati ilitekeleza jukumu la kukutana na Kamati ya Maadili kutoka Bunge la Kenya na Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawakilishi - Zanzibar zilizotembelea Bunge letu baada ya kupewa maelekezo na Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na wajumbe hao kutoka Kenya tarehe 14 Septemba, 2016 na waliotoka Baraza la Wawakilishi - Zanzibar siku ya tarehe 2 Februari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao hivyo, tuliweza kubadilishana uzoefu katika masuala na mbinu mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Ni maoni ya Kamati kuwa ziara kama hizi ni muhimu hata kwa upande wetu kwa kuwa zinawezesha kujua mambo mapya na tumeweza kubadilishana uzoefu, na hapa niseme tu kwamba hata wale wenzetu wa Kenya walitumbua wana tatizo wanapokwenda kwenye tatizo, wanapokwenda kwenye Kamati ya Maadili Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ni Spika na anayepeleka mashtaka kwenye Kamati ya Maadili ni Spika, hoja ikawa unakuwaje wewe mtoa mashtaka na wewe ndiyo jaji, wakasema kwamba utaratibu wa kwetu ni mzuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia masuala haya, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ukwepaji wa kupokea hati za wito. Baadhi ya mashahidi walioitwa mbele ya Kamati walikwepa kupokea hati ya wito (*summons*) hivyo, kuchelewesha shughuli za Kamati. Katika mazingira haya Kamati lililazimika kutumia Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Kanuni zetu tumetaja pale kifungu kinachoruhusu kwamba ukiiwa kama hukuja utaletwa kwa msaada wa polisi. (Makofi)

Aidha, katika kukwepa kupokea hati za wito baadhi ya mashahidi walitoa sababu mbalimbali za uongo kwa lengo la kukwepa kufika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa mafunzo kwa Kamati. Pamoja na kwamba Kamati ilipatiwa mafunzo mara baada ya kuundwa kwake yaliyoiwesha kufanya kazi hii, ni maoni ya Kamati kuwa bado mafunzo zaidi yanahitajika hususan mafunzo kupitia uzoefu wa Mabunge mengine duniani ili Kamati hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi bila kumuonea mtu wala uoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuandaa uamuzi mbadala. Tatizo lingine katika lililojitokeza katika kushughulikia shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo siku ya tarehe 27 Januari, 2016 ilijitokeza changamoto ya kuwa na maamuzi ya Kamati yanayotofautiana na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Kambi ya Upinzani waliandaa maoni mbadala (*dissenting opinion*). Hata hivyo Spika alikataa maoni hayo kupokelewa kwa kuwa jambo hili halitambuliwi Kikanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa muda; kazi ya kushughulikia masuala yanayoletwa na Spika hufanyika kipindi cha Bunge ambapo shughuli nyingine za Bunge huwa zinaendelea. Kwa mantiki hiyo, Wajumbe wa Kamati hupaswa kutekeleza majukumu mengine ya Kibunge kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika mazingira haya Wajumbe wa Kamati hulazimika kutumia muda wa mapumziko na siku za mapumziko ili kukamilisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Kamati; katika kushughulikia makosa ya ukiukwaji wa Kanuni uliofanywa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni maoni ya Kamati kuwa kwa kiasi kikubwa humu ndani nidhamu, ustahimilivu, heshima, utulivu na uzingatiaji wa Kanuni za Majadiliano Bungeni umeanza kuimarika kuliko ilivyokuwa wakati Bunge hili linaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Kamati iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuondokana na changamoto zilizotajwa, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Wajumbe wa Kamati wapewe mafunzo zaidi na ya mara kwa mara kuhusu wajibu wao katika Kamati na umuhimu wa kutanguliza maslahi ya Taifa katika kutekeleza wajibu wao. Ndani ya Kamati yetu tunaambiana wakati wote, tuweke pembeni maslahi ya Vyama vyetu tutangulize maslahi ya Taifa.

(ii) Wabunge wote wa Bunge hili wapewe mafunzo kuhusu Haki, Kinga na Maadili pamoja na ufafanuzi wa majukumu ya Kamati hii ili waweze kutoa ushirikiano kwa Kamati, sisi Kamati tumepata mafunzo juu ya sheria na kadhalika. Lakini siyo Wabunge wengine wengi hamjapata mafunzo tuliyopata, tunaamini kwamba tukipata mafunzo wote yanayofanana tutakwenda vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa.

(iii) Kamati ipewe muda wa kutosha kushughulikia mashauri yanayoletwa na Spika na kuyakamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa niaba ya Kamati. Napenda nitumie fursa hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vema shughuli za Bunge na kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati yangu ulioiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Almas Maige, Makamu mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kushughulikia mashauri yaliyoletwa na Mheshimiwa Spika, na kwa heshima kwa kutopoteza muda tumeorodhesha majina ya Wajumbe wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ninawashukuru sana.

Napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashiillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndugu Pius Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Matamus Fungo, Ndugu Mariam Mbaruku na Ndugu Seraphine Tamba - Makatibu wa Kamati pamoja na Ndugu Editruda Kilapilo Msaidizi wa Kamati na Ndugu Lweli Lupondo, mtalaamu wa *Hansard* kwa kuratibu vema kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi na utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na mapendekezo yaliyoletwa katika taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA KIPINDI CHA KUENZIA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017, KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya na uzima. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kuniamini na kunichagua kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na kwa ushirikiano wanaonipatia. Aidha, napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la uchaguzi la Newala Mjini kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano na msaada wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kibunge kwa ufanisi.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Majukumu hayo yalitekelezwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi mwezi Januari 2017. Masharti ya Kanuni hii yanataka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge iwasilishe Bungeni taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli zake ili zijadiliwe na Bunge lako tukufu katika Mkutano wa Mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imeundwa chini ya Kanuni ya 118 (1) & (2) ikisomwa pamoja na fasili ya 1(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa mujibu wa fasili ya 4 (1) ya Nyongeza ya Nane, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;

(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.

1.4 **Mheshimiwa Spika**, kabla Kamati haijaanza kutekeleza majukumu yake Wajumbe wa Kamati walipatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Mafunzo hayo yalikuwa na manufaa kwa wajumbe kwa kuwa ilikuwa ni mwanzo wa Bunge jipya la Kumi na Moja, ambapo Wajumbe wengi wa Kamati walikuwa ni wapya. Mafunzo yalifanyika mwezi Januari na Februari 2016 jijini Dar es salaam.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitekeleza majukumu ya kikanuni kama ifuatavyo:-

2.1 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016;

2.2 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Hussein Mwinyi (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa dhidi ya Mhe. Saeed Kubenea (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni;

2.3 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Hamad Masauni (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi dhidi ya Mhe. Suzan Lyimo (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni;

2.4 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. William Lukuvi (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi dhidi ya Mhe. Anatropia Theonest (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni;

2.5 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu dhidi ya Mhe. James Kinyasi Millya (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni;

2.6 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya kusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani lililowasilishwa na Mhe James Millya (Mb).

2.7 Kusikiliza shauri la Mhe. Joseph Mbilinyi (Mb) kuhusu kitendo cha kutoa ishara ya matusi Bungeni.

2.8 Kutoa tafsiri kwa Spika kuhusu adhabu zilizotolewa kwa waheshimiwa Wabunge kwa kusimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge.

3.0 UFAFANUZI WA MASHAURI YALIYOSHUGHULIKIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuorodhesha shughuli zilizofanywa na Kamati, ni vema sasa kutoaufafanuzi wa shughuli hizo kama ifuatavyo:-

3.1 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Shauri la baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni siku ya tarehe 27 Januari, 2016 lilikuwa na makosa matatu ambayo ni:-

1. *Kusimama na kuomba mwongozo kuhusiana na jambo ambalo limekwishatolewa uamuzi kinyume na Kanuni ya 72(1) na 68 (10) ya Kanuni za kudumu za Bunge.*
2. *Kusimama na kuzungumza bila utaratibu kinyume na Kanuni ya 60(2)(12) ya Kanuni za Kudumu za Bunge jambo ambalo lilileta fujo na kuvuruga shughuli za Bunge.*
3. *Kudharau mamlaka ya Spika na kudharau shughuli za Bunge kinyume na Kifungu cha 24 (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge Sura 296 na Kanuni ya 74 (1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.*

Mheshimiwa Spika, Shauri hilililiwahusu waheshimiwa Wabunge wafuatao :-

- (i) Mhe. Tundu Lissu (Mb)
- (ii) Mhe. Ester Bulaya (Mb)
- (iii) Mhe. Godbless Lema (Mb)
- (iv) Mhe. Pauline Gekul (Mb)
- (v) Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe (Mb)
- (vi) Mhe. John Heche (Mb) na
- (vii) Mhe. Halima J. Mdee (Mb)

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kusikiliza shauri hili iliwakuta na hatia Waheshimiwa Wabunge waliohusika. Wabunge waliokutwa na hatia kwa makosa yote ni Mhe. Ester Bulaya na Mhe. Tundu Lissu na kupendekeza kuwa wasihudhurie vikao vya Mkutano wa Tatu vilivyokuwa vimebaki na vikao vyote vya Mkutano wa Nne.

Aidha, Kamati ilipendekeza kuwa Wabunge waliotiwa hatiani kwa baadhi ya makosa ambao ni Mheshimiwa Pauline Gekul (Mb), Mhe. Godbless Lema (Mb), Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe (Mb) na Mhe. Halima James Mdee (Mb) wasihudhurie vikao vilivyokuwa vimebaki vya Mkutano wa Tatu. Vilevile Kamati ilipendekeza Mhe. John Heche (Mb) asihudhurie vikao kumi vya Mkutano wa Tatu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya adhabu hizi yalizingatia namna kila Mbunge alivyoshiriki katika tukio hilo la uvunjwaji wa Kanuni. Mapendekezo hayo yaliridhiwa na kuazimiwa na Bunge lako tukufu mnamo tarehe 30 Mei, 2016.

3.2 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo kuhusu malalamiko ya Mhe. Hussein Mwinyi (Mb) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa dhidi ya Mhe. Saeed Kubenea (Mb) kuwa alisema uongo Bungeni;**

Mheshimiwa Spika, Katika Shauri hili Mhe Hussein Mwinyi (Mb) alimlalamikia Mhe. Saeed Kubenea (Mb) kwa kusema uongo dhidi ya Jeshi la Wananchi kuwa limeingia mkataba na kampuni ya *Henan Guiji Industry Investment Co. Ltd* wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi. Mhe Saeed Kubenea (Mb) alieleza kuwa Jeshi la Wananchi lilikabidhi kampuni hiyo eneo lake lililopo Kitalu namba 1255 Masaki jijini Dar es salaam na ujenzi ukikamilika kampuni hiyo itaendesha eneo hilo kwa muda wa miaka 40 na baada ya hapo eneo litarudishwa jeshini.

Aidha, aliongeza kuwa katika mkataba huo, kilikuwepo kipengele kwamba Mhe. Waziri atajengewa nyumba katika Kitalu Namba 2435/5 eneo la Sea View Upanga Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulifanyia kazi shauri hili Kamati ilibaini kuwa kauli za Mhe. Kubenea hazikuwa na ukweli wowote. Hivyo Kamati ilipendekeza kuwa Mhe. Kubenea achukuliwe hatua kwa mujibu wa Kanuni. Spika alikubaliana na ushauri wa Kamati na Mhe. Kubenea alisimamishwa kuhudhuria vikao vitano vya Bunge.

3.3 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Hamad Masauni (Mb) Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi dhidi ya Mhe. Suzan A. Lyimo (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni**

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili Mhe. Hamad Masauni (Mb) Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alimlalamikia Mhe. Suzan Lyimo (Mb) kwa kauli aliyotoa wakati akichangia hotuba ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii kwa kudai kuwa Serikali imenunua na kuingiza nchini magari ya washawasha 777 badala ya kununua CT-Scanner na MRI. Kamati ililifanyia kazi shauri hili na kubaini kuwa maneno aliyoyasema Mhe. Suzan Lyimo hayakuwa na ukweli. Kamati ilipendekeza Mhe. Suzan Lyimo asimamishwe kuhudhuria vikao vitano vya Bunge lililokuwa linaendelea. Mapendekezo hayo yaliridhiwa.

3.4 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. William V. Lukuvi (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi dhidi ya Mhe. Anatropia Theonest (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni**

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili Mhe. Anatropia Theonest (Mb) alilalamikiwa na Mhe. William Lukuvi (Mb) Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu kauli aliyotoa Bungeni kwamba Mhe. William Lukuvi mnamo mwaka 2011 akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam alihusika na uporaji wa viwanja vya waathirika wa mabondeni.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati inafanya uchunguzi wake, Mhe. Anatropia bila kupoteza muda wa Kamati, alikiri mbele ya Kamati kuwa kauli yake haikuwa na ukweli. Katika mazingira hayo Kamati ilipendekeza Mhe. Anatropia asimamishwe kuhudhuria vikao vitatu vya Bunge katika mkutano uliokuwa unaendelea. Ushauri na mapendekezo haya yalikubaliwa. Kamati ilimpongeza Mhe. Anatropia Theonest (mb) kwa ushirikiano aliutoa kwa Kamati.

3.5 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu dhidi ya Mhe. James Kinyasi Millya (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni**

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili Mhe. James Millya (Mb) wakati akichangia mjadala wa Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini alimtaja Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu kuwa ni shemeji wa mmoja wa mbia wa kampuni ya *Sky Associate* inayomiliki mgodi wa *Tanzanite One*. Kampuni hiyo ilikuwa inadaiwa kunyanyasa wananchi wa Mererani Mkoani Arusha. Maelezo hayo yalilalamikiwa na Mhe. Jenista Mhagama kuwa ni ya uongo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichunguza malalamiko haya na kubaini kuwa kauli ya Mhe. Millya haikuwa na ukweli na ilikiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a). Hivyo Kamati ilipendekeza Mhe. Millya

asimamishwe kuhudhuria vikao vitano (5) vya Bunge lililokuwa linaendelea. Mheshimiwa Spika alikubali mapendekezo hayo.

3.6 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la kusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani lililowasilishwa na Mhe. James Millya (Mb)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokeakusudio la kuleta hoja ya kumwondoa Naibu Spika madarakani. Kusudio hilo liliwasilishwa na Mhe. James Millya (Mb) ambaye katika kujenga hoja yake aliainisha sababu tano ambazo ni:-

3.6.1 Kwamba Naibu Spika ameweka maslahi ya Chama chake cha siasa mbele kuliko maslahi ya Bunge.

3.6.2 Kwamba Naibu Spika alitumia vibaya madaraka kwa kutothamini heshima wanayostahili wanawake wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

3.6.3 Kwamba Mhe. Naibu Spika alimdhaliisha Mhe. Selemani Bungala (Bwege) kwa kumwambia mheshimiwa Bwege aache ubwege wake.

3.6.4 Kwamba Mhe Naibu Spika alivunja Katiba kwa kumzuia Mhe. Joshua Nassari (Mb) kutekeleza jukumu la kuishauri serikali pale ambapo alikataa hoja ya Mhe. Joshua Nassari (Mb) ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura kuhusu kufukuzwa kwa wanafunzi wa diploma maalum wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

3.6.5 Kwamba Naibu Spika alitisha kikao cha Kamati ya Kanuni tarehe 26 Mei, 2016 ambacho kilibadili hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ililifanyia kazi suala hili na kubaini pamoja na mambo mengine kuwa orodha ya majina ya wabunge iliyoambatanishwa katika hoja hiyo kuwa ni wabunge wanaounga mkono hoja hiyo haikuwa sahihi ambapo:

(a) Orodha ya iliyoambatanishwa ilikuwa ni majina ya wabunge wa UKAWA waliohudhuria kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 31 Mei,2016

(b) Aidha tarehe ya kusudio la kumwondoa Naibu Spika madarakani na tarehe ya mahudhurio ya kikao cha UKAWA zilitofautiana, kwani orodha ya mahudhurio ni tarehe 31 Mei,2016 na kusudio liliandaliwa tarehe 1 Juni,2016.

Mheshimiwa Spika,Baada ya kamati kubaini hayo ilijielekeza katika Kanuni ya 138(2) ambayo inaeleza utaratibu wa kumwondoa Naibu Spika Madarakani.Sehemu ya Kanuni inaeleza,nanukuu

"138(2) endapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaridhika kuwa zipo tuhuma mahususi dhidi ya Naibu Spika zinazohusu uvunjaji wa Katiba, sheria au kanuni zinazoongoza shughuli za Bunge,basi Kamati hiyo itaidhinisha kuwa hoja hiyo ipelekwe Bungeni ili iamuliwe"

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia ushahidi ulioletwa kama ilivyoelezwa hapo juu na kwa mujibu wa Kanuni hii,Kamati haikuridhika na ushahidi ulioletwa kuthibitisha hoja hiyo, hivyo, Kamati haikuridhia hoja kuletwa Bunge.

3.7 Kusikiliza na kutoa mapendekezo kuhusu shauri la Mhe. Joseph Mbilinyi (Mb) kuhusu kitendo cha kutoa ishara ya matusi Bungeni

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili Mhe. Joseph Mbilinyi (Mb) ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilidaiwa kuwa mnamo tarehe 6 Juni, 2016 baada ya kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni, wakati akitoka nje ya Ukumbi wa Bunge alionesha ishara ya matusi.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizi ilibaini kuwa ni kweli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi (Mb) alitenda kosa na pia Mhe. Mbunge huyo alikiri mbele ya Kamati kufanya kosa hilo. Kwa mazingira hayo Kamati ilitia hatiani na kupendekeza asimamishwe kuhudhuria vikao kumi (10) vya Mikutano ya Bunge na pendekezo hilo lilikubaliwa na Bunge.

3.8 Kamati kutakiwa kutoa tafsiri kuhusu Kanuni ya 75 kwa kuzingatia adhabu walizokuwa wamepewa baadhi ya Wabunge waliofanya fujo siku ya tarehe 27 mwezi Januari, 2016 na Wabunge wengine waliosimamishwa.

Mheshimiwa Spika, Baada ya Kamati kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua kwa baadhi ya Wabunge waliokutwa na hatia ya kufanya vurugu siku tajwa hapo juu, na Bunge kuazimia kulingana na mapendekezo ya Kamati, suala la matumizi ya Kanuni ya 75 lilijitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa tafsiri hiyo kwa Bunge kuwa, Kanuni ya 75 inahusu Mbunge aliyesimamishwa kwa mujibu wa Kanuni kutoka katika Bunge na kutoingia sehemu yoyote ya Ukumbi wa Bunge na maeneo mengine ya Bunge kwa muda wote atakaokuwa amesimamishwa. Aidha, Kanuni hiyo inaeleza kuwa Mbunge aliyesimamishwa atalipwa nusu mshahara na nusu posho zinazoambatana na mshahara huo.

3.9 Shauri linalowahusu Mhe. Ester Bulaya (Mb) na Mhe. Joshua Nasari (Mb)

Mheshimiwa Spika, Katika shauri hili Waheshimiwa hawa walituhumiwa kudharau Mamlaka ya Spika kwa kufanya fujo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Usikilizaji wa shauri hili haukukamilika kutokana na Waheshimiwa hawa kuwa na udhuru. Mhe. Joshua Nassari (Mb) alitoa taarifa kuwa alikuwa kwenye Mitihani ya Shahada ya pili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mhe. Ester Bulaya (Mb) alitoa taarifa kuwa anasafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu. Kamati iliridhia maombi yao na kuamua kuwa shauri hili litasikilizwa wakati mwingine. Aidha baadaye Mhe. Ester Bulaya, (mb) alitwa na kufika mbele ya Kamati ambapo kabla shauri lake halijaanza kusikilizwa, Kamati liahirisha usikilizwaji huo.

3.10 Kamati kukutana na Kamati za Maadili za Bunge la Kenya na Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kamati ilitekeleza jukumu la kukutana na Kamati ya Maadili kutoka Bunge la Kenya na Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawakilishi –Zanzibar zilizotembelea Bunge letu. Baada ya kupewa Maelekezo na Mheshimiwa Spika Kamati ilikutana na wajumbe hao kutoka Kenya tarehe 14 Septemba, 2016 na waliotoka Baraza la Wawakilishi siku ya tarehe 2 Februari, 2017

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo, tuliweza kubadilishana uzoefu katika masuala na mbinu mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Ni maoni ya Kamati kuwa ziara kama hizi ni muhimu hata kwa upande wetu kwa kuwa zinawezesha kujua mambo mapya na kujenga uzoefu wa Kamati.

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Katika kushughulikia mashauri haya, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

4.1 Ukwepaji wa kupokea Hati za wito

(a) Baadhi ya Mashahidi walioitwa mbele ya Kamati walikwepa kupokea Hati za Wito (Summons) hivyo, kuchelewesha shughuli za Kamati. Katika mazingira haya Kamati ililazimika kutumia Jeshi la Polisi kwa mujibu wa kifungu cha 15(3) cha sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge Sura ya 296 kuwafikishia mashahidi hao Hati za wito kwa lengo la kufanikisha kazi za Kamati.

(b) Aidha, katika kukwepa kupokea Hati za Wito baadhi ya mashahidi walitoa sababu mbalimbali za uongo kwa lengo la kukwepa kufika mbele ya Kamati.

4.3 Uhitaji wa Mafunzo kwa Kamati

Pamoja na kwamba Kamati ilipatiwa mafunzo mara baada ya kuundwa kwake yaliyoivezesha kufanya kazi hii, ni maoni ya Kamati kuwa bado mafunzo zaidi yanahitajika hususan mafunzo kupitia uzoefu wa mabunge mengine duniani ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

4.4 Kuandaa uamuzi mbadala (*Dissenting opinion*)

Katika kushughulikia shauri la baadhi ya wabunge kufanya fujo siku ya tarehe 27 Januari, 2016 ilijitokeza changamoto ya kuwa na maamuzi ya Kamati yanayotofautiana Wabunge wa Kambi ya Upinzani waliandaa maoni mbadala (*dissenting opinion*). Hata hivyo Spika alikataa maoni hayo kupokelewa kwa kuwa jambo hili halitambuliwi kikanuni.

4.6 Ufinyu wa muda

Kazi ya kushughulikia masuala yanayoletwa na Spika hufanyika kipindi cha Bunge ambapo shughuli nyingine za Bunge huwa zinaendelea. Kwa mantiki hiyo, Wajumbe wa Kamati hupaswa kutekeleza majukumu mengine ya Kibunge kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika mazingira haya wajumbe wa Kamati hulazimika kutumia muda wa mapumziko na siku za mapumziko ili kukamilisha shughuli za Kamati.

5.0 MAFANIKIO

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia makosa ya ukiukwaji wa Kanuni uliofanywa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ni maoni ya Kamati kuwa, kwa kiasi kikubwa nidhamu, ustahimilivu, heshima, utulivu na uzingatiaji wa Kanuni za Majadiliano bungeni umeimarika kuliko ilivyokuwa mwanzoni mwa Bunge hili.

6.0 MAPENDEKEZO

Mheshimiwa Spika, ili Kamati iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuondokana na changamoto zilizotajwa, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

6.1 Wajumbe wa Kamati wapewe mafunzo zaidi na ya mara kwa mara kuhusu wajibu wao katika Kamati na umuhimu wa kutanguliza maslahi ya Taifa katika kutekeleza wajibu wao.

6.2 Wabunge wote wa Bunge hili wapewe mafunzo kuhusu Haki, Kinga, na Maadili pamoja na ufafanuzi wa majukumu ya Kamati ili waweze kutoa ushirikiano kwa Kamati pale inapobidi.

6.3 Kamati ipewe muda wa kutosha kushughulikia mashauri yanayoletwa na Spika na kuyakamilisha kwa wakati.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa niaba ya Kamati. Napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyekiti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema shughuli za Bunge na kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati yangu iliyoiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kumshukuru Mhe. Almas Maige (Mb) Makamu mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kushughulikia mashauri yaliyoletwa na Mhe. Spika, kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Kapt(Mst), George H. Mkuchika, (Mb) - M/kiti

- (ii) Mhe. Almas Maige (Mb) - Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb).....Mjumbe
- (iv) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb).....Mjumbe
- (v) Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb).....Mjumbe
- (vi) Mhe. Othman Omar Haji (Mb).....Mjumbe
- (vii) Mhe. Rose Kamili Sukum (Mb).....Mjumbe
- (viii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb).....Mjumbe
- (ix) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb).....Mjumbe
- (x) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)Mjumbe
- (xi) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb).....Mjumbe
- (xii) Mhe. Asha Abdallah Juma (Mb).....Mjumbe
- (xiii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)Mjumbe
- (xiv) Marehemu Mhe. Hafidh Ali Tahir (Mb)alikuwa Mjumbe
- (xv) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)..... Mjumbe
- (xvi) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb) ... Mjumbe.

Napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Matamus Fungo, Ndugu Mariam Mbaruku na Ndugu Seraphine Tamba Makatibu wa Kamati pamoja na Ndugu Editruda Kilapilo Msaidizi wa Kamati na Ndugu Lweli Lupondo, mtalaamu wa Hansard kwa kuratibu vyema kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mhe. Capt. (Mst) George Huruma Mkuchika (Mb)
MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE
Januari, 2017

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Tunamaliazia na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Karibu Mwenyekiti.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa hoja kwa idhini yako na kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, napenda kumpongeza sana Jenerali Venance Salvatory Mabheyo kwa kuteuliwa kuwa Jenerali na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF), aidha nampongeza Jenerali Dkt. Juma Ali Malewa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Jeshi la Magereza. Pamoja na hayo pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi wa Mabalazi 21, kujaza nafasi 15 ambazo zilikuwa wazi nje ya nchi pamoja na wengine sita kufungua Balozi mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Nne zifuatazo; sehemu ya kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla, sehemu ya pili inahusu uchambuzi namatokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, sehemu ya tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya mwisho ya nne ambayo ni hitimisho ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, yameainishwa katika ukurasa wa pili hadi wa nane wa taarifa hii na ambayo yameorodheshwa vizuri katika Kanuni ya 119 ya Kununi za Kudumu za Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imefanya shughuli nyingi lakini katika kipindi cha Januari, 2016 mpaka Januari, 2017 Kamati hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa Wajumbe kuhusu kazi na majukumu ya Kamati, mafunzo kwa Wajumbe kuhusu muundo wa majukumu ya Wizara, kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji za Wizara, kufatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo Wizarani, kuchambua taarifa za Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Pia Kamati imepitia taarifa za Wawakilishi wetu wa Bunge katika Mabunge ya SADC-PF, PAP, IPU na EALA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imefanya uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Masuala yatakatolewa katika taarifa hii ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo yameorodheshwa katika ukurasa wa kumi na kumi na moja wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu masuala yaliyoainishwa katika sehemu ya taarifa inayofuata. Kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa Wizara zote tatu inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya miradi iliyotembelewa haikutekelezwa kutokana na kutopatiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitengewa jumla ya shilingi bilioni nane ambazo hadi Kamati inakagua miradi iliyoidhinishwa fedha nchini Msumbiji na Sweden mwezi Juni, 2016, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa. Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2016 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 3,489,315,000 ambayo ni asilimia 43.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo shilingi 1,316,000,000 ni kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa lililopo Ubalizi wa Tanzania Maputo, Msumbiji na shilingi 2,172,000,000 ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balizi na nyumba za watumishi zilizopo Stockholm, Sweden. Ni imani ya Kamati kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo zitatolewa kwa ukamilifu wake hadi kufikia mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na JKT na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hazikutolewa kwa ukamilifu wake kama inavyoonyesha katika uchambuzi wa Kamati ukurasa wa 12 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini. Pamoja na mambo mengine, hali hii inachangiwa sana na:-

(i) Uwepo wa magereza machache nchini ikilinganishwa na idadi ya wafungwa na mahabusu;

(ii) Matumizi hafifu ya sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na mpango wa Parole wa huduma kwa jamii;

(iii) Kutotolewa maamuzi kwa wafungwa wa muda mrefu waliohukumiwa kunyongwa;

(iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu;

(v) Kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa; na

(vi) Kutosikilizwa kwa muda mrefu kwa kesi za mauaji na kesi za dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliingalia jinsi Jeshi la Polisi linavyopambana na uhalifu katika jamii. Uwezo wa Jeshi la Polisi wa kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu hauna budi kuwa na

uwiano na idadi ya matukio ya uhalifu nchini. Hata hivyo, pamoja na juhudi kubwa ambazo Jeshi la Polisi inazifanya lakini uwiano huo haupo kutokana na ongezeko kubwa la watu ukilinganisha na idadi ya askari ambao ni wachache wa vitendea kazi na uhaba wa fedha pia vinachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi, ilibaini kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya operesheni maalum za kuzuia uhalifu hazitoshelezi mahitaji halisi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi hilo lilitengewa shilingi 969,700,000 tu kwa ajili ya shughuli hiyo. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi za utekelezaji wa mikakati ya Jeshi la Polisi katika upambanaji na kupunguza uhalifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali za barabarani zimeongezeka na kusababisha athari kubwa nyingi za kiuchumi na kijamii kwa Taifa na wahanga wa ajali. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi - Kikosi cha Usalama Barabarani kwa mwaka 2016 ajali 9,856 zilirekodiwa na kusababisha vifo 3,256 na majeruhi 8,958 kama inavyoonekana kwenye jedwali katika ukurasa wa 15 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vingi vya ajali zinazotokea Tanzania husababishwa na makosa ya kibinadamu yanayohusisha matumizi mabaya ya utumiaji wa barabara kwa mujibu wa Taarifa za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuainisha vyanzo hivyo vya ajali, Kamati imebaini kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 ambayo ndiyo sheria mama inayosimamia suala la usalama barabarani kwa kiasi kikubwa imeweza kukabiliana na tatizo hilo la ajali. Hata hivyo, kutokana na utafiti imeweza kukabiliana na tatizo la ajali lakini pameonekana pana mapungufu ambayo sheria hiyo ya usalama barabarani haitoshelezi kusaidia kupunguza tatizo sugu la ajali za barabarani. Mapungufu ya sheria yanaonekana katika visababishi vitano vya ajali ambavyo ni:-

- (i) Mwendokasi;
- (ii) Uvaaji wa kofia ngumu;
- (iii) Ufungaji wa mikanda;
- (iv) Matumizi ya kilevi; na
- (v) Vizuizi vya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya muda mrefu ya majeshi ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 hadi 2014/2015 deni la Jeshi la Polisi lilikuwa limefikwa shilingi 385,033,500,000; kipindi cha kuanzia mwaka 2012 hadi Disemba 2015, deni la Jeshi la magereza lilikuwa shilingi 62,516,708,378. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2016, Idara ya Uhamiaji lilikuwa linadaiwa shilingi 5,627,974,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa sheria tajwa, Jeshi hilo limekuwa halipewi uzito unaostahili kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wao. Changamoto hizo ni nyingi na zimeorodheshwa katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa sheria hii ina mapungufu mbalimbali na hivyo kuathiri utekelezaji wake. Baadhi ya upungufu ulioelezwa ni pamoja na:-

- (i) Sheria kutolipa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mamlaka ya kumiliki silaha jambo linalopelekea kushindwa kufanya majukumu yake ipasavyo hususan kwenye baadhi ya matukio ya uokoaji ambapo wananchi wanafanya fujo;
- (ii) Sheria kutolipa Jeshi Mamlaka ya kukamata, jambo linalopelekea wananchi wengi kukaidi Sheria na Kanuni zake; na
- (iii) Sheria kutolitambua Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama Mjumbe kwenye Tume ya Utumishi wa Polisi na Magereza, jambo linalosababisha ugumu katika kuwapandisha vyeo maafisa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria; mwaka 2014 Serikali ya Tanzania ilitoa uraia kwa wakimbizi wa Burundi 162,156 waliokuwa wakiishi katika makambi ya Mishamo, Katumba na Ulyankulu kwa zaidi ya miaka 40. Hata hivyo, pamoja na kuwa jambo hilo lilifanyika kwa nia njema, wakimbizi hao waliopewa uraia hawakusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini na badala yake waliachwa katika makazi yao ya awali kinyume na matakwa ya Sheria Namba 19 ya Wakimbizi ya mwaka 1998, inayotaka wakimbizi pekee kuishi katika eneo la makazi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofanya ziara katika makazi ya Ulyankulu mwezi Januari, 2017, ilibaini kutokuwepo kwa mpango wowote wa Serikali wa kuwahamisha wakimbizi hao waliopewa uraia kutoka katika makazi hayo na hakukuwa na maandalizi yoyote ya maeneo watakayopelekwa raia hao wapya.

Aidha, suala zima la wakimbizi bado lipo kwenye mchakato wa uboreshaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa namba 16 ya mwaka 1964. Sheria hii inatoa uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kuandikisha vijana wa kulitumikia Jeshi hilo. Tangu kuanzishwa kwa JKT, sheria hii imeshafanyiwa marekebisho mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho hayo mbalimbali yaliyofanyika, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya maeneo hayajatajwa kabisa katika Sheria hii na hivyo kuwepo na uhitaji wa kufanya marekebisho zaidi. Kwa mfano, suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT halijatajwa chini ya sheria hii ili kuwawezesha vijana walio kwenye mafunzo kupata fidia pale wanapoumia wakiwa mafunzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi ulianza tangu Bunge la Kumi ambapo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama iliishauri Serikali katika taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2013 kuharakisha utayarishwaji wa sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa hadi sasa Sera hii haipo na Serikali inaendelea kutoa maelezo kuwa mchakato bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alama za mipaka ya nchi; wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake, Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo la kukosekana na kung'olewa kwa alama za mipaka (*beacons*) katika maeneo mengi ya mipaka ya nchi. Pamoja na kwamba Kamati hii imekuwa ikizungumzia kuwepo kwa tatizo hili, bado hakuna hatua za kuridhisha zilizochukuliwa na Serikali ili kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa sheria. Vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa sheria ni wale wanaohitimu kidato cha sita, na kila mwaka takribani vijana 60,000 wanamaliza Kidato cha Sita. Hata hivyo, Jeshi la Kujenga Taifa lina uwezo wa kuchukua vijana wa kujiunga na JKT kwa mujibu wa sheria wapatao 35,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwezo wa JKT kutoa mafunzo kwa vijana wachache ikilinganishwa na idadi ya wahitimu, Kamati imebaini kuwa JKT inashindwa kutoa mafunzo kwa vijana 35,000 ambao ndiyo uwezo wa Jeshi hilo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni vijana 20,100 tu walipatiwa mafunzo na kwa mwaka wa fedha 2016/2017 idadi hiyo ilipungua kufikia 14,000.

Kamati ilielezwa kuwa upungufu huu unasababishwa na ukosefu wa fedha ambapo kati ya shilingi bilioni nane zilizotengwa kwa ajili hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni shilingi bilioni moja tu iliyotolewa ambayo ni asilimia 12.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa *African Peer Review Mechanism (APRM)* – Tanzania. APRM ni mpango wa Nchi 35 za Kiafrika wa kujitathmini kwa vigezo vya utawala bora. Mpango huu unalenga kukuza maendeleo ya nchi za Kiafrika Tanzania ikiwa mojawapo, kwa kuimarisha utawala bora katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza majukumu ya APRM- Tanzania, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wake. Changamoto hizo nimeziordhesha katika taarifa yangu. Aidha, kamati inapenda kumpongeza Balozi Ombeni Sefue kuingizwa kwenye Kamati ya watu mashuhuri wa Afrika katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la Chuo cha Diplomasia ni kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia na usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani. Hata hivyo, chuo hiki kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo nimezieleza kwa kirefu katika taarifa yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Balozi za Tanzania nje kutopata fedha kwa wakati, kwa muda mrefu Balozi zetu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kutokupata fedha kwa wakati. Jambo hili limeendelea kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo, licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii kuanzia Bunge la Kumi kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo. Kamati inaona kuwa Serikali bado haina nia thabiti ya kutekeleza ushauri huo kwani upatikanaji wa fedha katika Balozi nyingi haupo katika mtiririko wa kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za safari za viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Kimataifa. Serikali imeendelea kutenga fedha za safari za viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tangu mwaka wa fedha 2011 Kamati ilikuwa inashauri malipo ya safari za viongozi nje ya nchi yagharimiwe moja kwa moja katika Mafungu chini ya Hazina, hata hivyo ushauri huu haujatekelezwa. Hali hii inapelekea Fungu la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuonekana linatengewa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ilihali halisi fedha nyingi huwa ni kwa ajili ya safari za viongozi na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kimsingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi; Majengo ya baadhi ya Balozi zetu yameendelea kuwa chakavu kwa kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Kamati ilipofanya ziara zake katika ukaguzi wa miradi wa ukarabati wa majengo katika Balozi za Tanzania nchini Sweden Juni, 2016 ilishuhudia uchakavu uliokithiri wa majengo ya makazi ya Balozi mwenyewe na nyumba za watumishi wa Ubalozi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa majengo yote mawili yalitakiwa kufanyiwa ukarabati tangu mwaka wa fedha 2014/2015 lakini kutokana na uhaba wa fedha ukarabati huo haujafanyika na hivyo kusababisha kutotumika kwa sasa. Ni dhahiri kuwa hali hii inaathiri taswira yetu nje ya nchi, hiyo ni moja tu ya mifano lakini Balozi nyingi haziko katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Jitihada za usuluhishi kwa njia ya kidiplomasia bado zinaendelea ambapo majadiliano ya mwisho yamefanyika tarehe 24 Januari, 2017 na yanatarajiwa kuendelea mwezi wa Aprili, 2017. Ni matumaini ya Kamati kuwa mgogoro huo utamalizika kwa njia ya amani na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera mpya ya mambo ya nje. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya mambo ya nje. Sera hii, pamoja na mambo mengine ina lenga kukuza na kuendeleza Diplomasia ya Uchumi nchini. Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwezi Machi, 2016, ilielezwa kuwa Sera hii mpya ya Mambo ya Nje ilitungwa mwaka 2001. Ni dhahiri kuwa sera hii imeendelea kutumika kwa muda mrefu bila kuzingatia mabadiliko ya sasa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba iliyosainiwa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Januari, 2017 ilielezwa kuwa mikataba isiyopungua 43 ambayo imesainiwa na bado

hajjaridhiwa na Bunge. Taarifa hiyo ilionesha mikataba iliyosainiwa ni ile ya kuanzia mwaka mwaka 1972 hadi 2016. Kamati ilielezwa kuwa mikataba mingi iliyokwisha kusainiwa hucheleva kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kwa kuwa inapaswa kufanyiwa tathmini ya kina ili kujua umuhimu na manufaa yake kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kujiridhisha kuhusu manufaa ya mikataba hiyo kwa Taifa letu, ni dhahiri kuwa baadhi ya mikataba ni ya muda mrefu na Kamati haiafiki kuwa Serikali inahitaji zaidi ya miaka Mitano au Kumi kujiridhisha kuhusu manufaa ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika vyama mbalimbali vya Kibunge; kama ilivyoelezwa hapo awali, Bunge letu huwakilishwa kwenye vyama mbalimbali vya Kibunge vikiwemo CPA, ACP- EUna IPU na kwenye Mabunge ya SADC – PF na Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Uwakilishi huu pamoja na mambo mengine, ni njia mojawapo ya kutekeleza Diplomasia ya Kibunge ambapo wawakilishi hawa wakishiriki ipasavyo mikutano ya vyama hivyo vya Kibunge na Mabunge hayo, huliiongezea Bunge lako Tukufu uwezo wa ushawishi wa Kibunge katika Afrika, Kanda ya SADC, Afrika Mashariki na Jumuiya ya Madola. Aidha, Uwakilishi huu unalipa Bunge lako nguvu ya kuchochea kasi ya kuridhia mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu mkubwa wa wawakilishi hawa katika kutekeleza Diplomasia ya Kibunge, imebainika kuwa katika kipindi cha Januari 2016 hadi 2017, baadhi ya wawakilishi wameshindwa kuhudhuria mikutano ya vyama vya kibunge na wengine kucheleva kuwasili katika vikao hivyo kutokana na kucheleva kupatikana kwa vibali vya kusafiri nje ya nchi. Hali hiyo imeathiri fursa ya kushiriki ipasavyo masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika mikutano hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya jumla; Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Wizara zote tatu tunazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; kutokutekelezwa kwa Sheria ya Msamaha (*Parole*) na Sheria ya *Community Service* kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani.

Pia kutokusikilizwa kwa kesi haraka kunasababisha msongamano wa mahabusu magerezani hususan kesi za mauaji na kesi za madawa ya kulevya na kadhalika.

Aidha, kutokutolewa maamuzi kwa wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwarudisha makwao wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kunaiongezea Serikali gharama za kuwatunza wahamiaji hao magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa kunachangia malalamiko mengi ya wafungwa kutokutendewa haki yao Kikatiba.

Aidha, msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani pamoja na kuhatarisha afya za wafungwa, unaiiongezea Serikali gharama za kuwatunza wafungwa na mahabusu.

Kutokusambazwa kwa wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania katika maeneo mbalimbali nchini kuna hatarisha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo ya makazi. Aidha, kutosambazwa kwa raia hao wapya ni kinyume cha matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokupewa fedha za kutosha Jeshi la Polisi ili wakabiliane na uhalifu mbalimbali kunawafanya polisi wasikabiliane na wahalifu hao kwa ukamilifu.

Kutokutenga fedha za kutosha kwa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Jeshi hilo. Upungufu uliopo kwenye Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Ukoaji unapunguza ufanisi katika utekelezaji wa sheria hiyo. Aidha, kutokuwepo kwa mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki ambao unaziunganisha ofisi za Uhamiaji Mkoa, Wilaya, Vituo vya Mipakani na Makao Makuu kunaathiri udhibiti wa uingiaji na utokaji wa watu hususan utambuzi wa wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara ya Ulinzi na JKT; kutokutolewa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wote wanaohitimu kidato cha sita kunachangia kupunguza uzalendo, kuzorotesha maadili ya vijana wetu nchini na kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (*National Defence Policy*) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo. Kukosekana kwa Balozi ndogo au uwakilishi wa heshima kwenye baadhi ya miji yenye fursa nyingi za kiuchumi kunaathiri malengo ya Serikali ya kukuza uchumi wa nchi kupitia diplomasia ya uchumi. Tunashukuru Mheshimiwa Rais kuongeza baadhi ya Balozi sita mpya, naamini kwamba kuongezeka kwa Balozi hizo kutasaidia sana kwenye diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, APRM Tanzania kutokuwa na hadhi ya Kisheria (*legal entity*) kunaikwamisha taasisi hii kuwa na kasma yake ya kibajeti na hivyo kuathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti. Malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika Taasisi ya APRM Afrika yanapunguza hadhi ya nchi yetu mbele ya jamii ya Kimataifa. Kutokutolewa kwa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu APRM kunasababisha wananchi wengi wasijue kuhusu APRM na faida zake kwa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kunachangia Chuo cha Diplomasia kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hali inayoweza kusababisha chuo hicho kufutiwa usajili na NACTE.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga fedha kwa ajili ya safari za viongozi nchi za nje kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kunaathiri utengwaji wa Bajeti yenye uhalisia wa Wizara hiyo kuweza kutekeleza majukumu yake. Kutokukarabatiwa kwa majengo ya Balozi zetu siyo tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia yanaweza kushusha hadhi ya nchi yetu inayopewa heshima kubwa duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika vyama mbalimbali vya Kibunge kutoshiriki mikutano ya vyama hivyo kikamilifu kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine ya Afrika na duniani kwa ujumla kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge.

Pia kukosekana kwa kitengo maalum cha kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyosainia na Tanzania kunachewelesha mikataba mingi kufikishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa. Sera ya Mambo Nje ni ya muda mrefu na haiendani na mabadiliko ya sera ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, Mazingira yanayotokea duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maoni ya Kamati naomba kutoa mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutolewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo hutegemea upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hazikupokolewa kutoka Hazina, jambo ambalo lilikwamisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa kutokutekelezwa kwa miradi hiyo kutokana na kutokupokelewa fedha kumesababisha hasara kwa kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi.

Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuteleza miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa na Bunge ili kufanikisha azma ya Serikali kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani; kwa kuwa hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu na kuingoza Serikali gharama za kuwatunza.

Hivyo basi, Serikali itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole*; itekeleza sheria inayowataka wahalifu wenye makosa madogo kupewa dhamana ya vifungo vya nje ili watumikie jamii; ihakikishe kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi hizo kutolewa kwa wakati; itolee maamuzi kuhusu suala la wafungwa waliohukumikiwa adhabu ya kuyongwa hadi kufa (*condemned*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iwarudishe makwao wahamiaji hao ili kupunguza mzigo wa kuendelea kuwatunza katika magereza yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makazi ya wakimbizi ya Ulyankulu. Kwa kuwa eneo la makazi ya Ulyankulu liko kwenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,200 ilikuwa ni sehemu ya hifadhi ya Pori la Akiba la Ulyankulu, na watu wanaoishi katika eneo hilo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umalizie, muda umekwenda.

MHE. BAL. ADADI M. RAJABU – KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa taarifa hii, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2016 na Januari, 2017, Kamati ina imani kuwa fursa hii inatokana na masharti ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba maoni na mapendekezo ambayo nimeyaeleza yachukuliwe kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza tangu kuundwa kwa Kamati hii mwezi Januari 2016, ambapo uliteuwa Wajumbe ishirini na tatu (23). Kwa sasa Kamati ina Wajumbe 27 na naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Capt (Mst) George Huruma Mkuchika, Mb- Mjumbe
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb- “
5. Mhe. Prosper J. Mbeni, Mb- “
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb- “
7. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb- “
8. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb- “
9. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb- “
10. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb- “
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb- “
12. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb- “
13. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb- “
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb- “
15. Mhe. Kiswaga Bonventura Destery, Mb- “
16. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb- “
17. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb- “
18. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb- “
19. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb- “
20. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb- “
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb- “
22. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb- “
23. Mhe. Stephen J. Masele, Mb- “
24. Mhe. Machano Othman Said, Mb- “
25. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb- “
26. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb- “
27. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb- “

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyoinishwa katika fasili ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuteuwa Wajumbe wenye Taaluma, Uzoefu na sifa nyingine muhimu kwa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla;
- ii. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- iv. Sehemu ya Nne ambayo ni hitimisho la taarifa hii.

Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta inayosimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Majukumu ya Kamati hii ni kama yafuatayo:-

- i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia;

ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

iii. Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara, Kamati ina majukumu mengine matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni:-

i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;

iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;

iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na

v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

Mheshimiwa Spika, mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imetoa ruhusa kwa Kamati yoyote ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kupendekeza kwa Spika majukumu mengine ya nyongeza. Majukumu hayo ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni ya 119 yanatekelezwa kwa namna mbili zifuatazo:-

a) Kamati kupendekeza ipewe jukumu la nyongeza; na

b) Mheshimiwa Spika kukabidhi Kamati jambo lingine lolote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kinachotolewa taarifa hii, Kamati haikuwa na jukumu lolote la nyongeza kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 119.

1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) na (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Njia zilizotumika ni:-

i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;

ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili utekelezaji wa majukumu yao;

iii. Kuwataka Mawaziri wafafanue na kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;

iv. Ziara za kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha wa 2016/2017; na

vi. Kubadilishana mawazo na uzoefu na Kamati zinazosimamia Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama za Mabunge ya nchi nyingine.

1.4 Shughuli zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa Kamati walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha Januari, 2016 - Januari, 2017 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1.4.1 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Wajumbe wa Kamati ni wapya, walipatiwa mafunzo kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati, ili waweze kufahamu kazi na majukumu ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 21 Januari, 2016.

Aidha, baada ya kupokea mafunzo hayo, tarehe 23 Januari, 2016 Wajumbe waliandaa Mpango Kazi wa Kamati kwa kipindi cha Januari - Juni 2016.

1.4.2 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa hapo awali, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa kwa mara ya kwanza mwezi Januari, 2016. Hivyo, kwa kuzingatia jukumu la Kamati la kuzisimamia Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mambo ya Ndani ya Nchi na ile ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wajumbe walipatiwa mafunzo haya ili waweze kufahamu kwa kina kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara hizo pamoja na Sera na Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara hizo. Mafunzo haya yalifanyika mwezi Februari, 2016.

1.4.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

i) Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu:-

- Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mafanikio na changamoto kwa Kipindi cha Julai hadi Disemba, 2016;
- Utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Diplomasia, mafanikio na changamoto;
- Taarifa ya Sekretarieti ya *African Peer Review Mechanism (APRM)* Tanzania kuhusu utekelezaji wa majukumu yake, mafanikio na changamoto;
- Utekelezaji wa majukumu ya *Arusha International Conference Centre (AICC)*, mafanikio na changamoto;
- Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi na nafasi ya Tanzania katika Uchumi wa dunia;
- Hatua iliyofikiwa katika kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi;
- Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo haijaridhiwa na Bunge; na

- Utekelezaji wa Hati za Mkubaliano zilizosainiwa kati ya Tanzania na China wakati wa Ziara ya Rais wa Jamhuri ya Watu wa China iliyofanyika nchini Mwanzoni mwa Mwaka 2016;

ii) Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu:-

- Utekelezaji wa Sheria Namba 14 ya Mwaka 2007 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mafanikio na changamoto;

- Utekelezaji wa Majukumu ya Idara ya Wakimbizi mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo;
- Changamoto zinazoikabili Serikali baada ya kutoa Uraia kwa Wakimbizi katika kambi za wakimbizi Mishamo, Katumba na Ulyankulu; na

- Jeshi la Polisi kuhusu mikakati iliyopo ya kuzuia uhalifu nchini, mafanikio na changamoto.

iii) Taarifa ya Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi na Usalama wa Raia na Mali zao;

iv) Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na JKT kuhusu:-

- Utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Ulinzi wa Taifa, mafanikio na changamoto;na

- Hali halisi ya ulinzi katika maeneo ya Ziwa Nyasa kufuatia mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Spika, lengo la kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati yangu ilikagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara inazozisimia na iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ipo chini ya vifungu vifuatavyo:-

- Fungu 34- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- Fungu 29- Magereza;
- Fungu 93- Uhamiaji;
- Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;
- Fungu 38- Ngome; na
- Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Jumla ya miradi 13 ilikaguliwa na miradi hiyo imeambatanishwa katika taarifa hii (Tazama kiambatisho Na. 1)

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yalioathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

1.4.5 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Kamati yangu ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

1.4.6 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC PF, PAP, IPU na EALA

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC - PF, PAP, IPU na taarifa ya Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Nakala za Taarifa za Wawakilishi hao zimeambatishwa na Taarifa hii. Nakala hizo ni:-

- i) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge la Dunia (IPU) (Kiambatisho Na. 2)
- ii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge la Afrika (PAP) (Kiambatisho Na. 3)
- iii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Jumuiya ya Maendeleo ya Mabunge katika Nchi za kusini mwa Afrika (SADC- PF) (Kiambatisho Na. 4)
- iv) Taarifa ya Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (Kiambatisho Na. 5)

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Januari 2017, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati iktekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni:-

a) Masuala ya Ujumla

- Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- Msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza;
- Uhalifu katika jamii;
- Ajali za Barabarani;
- Madeni ya muda mrefu ya Majeshi ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji;
- Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
- Upungufu wa Sheria namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007;
- Wakimbizi wa Burundi waliopewa Uraia wa Tanzania; na
- Wahamiaji haramu.

c) Wizara ya Ulinzi na JKT

- Marekebisho ya Sheria Namba 16 ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 (National Service Act 1964)
- Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy);
- Alama za Mipaka ya Nchi; na
- Idadi ya vijana wanaotakiwa kujiunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria.

d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

- Utendaji wa *African Peer Review Mechanism*;
- Utendaji wa Chuo cha Diplomasia;
- Utaratibu wa kuzipatia fedha Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi
- Fedha kwa ajili ya safari za viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- Uchakavu wa Majengo ya Balozi za Tanzania nje ya Nchi;
- Utatuzi wa mgogoro wa Mpaka kati ya Tanzania na Malawi;
- Sera Mpya ya Mambo ya Nje (New Foreign Policy); na
- Mikataba na Itifaki iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

e) Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu katika sehemu ya taarifa inayofuata.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

2.2.1 Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa Wizara zote inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya miradi iliyotembelewa haikutekelezwa kutokana na kutopatiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitengewa jumla ya Shilingi **8,000,000,000.00** ambazo hadi Kamati inakagua miradi iliyoidhinishwa fedha nchini Msumbiji na Sweden Mwezi Juni, 2016, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2016 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi **3,489,315,000.00** sawa na asilimia 43.6 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi **1,316,435,000.00** ni kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa lililopo Ubalazi wa Tanzania Maputo, Msumbiji na Shilingi **2,172,880,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi na nyumba za watumishi zilizopo Stockholm, Sweden. Ni imani ya Kamati kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo zitatolewa kwa ukamilifu wake hadi kufikia Mwezi Juni, 2017.

Vilevile, Wizara ya Ulinzi na JKT iliidhinishwa Jumla ya Shilingi **232,137,958,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2016 Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi **40,000,000,000.00**, sawa na asilimia 17.2 tu ya bajeti yote ya maendeleo.

Hali kadhalika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 5,984,023,924** kati ya **Shilingi 79,689,945,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 7.5 tu ya bajeti yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini kuwa fedha za maendeleo zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2011/2012 hadi 2015/2016 kwa Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa fedha za maendeleo zimeendelea kutolewa pungufu ikilinganishwa na Bajeti halisi inayopitishwa na Bunge, hali ambayo imeendelea kuathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kama inavyoonekana kwenye mfano unaotolewa hapa chini kwa Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57).

MWENENDO WA FEDHA ZA MAENDELEO KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, FUNGU 57 (2011/2012- 2015/2016)

BAJETI ILIYOIDHINISHWA		FEDHA ZILIZOTOLEWA	FEDHA ZILIZOTOLEWA (%)
2011/2012	129,017,767,000.00	129,000,000,000.00	99%
2012/2013	389,186,566,000.00	218,000,000,000.00	56%
2013/2014	229,582,027,000.00	87,216,816,585.00	37%
2014/2015	229,842,500,000.00	70,500,000,000.00	30%
2015/2016	220,137,958,000.00	40,000,000,000.00	18%

Chanzo: Taarifa ya Wizara

2.2.2 Msongamano wa wafungwa katika Magereza

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini. Pamoja na mambo mengine, hali hii inachangiwa sana na:-

- (i) Uwepo wa magereza machache nchini ikilinganishwa na idadi ya wafungwa/mahabusu;
- (ii) Matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na mpango wa *Parole* wa huduma kwa jamii;
- (iii) Kutotolewa maamuzi kwa wafungwa wa muda mrefu waliohukumiwa kunyongwa;
- (iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu;
- (v) Kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa;na
- (vi) Kutosikilizwa kwa muda mrefu kwa kesi za mauaji na madawa ya kulevya.

2.2.3 Jeshi la Polisi linavyopambana na Uhalifu katika Jamii

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Jeshi la Polisi yameainishwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Watoa Huduma Wasaidizi wa polisi Sura ya 322 kama ilivyoboreshwa mwaka 2002. Majukumu hayo ni pamoja na kulinda amani, kulinda raia na mali zao, kuzuia makosa kabla hayajatatendeka, kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za nchi.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Jeshi la Polisi wa kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu hauna budi kuwa na uwiano na idadi ya matukio ya uhalifu nchini. Hata hivyo, uwiano huo haupo

kutokana na ongezeko kubwa la watu ukilinganisha na idadi ya askari, uchache wa vitendea kazi na uhaba wa fedha¹.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi, ilibaini kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Operesheni maalum za kuzuia uhalifu hazitoshelezi mahitaji halisi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi hilo lilitengewa Tsh. 969,700,000/= tu kwa ajili ya shughuli hiyo. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi za utekelezaji wa mikakati ya Jeshi hilo katika kupunguza uhalifu katika Jamii.

2.2.4 Ajali za Barabarani

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani zimeendelea kusababisha athari nyingi za kiuchumi na kijamii kwa taifa na wahanga wa ajali. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, kwa mwaka 2016 ajali 9,856 zilirekodiwa na kusababisha vifo 3,256 na majeruhi 8,958 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

MCHANGANUO WA AJALI, VIFO NA MAJERUHI KWA AINA YA VYOMBO VILIVYOSABABISHA AJALI ZA BARABARANI KWA MWAKA 2016

AINA YA CHOMBO	AJALI	%	VIFO	%	MAJERUHI	%
MAGARI BINAFSI	3,649	37.0	758	23.3	2,170	24.2
MABASI (PSV)	346	3.5	344	10.6	1,319	14.7
DALADALA (PSV)	947	9.6	342	10.5	1,379	15.4
TAXI CAB (PSV)	166	1.7	51	1.6	108	1.2
MAGARI YA KUKODI (PSV)	120	1.2	71	2.2	125	1.4
MAROLI YA TELA (HDV)	920	9.3	513	15.8	955	10.7
PIKIPIKI	2,544	25.8	890	27.3	2,128	23.8
BAISKELI	271	2.7	149	4.6	193	2.2
PICK-UPS	884	9.0	136	4.2	573	6.4
MIKOKOTENI	9	0.1	2	0.1	8	0.1
JUMLA	9,856	100.0	3,256	100.0	8,958	100.0

2

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vingi vya ajali zinazotokea Tanzania husababishwa na makosa ya kibinadamu yanayohusisha matumizi mabaya ya watumiaji wa barabara. Kwa mujibu wa Taarifa za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, makosa ya kibinadamu hasa yale yatokanayo na uzembe wa watumiaji wa barabara husababisha asilimia 76 ya ajali zote zinazotokea barabarani. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 8 ya ajali zinachangiwa na ubovu wa miundombinu ya barabara na asilimia 16 ya ajali hizo husababishwa na ubovu wa vyombo vya moto vitumikavyo barabarani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuainisha vyanzo hivyo vya ajali, Kamati imebaini kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ambayo ndio Sheria mama inayosimamia suala la usalama barabarani kwa kiasi kikubwa imeweza kukabiliana na tatizo la ajali barabarani. Hata hivyo, kutokana na utafiti uliofanywa na Asasi za kiraia zinazotetea mabadiliko ya Sheria na Sera ya Usalama barabarani, ilibainika kuwa Sheria ya Usalama barabarani ina mapungufu na haijitoshelezi kusaidia kupunguza tatizo sugu la ajali za barabarani³. Mapungufu ya Sheria yanaonekana katika visababishi vitano vya ajali ambavyo ni:-

- (i) Mwendokasi;
- (ii) Uvaaji wa kofia ngumu;

¹Takwimu ya Hali ya Uhalifu nchini Januari, 2015

²Taarifa ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani 24/05/2016

³Taarifa ya Muungano wa Asasi za Kiraia zinazotetea Mabadiliko ya Sheria na Sera ya Usalama Barabarani iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 26/01/2017

- (iii) Ufungaji wa mikanda;
- (iv) Matumizi ya kilevi; na
- (v) Vizuizi vya watoto.

2.2.5 Madeni ya muda mrefu ya Majeshi ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Februari 2016, ilibaini kuwepo kwa tatizo la madeni ya muda mrefu. Madeni haya yanajumuisha madeni ya watumishi, wazabuni na malipo ya ankara za umeme, maji na simu. Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2009/2010 hadi 2014/2015 deni la Jeshi la Polisi lilikuwa limefikwa **Tsh. 385,033,500,342.50**; na kipindi cha kuanzia Mwaka 2012 hadi Desemba 2015, deni la Jeshi la magereza lilikuwa **Shilingi 62,516,708,378.87**. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2016, Idara ya Uhamiaji lilikuwa linadaiwa Shilingi **5,627,974,474.00**

2.2.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilianzishwa kwa Sheria Namba 14 ya Mwaka 2007. Sheria hii iliunganisha vikosi vyote vya zimamoto na uokoaji vilivyokuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na vile vya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania Bara kuwa chini ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, Sheria hii inataja jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kuinga na kupunguza vifo, majeruhi na uharibifu wa mali unaotokana na moto, mafuriko, ajali za barabarani na dharura zote zisizo za jinai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa Sheria tajwa, Jeshi hilo limekuwa halipewi uzito unaostahili na kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

i) Uhaba wa vitendea kazi vikiwemo magari ya kuzimia moto, vifaa vya uokozi na visima vya kuhifadha maji, hivyo kushindwa kuzima moto na kufanya uokozi kwa ufanisi zaidi;

ii) Kushindwa kuyafikia maeneo mengi zaidi kwa ajili ya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kutokana na uchache wa rasilimali watu na magari ya ukaguzi;

iii) Kushindwa kuzifikia wilaya zote nchini kwa lengo la kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Aidha, ni Wilaya 15 tu kati ya Wilaya 141 nchini zenye vituo vya zimamoto na uokoaji; na

iv) Kushindwa kuviunganisha vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vilivyo chini ya Mamlaka ya Bandari na Viwanja vya Ndege kuwa chini ya Kamandi ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama Sheria inavyomtaka, hivyo kuleta ugumu katika kusimamia utekelezaji wa huduma za zimamoto na uokoaji nchini.

Upungufu wa Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (2007)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa Sheria hii ina mapungufu mbalimbali na hivyo kuathiri utekelezaji wake. Baadhi ya Upungufu ulioelezwa ni pamoja na:-

(i) Sheria kutolipa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mamlaka ya kumiliki silaha jambo linalopelekea kushindwa kufanya majukumu yake ipasavyo hususan kwenye baadhi ya matukio ya uokoaji ambapo wananchi wanafanya fujo;

(ii) Sheria kutolipa Jeshi Mamlaka ya kukamata, jambo linalopelekea wananchi wengi kukaidi Sheria na Kanuni zake;

(iii) Sheria kutolitambua Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama Mjumbe kwenye Tume ya Utumishi wa Polisi na Magereza, jambo linalosababisha ugumu katika kuwapandisha vyeo Maafisa wake; na

(iv) Sheria kutokutoa adhabu kali kwa wanaokaidi kufuata maelekezo ya Jeshi la Zimamoto hasa wale wanaogoma kulipa tozo na kutokufuata ushauri wa mifumo stahiki ya kufunga kwenye majengo yao.

2.2.8 Wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania kwa Mujibu wa Sheria

Mheshimiwa Spika, Mnamo Mwaka 2014 Serikali ya Tanzania ilitoa uraia kwa wakimbizi wa Burundi 162,156 waliokuwa wakiishi katika makazi ya Mishamo, Katumba na Ulyankulu kwa zaidi ya miaka 40. Hata hivyo, pamoja na kuwa jambo hilo lilifanyika kwa nia njema, wakimbizi hao waliopewa uraia hawakusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini na badala yake waliachwa katika makazi yao ya awali kinyume na matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998, inayotaka wakimbizi pekee kuishi katika eneo la Makazi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofanya ziara katika makazi ya Ulyankulu Mwezi Januari, 2017, ilibaini kutokuwepo kwa mpango wowote wa Serikali wa kuwahamisha wakimbizi wote waliopewa uraia kutoka katika makazi hayo, na hakukuwa na maandalizi yoyote ya maeneo watakayopelekwa raia hao wapya. Aidha, suala zima la wakimbizi bado lipo kwenye mchakato wa uboreshaji wake.

2.2.9 Sheria namba 16 ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 (National Service Act 1964)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa namba 16 ya Mwaka 1964. Sheria hii inatoa uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kuandikisha vijana wa kulitumikia Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa JKT, Sheria hii imeshafanyiwa marekebisho yafuatayo:-

- Marekebisho ya Mwaka 1966 ambapo Sheria ilirekebishwa ili Jeshi liweze kuandikisha vijana wenye taaluma zaidi ya kidato cha nne kwa mujibu wa Sheria; na
- Marekebisho ya Mwaka 1975 ambapo Sheria ilirekebishwa ili kuruhusu JKT kuungana rasmi na JWTZ kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa Taifa na hivyo kulifanya JKT kuwa moja ya Kamandi zilizo chini ya JWTZ.

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho yaliyofanyika, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya maeneo hayajatajwa kabisa katika Sheria hii na hivyo kuwepo na uhitaji wa kufanya marekebisho zaidi. Kwa mfano, suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT halijatajwa chini ya Sheria hii ili kuwawezesha vijana walio kwenye mafunzo kupata fidia pale wanapoumia wakiwa mafunzoni.

2.2.10 Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy)

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi ulianza tangu Bunge la 10 ambapo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama iliishauri Serikali katika Taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake kwa Mwaka 2013, kuharakisha utayarishwaji wa Sera hii, na naomba kunukuu kipengele hicho kama ifuatavyo:-

Kuhusu utayarishwaji wa Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar waweze kutoa maoni yao mapema iwezekanavyo yatakayowezesha kukamilishwa kwa Sera ya Taifa ya Ulinzi na hatimaye Sheria ya Taifa ya Ulinzi na Usalama⁴

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa hadi sasa Sera hii haipo na Serikali inaendelea kutoa maelezo kuwa mchakato unaendelea.

⁴Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama 2013:16

2.2.11 Alama za Mipaka ya Nchi

Mheshimiwa Spika, wakati ikitekeleza majukumu yake, Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo la kukosekana/kung'olewa kwa alama za mipaka (beacons) katika maeneo mengi ya mipaka ya nchi. Pamoja na kwamba Kamati hii imekuwa ikizungumzia kuwepo kwa tatizo hili, bado hakuna hatua za kuridhisha zilizochukuliwa na Serikali ili kulimaliza.

2.2.12 Idadi ya vijana wanaotakiwa kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria

Mheshimiwa Spika, vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria ni wale wanaohitimu Kidato cha Sita, na kila mwaka takribani vijana 60,000 wanamaliza Kidato cha Sita. **Hata hivyo**, Jeshi la Kujenga Taifa lina uwezo wa kuchukua vijana wa kujiunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria wapatao 35,000 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo wa JKT kutoa mafunzo kwa vijana wachache ikilinganishwa na idadi ya wahitimu, Kamati imebaini kuwa JKT inashindwa kutoa mafunzo kwa vijana 35,000 ambao ndio uwezo wa Jeshi hilo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni vijana 20,100 tu walipatiwa mafunzo na kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 idadi hiyo ilipungua kufikia 14,000. Kamati ilielezwa kuwa upungufu huu unasababishwa na ukosefu wa fedha ambapo kati ya Shilingi Bilioni 8 zilizotengwa kwa ajili hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ni Shilingi Bilioni 1 tu iliyotolewa sawa na asilimia 12.5.

2.2.13 Utendaji wa African Peer Review Mechanism (APRM) - Tanzania

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, Kamati inampongeza Balozi Ombeni Sefue kuingizwa kwenye Kamati ya watu mashuhuri wa Afrika katika Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, APRM ni Mpango wa Nchi 35 za Kiafrika wa Kujitathmini kwa vigezo vya Utawala Bora. Mpango huu unalenga kukuza maendeleo ya nchi za kiafrika, Tanzania ikiwa mojawapo, kwa kuimarisha utawala bora katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza majukumu ya APRM- Tanzania, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni:-

i) Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 mahitaji halisi yalikuwa **Shilingi 1,765,000,000.00**, wakati fedha zilizoidhinishwa na Bunge zilikuwa **Shilingi 620,160,000.00** sawa na asilimia 35 tu ya mahitaji halisi.

Fedha hizi zilitumika kulipa Mishahara na kugharamia mambo madogo madogo ya uendeshaji na hakukuwa na fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa kama vile kushindwa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu matokeo ya tathmini ya utawala bora katika nchi yao;

ii) APRM - Tanzania kutokuwa na hadhi ya Kisheria (Legal Entity). Hii inaikwamisha Taasisi hii kuwa Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, kukosekana kwa hadhi ya kisheria kunazuia APRM - Tanzania kuwa na Kasma yake na kutengewa bajeti kulingana na mahitaji yake;

iii) Malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika APRM Afrika ambapo mpaka Mwezi Agosti 2016, Tanzania ilikuwa hajachangia kiasi cha Dola za Kimarekani 396,032 sawa na Shilingi 871,240,000.000 ikiwa ni deni la Miaka Mitatu; na

iv) Uchakavu wa vitendea kazi kama vile magari na vifaa vya ofisini ambapo kwa mara ya mwisho magari na vifaa vilivyopo vilinunuliwa Mwaka 2007 wakati Sekretarieti ya APRM Tanzania inaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa changamoto tajwa hapo juu ndizo zinazoathiri utendaji wa Taasisi ya APRM - Tanzania.

Utendaji wa Chuo cha Diplomasia

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Chuo cha Diplomasia ni kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika masuala ya Diplomasia, uhusiano wa Kimataifa, Stratejia na usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani. Hata hivyo, Chuo hiki kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kutambua kuwa, Chuo hiki kilianzishwa Mwaka 1978 kwa ushirikiano wa Serikali mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji. Kwa Miaka Mitano tangu Chuo kilipoanzishwa nchi zote mbili zilishiriki katika uendeshaji wake. Hata hivyo, tangu Mwaka 1982 hadi sasa, Msumbiji iliacha kuchangia katika bajeti na kushiriki katika shughuli za uendeshaji, hivyo gharama zote za uendeshaji wa chuo zikabaki kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Msumbiji kujitoa katika ushiriki wa uendeshaji wa chuo hiki ni mojawapo ya changamoto zinazokikabili chuo. Changamoto nyingine ni pamoja na:-

i) Gharama kubwa za uendeshaji wa Chuo na ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Chuo kilitengewa bajeti ya matumizi mengineyo ya **Shilingi 2,524,570,000.00** na hadi kufikia Mwezi Juni 2015 kiasi kilichotolewa kilikuwa **Shilingi 767,553,532.00** sawa na asilimia 30 tu ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, ufinyu wa bajeti unasababisha malimbikizo ya madeni ambapo hadi kufikia Mwezi Juni 2016 Chuo kilikuwa kinadaiwa la **Shilingi 1,809,347,196.00**; na

ii) Ukosefu wa miundombinu ya kutosha hasa majengo ambapo yale yanayotumika hivi sasa mengi ni ya zamani na hayakidhi ongezeko la udahili na idadi ya wafanyakazi.

2.2.15 Balozi za Tanzania nje ya Nchi kutopata fedha kwa wakati

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Balozi zetu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kutopata fedha kwa wakati. Jambo hili limeendelea kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo, licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii kuanzia Bunge la Kumi kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Serikali bado haina nia thabiti ya kutekeleza ushauri huo kwani upatikanaji wa fedha katika Balozi nyingi haupo katika mtiririko wa kuridhisha.

2.2.16 Fedha za safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha za safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tangu Mwaka wa Fedha 2010/2011 Kamati ilishauri malipo ya safari za Viongozi nje ya nchi yagharimiwe moja kwa moja kwa mafungu yaliyo chini ya Hazina, hata hivyo ushauri huu haujatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hali hii inapelekea Fungu la Wizara kuonekana limetengewa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ilihali katika hali halisi fedha nyingi huwa ni kwa ajili ya safari za Viongozi na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

2.2.17 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania

Mheshimiwa Spika, majengo ya baadhi ya Balozi zetu yameendelea kuwa chakavu kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Kamati yangu ilipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ukarabati wa majengo katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden Mwezi Juni, 2016, ilishuhudia uchakavu uliokithiri wa majengo ya makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi wa Ubalozi huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa majengo yote mawili yalitakiwa kufanyiwa ukarabati tangu Mwaka wa Fedha 2014/2015 lakini kutokana na uhaba wa fedha ukarabati huo haukufanyika

na hivyo kusababisha kutotumika kwa sasa. Ni dhahiri kuwa hali hii inaathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi.

2.2.18 Utatuzi wa Mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hatua zilizofikiwa katika kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi na hivyo ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Oktoba, 2016.

Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa mgogoro wa mpaka kati ya nchi hizi mbili unatokana na kutokukubaliana kuhusu mapitio ya mpaka kwenye Ziwa Nyasa. Aidha, ilielezwa kuwa kiini cha mgogoro huo ni Mkataba wa Heligoland uliowekwa saina kati ya Uingereza na Ujerumani tarehe 01 Julai, 1890, ambapo Ibara ya 1 (2) ya Mkataba huo inaeleza kuwa:-

"...to the south by a line which, starting on the coast at the northern limit of the province of Mozambique, follows the course of the river Ruvuma to the point of confluence of the Msinje; thence it runs westwards along the parallel of the t point till it reaches Lake Nyassa; thence striking northwards it follows the eastern, northern and western shores of the lake to the northern bank of the mouth of River Songwe; it ascends that river...."

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo ndio iliyosimamiwa na nchi ya Malawi kuwa inawapa umiliki wa Ziwa lote. Hata hivyo, Tanzania yenyewe imesimamia Ibara ya VI inayoeleza kuwa:-

"All the lines of demarcation traced in articles 1 to IV shall be subject to rectification by agreement between the two powers in accordance with local requirements"

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania ina msimamo kuwa ibara inayosimamiwa na Malawi haina maana yoyote hadi hapo mpaka huo utakapopimwa kwa kuzingatia uhalisia wa mazingira na kuridhiwa na pande zote mbili, ambapo kwa mujibu wa ibara ya VI ya Mkataba huo Kamisheni ya Mipaka ilifanya marekebisho na kuhamisha mpaka huo katikati ya mto Songwe kupitia Mkataba wa Mwaka 1901.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa nchi zote mbili zimeshikilia misimamo yake japokuwa zipo tayari kwa usuluhishi wa mgogoro huo. Pande zote mbili zilifiki kuwasilisha ombi la kusuluhishiwa mgogoro huo kwenye jopo la Viongozi Wastaafu wa Afrika wa nchi za SADC kutoka Msumbiji, Afrika Kusini na Botswana Mwezi Disemba 2012. Usuluhishi huo unaendelea chini ya Uenyekiti wa Mhe. Joachim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji akisaidiwa na Mhe. Festus. Mogae, Rais Mstaafu wa Botswana na Mhe. Thabo Mbeki, Rais Mstaafu wa Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Jitihada za usuluhishi kwa njia ya kidiplomasia bado zinaendelea ambapo majadiliano ya mwisho yamefanyika tarehe 24 Januari, 2017 ambayo yanatarajiwa kuendelea mwezi wa Aprili, 2017. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa mgogoro huo utamalizika kwa njia za amani na salama.

Sera Mpya ya Mambo ya Nje

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje. Sera hii, pamoja na mambo mengine, ina lenga kukuza na kuendeleza Diplomasia ya uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Machi, 2016, ilielezwa kuwa Sera hii Mpya ya Mambo ya Nje ilitungwa Mwaka 2001. Ni dhahiri kuwa Sera hii imeendelea kutumika kwa muda mrefu bila kuzingatia mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

2.2.20 Mikataba iliyosainiwa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi Nyingine

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuratibu na kusimamia Mikataba na makubaliano ya kimataifa. Lengo la Mikataba hii ni

kuiwezesha nchi yetu kuimarisha na kudumisha ushirikiano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kimataifa na Kikanda kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na lengo zuri la Mikataba inayosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine, Kamati imebaini kuwepo kwa mikataba mingi iliyosainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haijaridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Januari, 2017 ilielezwa kuwa Mikataba isiyopungua 43 ambayo imesainiwa, bado haijaridhiwa na Bunge. Taarifa hiyo ilionesha Mikataba iliyosainiwa ni ile ya kuanzia Mwaka 1972 hadi 2016. Kamati ilielezwa kuwa, Mikataba mingi iliyokwisha kusainiwa huchelewa kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kwa kuwa inapaswa kufanyiwa tathmini ya kina ili kujua umuhimu na manufaa yake kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kujiridhisha kuhusu manufaa ya Mikataba hiyo kwa Taifa letu, ni dhahiri kuwa baadhi ya Mikataba ni ya muda mrefu na Kamati haiafiki kuwa Serikali inahitaji zaidi ya Miaka Mitano au Kumi kujiridhisha kuhusu manufaa ya Mikataba hiyo.

2.2.21 Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa hapo awali, Bunge letu huwakilishwa kwenye Vyama mbalimbali vya Kibunge vikiwemo CPA, ACP- EU na IPU, na kwenye Mabunge ya SADC (SADC- PF), Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Uwakilishi huu, pamoja na mambo mengine, ni njia mojawapo ya kutekeleza Diplomasiya ya Kibunge ambapo, wawakilishi hawa wakishiriki ipasavyo mikutano ya Vyama hivyo vya Kibunge na Mabunge hayo, huliiongezea Bunge lako Tukufu uwezo wa ushawishi wa kibunge katika Afrika, Kanda ya SADC, Afrika Mashariki na Jumuiya ya Madola. Aidha, uwakilishi huu unalipa Bunge lako nguvu ya kuchochea kasi ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo Mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na umuhimu mkubwa wa wawakilishi hawa katika kutekeleza Diplomasiya ya Kibunge, Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha Januari 2016 - Januari 2017, baadhi ya Wawakilishi wameshindwa kuhudhuria mikutano ya Mabunge/ Vyama vya Kibunge, na wengine kuchelewa kuwasili katika vikao hivyo kutokana na kuchelewa kupatikana kwa vibali vya kusafiri nje ya nchi. Hali hiyo iliathiri fursa ya kushiriki ipasavyo katika masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika mikutano hiyo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

a) Masuala ya Jumla

i) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Wizara zote tatu tunazozisimamia.

b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

ii) Kutotekelezwa kwa Sheria ya Msamaha (Parole) na Sheria ya *Community Service* nchini kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

iii) Kutokusikilizwa kwa kesi kwa haraka kunasababisha msongamano wa mahabusu magerezani hususan kesi za mauaji, madawa ya kulevya, n.k;

iv) Kutotolewa maamuzi kwa wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo;

v) Kutokuwarudisha makwao wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kunaiongezea Serikali gharama za kuwatunza wahamiaji hao magerezani;

vi) Kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa kunachangia malalamiko mengi ya wafungwa kutotendewa haki yao kikatiba;

vii) Msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani pamoja na kuhatarisha afya za wafungwa, unaiongezea Serikali gharama za kuwatunza wafungwa na mahabusu;

viii) Kutosambazwa kwa wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania katika maeneo mbalimbali nchini kuna hatarisha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo ya makazi; Aidha, kutosambazwa kwa raia hao wapya ni kinyume cha matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998;

ix) Kutokupewa fedha za kutosha Jeshi la Polisi ili wakabiliane na uhalifu mbalimbali nchini kutawafanya Polisi wasikabiliane na wahalifu hao kwa ukamilifu;

x) Kutotenga fedha za kutosha kwa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Msingi ya Jeshi hilo;

xi) Upungufu uliopo kwenye Sheria namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Ukoaji unapunguza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hiyo;

xii) Kutokuwepo kwa mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki ambao unaziunganisha Ofisi za Uhamiaji Mkoa, Wilaya, Vituo vya Mipakani na makao makuu kunaathiri uhibitaji wa uingiaji na utokaji wa watu hususan utambuzi wa wahamiaji haramu;

c) Wizara ya Ulinzi na JKT

xiii) Kutokutolewa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wote wanaohitimu Kidato cha Sita kunachangia kupunguza uzalendo na kuzorotesha maadili ya vijana wengi nchini;

xiv) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa.

d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

xv) Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo;

xvi) Kukosekana kwa Balozi ndogo/uwakilishi wa heshima kwenye baadhi ya miji yenye fursa nyingi za kiuchumi kunaathiri malengo ya Serikali ya kukuza uchumi wa nchi kupitia Diplomasia ya uchumi;

xvii) APRM Tanzania kutokuwa na hadhi ya Kisheria (legal entity) kunaikwamisha Taasisi hii kuwa na Kasma yake ya Kibajeti na hivyo kuathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti;

xviii) Malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika Taasisi ya APRM Afrika yanapunguza hadhi ya nchi yetu mbele ya jamii ya Kimataifa;

xix) Kutokutolewa kwa elimu ya kutosha kwa Umma kuhusu APRM kunasababisha wananchi wengi wasijue kuhusu APRM na faida zake kwa nchi;

xx) Ufinyu wa Bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kunachangia Chuo cha Diplomasia kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hali inayoweza kusababisha Chuo hicho kufutiwa usajili na NACTE;

xxi) Kutenga fedha kwa ajili ya safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kunaathiri utengwaji wa Bajeti yenye uhalisia wa Wizara hiyo kuweza kutekeleza majukumu yake;

xxii) Kutokarabati majengo ya Balozi zetu si tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia yanaweza kushusha hadhi ya nchi yetu inayopewa heshima kubwa duniani;

xxiii) Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika vyama mbalimbali vya Kibunge kutoshiriki mikutano ya vyama hivyo kikamilifu kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine ya Afrika na Duniani kwa ujumla kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge;

xxiv) Kukosekana kwa kitengo maalum cha kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyosainia na Tanzania kunachewelesha mikataba mingi kufikishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa; na

xxv) Sera ya Mambo Nje ni ya muda mrefu na haiendani na mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

3.2.1 Kutokutolewa kwa fedha za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo hutegemea upatikanaji wa fedha na kwamba fedha kwa ajili ya miradi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hazikupokolewa kutoka Hazina, jambo ambalo lilikwamisha utekelezaji wa miradi hiyo,

Na kwa kuwa kutokutekelezwa kwa miradi hiyo kutokana na kutopelekewa fedha kumesababisha hasara kwa kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi,

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuteleza miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma ya Serikali kwa miradi hiyo.

3.2.2 Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani

Kwa kuwa imebainika kuwa tatizo lamsongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza nchini limeendelea kuongezeka kutokana na:

- i) Kutokutekelezwa ipasavyo kwa utaratibu wa *Parole*;
- ii) Kutokutumika kwa Sheria zinazohusu adhabu mbadala kwa wafungwa;
- iii) Kutokukutana ipasavyo kwa Kamati za Kusukuma kesi;na
- iv) Kutowezekana kutekelezwa kwa hukumu ya adhabu ya kunyongwa hadi kufa;

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu (watu ambao hawajahukumiwa) na kuingoza Serikali gharama za kuwatunza;

Kwa hiyo basi, Serikali:-

- i) Itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole* kwa mujibu wa Sheria;
- ii) Itekeleza Sheria inayowataka wahalifu wenye makosa madogo kupewa adhabu ya vifungo vya nje ili watumikie jamii (*Community Service Act*);

iii) Ihakikishe kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi hizo kutolewa kwa wakati; na

iv) Itolee maamuzi suala la wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa (condemned).

3.2.3 Kuwarejesha wahamiaji haramu

Kwa kuwa magereza mengi nchini yanakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu,

Na kwakuwa kati ya wafungwa/mahabusu hao wengine ni wahamiaji haramu ambao hukaa kwa muda mrefu bila ya kurudishwa makwao,

Kwa hiyo basi, Serikali iwarudishe makwao wahamiaji hao ili kupunguza mzigo wa kuendelea kuwatunza katika Magereza yetu.

3.2.4 Makazi ya Wakimbizi ya Ulyankulu

Kwa kuwa makazi ya wakimbizi ya Ulyankulu yanakaliwa na watu 93,062 ambao kati yao 15,220 ni wazawa na 3,985 ni wakimbizi ambao hawana uraia wa Tanzania,

Na kwa kuwa Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998 inatamka kuwa mtu yeyote ambaye ni Raia haruhusiwi kukaa ndani ya makazi ya wakimbizi isipokuwa wakimbizi tu,

Na kwa kuwa eneo la makazi ya Ulyankulu lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 1200 ilikuwa ni sehemu ya hifadhi ya Pori la Akiba la Ulyankulu, na watu wanaoishi katika eneo hilo wanaendelea na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo na ufugaji ambazo zinaathiri uhifadhi wa mazingira katika eneo hilo,

Kwa hiyo basi, Serikali iweke utaratibu wa kutekeleza matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998 ili kuliinda hifadhi ya Pori la Akiba la Ulyankulu ambalo ni muhimu kwa ustawi wa mazingira katika ukanda ule. Aidha, pale itakapobidi, Serikali ifanye marekebisho ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ili iendane na mazingira ya sasa ya wakimbizi.

Jeshi la Polisi Kukabiliana na Uhalifu

Kwa kuwa vitendo vya uhalifu mbalimbali katika jamii vimeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa,

Na kwakuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu ni ndogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mafuta, magari na vitendea kazi,

Kwa hiyo basi Serikali iongeze Bajeti ya Jeshi la Polisi ili liweze kukabiliana na uhalifu unaoendelea kufanyika. Aidha, kama ilivyo kwa mradi wa BRN wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni unaolenga kupunguza uhalifu kwa kiasi kikubwa katika Mkoa huo, Serikali ihamasishe uanzishwaji wa miradi ya aina hiyo katika Mikoa yote Tanzania.

3.2.6 Ajali za Barabarani

Kwa kuwa ajali za barabarani zimeendelea kusababisha athari nyingi kiuchumi na kijamii kwa Taifa,

Na kwa kuwa imebainika kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ina mapungufu na ikibaki kama ilivyo sasa itashindwa kupunguza tatizo hilo sugu linaloendelea kukua kila siku,

Kwa hiyo basi, Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho kwa kuvielezea kwa kiwango kamili visababishi vyote vya ajali za barabarani ili kuweza kudhibiti na kupunguza ajali za barabarani.

3.2.7 Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi

Kwa kuwa utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu unataka fedha hizo zipitishwe katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,

Na kwa kuwa utaratibu huo umebainika kuwa na urasimu usio wa lazima na hivyo kuchelewesha kutuma fedha kwa mtiririko unaotakiwa,

Kwa hiyo basi, Serikali ipeleke fedha za Balozi moja kwa moja bila kupitisha Wizarani kama ilivyo kwa Halmashauri zote nchini ambapo fedha hutumwa moja kwa moja bia kupitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

3.2.8 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania

Kwa kuwa majengo mengi ya Balozi zetu nje ya nchi ni chakavu sana,

Na kwa kuwa kutokarabati majengo hayo kumeendelea kuiongezea gharama Serikali kwani baadhi ya Balozi zinalazimika kukodi majengo mengine mbadala,

Kwa hiyo basi, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali itenge fedha za ukarabati wa majengo ya Balozi kwa awamu kwa kuanza na Balozi ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya zaidi kama vile majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden.

3.2.9 Uendelezaji wa viwanja vya Balozi za Tanzania

Kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya kuendeleza viwanja vya Balozi zetu nje ya nchi kwa mfano kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania mjini Maputo kilichopatikana Mwaka 1978,

Na kwa kuwa kutoviendeleza viwanja hivyo kunaisababishia Serikali kupoteza mapato na vilevile kuwepo uwezekano wa viwanja hivyo kuchukuliwa na Mamlaka za nchi husika,

Kwa hiyo basi, Serikali itafute fedha kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na vyanzo vingine kwa ajili ya kuviendeleza viwanja hivyo ambapo majengo yatakayojengwa yanaweza kutumika kama kifega uchumi na hivyo kuongeza pato la Serikali.

3.2.10 Sera Mpya ya Mambo ya Nje

Kwa kuwa Sera ya Mambo ya Nje (2001) imeendelea kutumika kwa muda mrefu,

Na kwa kuwa Sera hiyo kwa sasa haizingatii mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na Kimazingira yanayotokea duniani,

Hivyo basi, Serikali iongeze kasi ya kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ili kuwa na Sera itakayozingatia kukuza na kuendeleza dhana ya Diplomasia ya Uchumi kwa mapana yake.

3.2.11 Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kwa kuwa ipo mikataba mingi na ya muda mrefu iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haijaridhiwa na Bunge,

Na kwa kuwa kutoridhiwa kwa Mikataba hiyo na Bunge lako tukufu kunachelewesha kuanza kwa utekelezaji wa mikataba hiyo,

Hivyo basi, Serikali ianzishe kitengo au Idara maalum ya kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyosainiwa na nchi yetu ili kuongeza ufanisi, tija na heshima ya nchi yetu.

3.2.12 Upatikanaji wa vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa Wawakilishi wa Bunge katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge

Kwa kuwa baadhi ya Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawakuweza kushiriki kikamilifu mikutano ya vyama mbalimbali kutokana na kuchelewa kupata vibali vya kusafiri nje ya nchi,

Na kwakuwa kutoshiriki vikao hivyo kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine ya Afrika na Duniani kwa ujumla kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge,

Hivyo basi, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kuwa na utaratibu wa kuwasilisha Serikalini maombi ya vibali vya kusafiri nje ya nchi mapema kulingana na ratiba ya vikao hivyo, na vilevile Serikali itoe fedha na vibali hivyo kwa wakati muafaka.

SEHEMU YA NNE

5.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari, 2017. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angela Kairuki (Mb), na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas Kashilillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Issa, Bi. Grace Bidya na Ndg. Hamisi Mwinyimkuu wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

10 Februari, 2017

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana Mwenyekiti. Tumemaliza kupokea taarifa za Wenyeviti wote sasa tunaingia kwenye mjadala wa jumla, lakini kwa vile muda umebaki mdogo tutaanza na Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa Allan Kiula, wamegawana dakika tano, tano, tutaendelea na Mheshimiwa Kanali Masoud na Mheshimiwa Mattar wamegawana dakika tano, tano halafu tutaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Kamati yangu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama nikiwa Mjumbe wa Kamati hiyo. Nianze moja kwa moja kuzungumzia namna ambavyo bajeti inaathiri utendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Taarifa ya Kamati imejieleza, kwa muda mrefu sana Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imekuwa ikishindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na bajeti ambayo imekuwa ikitengwa, haifiki kwa wakati na hata ile ambayo ni ndogo ambayo imekuwa ikitengwa kwa ajili ya Kamati hiyo imekuwa haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ripoti imesema ukienda kuangalia Balozi zetu zina hali mbaya. Balozi zetu katika nchi za nje kwa kweli zimechakaa, fedha za matengenezo hakuna. Kama haitoshi, inafika mahali kama Kamati tunaona kwamba sasa lile lengo la kuwa na hizi Balozi nje haina maana. Kwa sababu lengo mojawapo la kuwa na Balozi katika nchi za nje ni kuhakikisha kwamba tunakuza diplomasia ya kiuchumi, lakini ukiangalia uhalisia huo kwa sasa haupo, Balozi zetu zinashindwa kufanya kazi kutokana na kwamba fedha za maendeleo zimekuwa hazipelekiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watumishi ambao wanafanya kazi katika Balozi hizo wamekuwa ni watu wa kupewa mishahara, lakini wanashindwa kutekeleza yale majukumu yao ya kimsingi kutokana na kwamba fedha zimekuwa haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri juu ya hilo kwamba ni vema sasa kama Wizara, ikaangalia utaratibu hizi fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya Wizara hiyo zikaenda moja kwa moja kwenye Balozi kama ambavyo fedha za maendeleo zimekuwa zikienda katika Halmashauri zetu. Kwa kufanya hivyo naamini kwamba itarahisisha utendaji kazi wa hizo Balozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata shughuli za Kamati katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 kwa kiasi fulani Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tumeshindwa kutekeleza majukumu yetu kama ambavyo tunapaswa kutekeleza, hususan kwa suala la mambo ya nje. Sisi kama Wajumbe wa hii Kamati tunavyozungumzia kwenda kutekeleza majukumu yetu, mojawapo ni kwenda kutembelea hizi Balozi kuangalia kama zinatekeleza majukumu yao ya kukuza diplomasia ya kiuchumi. Ni wazi kwamba kama Kamati haijawezeshwa kutekeleza jukumu hilo, sasa inafika mahali sisi Wajumbe tunakuja kuchangia hapa Bungeni kwa vitu ambavyo tumeletewa ripoti ya kwenye makaratasi, kitu ambacho sio kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kushauri katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2017/2018 nashauri kwamba Wizara iweze kuangalia utaratibu mpya kwamba fedha ambazo zinatengwa ziende kama zilivyopangwa na siyo kama ambavyo imetokea katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Wizara imetengewa bilioni nane lakini imeenda bilioni tatu. Haijafika hata nusu yay ale malengo ambayo, kama Wizara ilikuwa imejiwekea.

Vilevile hata vyama vya kibunge; kuna vyama kwa mfano PAP, ilikuja kwenye Kamati yetu lakini wakasema sisi hatuna kitu cha kuwasilisha kwa sababu hatujaenda popote. Ninaomba sana suala hili la bajeti liweze kuzingatiwa. Kwa kufanya hivyo tutaongeza ufanisi katika Bunge kama muhimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba pia nizungumzie suala lingine kama Kamati tuliweza kutembelea magereza mbalimbali. Tumetembelea Gereza la Songwe, gereza ambalo linajishughulisha na shughuli za uzalishaji mali na wamekuwa wakifanya hivyo na kuweza kulisha magereza mengine. Tatizo kubwa ni kwamba wamekuwa hawalipwi fedha zao kwa wakati na hiyo inasababisha kuwavunja moyo na inawaondolea ile hali ya kuendelea kuzalisha zaidi.

Nashauri Wizara iangalie katika bajeti ijayo basi waweze kuzingatia yale madeni ambayo gereza linakuwa linaidai Serikali yaweze kwenda kulipwa kwa wakati kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la polisi. Siku zote polisi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, lakini niipongeze Serikali kwa sababu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umeisha.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia machache katika Kamati yetu hii. Mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Mapendekezo mengi tumeyatoa, lakini yapo mambo yanatukwamisha sisi wenyewe kwa kutokuwa watekelezaji wazuri wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo tumeliona katika magereza yetu, mimi mwenyewe nilipata nafasi ya kutembelea magereza mengi hapa nchini lakini ninayoyakuta huko nashangaa kwa nini tunashindwa kuyasimamia. Wabunge wengi wanasimama hapa wanasema magereza wana maeneo makubwa ya kilimo na magereza wanaweza wakajiwezesha. Wanayo maeneo ya kilimo, tunawasaidiaje kuweza kuyalima hayo maeneo? Hilo ndiyo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Songwe mfano, wanasema wao wanaomba matrekta kwa ajili ya kufanyia kazi na mimi kwa mara ya kwanza toka nimezaliwa sijawahi kumuona mfungwa anaomba pembejeo, mfungwa analalamika hatuletewi pembejeo, hatuletewi matrekta, kumbe watu wanataka kufanyakazi lakini sisi wenyewe tunashindwa kuwawezesha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakwambia wanadai pesa nyingi ambazo hata hayo matrekta wangeweza kujinunulia, wanajilisha wenyewe, wanajitosheleza kwa chakula na wanalisha na magereza nyingine lakini bado tunashindwa kuwawezesha kuwapa vifaa vya kuongeza kilimo. Mimi nilikuwa naomba sana tuliangalie hili na ikiwezekana tuwapatie uwezo wa kukopeshwa hayo matrekta kama upo uwezo ili wafanyakazi watuzalishie na inawezekana wakaweza kulisha magereza mengi zaidi hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine nilikuta pia gereza moja hapa Morogoro; ni gereza linazalisha maziwa kwa wingi tu, lakini wanakwambia gari la kupelekea maziwa sokoni hawana. Sasa tufanyeje tuwaache wenyewe wanywe maziwa au tufanye nini? Lakini cha msingi kama kweli wanazalisha, wana uwezo mkubwa kwa nini tusiwapatie hata gari la kupeleka maziwa sokoni? Halafu ukiwauliza wanakwambia kwenye akaunti yao wanazo milioni 40; kwa nini hamnunui wanasema aah, utaratibu hauturuhusu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi sielewi mtu anakuzalishia, anakupatia pesa, lakini wewe kumuwezesha ili azidishe kuzalisha huwezi, mambo mengine haya hayataki kusoma shule wala wapi. Tukae kitako tu tuamue ili wenzetu hawa wapate kuzalisha na waweze kusaidia magereza mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niliongezee hapa kuna hawa wafungwa waliohukumiwa kunyongwa; wameshahukumiwa wale wanasema, mimi nimeshawatembelea nimezungumza nao na ni hatari kuzungumza na watu wale, lakini tumezungumza nao maana wamekaa mia mbili, mia tatu kama hivi wakikutizama unaweza ukachanganyikiwa. Wanasema haki yetu tuliyoipata mahakamani ni kunyongwa, sasa kwa nini hatunyongwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaona maana kuna viongozi wengine hapa tunatunga sheria, tunatakiwa tuzitekeleze lakini tunaogopa dhambi. Sasa kama lengo ni kuogopa dhambi kwamba hatuwezi kunyonga basi sheria ibadilishwe, lakini kama sheria imewekwa inatakiwa itekelezwe basi kila mtu atekeleze. Tunahimiza kila siku kila mtu atekeleze wajibu wake, kama hukumu ya kunyongwa imetolewa na hatuwezi kunyonga tubadili sheria au kama tunaweza kunyonga basi tunyonge maana wale wanadai haki yao na haki yao ni kunyongwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumza hapa lililonisikitisha sana zaidi kule Mbeya; tumekwenda tunaambiwa kule hakuna gari la Zimamoto lakini tunaambiwa ikitokea tatizo la moto gari lazima litokee uwanja wa ndege. Sasa hebu tujiulizeni Waheshimiwa Wabunge hapa gari ya uwanja wa ndege; ndege bado dakika kumi ndege itatua na moto unawaka,

tunafanya nini? Lakini la kushangaza zaidi tunaambiwa gari moja ya zimamoto limetolewa Mbeya kupelekwa Dar es Salaam kwa matengenezo. Mimi huwa najjuliza gari hili hivi fundi hawezi kupelekwa Mbeya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata kama lina mambo ya kiufundi, huyo fundi hawezi kwenda Mbeya akalicheki gari na baadae akarudi Dar es Salaam akachukua spea; gharama zake hapa zinakuwaje? Gharama za kupeleka gari Dar es Salaam na gharama ya kumpeleka fundi ipi ndogo? Lazima tukae wakati mwingine tuangalie haya mambo na pia tuyachukulie hatua zinazofaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza haraka ni huu msongamano unaozungumzwa wa magereza. Msongamano huu unasababishwa na mambo mengi likiwemo pia baadhi ya Wilaya zetu hapa nchini kukosa magereza kabisa. Niombe sasa tujitahidi hasa kule Chunya tupate magereza ili wafungwa sasa waweze kuwekwa kule na kupunguza msongamano kule Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani katika kuyafanyia kazi mambo yenu haya muwape uwezo pia ndugu zetu wa polisi wa kule Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kanali, tunaendelea na Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii lakini hujaniambia nitachangia dakika ngapi?

MWENYEKITI: Dakika tano tu.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Kamati hii ya Mambo ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite sana katika masuala ya kuchukua vijana wa JKT hasa kwa upande wa Zanzibar. Kuchukua vijana wa JKT kwa upande wa Zanzibar ni suala zuri sana, lakini kutokana na utaratibu ambao unachukuliwa hawa vijana siyo utaratibu ambao unaridhisha. Kupitishia vijana kwa Wakuu wetu wa Mikoa kwa upande wa Zanzibar ni tatizo sugu sana. Kule Zanzibar tuna Kikosi cha JKU ambacho kikosi hiki kinafanana na Kikosi cha JKT kina mahusiano mazuri na Kikosi hiki cha JKT. Namuomba Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Dkt. Hussein Mwinyi akubaliane na masuala haya tuhakikishe vijana wanaochukuliwa kwa upande wa Zanzibar kuja katika Kikosi cha JKT wapitie katika kikosi hiki cha JKU, ninaamini tutapata vijana wazuri ambao ni wasikivu na imara ambao tunawataka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana hata bajeti nilichangia suala hili tuwaongeze vijana katika upande wa Zanzibar; vijana wanaotakiwa kuchukuliwa kwa upande wa Zanzibar angalau tufikishe asilimia kumi. Katika vijana 5,000 ambao wanatakiwa kuchukuliwa katika Jeshi la JKT angalau vijana 500 watoke upande wa Zanzibar, tupunguze msongamano wa ajira kwa upande wa Zanzibar. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa katika bajeti yako ambayo umezungumza fedha zako hazitoshi, lakini uwezo wa kuchukua vijana hawa unao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali itusaidie sana kwa upande wa wizara hii iwaongeze bajeti ya fedha ili waweze kuchukua vijana wengi kupunguza msongamano wa vijana katika jamii zetu. Nikuombe sana na tuiombe Serikali itusaidie juu ya hili kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema nafasi anayo kubwa ya kuchukua vijana na anao uwezo mkubwa lakini tatizo ni fedha kidogo. Tumuombe Waziri wa Fedha akija na bajeti aweze kutusaidia atuongeze bajeti ili tuweze kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri aweze kuchukua vijana wengi kwenda katika Jeshi la JKT. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie na suala la Wizara ya Mambo ya Ndani. Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi zake vizuri lakini vilevile tatizo ni fedha. Hawa askari wetu wanaishi maisha duni ambayo hata hayahesabiki, wanakaa katika makazi mabovu suala hili Mheshimiwa Waziri

tunalizungumza kila siku ndani ya Bunge hili halijapatiwa ufumbuzi. Hebu leo nataka ukija utueleze hapo mbele, hivi nyumba za hawa askari ni lini utaanza kuzijenga? Isiwe kila siku maneno tu hapa katika Bunge lako hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la fedha kwa Wakuu wa Vituo vyetu hawa wanahudumia mahabusu wao wenyewe, kuwalisha wao wenyewe na hata umeme ndani ya vituo vyetu hivi vya polisi wanatoa wenyewe Wakuu wa Vituo. Ukiangalia kiukweli hii kadhaa kubwa katika nchi yetu. Ni aibu Mkuu wa Kituo mshahara wake tunaujua basi anaendelea kuwalisha mahabusu kwa nguvu zake yeye mwenyewe. Tunakwenda wapi katika Wizara hii? Tukigusa makazi mabovu, uendeshaji mbovu na ndani ya vituo vyetu magari hatuna na nyumba za askari mbovu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama pale Ziwani wakati mmoja nilienda kutembelea pale Ziwani tumekuta nyumba za askari zinashangaza sana nyumba hizi na ni hatari kubwa. Mtu anaingia kwa kuinama, kama hakuna uwezo wa kuzitengeneza nyumba hizi basi hata marekebisha ya kuzifanyia *repair* hizi nyumba upatikane....

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Tunaendelea na Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, nianze kwa kusema kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa hiyo ninaunga mkono hoja na nipongeze Wajumbe wenzangu wa Kamati pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, ninaamini tumefanyakazi nzuri na tunaiomba Serikali ipokee ushauri ambao tumeishauri kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mjumbe nilitaka nizungumze kwa ujumla mambo yanayohusiana na amani na utulivu wa nchi yetu. Ripoti ya utafiti iliyotolewa na *Institute of Economics and Peace* inazungumzia na inaonesha kwamba Tanzania ni nchi ya 64 kati ya nchi 64 ambayo ipo hatarini kutoweka kwa amani. Kwa hiyo, Kamati yetu inahusika na mambo ya nje, ulinzi na usalama na ili ustawi wa amani katika nchi yetu ni lazima eneo hili liendeshwe kwa weledi, kwa utadalam, huku demokrasia ikishamiri katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii imetaja ma-group manne ya nchi namna ambavyo yana-exercise utawala wake. Inasema pale ambapo kuna *full democracy* kunakuwa kuna amani ya kutosha na kunakuwa na maendeleo ya kutosha kwa sababu watu wanakuwa na uhuru wa kutoa mawazo yao, watu wanaweza waka-challenge na kukosoana kwa amani kwa sababu kuna *full democracy*. Kwa hiyo, katika ripoti hii inaonesha kwamba kukiwa na *full democracy* nchi huwa ina flourish. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii imeeleza vilevile kuna *frauddemocracy*, *democracy* ya kiasi; kunapokuwa kuna *democracy* ya kiasi kunaanza kuwa na viashiria vya uvunjivu wa amani. Kipengele cha tatu kuna *hybrid regime* ambayo ndiyo Tanzania tunaangukia hapo kwamba tuna utawala wa kichotara ambapo kuna aina fulani ya demokrasia, lakini kuna aina fulani ya udikteta. (Makofi)

Katika ripoti hii inasema nchi yoyote ambayo inaangukia katika eneo hili inakuwa kwenye hatari ya kupoteza amani na Tanzania tupo kwenye hatari ya kupoteza amani kwa sababu tupo kwenye *hybrid regime*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni *authoritarian regime* ambayo hiyo ni ya kidikteta kabisa ambako bado hatujafika na tumeona madhara ya kuwa na *regime* za namna hii. Kwa hiyo, tunapozungumzia suala la ulinzi na usalama ni jambo la msingi na ni jambo la muhimu sana tukifuata taratibu, sheria na kanuni tulizojiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyazungumza yote haya kuweka kama msingi. Taifa letu ili tusingie kuwa eneo la mwisho kabisa ambalo ni hatari, ni lazima tuzingatie sheria na taratibu ambazo

tumejiwekea wenyewe. Kwa hiyo, ningeomba vyombo vya ulinzi na usalama na ningeomba watawala wanaohusika sheria ambazo tunazitunga hapa tukizifuata wote tutajikuta tunaiweka nchi yetu katika usalama na hatimaye uchumi wa nchi yetu utakua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nikiangalia Wizara ya Mambo ya Ndani nataka nimnukuu Mheshimiwa Kafulilla jana ali-tweet, amezungumzia tuna chombo kwa mfano hiki cha *National Drug Control Council* ambapo ndani ya chombo hiki yupo Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani, ambao hawa wote wanashughulika na chombo hiki kwa ajili ya kudhibiti pamoja na Waziri wa Afya naye yumo na wengineo. Hawa wote ni chombo ambacho kimeundwa kwa ajili ya kudhibiti dawa za kulevya na kipo kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimezungumzia masuala ya ulinzi, kila Kiongozi ana mipaka yake na kila Kiongozi amepewa majukumu yake. Kuna chombo kama hiki nilitaka niulize Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwigulu upo hapa, kumetokea kitu gani badala ya hiki chombo kushughulika na masuala ya msingi kama haya ambayo sisi sote tunaunga mkono vita ya kupambana na dawa za kulevya, leo siwaoni Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri wa Afya mkishughulika na mkitoa matamko kwa sababu ninyi ndiyo wenye chombo hiki, tunamuona Makonda ndiyo amebeba bango la nchi nzima ambaye ni kiongozi na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam sawa tu na Mheshimiwa Amina Masenza, Mkuu wangu wa Mkoa pale Iringa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mheshimiwa Makonda yeye ndiyo abebe bango na chombo kikubwa ambacho kinatakiwa kifanye kazi hiki kikae kimya. Ningeomba haya mambo Serikali ijaribu kufafanua, kwa sababu haya ndiyo mambo ambayo yanasababisha utengamavu na utulivu wa nchi yetu upotee bila sababu. Mtoto aliyehongwana mama yake huwa tunamuita *mummy's boy* au *mummy's girl* lakini inaonekana Makonda labda ningemuita *daddy's boy*. Kwa sababu anaweza akasema chochote anachotaka wakati wowote hajui na mipaka yake, hii inaweza ikatuletea matatizo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makonda siyo mtaalam wa mambo ya uchunguzi. Mwenyekiti wangu wa Kamati umekaa kwenye kitengo hicho utaweza kutusaidia. Polisi wamesomea, wanaweza kufanya *investigation* ya mambo haya, sasa watu wote tumekaa kimya nchi hii *where are the lawyers?* tuna *Tanganyika Law Society, where are the lawyers*, tunapona mambo yanaenda vibaya tumekaa kimya. *Where are the judges* hatuoni Majaji wakitoa matamko kuonesha kwamba kila mtu akae kwenye msimamo wake ili nchi yetu iweze kuwa na utulivu na amani, watu wote wamekaa kimya, tunalipeleka wapi Taifa ambalo kila mtu akiamka asubuhi anaamua kufanya jambo analolitaka na wachungaji wamekaa kimya, lakini wengine tunaona wakipewa zawadi wanasema *at least* mimi nasema hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuna *checks and balance*, wahenga/wataalam wa mambo ya utawala walivyoamua kuweka mihimili mitatu hawakuwa wajinga, waliona anaweza akatokea kichaa mmoja akaamua kufanya anavyotaka, Bunge letu hili lipo kwa ajili ya kazi hiyo mambo yanapokwenda hovyoy lazima tusimame kama muhimili kumrudisha nyuma yule anaekwenda vibaya na maamuzi tuliyoyafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *my question is where are the judges in this country and where are the lawyers*, tunawasomesha kwa gharama kubwa wanasoma sheria ili iweje? Lengo tunataka tukae katika nchi yetu kwa usalama na haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii imezungumza vizuri sana juu ya jinsi ambavyo amani inaweza kutoweka. Lakini kwa sababu ya muda ninataka kusema Bunge hili kwa sababu ya kutokujua au kwa makusudi tulitoa maamuzi ambayo mengine ni ya hovyoy katika nchi yetu, ni wakati sisi kama watunga sheria na muhimili ambao ni wa muhimu katika Taifa letu tufike mahali tujitafakari. Kwa mfano, tulipitisha sheria ambayo inaminyu upatikanaji wa habari ambayo inawasaidia watu wachache, hii sheria tulipitisha hapa lakini mwisho wa siku itatugeuka ni kiashiria ambacho kinaweza kikasababisha tuvunje amani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Bunge letu hili ambao ni muhimili muhimu katika taifa letu limekosa uhuru, limekuwa ni Bunge ambalo linaminywa, hatuwezi kuikemea Serikali tena, *why are we here?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo hapa kufanya nini kama hatuwezi kuidhibiti Serikali na tunapoidhibiti Serikali siyo maana yake tunataka kuiangusha, tunataka itembee katika mkondo wake ili amani yetu itulie na ndiyo kazi ya Bunge. Kazi ya Bunge ni kuidhibiti na kuisimamia Serikali ienende kama inavyopaswa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mwenzangu hapa ametoa mwongozo tunaye Katibu wa Bunge hapa anayetakiwa atuongoze tunapokaa hapa; sasa leo anaenda kwenye vyombo vya habari anasema Bunge limekosea. Na yeye anafanya kazi yetu ya Bunge hatujaajiriwa na yeye hapa *with duerespect*, anafanya kazi ya Bunge hajatuajiri yeye sisi hapa; anatakiwa afuate maagizo yetu. Na ana wataalam wanaotushauri anatakiwa atuelekeze *where are we heading?* Haya ni masuala tunahitaji tujadiliane siyo kwa kugombana ni kwa kujadiliana wote kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili ni Serikali kupiga marufuku vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, huko ndiyo tunaweza kuona mambo mengi ambayo yanaenda hovyoy, tukaongea kwa uhuru, tukaisaidia Serikali ienende vizuri. Haya mambo tunakaa kimya tunashangilia mtu mmoja anaamua halafu tunakaa kimya watu wote, *where are we heading?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Asasi za Kiraia zikijaribu kuzungumza nazo zinazuiwa na zinakatazwa, haya ni masuala ambayo tunapaswa tujulize tunakwenda wapi. Ni maoni yangu kwamba ni vizuri tukasonga mbele na ni vizuri tukatafakari kama Bunge, je, tunafanya wajibu wetu, tunatimiza wajibu wetu kama muhimili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, dakika moja tu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme hii nchi yenye Bunge kibogoyo, TAKUKURU kibogoyo, vyombo vya habari bubu, NGO bubu na siasa bubu, polisi kibogoyo na *National Drug Control* kibogoyo, hatuwezi kuepusha michafuko katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe wote kwa pamoja na kwa kumaliza dakika ya mwisho kabisa mchungaji mmoja kule Ujerumani wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia aliwahi kusema; *"Silence in the face of evil it is evil itself, God will not hold us guiltless not to speak is to speak, not to act is to act."* Kwa hiyo, hatupaswi tukae kimya katika haya mambo haya mabaya, ningewaomba Wabunge tushirikiane wote kwa pamoja tuulinde muhimili wetu, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa muda wako umeisha.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya na muda wetu umefikia hapa mwisho kwa mchana huu, kabla sijaitisha shughuli za Bunge naomba niwataje Wabunge ambao watachangia kwa siku ya leo jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka atafuatiwa Mheshimiwa Cosato Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Machano Othman, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Joseph Selasini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi hadi saa kumi jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo
na
Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge
na
Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa na majadiliano yetu, tunaanza sasa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na baadaye Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nijue utaratibu ni dakika ngapi.

MWENYEKITI: Una dakika kumi.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi muda huu, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili kwa awamu hii kwa kikao hiki kwanza kabisa nianze na pongezi. Nawapongeza kwa dhati Wabunge wetu wapya wateule wa Mheshimiwa Rais ambao wameungana na sisi, uteuzi huo mimi mwenyewe umenifurahisha sana, natoa pongezi na nimefarijika sana kumuona Mwenyekiti wa Baraza la Wazazi wa CCM, Mheshimiwa Abdallah Bulembo akiwa na sisi. Hii ni waziwazi kwamba Mheshimiwa Rais anataka Bunge hili pia tuwe na weledi katika malezi ya vijana wetu, kwa hiyo hongereni sana.

Pia nampongeza msomi mwenzangu, Mheshimiwa Profesa Kabudi ambaye na yeye ameungana na sisi na nitoe taarifa kwako Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba jana sisi katika *Bunge Readers' Club* tayari tumeshaanza kumfaidi aliweza kutoa mada ya matumaini yake katika Bunge hili. Kwa hiyo, tunaona kwamba uzoefu wetu katika fani ya sheria ambazo tunatunga unaendelea kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela ambaye anarejea nyumbani, waswahili wanasema mwenda kwao siyo mtoro, hapa ni nyumbani kwake. Natoa pia pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dkt. Possi ambaye amepangiwa kazi nyingine ambaye sasa hivi ni Balozi katika Diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wetu mpya wa Majeshi aliyeteuliwa na kutoa pongezi zangu, ziwekwe *on record*, kwa Jenerali Mwamunyange ambaye amemaliza kipindi chake kwa utekelezaji uliotukuka, hapo hatuna budi kabisa kusema kwamba tulikuwa katika mikono salama na leo tunaangalia ulinzi na usalama wa Taifa hili. Naendelea pia kutoa pongezi zangu kwa....

MBUNGE FULANI: Mmmh!

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Ndiyo, kwa sababu ni sehemu ya ulinzi na usalama kama unashangaa ni *conceptual framework*, maana yake mambo haya huu ndiyo ulinzi na usalama wenyewe huu, kwa sababu watu wanafikiria kwamba ulinzi na usalama ni mitutu ya bunduki hapana, ni amani, ni maendeleo, ni upendo, ni kufahamiana ni kutambuana na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina budi kuwapongeza waliokuwa kwenye uchaguzi mdogo, naipongeza CCM na mimi mwenyewe najipongeza kwa kushinda kwa kishindo na wenzetu nasema kwamba kujikwaa siyo kuanguka, lakini wapiga kura kwa kweli walikwenda vizuri kwa sababu ulikuwa ni uchaguzi wa amani. Kule kwangu Muleba ninapozungumza hili sina budi kuwatambua kabisa wananchi wa Muleba Kata ya Kimwani na kumpongeza Ndugu Daudi Kiruma aliyeibuka mshindi akaleta ushindi wa CCM. Niwashukuru sana watu wote waliohiriki katika zoezi hili

ambalo lilikwenda katika hali ya ustaarabu na demokrasia ya kisasa, nawapongeza sana, ngazi ya Taifa hawakututupa, ngazi ya Mkoa, Wilaya mpaka kwenye Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mkoa wa Kagera, mimi ni mwakilishi kutoka Mkoa wa Kagera na katika hali ya kuangalia hali ya ulinzi, usalama na ujirani mwema wetu mnajua kwamba tulipata tetemeko na kwa mara nyingine tena ninatoa shukrani kwa mchango wa Waheshimiwa Wabunge ambao mlitupa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Mheshimiwa Rais ambaye tarehe Mosi, mwaka huu alikuja akasali na Wanakagera, akatufaraji na sisi tulifarajika. Nilishangaa sana kuona watu ambao wazungu wanasema watoa machozi ya mamba (*crocodile tears*) wakijaribu kubeza ziara hiyo iliyofanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanakagera tulifarajika sana na hasa tuliweza kupata misaada mbalimbali. Mheshimiwa Rais alikuja amejipanga vizuri alikuja na Balozi wa Uingereza ambaye atasaidia katika kurekebisha miundombinu. Mambo haya siyo haba, tumeyashuhudia. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba katika suala la kumshukuru Rais kuja kututembelea na hata Mheshimiwa Jenista aliandamana naye Mawaziri kadhaa walikuwepo pale nawashukuruni sana na changamoto waliziona.

Sasa kitu kikubwa ambacho napenda kusema kinahusiana na mada ya sasa hivi ni kwamba makazi kwa wananchi wa Kagera yanaendelea kuwa ya wasiwasi kwa sababu watu ambao nyumba zao ziliporomoka wengi bado wako katika hali hatarishi kiulinzi na kiusalama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nichukue nafasi hii kuomba kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama pia iangalie jambo hili kwa mapana yake na kuangalia sasa tunapojipanga na Waheshimiwa Mawaziri Serikali mnapojipanga, mnawasaidiaje wananchi ambao sasa hivi bado wanaendelea kuwa nje kwa sababu hawana makazi. Mheshimiwa Rais alifafanua vizuri sana, mimi naweza nikasema kwamba nimeshughulikia mambo ya maafa kwa ngazi za Kimataifa, Serikali huwa haijengi nyumba hata na Japan hawajengi nyumba hiyo ni *international standard*, jambo hili linaonekana geni kwa watu wengi lakini ndivyo sheria za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi ambalo tunaweka mezani kuwasaidia wale wahanga sasa kupata vifaa vya ujenzi kwa bei nafuu, ni suala la kiusalama na kiulinzi na kimiundombinu kwamba sasa hivi mtu ambaye nyumba yake imeporomoka sasa analipa kodi ya VAT kwenye mabati, kwenye simenti, kitu hiki kina ukakasi na tukiangalie sasa kwa mapana marefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, dakika ngapi sasa hizi tano, bado ninazo tano, sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika zangu tano ambazo sasa zimebaki, naomba nianze na suala la ulinzi na usalama kabisa ambalo limeongelewa sana na watu, na ninaomba nikabidhi kwa rekodi ya *Hansard*, naomba nikabidhi barua ya Makamu wa Rais wa nchi ya tarehe 30, Mei alipositisha zoezi la kufukuza mifugo kutoka kwenye Mpori ya Akiba na Hifadhi nyingine ndogo ndogo. Kuna barua hapa naomba ipokelewe, wahudumu nisaidie, iwe kwenye rekodi za *Hansard*, sasa hao watu ambao wanaendelea kukiuka maagizo ya Makamu wa Rais wa Nchi kwamba zoezi hili limesitishwa wakati Serikali inajipanga watuambie wenyewe mamlaka yao wanayapata wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza sasa hivi, katika Wilaya ya Misenyi kuna watu sasa hivi wanachomewa nyumba zao, kuna wafugaji ambao wanahangaishwa, kuna wafugaji wengine Wabunge wengine nimesikia mnasema watu wameuawa, ninaomba tusipopata maelezo ya kutosha basi Bunge hili liazimie kwamba tuwe na *Judicial Enquiry* katika vifo vinavyoendelea kwa wafugaji. Kwa sababu, haiwezi kukubalika, tuliona Operesheni Tokomeza ilipotufikisha, sasa inakuaje watu wanapigwa risasi na Maafisa Wanyamapori na inakuwa *business as usual*, jambo hili haliwezi kukubalika naomba barua ya Makamu iwe sehemu ya *Hansard*. Kama imefichwa iliandikwa kwa Wakuu wa Mikoa wa Tanzania Bara wote, ninayo hapa naiweka *for the record*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nisisitize, mimi kwangu Muleba tuna tatizo la usalama wa wavuvi, wavuvi wangu wanahangaishwa. Naomba Serikali itufafanulie, ulinzi wa wavuvi, wavuvi ni kama wametelekezwa inabidi walipe wao vituo vya Polisi, wajitafutie zana na mambo kama hayo. Kwa hiyo, naomba Kamati ya Ulinzi na Usalama ije itutembelee na akina mama katika Kamati ile na ninyi wawabebe kama wanavyonibeba mimi kuingia kwenye mitumbwi maana yake kule hakuna hata gatiza kuweza kupaki boti, ni suala la ulinzi na usalama ni suala nyeti, naomba lifanyiwe kazi kwa mtazamo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ulinzi na usalama pia kuna suala la chakula. Kule kwangu Muleba sisi ni wakulima, tunafanya kazi kwa bidii lakini tulikuwa na ukame, kuna upungufu wa chakula, kwa hiyo chakula hakitoshi, na penyewe tuangaliwe kwa mtizamo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tibaijuka, tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi pamoja na Mheshimiwa Rweikiza dakika tano, tano.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi japo nilikuwa najua nina dakika kumi, nimeshutukiziwa ziko tano, *anyway* nitajaribu kuzitumia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuunga mkono na kupongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kufungua Balozi katika nchi sita ikiwemo Israel, Korea, Algeria na nyinginezo pamoja na Uturuki. Itakumbukwa wakati fulani hapa alipofanya ziara Mfalme wa Morocco ilitokea hali kama ya sintofahamu kwamba kwa kuwa sisi tunaunga mkono Polisario inakuwaje tunapokea ugeni kutoka Morocco, lakini nieleze tu kwa uzoefu wangu kwamba misimamo mbalimbali haikuzuii kuwa na *bilateral relations* ndiyo maana hata Polisario *headquarters* yao ipo Algeria, lakini bado wana uhusiano Algeria na Morocco. Vivyo hivyo sisi msimamo wetu kuhusu PLO unajulikana lakini ndiyo maana tunafungua Ubalozi Israel kwa sababu tunapokwenda kujenga uchumi wa viwanda lazima tufungue milango zaidi ya kiushirikiano na nchi ambazo zimepiga hatua katika nyanja mbalimbali, mfano nchi ya Israel wako mbali katika teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji, kwa hiyo naunga mkono sana jitihada hizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye Kamati na mimi ni Mjumbe wa Kamati, kuchanganya fedha za ziara za viongozi na fedha za Wizara zinaonyesha picha kubwa kwamba Wizara hii ina fedha nyingi, lakini kumbe fedha zile siyo za kwake, matokeo yake Wizara inashindwa kufanya kazi nyingi za msingi. Mfano mmojawapo ni ukarabati wa majengo ya Kibalozi, tuna eneo kule Maputo ambalo tumepewa na Serikali ya Msumbiji toka mwaka 1978, liko eneo ambalo ni *prime*, lakini mpaka leo halijajengwa. Sasa ni muhimu sana Serikali ikaanza kuangalia maeneo kama hayo ambayo ni *prime* lakini tumepewa zaidi ya miaka karibu 40 sasa hivi, tuone tunayafanyaje ili hata wale waliotupa wasije wakajatua kutupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu mikataba; ukiangalia katika ripoti ya Kamati mikataba zaidi ya 43 bado haijaridhiwa na Bunge na hapa niseme jambo moja, Wizara ya Mambo ya Nje kazi yake ni kuratibu masuala haya, ninaishauri Serikali tuwe na kitengo maalum kama kitakuwa chini ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Rais ambacho kitakuwa kinafuatilia masuala yote kama haya. Tumeona mikataba mingi inasainiwa, lakini Wizara za kisekta zinashindwa ku-*finalize* kuifanya ile mikataba ifikie hatua ya kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kuifikisha kwenye Bunge letu kwa ajili ya kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuondokane na jambo hilo pengine tungekuwa na kitengo maalum, kwa sababu ninavyofahamu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje hawezi kumuagiza Katibu Mkuu wa Kilimo au Viwanda na Biashara kwamba jambo hili mbona halijatekelezwa, lakini tukiwa na kitengo maalum cha kufuatilia masuala kama haya inaweza ikatusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo pia linagusa Wizara ya Fedha, wawekezaji wengi ukizungumza wanalamika sana kuhusu *double taxation* na *protection of investment*. Ukizungumza na Jumuiya za Kibalozi zinasema kwamba wawekezaji wao wangependa kuja kuwekeza lakini kwa sababu hatuna mikataba ambayo inaruhusu *double taxation* kuondolewa na

protection of investment inawa-discourage. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Fedha ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje kwa ukaribu kwa sababu hata kama tunataka kukusanya pesa tu bila kujenga misingi imara ya wapi tutakusanya tutakuwa hatuwezi kufikia malengo tunayokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho au la pili kutoka mwisho kutokana na dakika chache nilizonazo ni kuhusu wahamiaji hasa wale ambao tumewapa uraia kule Ulyankulu. Kwa kweli Serikali ya Mkoa wa Tabora na Serikali ya Wilaya ya Kaliua inatumia muda mwingi na *resources* nyingi katika kuhangaika na masuala yaliyopo kwenye maeneo yaliyokuwa ya wakimbizi ya Ulyankulu. Kwa jinsi tulivyotembelea Kamati wanasema, sijui kama lugha hii itakuwa nadhifu, lakini jambo lile ni kama vile kumbemenda mtoto, sasa ku-*deal* nalo *its very delicate*. Tumewapa watu uraia, wanataka kuwa na nchi ndani ya nchi, sasa jambo hili tujifunze wakati ujao, sisi tulikuwa nchi ya kwanza kutoa uraia kwa watu wengi duniani kwa wakati mmoja, tutizame jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Mimi ninachangia taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imezungukwa na mataifa kadha wa kadha tunayafahamu wote; Kenya, Burundi na mengine na tunafahamu kwamba pia baada ya Kenya pale mbele kidogo kuna Somalia, Sudan Kusini, kuna Sudan kuna nchi nyingine pale, Eritrea na nyingine ambazo zimekuwa na hali mbaya ya kiusalama. Pale Somalia tunafahamu kuna tatizo la Al-Shabaab kundi la magaidi ambao wanavuruga sana usalama wa nchi hiyo na siyo peke yake hata nchi jirani Kenya imekuwa inashambuliwa mara kwa mara na Al-Shabaab.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi Tanzania inaaminika mashambulizi yale ya mwaka jana au mwaka juzi pale Tanga na Mwanza walikuwa ni Al-Shabaab wamekuja ndiyo wakaua watu pale halafu wakaondoka, hatukujua imetokea nini baadaye kama walikamatwa au iliishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali ya usalama siyo nzuri kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba tuko salama, ukanda huu tuko kwenye matatizo hayo ya ulinzi na usalama. Hao Al-Shabaab inasemekana wanafanya kazi pamoja na Boko Haram ambao wako Nigeria na kuna taarifa za uhakika kwamba Al-Shabaab na Boko Haram sasa hivi wanatafuta au wameshapata silaha za maangamizi, silaha za sumu (*biological weapons*) ambazo kwa kweli kama wakizitumia hizo ni hatari kubwa sana kwa yeyote ambaye zitamfikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Silaha za Maangamizi (*Convention on Biological Weapons*) na umekuwepo muda mrefu, umewekwa pale UN nafikiri mwaka 1972 kwa nchi kusaini na ku-*ratify* na kufikia mwaka jana mwishoni nchi nyingi zimeshasaini mkataba huo na zime-*ratify*, nafikiri kama taarifa zangu ziko sahihi nchi karibu 200 zimeusaini mkataba huo na zimeu-*ratify* na zinautekeleza. Tanzania bado hatujasaini mkataba huo wa *Convention on Biological Weapons* na Mwenyekiti amesema pale wakati akiwasilisha kwamba mikataba mingi haijawa *ratified*, haijawa *signed*, sababu hazijulikani. Huu wa *Biological Weapons Convention* kwa umuhimu wake kwa nchi hii ilibidi tuwe tumeusaini siku nyingi sana na tumeu-*ratify* na tunautekeleza ili tuweze kuwa wanachama katika hiyo *convention* tupate msaada unaotakiwa linapotokea tatizo au tishio la kutumiwa kwa silaha za maangamizi, silaha za sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Waziri atakapokuwa anatoa maelezo atuambie kwa nini hatujasaini mkataba huo na kuu-*ratify*, nini kimetucheleweshwa tangu mwaka 1972 mpaka leo wenzetu wamesaini wengi tu nchi 200. Kwa nini, tumeshindwa kuusaini tunajiamini nini, tunasubiri tushambuliwe ndiyo tusaini mkataba huo au una matatizo gani, gharama labda kubwa sana au una masharti mbalimbali tujue nini kinazuia kuusaini mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa kwa mfano mkataba wa *EPA* juzi hapa, mwaka jana, hatukusaini kwa sababu kadha wa kadha za kibiashara, za kisiasa, huu wa kujikinga na silaha za maangamizi ni kitu gani kinatuzuia kusaini mkataba huu ili tujilinde zaidi na hali hiyo ambayo ni tishio kubwa sana kwetu. Tumeonja mashambulizi ya Al-Shabaab pale Tanga na Mwanza na siyo kwamba wameacha, tunasikia kila siku wanashambulia Kenya wako Somalia, kila mahali, Eritrea kule

wanakwenda wanaua watu na maeneo mengine na mengine. Kwa hiyo napenda kujua sana hili jambo kwa nini hatukusaini na kama tunausaini hauna madhara tunausaini lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa dakika tano hizi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rweikiza, tunaendelea na Mheshimiwa Anna Lupembe pamoja na Mheshimiwa Hussein Bashe kwa dakika tano tano.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninaomba niunge mkono hoja za ripoti za Kamati zote tatu ambazo zimewasilishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye nyumba za askari wetu. Askari wetu wanaishi kwenye mazingira magumu sana katika nchi yetu ya Tanzania, unaweza ukasema labda Mkoa wa Katavi wanaishi labda vibaya, hawana nyumba, hawana nini, lakini ukitoka ukienda sehemu nyingine unasema loh, afadhali kwangu kuliko sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali hizi bajeti tunazipanga ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaomba zifike kwa wakati ili askari wetu waweze kujengewa nyumba au hata kuboreshewa nyumba wanazoishi, kwa sababu askari wetu ndiyo wanaotuweka sisi kwenye mazingira ya amani na upendo katika maeneo yetu husika. Tunaomba Serikali ijipange kuangalia hao askari. Tunawapa majukumu mengi makubwa ambayo wanatakiwa watekeleze lakini mazingira yao ambayo wanaishi sio mazingira rafiki. Tunaiomba Serikali hizi bajeti tunazopitisha safari hii Serikali ijipange kujenga nyumba angalau nyumba za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeona *at least* Jeshi la Kujenga Taifa wamejengewa maghorofa sehemu mbalimbali, hapo tunaweza tukawapongeza kwa sababu wamejitahidi kwa upande mwingine, lakini kwa upande wa askari polisi bado hatujawatendea haki, wanaishi kwenye mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende upande wa bodaboda. Bodaboda ni vijana wetu ambao wanajitafutia tuseme maisha yao na maisha haya wanajitafutia kutoka vyombo hivi ambavyo vimekuja kuwarahisishia maisha yao, lakini unakuta sasa ndani ya maeneo yetu kuna baadhi ya maaskari wanawanyanya sana bodaboda. Ninaomba basi Serikali, tunajua wale ni watoto wetu tumewapa ajira, wamejitafutia ajira kupitia bodaboda, tupange mikakati ya kuwafundisha usalama barabarani kwa sababu tunaona labda wanafanya vitendo vibaya, wanakwenda vibaya, wanaumia, wanapata ajali usiku na mchana, tufanye mikakati ya kuweza kuwapa semina ili waweze kujua jinsi gani watakavyotumia zile bodaboda. Ninaomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itekeleze hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda upande wa magereza. Magereza zetu zimejaa sana; sasa mimi najiuliza, kuna wengine wamekaa kule magerezani miaka kumi, kesi zao haziishi, uchunguzi bado unachunguzwa. Tunaomba Serikali sasa hivi ifanye mikakati ya kuwatoa wale watu wenye kesi zao za muda mrefu waweze kutoka mule ndani kwa sabaabu wanakula bure, wamekaa kama vile mahabusu wengine mpaka leo wamekaa miaka sita, saba, nane hawajahukumiwa sasa wanajaza magereza na chakula kila siku tunasema kinapotea, tunaendelea kuwaweka watu ambao wanatakiwa waweze kuondoka ili magereza ile iweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama ndani ya nchi yetu. Mahakama bado, kama sisi kwetu Katavi mahakama hatuna ya Mkoa, hatuna hata Mahakama ya Wilaya huwezi ukasema kama tuna mMahakama. Tunaomba basi Serikali ijitahidi kujenga mahakama ndani ya nchi yetu ili tuweze kupata urahisi katika huduma mbalimbali za kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye Balozi zetu. Balozi zetu Wabunge wengi wamesema pesa haziendi kwa wakati. Wako nchi za nje huko wanaishi kwenye mazingira magumu sana. Tazameni Balozi zetu kuzipelekea pesa, unakuta sehemu nyingine balozi nyingine mazingira wanayoishi na lile jumba walionalo utafikiri ni gofu. Hampeleki pesa za kutengeneza majengo

ambayo yako maeneo hayo. Tunaomba Serikali, jitahidini jamani bajeti tunazopitisha, tafuteni pesa za kupeleka maeneo hayo ili mazingira yawe rafiki kwa wale watu tunaowapeleka.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Bashe dakika tano halafu atafuatia Mheshimiwa Zitto Kabwe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa, mimi nataka nichangie mambo machache na nataka nijielekeze kwenye Kamati ya Mambo ya Nje na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya usalama ina mitazamo mingi, lakini usalama wa nchi yoyote duniani huanza na raia wake. Raia ndiye mlinzi namba moja wa nchi yake. Unaweza ukawa na jeshi kubwa, lina vifaru vingi, bunduki nyingi, askari wengi lakini raia kama hawako tayari kulinda usalama wa nchi yao, nchi hiyo haiwezi kuwa na usalama, itakuwa na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitakwimu duniani, Tanzania ni moja kati ya nchi 20 za mwisho ambazo raia wake wanafuraha. Raia wanapokuwa hawana furaha, kuna mambo mengi yanayochangia. Sasa msingi wa yote haya ni nini, ni haki. Jambo la kwanza ambalo kama Taifa muhimu kabisa kulipa kipaumbele katika kuhakikisha usalama wa nchi yetu unaendelea kushamiri ili mambo mengine yaweze kufanikiwa ni haki za raia kuheshimiwa na haki hizi ni haki za kiraia, lakini vilevile haki za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano michache. Leo Bunge sisi tunapitisha sheria, nataka nitolee mfano sheria ya *SUMATRA*. Basi lenye kubeba abiria 40 ili lipate leseni ya *SUMATRA* linatakiwa kulipa shilingi 80,000. Ukiangalia *cost per unit* maana yake kila kiti cha abiria ni shilingi 2,000. Lakini bodaboda ili afanye biashara yake anatakiwa alipie *SUMATRA* shilingi 20,000 maana yake kiti kimoja kile cha abiria yeye anakilipia shilingi 20,000 hakuna haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi wa Chuo Kikuu anaenda chuoni hana uhakika wa maisha yake, mfanyabiashara anayeenda sokoni kufanya biashara yake hana uhakika wa kufanya biashara yake katika mazingira salama. Maana yake tumetengeneza sheria nyingi ambazo hazimfanyi mtu masikini kuweza kuwa na uhakika wa maisha yake, hii ni hatarishi kwa usalama wa nchi yetu. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Serikali, hakuna jambo la msingi kulliko jambo lolote kama haki za raia kuheshimiwa. Tunapoanza kujenga msingi wa kukandamiza haki za raia katika nchi, tunajenga Taifa la watu wanaonung'unika ambao hawatakuwa na uzalendo katika moyo wao, ambao hawatokuwa tayari kulipigania Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za dunia za *United Nations* za mwaka 1974, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi ya 107 katika nchi ambazo raia wake wanafuraha, leo imeporomoka, ni swali muhimu la kujiuliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kama Taifa tulikuwa na heshima yetu katika medani ya kimataifa, heshima ambayo ililijenga na kujenga taswira ya nchi hii kutokuungana na watu wanaokandamiza watu wao, leo Serikali iko katika mchakato wa kufungua Ubalozi wa Israel. Mwalimu alim-consider Muisraeli kuwa ni mkandamizaji wa haki za watu duniani ambaye amekalia kimabavu Taifa la watu wengine, sisi tumeondoka kwenye msingi uliojenga Taifa hili kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana, *African Union* kuichukua nchi ya Morocco kuiingiza katika Jumuiya ya Nchi za Afrika na sisi kama Taifa hatujatoa *stand* mpaka leo, ni jambo la kusikitisha sana kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bashe. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto Kabwe dakika saba na atamgawia heshimiwa Nswanzugwako dakika tatu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Kamati hizi ambazo ziko mbele yetu leo, nitaanza na upande wa Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1974 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Nyerere, aliwaondoa watu wawili kutoka Jeshini, Mkuu wa Majeshi na Mnadhimu Mkuu na kuwapeleka kwenye shughuli za kiraia. Mkuu wa Majeshi akawa Waziri wa Vijana na Michezo na Mnadhimu Mkuu akawa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Sukari la Taifa. Huyu ambaye alienda kuwa Waziri na baadae Balozi tayari amefanyiwa taratibu za kijeshi za kustaafishwa na kupata mafao yake inavyostahili. Huyu ambaye alikwenda kuanzisha SUDECO mpaka leo tunavyozungumza, Jeshi halijamfanyia taratibu za kustafishwa kama mwanajeshi. Toka mwaka jana mwezi Februari nimekuwa nikileta swali hapa Bungeni kuhusiana na Kanali Kashmir kuhusu haki yake ya kustaafishwa kama mwanajeshi ili aweze kupata haki, swali hilo limekuwa likipigwa danadana, napata majibu kwamba Wizara ya Ulinzi haina majibu bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo Waziri wa Ulinzi alieleze Bunge hili Tukufu, Mzee huyu ambaye sasa ana miaka 80 wanataka apoteze maisha kabla ya kupewa haki zake? Kwa sababu siyo yeye aliyetoka Jeshini kwenda uraiani, ameondolewa na Amiri Jeshi Mkuu Mwalimu Nyerere. Mwenzake aliyetoka naye Mkuu wa Majeshi wa zamani amestaafishwa rasmi wakati wa utawala wa Mzee Mkapu, tatizo ni nini kwa Kanali Kashmir?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kunaanza kujengeka hisia, Kanali Kashmir ni Mtanzania mwenye asili ya kiasia. Kuna hisia zinaendelea miongoni mwa Watanzania wenye jamii ya kiasia kwamba yeye anatengwa kwa rangi yake, wakati ni mtu ambaye alilitumikia Jeshi letu na alitumikia nchi hii kwa uzalendo wa hali ya juu sana. Kwa hiyo naomba leo Waziri wamenikwepa kwenye maswali sasa *at least* Kamati imekuja na ninaiomba Kamati pia kama majibu ya Waziri hayakutosheleza imtembelee Kanali Kashmir apate haki yake na tumuombe Mungu ampe uhai mpaka hapo aweze kupata haki yake kabla Mwenyezi Mungu hajamchukua, ana umri wa miaka 80 sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka kulizungumzia ni Sera ya Mambo ya Nje. Sasa hivi kuna tatizo kidogo, nakubaliana kabisa na ndugu yangu Mheshimiwa Chumi kwamba ni lazima Sera ya Mambo ya Nje ibadilike kuendana na wakati lakini kuna tatizo la kubadilisha misimamo bila kufuata misingi ya Sera ya Mambo ya Nje. Ni kweli tumempokea Mfalme wa Morocco hapa siyo nchi ya kutengeneza maadui lazima tutengeneze marafiki, lakini unapompokea si lazima uhoji kile ambacho umekuwa ukikisimamia kwa takribani mika 40?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu hakwenda kwenye vikao vingine vyote vya AU, vikao viwili hakwenda, inawezekana kuna maelezo ya kwa nini Rais hakuhudhuria vikao vya AU, lakini kikao cha AU kinachohusiana na kuirudisha Morocco Rais amekwenda na humu ndani Wizara ya Mambo ya Nje haijatupa maelezo yoyote kuhusiana na haki za watu wa Saharawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Azimio la Umoja wa Mataifa Azimio Namba 2285 la mwaka 2016 linalotaka kura ya maoni ya watu wa Sahara Magharibi kuamua hatima yao. Sasa juzi wenzetu wa SADC wamepiga kura kukataa Morocco kurudishwa ndani ya *African Union*. Sisi tuko SADC, tunahitaji maelezo ya Serikali tulipigaje kura yetu? Haya siyo mambo ya kuchezea, tukiacha watu wafinyange finyange Sera ya Mambo ya Nje ambayo ndiyo imetengeneza nchi hii hatutakuwa na nchi, kwa sababu ukishavunja *principles* unabaki nani wewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the same thing to Israel* mimi sipingani kabisa kufungua Ubalozi Israel, kuna watu wetu wengi Watanzania wanahitaji huduma za viza, wanahitaji huduma za kibalozi kwa ajili ya Hijja wanapokwenda Israel, lakini sisi ni waumini wa *two state solution*. Tumekwenda UNESCO, tumepiga kura, kura yetu inaendana kinyume na maamuzi yetu ya *two state solution*, kura tuliyopiga Paris tarehe 16 Oktoba mwaka jana. Tunaambiwa na Afisa wa Mambo ya Nje ambaye alipiga kura ile pamoja na Israel kinyume na maelekezo ya Wizara ya Mambo ya Nje kwamba amechukuliwa hatua, tunahitaji maelezo ya Serikali, hapa kwa sababu hizi ni *matters of principle*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungua Ubalazi Misri waligombana na Israel wana Ubalazi, *there is no problem about that*, lakini tunachokitaka ni kuhakikisha kwamba yale mambo ambayo tunayasimamia yale tusiende kinyume nayo. Ninaomba Kamati ya Mambo ya Nje na wakina Mheshimiwa Msigwa Wajumbe huko wananisikia, haya ndiyo mambo ya kwenda *kui-pin down* Serikali kwenye Kamati, kwa sababu ni *principle* atakuja mtu hapa atavuruga tu, anaweza akaanza akasema kwamba *apartheid was right*, kwa sababu tu tumevuruga vuruga misingi ambayo tunayo. (Makofi)

Jambo la mwisho napenda nimpongeze Rais kwa kufanya uteuzi wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, hii Waheshimiwa Wabunge ndiyo kazi ya Bunge. Tusingepiga kelele humu ndani na kuikumbusha Serikali kwamba kuna jambo hili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Zitto, dakika saba hizo zimeisha tunamalizia dakika tatu kwa Mheshimiwa Nsanzugwanko ndivyo walivyokubaliana.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, ningejua kama Mheshimiwa Zitto ana utamu huu ningempa hizo dakika tatu lakini ngoja niendele. Hilo la mwendelezo ni la msingi sana kwamba amemteua Kamishna na mimi nimesikia kwenye redio wakati nakuja, ni jambo jema kwamba sasa kuna chombo maalum kinashughulikia dawa za kulevya ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo mawili tu ya kwa haraka. La kwanza, ukurasa wa 35 wa kitabu hiki cha repoti kinazungumzia Sera ya Mambo ya Nchi za Nje kwamba mpaka sasa tunavyozungumza Sera ya Mambo ya Nchi za Nje inayotumika ni sera ya mwaka 2001. Nafikiri wasemeji waliopita akiwemo Mheshimiwa Zitto nimemsikia na Mheshimiwa Bashe akizungumza shida iko hapo. Kwa mujibu wa repoti hiyo ukurasa wa 35 wanasema sera mpya na mapitio ya sera hiyo ya mambo ya nchi za nje inayozingatia diplomasia ya kiuchumi na mapana yake bado haijafanyiwa kazi. Mimi nilikuwa nafikiria Waheshimiwa Wabunge hapo ndipo kwenye shida. Tuiombe Serikali kama ni kalenda ya miezi sita, ya mwaka mmoja basi wenzetu wa Mambo ya Nchi za Nje wawe wametuletea sera hiyo ambayo inafanyiwa mapitio tangu mwaka 2001, haiwezekani sera ifanyiwe mapitio tangu mwaka 2001 mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya kuzingatia diplomasia ya uchumi ndiyo masuala ya msingi ya sera mpya ambayo kila siku tunaisema lakini kwa mujibu wa taarifa ya wenzetu wa Kamati na ndugu yangu Mheshimiwa Balazi Adadi mmefanya kazi nzuri sana kuikumbusha Serikali kwamba lazima tuipe *time frame*. Kama ni miezi sita, kama ni mwaka mmoja watuletee sera hiyo ambayo imefanyiwa mapitio inayozingatia diplomasia ya kiuchumi.

Hoja yangu ya pili nimeshangaa kidogo na Waziri wa Ulinzi uko hapa nimeshangaa kidogo. Ukurasa wa 30 wa repoti hii wanasema, hatuna Sera ya Ulinzi, hilo jambo limenishtua Waheshimiwa Wabunge, kama hatuna sera ya ulinzi tumepelekaje askari wetu Congo, Darfur, Lebanon na kwingineko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate maelezo wakati Mwenyekiti unahitimisha ni kwa nini hakuna sera...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa muda wako umeisha.

MHE. DANIEL N. SANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo dakika tatu hizo.

MWENYEKITI: Tayari dakika tatu hizo. Mheshimiwa Joseph Selasini sasa anaweze kuchangia halafu baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Riziki Shahari na Mheshimiwa Abdallah Mtolea kwa dakika tano, tano.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Kamishna wa Tume ya Kuzua Dawu za Kulevya. Hiki ndicho kilikuwa kilio cha Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge walikuwa wanapiga kelele mambo ya nchi yaendeshwe kwa mujibu wa sheria na kwa sababu sisi ndiyo watunzi wa sheria ilikuwa ni muhimu kupiga kelele ili sheria iweze kufuata mkondo wake. Haikuwa dhamira ya Mbunge yeyote aliyesimama katika Bunge hili ku-*challenge* utaratibu uliokuwa unatumika na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, haikuwa dhamira ya Mbunge yoyote kubeza kazi ambayo ilikuwa inafanyika na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, lakini dhamira ya Wabunge ilikuwa kilio cha kufuata taratibu ambazo nchi imejiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiruhusu Nchi hii ikiendeshwa kwa viongozi wake kuvunja sheria tutaichana chana vipande vipande nchi yetu. Tunayo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo tunaamini viongozi wake. Waziri wa Mambo ya Ndani, Katibu Mkuu na wengine wote wanaendesha Wizara ile kwa taratibu ambazo zimewekwa.

Kwa hiyo, lilikuwa ni jambo la kusikitisha kusikia Mkuu wa Mkoa anatamka kama vile yeye ni *Arresting Officer*, watu waende wakaripoti kwake. Kila mtu mwenye akili na fahamu sawasawa, lazima alikuwa anapaswa ahangae. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alichokifanya pamoja na kwamba dhamira yake pengine kwa viwango vyake ilikuwa sahihi, lakini viongozi wa nchi yetu wasipodhibiti vitendo vya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Bwana Makonda na wengine wa aina hiyo, nchi hii inakwenda kupasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukasimama tu ukamtuhumu Askofu na Kanisa lake kwa sababu kumtuhumu Askofu ni kutuhumu Kanisa zima, ni kutuhumu wenye imani hiyo, ni kuleta fujo! Huwezi kumtuhumu mtu halafu ukasema kwamba tutampekua halafu tukigundua kwamba hana tatizo tutamuachia. Umeshamchafua, utamsafisha namna gani? DCI ndiyo ana mamlaka ya kufanya upelelezi katika Jeshi la Polisi na anasimamia makachero wote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini vita ya madawa ya kulevya imekuwa ikiendelea kwa miongo yote ya utawala wa nchi hii kwa hatua mbalimbali. Alikuwa Waziri Kitwanga hapa akatuambia ana majina 550, nina imani Mheshimiwa Mwigulu halali na hajalala anaendelea kufanya kazi hiyo, anaendelea kufanya shughuli hiyo. Isije ikajengwa hoja kwamba sasa Makonda anafanya kazi kuliko Waziri Mwigulu. Waziri Mwigulu anafanya kazi hiyo, DCI anafanya kazi hiyo lakini kiherehere cha baadhi ya viongozi vijana watafanya kazi hii isiendeleo sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo makubwa sana ya kutia shaka. Iko tuhuma inajengwa na bila shaka mmekwishaisikia kwamba Mheshimiwa Makonda sasa ana utajiri mkubwa kuliko umri wa kukaa kwake madarakani. Tunasikia amenunua *apartment* pale *Viva Tower* ya shilingi milioni 600. Mheshimiwa Rais umeingia madarakani kwa ahadi ya kwamba unapiga vita rushwa, huyu anatumia kwa kununua *apartment* kwa shilingi milioni 600, siamini kama Rais utakaa kimya. Vilevile Makonda huyu huyu anatumia amempa zawadi ya *birthday* yake mke wake Benz ya dola 250,000 sawa na shilingi milioni 400, hatuwezi kukaa kimya lazima tuseme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu huyu Makonda, Rais amezuia safari za Mawaziri, safari za Wabunge lakini amekwenda Ufaransa na mke wake, ameingia kwenye ndege daraja la *business class* dola 7,000, yeye na mke wake wamekaa siku 21. Kwa nini tusifikirie kwamba kitendo cha Makonda kutangaza hadharani watu ambao nafikiri anawatumia ilikuwa ni mkakati wa kufanya wauza madawa ya kulevya wakimbie ndani ya nchi? Kwa sababu sasa hivi ni muuza madawa gani mjinga ambaye amebaki katika nchi hii? Maana yake ni kwamba Makonda amesaidia wauza unga kuondoka katika nchi hii. Kwa sababu inawezekana Makonda anashirikiana nao na ndiyo maana sasa ana utajiri huu mkubwa kiasi hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kuwaomba viongozi wa Jeshi la Polisi, Kamishna Siro leo ameibuka anasema Mbowe asipokuja tutamfuata. Siro unamfuata kwa *summons* ipi uliyompa? Mpe

summons kwa mujibu wa sheria ili aende. Kwa sababu sasa hivi kuna kiherehere tu, kila mtu anajifanya anafanya mambo sijui kwa namna gani anavizia uteuzi au Siro unataka u-IGP? Lazima tuseme kwa sababu hakuna mtu ambaye anaunga mkono madawa ya kulevya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi nina mtoto muathirika. Kwa hiyo, kama kuna mwenye uchungu, mimi nina uchungu kweli kweli, tena tangu darasa la nne lakini Makonda asivuruge vita hii, sisi tunataka hawa watu wakamatwe. Watu hawa hawawezi kukamatwa kwa kuropoka, hawawezi kukamatwa kwa kujisifu, hawawezi kukamatwa kwa majigambo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa viongozi, sisi tunataka *succession* ya uongozi, watu wazima tunaondoka vijana waingie. Mimi namshauri Rais, vijana anaingiza madarakani aangalie busara yao. Tulizungumza hapa juu ya DC Mnyeti yule wa Arumeru, lakini leo kwenye mtandao kuna habari DC alikaa hotelini na Afisa Sheria wa Arumeru anamwambia Rais, bwana mkubwa alinipigia simu ananiambia usiwe na wasiwasi fanya kazi, hawa Wabunge wajinga tu – hee! Hapo ndipo tulipofikia Waheshimiwa Wabunge. Makonda anaenda kwa wafanyabiashara, anampigia Rais simu halafu anaweka *loud speaker* ili wafanyabiashara wasikie Rais anavyowasiliana naye. Wale wote waliokuwa wanashughulikiwa kwa kukwepa kodi leo ndiyo marafiki wa Makonda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Boniphace Getere alisema hapa, tuache mambo ya CHADEMA na CCM, tujenge nchi. Wabunge tuwe wakali kusimamia sheria za nchi hii, kusimamia *principles*, nchi yetu isonge mbele. Kama kuna ukweli tuseme kwa sababu matatizo yakitokea CCM haitapona wala CHADEMA hatutapona. Nchi hii ikipasuka CCM haitapona, CHADEMA haitapona. Nchi hii ina *hierarchy* ya uongozi, haiwezekani Siro am-*supersede DCI*, haiwezekani, iko wapi, kwa sababu Jeshi linaenda kwa *command!* Sasa DCI anachunguza madawa ya kulevya, Siro anachunguza madawa ya kulevya kwa amri ya Makonda, DCI anashirikiana na Waziri, fujo! Jeshi likiwa na fujo linasambaratika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo niseme tu kwamba sisi Watanzania kwa ujumla wetu tunajua madhara ya madawa ya kulevya, hakuna asiyejua! CCM mnajua, CHADEMA mnajua, Watanzania wote mnajua. Watoto wetu wanaathirika, watoto wetu wanakuwa na tabia za ajabu ajabu. Tushirikiane ili vita hii iweze kufanikiwa lakini vita hii isiende kwa majigambo ya mtu mmoja ambaye anajifanya yeye ni bora na anaweza kupigana hii vita peke yake, hawezi! Atawaacha wale wanaohusika wakikimbia halafu matokeo yake vita itaishia njiani. Nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Shahari na Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wajiandae.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja...

MWENYEKITI: Dakika tano wote.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze tu kwa kusema kwamba nawapongeza Wajumbe wa Kamati zote tatu kwa kazi nzuri waliyofanya lakini nitachangia zaidi taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama na Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema ufike wakati sasa hili Bunge lijione kwamba ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa hiyo zile Wizara za Muungano zipewe kipaumbele, hadhi na uzito na ustahili. Wizara ya Ulinzi na Usalama na Wizara ya Mambo ya Nje ni Wizara za Muungano lakini siku zote huwekwa pembezoni na matokeo yake haijadiliwi ipasavyo. Ukiangalia hivi vijitabu tulivyopewa cha Mambo ya Nje na Ulinzi ndiyo kibaya kuliko vyote, hata pini hazijakaa sawa, maandalizi yake hovyoyote, wakati ni mambo muhimu sana ya Jamhuri ya Muungano. Naomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi hata zile taasisi zilizoko kwenye Wizara ya Mambo ya Nje kwa mfano na zenyewe pia hazipewi uzito unaostahili. Chuo cha Diplomasia ni taasisi nyeti sana. Nchi yoyote ile taasisi inayohusika na masuala ya mambo ya nchi za nje inapewa uzito.

Chuo hiki kimekuwa chuo utadhani sijui cha kutengeneza watu gani! Hakina miundombinu mizuri, hakina vifaa vya kufundishia, Walimu wake wako *so local!* Mtu anafanya *first degree* mpaka *PhD* Mlimani pale hatoki mpaka anastaafu – huyu mtu atafundisha vitu gani jamani? Lazima walimu hawa wapewe *exposure*, wapelekwe nje, wapewe *in service training periodically* ili waandaliwe na wao waweze kuandaa *foreign service officers* wetu ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano magerezani. Wamesema waliotangulia kwamba kuna watu wanawekwa mahabusu miaka. Tumeimba kesi chungu nzima, ya Masheikh tumeisema, sasa ni miaka minne ni mahabusu, kesi hazisemwi, watu mnaambiwa kumerundikana! Serikali haiamui, Serikali haiko *serious*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Bunge haziwezeswi ipasavyo. Nilitarajia Kamati ya Mambo ya Nje ionane na wadau, miongoni mwao wawepo pia wanafunzi wetu wanaosoma katika nchi mbalimbali basi angalau hao walioko kwenye nchi jirani hapa za Afrika Mashariki. Nimesikia baadhi ya wanafunzi wakilalamika wanavyokuwa *mistreated*, bahati mbaya ni katika nchi moja jirani mwenzetu Afrika Mashariki kwamba hawa wanalipishwa ada tofauti na vile ambavyo wangelipishwa na vilevile hawapati *treatment* kama *a member country* ya *East African Community*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hiyo *Inter-University Council* ya *East Africa* ambayo inasemekana inashughulikia masuala haya, lakini ni muda mrefu sana hayapati ufumbuzi. Kwa hiyo, naamini kama hizi Kamati zingewezeshwa watu kama hawa wangeweza kufikiwa na Kamati za Bunge na masuala yao yangeweza kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kidogo kuhusu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Dakika tano?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda unakwenda, ndiyo hivyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Mtolea na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wajiandae.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kulishukuru Bunge hili kwa maana ya Wabunge wote Mheshimiwa Spika na Mawaziri kwa namna ambavyo walinfariji mimi na familia yangu wakati nilipompoteza Mzee wangu mwezi Novemba mwaka jana. Mwenyezi Mungu awabariki sana. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Ameen.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka nijielekeze kwenye taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo. Imeonesha kuna umuhimu mkubwa sana wa Serikali kutunga Kanuni na Sheria Ndogo katika kuzisimamia rasilimali lakini wakati mwingine pia kuzipatia vipato Halmashauri. Mbali na changamoto ambazo Kamati imezionesha hapa za uandishi, uchapishaji, naliona tatizo lingine kubwa ambalo lipo katika utungaji wa hizi Kanuni na Sheria Ndogo kwenye Wizara lakini pia kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la kutokuwasiliana kwamba Kanuni au Sheria Ndogo inayotungwa na Wizara moja katika kulidhibiti jambo fulani haiangalii kitu gani kinafanywa na Wizara nyingine. Kwa mfano, watu wa *NEMC* wanaweka sheria za kudhibiti ukataji wa miti kwa maana ya matumizi ya mkaa na vitu vya namna hiyo. Watu wa Maliasili na wao pia wanatunga sheria za kuhakikisha kwamba wanalinda maliasili za nchi hii. Hata hivyo, unapotunga Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Mkaa lazima uangalie Wizara inayoshughulikia mbadala wa nishati inafanya kitu gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeona hapa kwa mfano Wizara ya Nishati inasema kwamba ina gesi ya kutosha lakini kwa sasa gesi hiyo haijaanza kutumika majumbani inasubiri TPDC wajenge miundombinu ya kuifikisha gesi hiyo majumbani. Jambo ambalo kwa maana ya kuipendzesha *presentation* linavutia sana, lakini ukija kwenye uhalisia unagundua hili jambo haliwezi kutekelezeka ndani ya miaka 50 au 100 ya hivi karibuni. Kwa sababu tukumbuke kujenga tu miundombinu ya kusambaza maji safi na maji taka mpaka leo hatujaweza kueneza nchi nzima, unawezaje kutegemea ndani ya muda mfupi kwamba TPDC watajenga miundombinu ya kuisambaza gesi nchi nzima? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta yanayofanyika huku sasa yanasababisha matumizi ya mkaa yaendeleo kuwa makubwa. Sasa kule tena mnatunga Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Mkaa maana yake bei ya mkaa itazidi kupanda na anayeteseka hapa ni mwananchi. Kwa hiyo, ugumu wa maisha tunaasababisha na namna ambavyo tunasimamia hizi rasilimali zetu. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara au Serikali ingekuwa yenyewe inaangalia hali halisi ikoje kabla haijatunga Sheria Ndogo kwa ajili ya kuzuia jambo fulani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia inapotokea migogoro ni vizuri Serikali ikaenda haraka kutunga Sheria na Kanuni kwa ajili ya kumaliza migogoro hiyo. Vinginevyo inakwenda kuligawa Taifa katika hali ya kubaguana. Tazama migogoro iliyopo katika masuala ya ardhi. Ukienda sehemu ukikuta viongozi ni wakulima wanasema wafugaji wametuingilia na ukienda maeneo mengine wanasema kwamba wakulima wametuingilia. Matokeo yake tunaanza kuchukiana kwa kubaguana, huyu ni mkulima, huyu ni mfugaji. Mfugaji anamwingilia mkulima, mkulima analalamika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa mlisikia Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema migogoro hii haishughulikiwi kwa sababu Waziri wa Kilimo ni mfugaji kwa hiyo anawaacha wafugaji waendeleo kulisha kwenye mashamba ya wakulima. Sasa haya mambo ya kutosimamia vizuri rasilimali ndiyo inakuwa chanzo cha kuzibadilisha rasilimali ambazo zilikuwa neema zianze kuwa laana kwenye Taifa hili na hivi viashiria tayari vimeanza kuonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama rasilimali zetu, tuna rasilimali ardhi, gesi, madini na tuna rasilimali watu. Kwenye ardhi tayari wakulima na wafugaji wanagombana. Kwenye gesi tumeona yaliyotokea Mtwara, kwenye madini unaona wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa wana migogoro. Kwenye rasilimali watu ndiyo hivyo, mtu mmoja anaweza kunyanyuka anawaambia nyie mnauza madawa ya kulevya. Hivi ni viashiria vya kuona kwamba sasa rasilimali zetu zinageuka kutoka neema kwenda kuwa laana. (Makofi)

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Radhiwani Kikwete na Mheshimiwa Innocent Bilakwate wajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naomba nichangie kwenye Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala zima la tozo ile ya *fire*. Tunapolipia *road licence* kuna shilingi karibia Sh.30,000 mpaka Sh.40,000 zinakwenda kwenye huduma za zimamoto kwa maana ya *fire*. Sasa nataka kujua kupitia Kamati na Wizara kwamba pesa hizi zinatumiwa katika eneo gani? Kwa sababu huduma za zimamoto katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga na Mbeya bado tunaona wanatumia magari ambayo hayana uwezo wa kutoa huduma hii katika maghorofa marefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba kwa sababu pesa hizi zinakusanywa kupitia TRA na zina uhakika wa kupatikana sasa zingekwenda kuboresha huduma ya hivi vyombo vya kuzimia moto katika manispaa zote ili angalau tuwe na vyombo vya zimamoto vya kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa Jiji la Dar es Salaam ambalo sasa hivi tuna huduma ya mabasi yaendayo kasi, ni kweli tumeingia katika dunia ya ushindani wa teknolojia lakini

gari hizi zinazobeba magari yaliyoharibika kwa maana ya *breakdown* bado wanaendelea kutumia *land rover* ambazo mara nyingi zinasababisha kuharibu zaidi hata hayo magari. Kwa sababu siyo magari yote yanayovutwa na *breakdown* ni mabovu, mengine labda wame-pack katika maeneo ambayo sio sahihi, kwa hiyo wakati wanayavuta haya magari wanasababisha uharibifu kwa magari yanayovutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani kwamba yeye ni kijana wa kisasa hebu alete huu usasa katika hizi *breakdown* tupate ambazo zinaendana na wakati tuliokuwa nao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie suala zima la ulinzi na usalama hasa katika Mkoa wetu wa Tanga ambapo tulikumbwa na tukio moja ambalo lina harufu ya ugaidi. Mwezi wa Nane na wa Tisa yalitokea mapigano, watu wenye silaha walivamia baadhi ya vijiji katika Jimbo la Mlalo na Lushoto wakafikia hatua wakachoma bwani la Chuo cha SEKOMU. Kwa hiyo, ni rai yangu kwamba kwa kuwa Mkoa wa Tanga uko pembezoni mwa nchi jirani ya Kenya na tunajua kabisa kwa kule upande wa Kenya kuna tishio la *Al-shabaab*, basi nataraji kwamba zile harufu lazima zitakuwa zinapenya katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wapo askari hodari ambao wameweza kupambana katika tukio hili, kuna *Inspector Joram* ambaye mara ya mwisho alifanikiwa kukamata magaidi wawili wa Kisomali katika hilo kundi na hawa ndiyo waliokwenda kuonesha silaha zaidi ya tisa zilizokuwa zimefichwa kwenye kaburi na wakasaidia angalau kuufuatilia ule mtandao. Nitoe rai kwa Waziri mwenye dhamana awaone hawa vijana ambao wanafanya kazi nzuri waweze kupongezwa kwa sababu kazi waliyofanya ni kazi ya kishujaa na kizalendo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa upande wa magereza tunalo gereza kongwe sana linaitwa Gereza la Kilimo la Mngalo, ni miongoni mwa magereza ya mwanzo kabisa yanayojishughulisha na kilimo. Hata hivyo, gereza hili linatumika chini ya kiwango kwa sababu lina uwezo wa kubeba wafungwa 100 lakini wapo 38. Niombe kule kwenye msongamano ikiwemo Rorya, Tarime na kwingineko basi unaweza ukawasogeza huku Mlalo waweze kutusaidia katika shughuli za kilimo. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Goodluck Mlinga wajiandae.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kuniona. Kutokana na muda nianze moja kwa moja na ku-*declare interest* kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo. Katika mijadala yetu ndani ya Kamati, ndiyo maana nimekaa upande huu ili niwaone vizuri Mawaziri kwa hili jambo ninalotaka kulisema ni kwamba Mawaziri wangu na Idara ya Uandishi wa Sheria Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kuna tatizo. Sheria nyingi zinakuja haziko tayari na *reference* zinazofanyika siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta *reference* ya Sheria ya Mifugo lakini ukirudi kwenye Sheria Mama unaona ni Sheria Inayozuia Vyombo Vinavyokwenda Mwendokasi. Sasa hili si jambo zuri na wewe ni mwalimu wangu na mimi nakuheshimu sana. Hili jambo napenda kidogo tuwe makini, kwa sababu sheria hizi zinaweza kuwa katika karatasi lakini unapokwenda kuzifanyia kazi ndipo matatizo yanapoanza. Sasa tungependa jambo hili nalo tuliweke vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nieleze masikitiko yangu niliposikia wakati Mheshimiwa Adadi anatoa ripoti yake kwamba nchi yetu haina Sera ya Ulinzi. Hili ni jambo la kusikitisha. Nchi yetu ni moja ya nchi ambayo inasifika sana kwa maana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viko mstari wa mbele, tuna jeshi ambalo limekuwa *credited* kwamba ni moja ya majeshi 10 bora duniani sasa.

Kama tena jeshi letu zuri, lenye sifa, lakini sera ya ulinzi haipo tayari, tunaweza tukaingia katika matatizo makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika jambo hili, mara kwa mara tumekuwa tunalalmika sisi Wabunge hasa mimi binafsi nikieleza juu ya matatizo yanayotokea katika eneo la Kibindu, Mvomero, Kwekonje na Kimange kwamba watu wanauana lakini majeshi yetu hayachukui hatua. Tusije kufikia sehemu tukaamini kwamba kumbe kwa sababu ya kukosekana kwa sera zinazotoa uelekeo wa jinsi ya kujipanga vizuri juu ya ulinzi ndiyo maana wananchi wangu wa Halmashauri na Jimbo la Chalinze wanaendelea kufa kwa sababu hakuna hatua zozote ambazo zinachukuliwa. Naomba sana jambo hili Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ilifanyie kazi ili sera hii ije mapema iwezekanavyo ili tuweze kupanga nchi yetu vizuri kwa faida ya leo, kesho na kesho kutwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo napenda nizungumzie suala la madeni kwenye vyombo vyetu. Nimesoma kwenye taarifa na nimesikiliza Mheshimiwa Adadi akiwa anatoa taarifa yake, vyombo vyetu vinadaiwa sana. Hebu sasa Serikali tujipange tumalize madeni haya kwa sababu itafika sehemu vyombo vyetu vitakuwa havikopesheki wala kupatiwa vifaa vya kisasa kwa sababu ya uzito wa kulipwa kwa madeni hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maadili kwa taarifa yake nzuri ambayo imeeleza jinsi walivyojadili masuala mbalimbali yaliyoifikia Kamati. Hata hivyo, jambo moja ambalo napenda niwaeleze wenzangu na hasa Mwenyekiti wetu ni kwamba mimi walionifundisha maisha walinifundisha kujiheshimu kwanza kabla wenzako hawajakuheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo ama tusipokuwa na *philosophy* ya namna hiyo kila siku kazi yetu itakuwa ni kupigishana makelele kama ambavyo unaona leo hii Wabunge wanasema ya kwao, huko Serikali inasema ya kwake, kunaonekana kama kuna mgogoro baina ya makundi haya mawili jambo ambalo linahatarisha hata usalama wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ulinambia unanipa dakika tano nisingependa kuzama sana kwenye mambo mengine niwaachie wenzangu nao waendeleo kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nipongeze Kamati zote. Hata hivyo, kabla sijaanza kuchangia, naomba nieleze jambo hili. Suala la vita ya madawa ya kulevya ni janga la Kitaifa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba mtu yeyote anayesimama kuanza kupambana na vita ya madawa ya kulevya aidha awe ni mwizi au vyovyote atakavyokuwa kwa pamoja tuungane mkono na tumuunge mkono mtu huyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo mimi nimekuwa nikijuliza, hivi huyu Makonda mali wanazosema alikuwa nazo kabla hajaanza kupambana na vita ya madawa ya kulevya mbona hamkumleta Bungeni? Waheshimiwa Wabunge tuwe makini kuna mchezo unaendelea na huu mchezo tuugundue, tuukatae, tuungane na Makonda kwa nguvu zetu zote kupambana na vita ya madawa ya kulevya. Mlikuwa wapi? Kwa nini hamkumleta Bungeni kusema ni mwizi, kusema ana mali kibao? Huo mchezo tumeugundua na hatukubali tunaungana na Makonda kama ana upungufu, atawajibika kwa upungufu wake, lakini vita ya madawa ya kulevya tutaendelea naye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niongelee suala la ulinzi na usalama. Niombe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani tuangalie mazingira wanayofanyia kazi ya jeshi letu la polisi kwa kweli sio mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sisi ambao tuko pembezoni tunaomba kwa kweli ulinzi uimarishwe kwenye mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Dokta Sware Semesi na Mheshimiwa Aida Joseph ajiandae.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia muda huu na mimi nichangie machache niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, jamani Waheshimiwa Wabunge sisi tumechaguliwa na wananchi kwa ajili ya kuwasaidia. Sasa basi tunaposhangilia hapa na tunapopitisha hivi vitu viwe kwa ajili ya maslahi ya wananchi. Kila Kamati iliyosimama hapa ilikuwa inalalamika kuhusu ufinyu wa bajeti. Bahati nzuri sasa hivi imeturudia sisi wenyewe na hii iwe fundisho kila kitu kinachokuja mnapitisha. Mimi ingekuwa amri yangu hizi meza zingekuwa za chuma ili kabla mtu hajapiga awe anafikiria maumivu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Kamati imepewa bajeti ya shilingi milioni 10 kwa ajili ya safari za nje. Jamani hebu tujulize Kamati ya chini kabisa ilikuwa na watu sio chini ya 18, hivi shilingi milioni 10 unaenda nchi gani, unatumia usafiri gani, bajaji? (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kitu ambacho nime-experience katika hizi Kamati kuwa Serikali inapokuja kujibu, inakuja timu ya watu 30 anayeongea ni mtu mmoja. Jamani huu ni ufujaji wa fedha hizi za wananchi kwani hamna kazi nyingine? Utakuta wanakuja wengi anajibu mtu mmoja, nusu saa halafu mistari yenyewe miwili wanaondoka, VX 8 zimekuja. Jamani huu ni ubadhirifu wa fedha za Watanzania. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu ni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje, sasa hivi kila mkoa unaoenda unakutana na Wachina. Jamani hawa Wachina nawahakikishia tukianza kukutana nao *labour ward* haki ya Mungu nchi hii mwaka 2030 tunafanya sensa wao watakuwa wengi kuliko sisi. Kwa hiyo, Wizara ya Mambo ya Nje, naomba mliangalie suala hili. Wako Wachina wanaishi hawana *passport* hawajui viza ndio nini, wanaingia tu lakini sisi kwenda kwao wanatudhibiti. Kwa hiyo, naomba mliangalie suala hili. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo tulifanya ziara kwa Mpiga Chapa wa Serikali. Jamani Mawaziri, namwomba Rais aende katika Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali, sijawahi kuona ofisi mbovu kama ile yaani ukienda huwezi ukategemea kama wanafanya kazi ya *printing*, haina tofauti na *station* ya TAZARA au ile *station* kubwa. Kwa hiyo, naomba Rais aende akatembelee pale, ina hali mbaya. Hawafanyi kazi yaani wakiletewa ku-*print* kazi ya Serikali wanaenda ku-*print* kwa Wahindi sasa siri za Serikali zinakuwa wapi tena? Siri si zinavuja huko mitaani halafu tunalalamika Serikali yetu haina siri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne, jamani mimi Mlinga sipingi vita dhidi ya madawa ya kulevya. Ninacholalamika na kulaani ni mtu kutumia madaraka yake kupigana vita binafsi kuigeuza kuwa vita ya Kitaifa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kweli! (Makofi)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho ninachopinga. Mimi Mlinga niko tayari kusimama mbele ya Rais kumwambia chanzo cha vita hii. Kumwambia ukweli, vita haijaanza kwa ajili ya madawa ya kulevya, vita imeanza na ugomvi binafsi, baada ya kuona ita-*backfire* wakaigeuza kuwa vita ya madawa ya kulevya. Niko tayari kusimama mbele ya Rais achunguze chanzo ni nini? Wale wasanii waliowekwa ndani chanzo kilikuwa nini, haikuwa vita dhidi ya madawa ya kulevya. Niko tayari kusimama mbele yake kumwelezea aangalie ukurupukaji huu utatusababishia uvunjifu wa amani Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmemtaja Gwajima ana watu, mmemtaja Mbowe wa CHADEMA watakaa pembeni, mtawataja akina Manji watu wa Yanga watakaa pembeni. Jamani

uchungu wa mambo haya, kama una familia ukija kutajwa utayaona machungu yake, siyo rahisi hivyo mnavyofikiria. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii umeniharibia heshima yangu mimi Mlinga na nina wananchi wangu kule Ulanga, nina mke wangu ana ndugu zake, nina watoto wangu wanasoma shule, hivi watoto wangu wanatembeaje huko walipo jamani. Leo hii nimekutaja wewe unahusika na madawa ya kulevya, hivi watu wanaonifahamu wanatembeaje huko waliko? Jamani haya mambo myasikie yasije yakawakuta. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amemteua IGP, Waziri wa Mambo ya Ndani, jamani mbona mko kimya, hamna shughuli za kufanya, kwa nini mnaachia watu wanadhaliishwa? Nchi yetu ina wakuu wa mikoa 25, nime-experience kinachoanzia Dar es Salaam Wakuu wa Mikoa wote wanafuata. Hivi kila Mkuu wa Mkoa akisimama akianza kufanya yale yanayofanyika Dar es Salaam jamani tutakuwa wapi? Kwa hiyo, tufikirie vitu kabla ya kufanya. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema sisi Wabunge siyo kwamba tunawaonea watu wivu. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Joseph, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi na Mheshimiwa Cecil Mwambe wajiandae dakika tano tano.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo na taarifa zote zilizowasilishwa. Siko mbali sana na wajumbe waliotangulia, kwanza nampongeza Mheshimiwa Goodluck kwa mara ya kwanza ameonesha ukomavu wa kisiasa kwamba msimamo wake unabaki pale pale. Kila mhimili unapaswa kuheshimiwa na lazima tulisimamie hilo, hatuwezi kukubali. Kuna kitu kimenishangaza sana, Maazimio ya juzi tu hapa lakini naona kuna watu wameanza kugeuka, Bunge hili hili, juzi tu hapa, kuna nini kimetokea? (Makofi)

MBUNGE FULANI: Njaa!

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tutaendelea kusema ukimtumumu mtu ambaye ana watu wengine nyuma hujamtumumu yeye, tunachokizungumzia sisi ni kwamba sheria zifuatwe. Kuna watu wanaohusika na hayo mambo wafuate utaratibu, sheria ziko wazi. Makonda hawezi kumwita mtu yeyote angeagiza Jeshi la Polisi lifuate utaratibu kuwaita hao watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika mazingira ya kawaida kama kuna Mbunge ametuhumiwa, sisi tulivyoambiwa tunalala msifikiri ni mtu mmoja alisikia, ni wananchi ambao wako nyuma yetu wamejua kwamba sisi tunalala usingizi. Sasa kama tunakubaliana na Makonda kwamba kweli tunalala usingizi, kiukweli mimi binafsi kama Aida, sisi Wafipa tuna misimamo yetu, mimi siwezi kukubaliana hata siku moja. Kama kuna mtu anajua amefanya vizuri kwa kusubiri uteuzi, sisi wengine hatuubiri uwaziri hata siku moja hatuubiri, tutasimamia ukweli. Kama kuna watu wanafanya hayo mambo hakuna mtu anafurahishwa ila afuate utaratibu mambo mengine yaendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye taarifa ya Kamati, niongelee kuhusu Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Ndugu zangu Wabunge pale ndipo sheria zinachapwa, mtu yeyote ambaye unahusika na mambo haya ukienda kuona pale na ukaacha unafiki, ukatimiza wajibu wako kama Mbunge utaelewa hiki ninachokizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia Mheshimiwa Jenista Mhagama kama kweli kuna utumbuaji kitu gani kinazuia kumtumbua yule mtu pale kwa sababu mambo yako wazi kabisa inakuwaje siri za Serikali zinakwenda kutolewa nje, kuna kitu gani kinaendelea? Tunaishauri Serikali ifanye utaratibu unaowezekana, kama mmefanya haraka kuhamia Dodoma mpaka kwenda

kwenye Chuo cha UDOM, fanyeni haraka kutafuta utaratibu wa kudhibiti mazingira ya pale, kwa sababu tu moja, kwa maslahi ya nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la wanasheria wetu, yawezekana shida ni taaluma waliyo nayo au hakuna utaratibu wa kuwaangalia hawa wanasheria wa Halmashauri jinsi wanavyowajibika. Kuna watu wamehukumiwa kwa sheria hizi za Halmashauri ambazo ziko kinyume kabisa na sheria mama. Tunaishauri Serikali kuna kila sababu ya kufanya semina kwa hawa wanasheria wa Halmashauri kama kweli tuna nia njema. Kwa sababu yawezekana wanafanya kwa kutojua au kwa makusudi kwa sababu wanajua mmewatelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukiangalia hata kesi nyingi za Halmashauri, nimewahi kukaa siku moja nikajiliza kwa nini kesi nyingi za Halmashauri tukienda mahakamani tunashindwa? Kuna mambo mawili hapa, yawezekana wanasheria wenyewe wanapiga deal na hawa watu waliopeleka kesi mahakamani au Wakurugenzi wanapokuwa wanafanya shughuli zingine wanashindwa kuwashirikisha wanasheria. Haya mambo lazima tuyatazame kwa maslahi ya Taifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Aida. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Silinde wajiandae dakika tano tano.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nitatoa maoni yangu na mapendekezo katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Kabla ya kutoa mapendekezo yangu nataka turejee katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara 63(2) kujikumbushia tu Waheshimiwa Wabunge. Sehemu hii inasema kwamba:-

"Bunge litakuwa chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii". (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kusema haya au kujikumbushia nini kinatuongoza katika nchi yetu kama Wabunge? Nina muda wa mwaka mmoja na zaidi hapa Bungeni, nikizingatia haya tuliyoambiwa, lakini ukiangalia mwenendo wetu nimeona kuna upungufu kwa jinsi ambavyo tunaishauri na kuifuatilia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasimama hapa Mbunge mmoja mmoja tunatoa mapendekezo yetu kwa Wizara husika, tunatoa mapendekezo yetu kama Kamati husika lakini sisi tunaotoa hayo mapendekezo hatufuatilii utendaji, hakuna *accountability* upande wa pili. Waziri atakuja kujibu atasema sawa nimepokea au sawa hili sikubaliani nalo au hili nitalifanyia kazi lakini ukija mwaka unaofuata au Bunge linalofuata hatujui nini kimetekeleza au kama kweli kimetekelezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano dhahiri, mwaka 2013 au 2014, kuliundwa Kamati Maalum ambayo ilikuwa inachunguza na kuleta mapendekezo juu ya hii migongano baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na mambo ya ardhi. Kamati ile ilitoa mapendekezo mazuri sana kwa Serikali lakini huu ni mwaka 2016 bado tunaongelea lugha hiyo hiyo. Kamati zinatoa mapendekezo hayo hayo hatuoni *accountability* kutoka upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine pia sisi ambao tulikuwa mtaani by then tulikuwa tunasikia kuhusu *ESCROW, RICHMOND*, Kamati zilitoa mapendekezo yake lakini sisi tuliotoka mtaani na sasa tumeingia Bungeni hatujui haya mapendekezo yaliishia wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kushauri, Kamati kama itaona inafaa waongeze katika mapendekezo yao kwamba Bunge linatakiwa liwe na *special monetary and evaluation plan*, mikakati ya kutathmini tunachokipendekeza kwa Serikali au tunachokishauri kwa Serikali je kinatekelezeka na kinatekelezeka kwa wakati gani. Hii itatusaidia kama Serikali yetu kuzipambanua hizi changamoto na ku-move forward. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza hapa na pale nikaambiwa wakati uliopita Bunge lilikuwa na kitengo cha kufuatilia ahadi za Serikali Bungeni, *the government assurance unit*. Sasa nataka kujua hiki kitengo kilikufa au kwa nini hakifanyi kazi kikatuambia ili tusiwe tunajirudiarudia kama Kamati au kwa Mbunge mmoja mmoja kushauri au kupendekeza mambo yale yale kila wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili napenda kugusia kwenye mambo ya maadili kwa Kamati hii husika. Nimesoma *booklet* nikaona muundo wa Kamati, ina wajumbe 10 kutoka Chama Tawala na wajumbe sita (6) kutoka upande wa Upinzani. Sasa maadam hii Kamati ni *special* siyo kama Kamati nyingine inayoshughulikia maadili ya Wabunge, napendekeza ingekuwa ina 50-50 *chance* ili kuwe na uwazi au kusiwe na upendeleo wa aina yoyote hata na hao wajumbe wahusika wawe na mawazo mbadala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilichokiona kwa Wabunge wenzetu waliopewa adhabu mbalimbali, *evidence* gani zilitumika? Hata vyombo vya habari, waandishi wetu wa habari wako hapa ndani, kukitokea tafrani humu ndani utaona upande wa Upinzani ndiyo unaoshutiwa kwamba wamefanya fujo. Hata hivyo, *in every action there is a reaction* yaani kwenye kila tukio lazima kuna sababu nyuma yake, lazima kuna mmoja...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Shabani Shekilindi wajiandae.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Katika dakika zangu tano nitatumia dakika mbili na nusu na mbili na nusu ntampatia Mheshimiwa Sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifupi tu nimwambie kaka yangu pale Mheshimiwa Bilakwate kwamba kwa kumtetea Makonda, Makonda siyo mamlaka ya uteuzi. Kwa hiyo, anatwanga maji kwenye kinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nataka kuona Bunge hili linavyoweza kushauri Serikali hasa kwenye mamlaka ya uteuzi. Tumeshuhudia sasa hivi kama tulivyosikia Wakuu wa Mikoa wanaamua tu kukurupuka na kutoa maagizo, kama alivyotoka kusema Ndugu yangu Mheshimiwa Mlinga hapa. Tumesikia pia Mkuu wa Mkoa wa Mtwara naye na nimeona mimi mwenyewe meseji jana, naye anaanza kuwambia watu kama wanafahamu watu wanaoshughulika na madawa ya kulevya basi wamtaarifu ili na yeye apate kiki kwenye vyombo vya habari kama ilivyofanyika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi huu ni uvunjifu wa maadili ya viongozi. Tumeona hapa Bunge likiwa haliheshimiwi, Wabunge wanakamatwa muda wowote, mimi mwenyewe ni mwathirika. Mkuu wetu wa Mkoa wa Mtwara alitoa taarifa kwa kuagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama Wabunge watatu wa Wilaya ya Masasi tukamatwe kwa sababu hatukutaka kuhudhuria mkutano wake aliokuwa anataka kujadili mambo ambayo Waziri Mkuu tayari alikuwa anayafanyia kazi. Bahati nzuri viongozi walituheshimu wakakataa kutekeleza maagizo yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kifupi tuone Bunge sasa linasimamia misingi yake. Tusipoweza kuishauri vyema Serikali hasa mamlaka ya uteuzi, tumwachie pia Waziri wa Mambo ya Ndani afanye kazi zake na Mawaziri wote wafanye kazi zao. Wateule wa Rais wameonesha kama wao ndiyo watu muhimu sana kwenye Taifa hili kuliko hata Mawaziri ambao wana mamlaka makubwa kimsingi kuliko Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata hofu kwa sababu vurugu kubwa zaidi zitatokea kuanzia mwakani. Hawa wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ni walewale ambao walikuwa makada na wanataka kwenda kugombea nafasi mbalimbali katika majimbo yao hasa zaidi Ubunge. Kwa hiyo, tutafika wakati misugvano au mivutano itakuwa mikubwa sana katika maeneo yetu, tuliangalie hili jambo kwa wema.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Dakika zako mbili na nusu zimeisha, naomba tumpe Mheshimiwa Sugu hizo dakika mbili na nusu zilizobakia.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Mkoa aina ya Makonda ndiyo wanafanya nchi iyumbe kiasi kwamba mitaani sasa hivi watu wanasema nchi ina Marais wawili, wanakurupukia mambo. Tumeujenga muziki wa Bongo Flewa kwa zaidi ya miaka 25 mpaka leo unatoa ajira halafu mtu kwa kutaka sifa tu anasimama kwenye *podium* anavuruga kila kitu kwa muda wa dakika 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu kama hivi haviwezi kukubalika na ndiyo maana tunasisitiza umuhimu wa viongozi wote ambao ni *presidential nominees* wafanyiwe *vetting* na Bunge. Mtu kama Makonda angepita kwenye Bunge hili kufanyiwa *vetting* asingepita kwa sababu kwanza hana adabu alimpiga Mzee Warioba, wote tunakumbuka na picha ipo. Mtu aliyempiga Waziri Mkuu Mstaafu na Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya Mwalimu Nyerere, anamkunja, leo hii unampa kazi nyeti kama Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni makosa makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anatuhumu watu, kama kutuhumu watu yeye Makonda anatuhumiwa kwamba ni mtoto na yeye tumwambie kwamba aende kwa Mganga Mkuu wa Serikali akapimwe marinda. Kwa sababu tufike mahali tuendeshe nchi kwa misingi. Waziri Mkuu upo, Waziri wa Mambo ya Ndani upo, Mawaziri mpo, Waziri wa Sheria upo, Serikali ipo, sasa hii nchi tunaipoleka vipi, tunaipumbisha. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuliheshimu Bunge ndugu zangu. Bunge liheshimike sana, hatutajenga viwanda kwa kumkamata Mheshimiwa Lissu na kumfunga kila siku na kupata dhamana. Hatutajenga viwanda kwa kumweka Mheshimiwa Lema *detention* hata kama atakaa kule ndani miaka kumi iko siku atatoka kwa sababu Mandela alikaa kwa miaka 27 na akatoka. Ndugu zangu, hii nchi ni yetu sote, tunaipenda, tunaomba sana tusikilizane, kama walivyosema waliotangulia kwamba sasa mambo ya CHADEMA, CCM yakae mbali tuwatolee macho na tuwakaripie watu kama Makonda, wanakuja hapa wanavurugavuruga nchi wakati nchi ilikuwa inakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Sawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Shabani Shekilindi na Mheshimiwa Daniel Mtuka wajandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bunge limekuwa kila siku moja ya ajenda yake ni kupata semina elekezi kupeleka kwa ma-RC pamoja na ma-DC. Lengo la hizi semina ni kwa sababu ya haya mambo yanayotokea, haya tunayoyasema kama hawa watu wangepatiwa semina elekezi wakajua mipaka ya mamlaka yao naamini yasingetokea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *mercury* ina tabia moja, ukiifukia chini ya ardhi hata kama ni kilometa tano chini ya ardhi, itapanda itaibuka juu. Sasa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ana tabia za *mercury* yaani ananyanyuka. Hali iliyopo sasa hivi ni kwamba yaani akitoka Rais anayefuatia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam yaani Waziri wa Mambo ya Ndani hayupo, IGP hayupo, Waziri Mkuu hayupo, hakuna mtu yeyote, Bunge kama mhimili halipo, yaani imefikia mahali...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Naomba ukae Mheshimiwa Silinde, Kuhusu Utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya 67(1), Kanuni ya 64 kwenye vipengele vyake vidogo. Mimi naona mjadala huu sasa hoja ambazo haziko Mezani ndizo zinazozungumzwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kusema jambo hili kwamba tunapozungumza mgawanyo wa madaraka ya utendaji wa kazi na hasa kwa kuzingatia Katiba inayomruhusu Mheshimiwa Rais kugawa madaraka yake kwa watu ambao wanamsaidia kufanya kazi, yanapotokea mambo yoyote yanayowahusu wale waliopewa madaraka basi yasihusianishwe na mhimili huu mkubwa ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hilo la kwanza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaporudi tena kwenye Kanuni ya 64 yapo mambo ambayo yanakatazwa. Mheshimiwa Silinde anasema sasa Mheshimiwa Makonda ndiye anayefuata kwa kutenda kazi baada ya Rais...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo sahihi, tuna Makamu wa Rais na tuna Waziri Mkuu bado wanaendelea kufanya kazi kwenye nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Makonda kama anafanya vitu vyake hivyo vingine havijadhihirisha kwamba hakuna Makamu wa Rais wala Waziri Mkuu katika nchi yetu ya Tanzania. Naomba Mheshimiwa Silinde ajielekeze kwenye hoja na asitake kuwaaminisha Watanzania kwamba Makonda sasa amechukua madaraka ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa!

TAARIFA

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri wa Nchi kufuatia maelezo ambayo ameyatoa hapa kumwelezea Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Silinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna incidences tatu ambazo zinathibitisha ambayo Mheshimiwa Silinde anayazungumza. *Incidence* ya kwanza, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliwahi kutamka na kumuamuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na masuala ya shisha. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mpole siku ile alionesha hasira zake kwa kumwambia afanye kazi yake na asiingilie kazi za wengine, hiyo ni ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam siku ya kufungua mradi wa mwendokasi alizungumza mbele ya Rais, kwamba yeye, tena kwa dharau, angekuwa Waziri wa Uchukuzi mambo ambayo yanaendelea yasingefanyika. Katika hali ya kawaida ya kiuongozi na kwa watu ambao wamepitia mafunzo ya uongozi, Rais alitakiwa palepale amuonye kwa sababu ya kulinda heshima ya Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam yuko *on record* kumuagiza Makamu wa Rais na nimesahau moja la nne, RAS wa Dar es Salaam...

MWENYEKITI: Fanya kwa ufupi Mheshimiwa!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho hili. RAS wa Dar es Salaam alikuwa anatakiwa ku-appear mbele ya Kamati ya LAAC. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akagoma asiende. Wabunge waka-communicate na Waziri. Waziri wa TAMISEMI akamuomba kwamba yule RAS aende lakini Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akamkatalia Waziri wa TAMISEMI ambaye katika hali ya kawaida ndiyo mkuu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mifano hii minne, Mbunge wa Momba, Mheshimiwa Silinde amekosea nini kiutaratibu kuonesha kwamba Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo namba mbili? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Yes!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, umemkalisha Mheshimiwa Mbunge mapema, naomba tu kusema kwamba naendelea kumpa taarifa Mheshimiwa Zitto...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunamsikiliza Mheshimiwa Zitto watu wote tulikuwa tumetulia. Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema, Katiba yetu Ibara ya 34(4)...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama tulivyowaheshimu na wao waheshimu kwa kusikiliza michango ya watu wengine.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane ili tumalize kwa uzuri tafadhali!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 34(4) inampa madaraka Mheshimiwa Rais kukasimu madaraka yake kwa viongozi wengine. Kukasimu madaraka alikokufanya Mheshimiwa Rais hakuhalalishi matendo ya wale waliokasimiwa madaraka, yanaelekeza kwamba yale ndiyo maagizo ya Rais katika utekelezaji wa kazi kwenye nchi yetu ya Tanzania.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Silinde aniambie hapa ni wapi Mheshimiwa Rais amesema na kutamka na kumwapisha Makonda kwamba ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Silinde waniambie ni wapi Mheshimiwa Rais...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

mHE. SAED A. KUBENEA: Kuhusu Utaratibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Amemwapisha Makonda kuwa Waziri...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Makonda kama analo tatizo...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Ahukumiwe kama Makonda.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jenista tumeelewa na naomba ...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Katika mjadala huu Mheshimiwa Rais hajafanya mabadiliko ya Serikali yake.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista, tumeelewa nafikiri utaratibu umeeleweka.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kulisimamia hili...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Tunajua hajafanya mabadiliko!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Na si sahihi kuendelea kuwaaminisha Watanzania kwamba Mheshimiwa Rais amekasimu madaraka ya viongozi wakubwa wa nchi hii kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Ahsante. Naomba tusikilizane tafadhali, tujielekeze kwenye hoja tumalizie na Mheshimiwa Silinde. Naona sasa hoja inaondoka tunakwenda kwingineko. Utaratibu ni kwamba nadharia ndiyo mnayozungumza na kiuhalisia sivyo, ndiyo anavyosema Mheshimiwa Jenista. Naomba tuendelee Mheshimiwa Silinde ili tumalizie kazi yetu.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana...

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuheshimiane ili tumalize kwa salama, Mheshimiwa Silinde naomba umalizie muda wako.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni vizuri nikali-clarify kidogo. Nafikiri Mheshimiwa Waziri hajaelewa au hajanisikia vizuri, hata akirudi kwenye *Hansard* ataona kitu ambacho nimekizungumza. Ninachokifanya hapa ni kutetea Baraza la Mawaziri pamoja na Waziri Mkuu, ndicho ninachokifanya hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM kabla ya mwaka 2015 ndiyo chama kilichokuwa kinasifika kwa *protocol*, chama ambacho kilikuwa kinajua kiongozi gani afanye nini kwa wakati gani, suala la *protocol* lilikuwepo. Hata hivyo, sasa hivi *protocol* ile ambayo tulikuwa sisi wachanga wa vyama tunajifunza kwenu leo haipo kabisa, *protocol* imevurugika, hicho ndicho nilichokuwa nakielekea. Ndiyo maana nikasema ni kama vile, yaani mambo anayoyafanya ni kama vile anaona kama hakuna Waziri Mkuu, tena nimetumia neno ni kama. Wewe leo unakuta mtu ana-suspect mtu mmoja, huyohuyo ana-arrest, huyohuyo ana-interrogate, huyohuyo anahukumu *just one person!* Hakuna utaratibu huo katika nchi hii! Ndiyo maana ya hiki tunachokifanya hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kitu kimoja, Rais anasikia, Wabunge tumelalamika kuhusu Tume leo ameteua Tume, anasikia. Rais akishauriwa vizuri mimi nina uhakika, akishauriwa vizuri kwa mawazo mtangamano akayasikiliza, atakuwa *the best President* lakini Rais akisikiliza mawazo ya upande mmoja hawezi kuwa Rais mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya hapa tunataka Bunge kama mhimili ufanye kazi yake na tunataka Mawaziri wafanye kazi yao. Mimi niwapongeze, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa busara uliyoionesha, nakupongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani kwa busara uliyoionesha katika kipindi hiki, hii lazima tupongeze, nampongeza sana Kiongozi wa Upinzani pamoja na IGP kwa busara waliyoionesha. Wangukuwa hawana busara nina uhakika sasa hivi hili jambo lingekuwa limesharibu utaratibu wote wa nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema kwamba hatutaki mgongano wa haya mambo. Ndiyo maana tangu mwanzoni nikaelezea tabia ya *mercury* ukiidumbukiza hata kilometa tano itanyanyuka sasa hizi tabia ndiyo wanazo watu. Sisi tuliokwenda Jeshini kule tunafahamu zile 22 *critics*. Sasa tunachotaka wapelekeni na hawa vijana kule Jeshini wakajifunze, wapeni semina elekezi, kinyume na hapo mnaharibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wasanii, mmejadili kuhusu wasanii, tumewatumia kwenye kampeni za uchaguzi pande zote mbili, leo unawalipa wema kwa ubaya watu ambao wamezunguka nchi nzima kufanya kampeni kwenu. Wafanyabiashara waliochangia vyama vyetu vya kisiasa kwa ajili ya kushinda uchaguzi leo unawalipa wema kwa ubaya, hatuwezi kuendesha nchi katika huo mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ya Taifa letu kama Tanzania au moja ya sifa kubwa ya Tanzania ni utu, kuheshimiana, busara, hekima na kusikilizana. Hayo ndiyo mambo ambayo

tumekuwa tukiyahitaji, ndiyo misingi ya Utanzania. Kwa hiyo, tunachokifanya hapa siku zote tunataka muende mkamrekebishe Mkuu wa Mkoa asijigeuze yeye mamlaka zaidi ya Bunge...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde umeeleweka.

MHE. DAVID E. SILINDE: Hatuwezi kukubaliana na jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunafunga mjadala sasa kwa Wabunge tunaelekea kwa Waheshimiwa Mawaziri na tutaanza na Mheshimiwa Dokta Susan Kolimba, Mheshimiwa Injini Masauni, Mheshimiwa Dokta Mwinyi na Mheshimiwa Mwigulu atamalizia.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mtuka amesahaulika.

MWENYEKITI: Muda umemalizika, naomba tafadhali tuendele tu na Mawaziri.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwakajoka amesahaulika!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dokta Kolimba!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nichangie hoja ya Kamati inayotusimamia ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Adadi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuwasilisha kwa ufasaha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati yake hususan masuala yaliyotekelezwa na Wizara yangu katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua na kushukuru mchango wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati katika kipindi chote ambapo wamewezesha Wizara yangu kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi na weledi. Wizara yangu kwa kuzingatia ushauri na miongozo ya Kamati yetu katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, imeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake pamoja na malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yamewezekana kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Wizara, Kamati yetu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Wizara ya Fedha, Wizara za kisekta, taasisi za Serikali na sekta binafsi. Ni dhamira ya Wizara yangu kuendelea kutekeleza dhima ya Hapa Kazi Tu kwa ufanisi na weledi ili kuwezesha nchi yetu kufikia maelengo na matarajio yake ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani zangu, naomba sasa kuchangia baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo ya Kamati na ambayo yameletwa katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ilikuwa ni mapendekezo ya Kamati ambapo ilikuwa inashauri kwamba Serikali itoe fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyo idhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma ya Serikali kuhusiana na miradi. Ushauri huu umepokelewa na Wizara yangu na itaendelea kupeleka fedha katika miradi ya maendeleo iliyopangwa kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda tu kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilitengewe kiasi cha shilingi bilioni nane kwa ajili ya bajeti ya maendeleo na hadi kufikia Februari, 2017 Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni 3.4

ambayo ni sawa na asilimia 43.62. Kiasi cha shilingi bilioni 2.1 zimepelekwa Ubalizi wa Stockholm (Sweden) na shilingi bilioni 1.3 zimepelekwa Maputo, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kukosekana kwa Balozi Ndogo na Uwakilishi wa Heshima kwenye baadhi ya miji yenye fursa nyingi za kiuchumi kunaathiri malengo ya Serikali ya kukuza uchumi wa nchi kupitia diplomasia ya uchumi, hilo sisi tunalipokea na tunakubaliana na jinsi Kamati ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nitoe tu *status* ya sasa hivi kwamba Mheshimiwa Rais ameweza kuruhusu kufungua balozi sita mpya ambazo ni katika Miji ya Doha (Qatar), Ankara (Uturuki), Tel Aviv (Israel), Seoul (Korea Kusini), Khartoum (Sudan) na Algeria (Algiers). Aidha, Serikali inatemegea kufungua *consular* zifuatazo ambazo ni za Balozi Ndogo katika Miji ya Lubumbashi - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lagos - Nigeria na Guangzhou - China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tatu ambalo lilikuwa linahusu APRM Tanzania kutokuwa na hadhi ya kisheria yaani kwa Kiingereza *legal entity*. Tunaweza kusema tu kwamba Wizara pamoja na taasisi hii ya APRM tulishawasilisha nyaraka katika Ofisi ya AG naye ameipitia na kwa sasa hivi imepelekwa katika Wizara ya Utumishi ili na wao waweze kuichambua na kuangalia upangaji wa muundo wa taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika Taasisi ya APRM ya Afrika kwamba yanapunguza hadhi ya nchi yetu mbele ya jamii ya kimataifa, Wizara inatambua umuhimu wa kulipa kwa wakati michango katika mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama. Wizara imekwishawasilisha orodha ya michango inayotakiwa kulipwa kwa ajili ya kutatua changamoto ambayo imetajwa na Kamati na sisi kama Wizara tutaendelea kufuatilia Hazina kuhusu ulipaji wa michango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalohusu APRM kutoa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu faida zake. Hili sisi tunapokea mchango wa Kamati na ushauri wake na tutafanyia kazi na tutahakikisha katika bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018 tuweke hilo ili tuweze kusimamia vizuri jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida, ya maendeleo, kunachangia Chuo cha Diplomasia kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hali inayoweza kusababisha chuo hicho kufutwa na usajili wa NACTE. Tunachoweza kusema ni kwamba Serikali inaendelea kuongeza bajeti ya Chuo cha Diplomasia ili kukidhi mahitaji ya NACTE. Pamoja na juhudi hizo kwa taarifa napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara kwa kupitia mahusiano yake mazuri na nchi rafiki imeingia makubaliano na nchi ya Kuwait ili kukiwezesha chuo katika nyanja ya kukijengea uwezo hususani...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu mengine nitawasilisha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo matatu. Nitazungumzia suala la madawa ya kulevya lakini nitazungumzia hali ya usalama hasa Zanzibar na muda ukipatikana nitamalizia na suala la magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nilieleze Bunge hili Tukufu kwamba kuna kazi kubwa sana ambayo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikiifanya, imefanya na inaendelea kufanya katika kukabiliana na janga hili la madawa ya kulevya katika nchi yetu. Yapo mambo yameendelea kufanyika waziwazi na yapo mambo ambayo yamefanyika kimya kimya hayajulikani na mengine hayatajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika haya mapambano ya dawa za kulevya, nataka niwahakikishie kwamba tunaendelea vizuri na imani yangu ni kwamba kwa mwelekeo huu tunaoenda nao tunaelekea kushinda na hatutarudi nyuma. Silaha yetu kubwa ni dhamira ya dhafi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. Wewe na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wakati Mheshimiwa Rais alivyokuja kuzindua Bunge hili alizungumza kwa msisitizo na toka wakati ule mambo mengi na makubwa yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ya msingi ni kwamba tumefanikiwa kiasi gani, changamoto ni zipi na tunaelekea wapi. Tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana, ni watumiaji na wauzaji wa madawa ya kulevya wakubwa, wa kati na wadogo wengi ambao wamekamatwa na wengi kesi zao zinaendelea na wapo wengi ambao wameshafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tukiri kwamba kulingana na mabadiliko ya mfumo wa kidunia zamani nchi yetu ilikuwa inatumika kama ni eneo la kupitishia madawa ya kulevya lakini sasa hivi ongezeko la matumizi ya ndani la madawa ya kulevya limekuwa ni kubwa. Madawa ya kulevya yanatumika hovyo, hilo lazima tukiri kama ni changamoto. Changamoto hii Serikali hatuwezi tukaifumbia macho na ndiyo maana tumebadilisha *style* ya kukabiliana na matatizo ya madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu hapa katika ziara zake nyingi Mheshimiwa Waziri ambazo amekuwa akifanya mara ya mwisho alikuwa Ifakara amezungumzia hilo, ametoa mwelekeo huo na mimi nilikuwepo Mbeya takribani wiki mbili zilizopita kabla hata ya operesheni moja haijafanyika ikiwemo ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tumewaelekeza ma-RPC kwamba kwa uzito wa tatizo la madawa ya kulevya katika nchi yetu, tuliwaelekeza Mbeya tukawaambia wafanye operesheni kabambe kabisa na wakafanya operesheni kali sana wakawakamata watumiaji wa madawa ya kulevya na wauzaji. Wale watumiaji wa madawa ya kulevya ndiyo waliotusaidia kuweza kuwapata wale ambao wanashughulika na kuuza madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulidhamiria kwamba tutumie utaratibu huo ili kuweza kupata taarifa na kuukamata mtandao mzima wa madawa ya kulevya na hatimaye kuangamiza na kupunguza matumizi makubwa ya madawa ya kulevya yaliyopo mitaani. Jambo hilo limefanyika kwa mafanikio makubwa sana kwa upande wa Mbeya peke yake watu zaidi ya 17 ambao walikuwa *either* wanatumia au wanauza madawa ya kulevya walikamatwa na kesi zao wengine zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Wakuu wa Mikoa ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mikoa yao ikiwemo Mkoa wa Mbeya wameendelea kusimamia hilo na mikoa mingine ikiwemo Dar es Salaam na Shinyanga na kadhalika. Kwa hiyo, tunataka tulihakikishie Bunge hili Tukufu kwamba vita hii ni vita ambayo hatutarudi nyuma na tunaomba ushirikiano wa wananchi na Waheshimiwa Wabunge waliomo humu kuweza kuhakikisha kwamba tunaimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la usalama wa nchi yetu. Naomba nigusie mambo madogo mawili kwa sababu ya muda. Kumekuwa kuna hoja ya mashaka kuhusiana na majibu ambayo tunatoa kuhusu hali ya ugaidi katika nchi yetu. Naomba nirudie tena kwamba nchi yetu hakuna ugaidi bali kuna vimelea vya ugaidi. Vimelea hivi vya ugaidi havijafanikiwa kuzaa matukio makubwa ya ugaidi kwa sababu ya kazi kubwa ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambayo vimeendelea kufanya katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia tukio moja ambalo limewahi kutokea katika miaka ya nyuma ya ulipujaji wa Ubalizi wa Marekani lakini mpaka sasa hivi tumeweza kudhibiti kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, msimamo wa Serikali ndiyo huo, msimamo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo huo na msimamo wa Wizara ya Katiba na Sheria kama alivyozungumza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ni hivyo hivyo hakuna mgongano wowote katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo limezungumzwa sana ni suala zima la hali ya usalama Zanzibar, tusichanganye vitu. Tulichokizungumza ni taarifa ambayo imekuwa ikiletwa hapa na Wabunge mbalimbali, wengine wamekuwa wakisambaza picha kwenye Facebook wakichukua

watu wengine hatujui walikuwa wanaumwa malaria au kitu gani wakisema tumepigwa na watu ambao wanaitwa Mazombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema kwamba Zanzibar hali ya usalama ni shwari na Tanzania hali ya usalama ni shwari. Hata hivyo, kwa kusema hivyo, hatuna maana kwamba hakuna *element* za uhalifu, wezi, walevi wanaokunywa pombe haramu watakuwepo na kadhalika. Hao watu ambao wanaitwa Mazombi sisi tumesema kabisa kwamba kama kuna mtu yeyote ana taarifa ya watu hawa aiwasilisha katika vyombo vya dola. Mpaka sasa hivi hakuna mtu yeyote ambaye amewasilisha taarifa hii rasmi katika vyombo vya dola na ndiyo maana msimamo wetu unaendelea kubaki pale pale kwamba taarifa hizo kama Serikali hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa haraka haraka kuzungumzia suala la magereza. Kuna mambo makubwa matatu ambayo tunayasimamia kwa nguvu zetu zote.

Jambo la kwanza, kama Mheshimiwa Rais alivyosema kwamba wafungwa wafanye kazi tumelisimamia hilo kwa mafanikio makubwa. Leo tunavyozungumza tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari Magereza Ukonga. Katika ujenzi ule tumetumia wafungwa na tumefanikiwa kuokoa fedha ambazo zimewezesha kujenga zaidi ya nyumba 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kana kwamba hiyo haitoshi matumizi ya wafungwa yametusaia sana katika kuweza kufanya kazi mbalimbali za ujenzi katika magereza yetu. Katika Wilaya na Nkasi kulikuwa kuna changamoto sana ya mahabusu. Tulifanya ziara huko hivi karibuni na hivi tunavyozungumza ni kwamba shughuli za ujenzi wa mahabusu katika Wilaya ya Nkasi zinaanza kwa matumizi ya nguvu kazi za wafungwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa mimi pamoja na watendaji wangu. Nataka niwahakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana nao. Aidha, nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tumekuwa tukifanya kazi pamoja nao tukitembelea maeneo mbalimbali na tunawashukuru sana kwa usimamizi wao na ushauri wao kwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kadhaa ambazo zimetolewa na napenda nianze na zile za Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *beacons* kutokuwepo katika mipaka yetu. Ni kweli hili ni tatizo la muda mrefu lakini napenda niseme kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa. Tumechukua hatua za aina mbili. Kwanza ni mazungumzo kati ya Wizara zinazohusika kwa upande wetu wa Tanzania pamoja na ule upande wa majirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imekamilika kwa mpaka wa Tanzania na Kenya na *beacons* zimeanza kurudishiwa na mazungumzo yapo katika hatua nzuri kwa upande wa Tanzania na Uganda. Ni mategemeo yetu kwamba baada ya kukamilika kwa mazungumzo hayo, basi tutarusha zile *beacons* na kuweka *buffer zone* ili wananchi wasiingilie ile mipaka kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeeleza juu ya suala la marekebisho ya Sheria ya JKT ili iweze kutoa fidia kwa vijana wanaoumia wakiwa kwenye mafunzo. Hili tunalikubali, ni ushauri mzuri sana na ni kweli kwamba wapo vijana wanaopata matatizo ya kiafya na wengine wanaoumia

kupitia yale mazoezi yanayofanyika kule. Kwa hiyo, ni jambo ambalo na sisi tunalipokea na tutafanya utaratibu wa kufanya marekebisho ili waweze kupata fidia iwapo watakuwa wameumia wakiwa katika mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya idadi ya vijana wa JKT waliochukuliwa mwaka huu. Napenda nitoe taarifa kwamba vijana waliochukuliwa kwenda JKT ni wa aina mbili; wale wa mujibu wa sheria ambao mwaka huu idadi yao ni 14,748 na wale wanaojitolea wamechukuliwa 9,848. Kwa hivyo, hao ndiyo ambao wamepata nafasi safari hii. Tunatambua kwamba idadi hii ni ndogo na inabidi tuwachukue wengi zaidi hususani wale wa mujibu wa sheria na tutaendelea kujenga miundombinu katika makambi yetu ili tuweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuweza kuwachukua walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hizo za Kamati sasa niingie kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja na nianze na ile ya Mheshimiwa Rweikiza ambaye ametaka kujua ni kwa nini hatujasaini na ku-ratify ule Mkataba wa *Biological Weapon Convention*. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Rweikiza kwamba kuna mikataba ya aina hii miwili; wa kwanza ni ule *Chemical Weapons Convention* na wa pili ni *Biological Weapons Convention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, *Chemical Weapons Convention* tulishasaini na tumeshauridhia, kwa hiyo, pale tumemaliza. Kwa upande wa *Biological Weapons Convention* kusaini tulishasaini kilichobaki ni kuridhia na ku-domesticate kwa maana ya kwamba kuingiza katika sheria za nchi ili uweze kutumika katika sheria za nchi. Kazi hiyo inaendelea na iko katika hatua ya *Cabinet Secretariat* ili hatimaye iweze kufika Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mattar alitoa mapendekezo kwamba asilimia ya vijana wanaochukuliwa kuingia JKT kutoka Zanzibar basi angalau ipatikane asilimia kumi ya wale wa jumla wanaochukuliwa. Tunaweza kusema kwamba kwa sasa hivi au kwa mwaka huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipewa nafasi 300 na tunaona umuhimu wa kuongeza nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuahidi kwamba mwaka hadi mwaka tutaendelea kuwa tunaongeza idadi hii japo siyo kwa kufikia asilimia kumi ili tuweze kupata vijana wengi zaidi kutoka upande wa pili wa Jamhuri yetu, lakini wakati huo huo lazima tujenge miundombinu zaidi ili tuweze kupata idadi kubwa zaidi ya vijana wanaoingia katika Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naye vilevile alishauri kwamba badala ya utaratibu unaotumika sasa ule wa kupitia Wilayani na Mikoani alishauri kwamba pengine vijana wachukuliwe kutoka JKU. Ambacho naweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge kuhusu hili ni kwamba uamuzi wa jambo hili upo juu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu sisi au mimi kama Waziri wa Ulinzi huwa napeleka nafasi zile kwa Makamu wa Pili wa Rais na tunawaachia jukumu la kuamua wao wanataka kutumia utaratibu gani. Mpaka sasa wamekuwa wakizigawa Wilayani na Mikoani. Kwa hivyo, naweza kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vyema akazungumza na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuangalia utaratibu kama huo wa JKU utakuwa ni bora zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ya kuhusu Kanali Kashmir kwamba hajastaafishwa rasmi. Kwanza nataka nimpe taarifa ya kwamba Kanali Kashmir ni kweli alikuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na cheo chake kilikuwa ni *Chief of Logistics and Engineering (CLE)* na sio *Chief of Staff*. *Chief of Staff* wakati wake yeye cheo hicho hakikuwepo ni baada ya yeye kutoka mwaka 1974 ndipo kilipoanzishwa cheo cha *Chief of Staff*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba kuhusu maslahi ya kustaafu ni suala la kisheria. Kama ni kweli kuna uthibitisho kwamba Kanali Kashmir hajalipwa jambo hili litaangaliwa kisheria aweze kupata mafao yake. Hata hivyo, taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba wakati anatoka Jeshini kwenda SUDECO fedha za Jeshi alikuwa ameshapata na baada ya kustaafu kule SUDECO alitakiwa alipwe upande ule ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengine nitayaleta kwa maandishi. Naunga mkono hoja na ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi tunamalizia na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniungeza timu katika Wizara yangu. Katika wiki hizi mbili ameteua Kamishna Mkuu mpya wa Magereza, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji aliyeteuliwa leo, Kamishna Mkuu wa Kupambana na Madawa ya Kulevya na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai. Hawa ni watu wa muhimu sana katika kazi hii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaambie, ndiyo kwanza kazi inaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niwashukuru sana Kamati kwa ushauri ambao wamekuwa wakitupatia Wizara. Niwaambie tu kwa ujumla wao mapendekezo na ushauri wote ambao wametupatia tutaufanyia kazi na hasa tunapoelekea katika maandalizi ya bajeti ya mwaka unaofuata. Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, wewe umekuwa *dictionary* yetu nzuri katika Wizara hii ukizingatia *institutional memory* uliyonayo ya kufanya kazi katika Wizara hii pamoja na timu yako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo tumelipokea, mmeongelea sana suala la vitendeakazi pamoja na maslahi ya askari wetu wa vyombo vyote ambavyo viko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Wenzetu wa Wizara ya Fedha tayari wameshatusaidia baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa vinadaiwa na askari wetu. Kuna baadhi ambavyo tayari wameshaanza kutoa na tunaamini kwa kadri ambavyo wamekuwa wakijitahidi wataendelea kutoa na vingine. Kwa hiyo, jambo hilo linafanywa kazi na stahili hizo zimekuwa zikitolewa na hivyo kupandisha morali ya kazi ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunasubiria magari, Waheshimiwa Wabunge wengi katika maeneo yenu mmeongelea suala la magari. Ni kweli nimepita katika maeneo mengi ambako nimeona umbali na uhitaji wa magari kwa ajili ya operesheni pamoja na mambo mengine ni mkubwa. Niwahidi, tutatoa vipaumbele kwa kadri ya maeneo yalivyo kadri tutakavyokuwa tumepata magari hayo ili kuweza kuongeza tija ya usalama wa raia pamoja na mali zao katika maeneo yenu, tutalifanyia kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pia maombi ya vituo, tutaendelea kushirikiana nanyi na hamasa mnazozifanya katika maeneo yenu ili hili nalo liweze kupewa uzito unaostahili. Sisi tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuweza kuhakikisha tunatengeneza mazingira hayo. Nia yetu ni moja ya kuweza kuhakikisha mazingira ya askari yanaendana na kazi wanayofanya ili raia waweze kujizalishia mali katika mazingira ambayo ni salama na wao waweze kufanya kazi wakiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limeongelewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge ni lile linalohusu wakimbizi pamoja na makazi ya wale raia ambao walipewa uraia baada ya kukaa kwa muda mrefu. Jambo hili tunaendelea kulijadili na wiki ijayo tutakaa kikao cha pamoja kuweza kujadiliana. Mambo ambayo tunategemea kuyajadili ni pamoja na njia nzuri. Wazo hili lilipoahirishwa mwanzoni ilikuwa hawa watu wapewe fedha za kwenda kuanzia maisha sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara mtazamo wetu uko sawasawa na mtazamo wa Kamati kwamba hatuwezi tukawapa watu uraia halafu wakatengeneza kanchi kao ndani ya nchi yetu kwa kukaa eneo lao, kwa kuwa na uongozi wao, wana lugha yao moja na tabia zao moja. Watu wakishapewa uraia wa Tanzania wanakuwa Watanzania na wanatakiwa waishi kwa desturi na Katiba ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo tutajadiliana na *development partners* pamoja na sisi wenyewe kuweka huo msimamo na tutalitolea uamuzi katika Serikali. Tutawajulisha Kamati

pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kadri tutakavyopata muda na forum zetu hizi ambazo ni za Kibunge za kupeana taarifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa wakimbizi tulifuta utaratibu wa wakimbizi kuingia kwa ujumla kwa sababu hali ya mara baada ya *tension* za kisiasa na kabla na sasa ilivyo ni tofauti. Kwa hiyo, tunatengeneza utaratibu ule ikiwa ni pamoja na udhibiti ili kuweza kudhibiti uhalifu kwani kuna wengine wanaweza wakaingia kwa gia ya ukimbizi na wakafanya vitu ambavyo ni vya kihalifu. Hii inadhihirika katika ukanda ambako wakimbizi wapo jinsi ambavyo matukio ya uhalifu yamekuwa yakizidi maeneo mengine na upatikanaji wa silaha ambazo si za Tanzania ukizidi katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na Mheshimiwa Naibu Waziri alilisemea kwa kiwango kikubwa nampongeza kwa hilo linahusu namna ya kuifanya Magereza ijitegemee. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari ameshaitisha kikao ambacho kitafanyika Jumatatu lakini lengo lake ni namna ya kutumia fursa tulizonazo katika Magereza kwenda kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipokuwa najibu swali nililisemea kwamba tunataka Magereza ambayo yana maeneo ya uzalishaji tuyatumie kwenye uzalishaji. Tutatoka kwenye uzalishaji wa kizamani kwenda kwenye uzalishaji wa kisasa ili maeneo yote yale yazalishwe kwa zaidi ya asilimia 85. Tukifanya hivyo tuna uhakika Magereza yatajitegemea kwa chakula lakini hata kwa fedha kwa sababu tunaamini uzalishaji huo ukishazidi kuna baadhi ya mazao ambayo tutauza NFRA pamoja na maeneo mengine na vilevile tunaweza hata tukapeleka kwenye shule za bwani ili watu wetu waweze kupata chakula hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho lililoongelewa sana ni hili la madawa ya kulevya. Vita hii ya madawa ya kulevya ni vita ya kila Mtanzania na vita hii haijaanza sasa.

MBUNGE FULANI:Yes!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tangu nilipofika nilikuta tayari Mheshimiwa Kitwanga ameshakamata mapapa wakubwa tu na tulivyotoka pale tumeendeleza. Ninachowaambia Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukatofautiana mtazamo kwenye *approach* na ninyi kama Wabunge na kama washauri wetu mkitushauri njia nzuri ya kufanikisha jambo hili sisi mara zote tutakuwa tunapokea ushauri huo. Kwa sababu vita hii si ya mtu mmoja, mkituambia tukifanya hivi tutafanikiwa zaidi maana yake vita ni yetu sote, sisi tutaendelea kupokea ushauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo nawahakikishia na ambalo nawaomba wote tuwe nalo, tusibadili lengo la kuhakikisha tunapambana na vita ya madawa ya kulevya, tuendelea nalo. Mheshimiwa Rais alishatoa dira hiyo na sisi wasaidizi wake tunatembea katika nyayo zile kuweza kuhakikisha tunafanikiwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine walikuwa wanasema mbona Waziri hujasema, nimeshazunguka mikoa yote kasoro Njombe, Ruvuma, Singida na Songwe. Kwenye mikoa yote huko nilikopita nimetoa maelekezo ya makosa ambayo ni ya kipaumbele ya kufanyiwa kazi:-

Moja, ni madawa ya kulevya, kila mkoa nimeelekeza, si jambo la mjadala. Mbili, ni uhalifu wa kutumia silaha, nimesema si jambo la mjadala. Tatu, nimesema ni ubakaji, si jambo la mjadala. Nne, nimesema ni ujangili, si jambo la mjadala. Tano, nimesema yale masuala yanayohusisha ugaidi, si mambo ya mjadala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishatoa maelekezo kama hayo sibi nafishi tena hiyo shughuli...

MBUNGE FULANI: Good!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mtanzania ambaye linamhusu jambo hili popote pale alipo na mkiwepo Waheshimiwa Wabunge lazima tusimamie mambo haya kwa upana wake kwa

maslahi ya Taifa letu. Jambo likishakuwa la aina hii kila mmoja anatakiwa atimize wajibu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika masuala haya ambayo ni ya Kitaifa tushirikiane wote, tusaidiane wote. Watu huwa hawagombani kwa ajili ya kazi, watu wanasaidiana kazi, tusaidiane kazi kuweza kuhakikisha kwamba inapofanikiwa inakuwa yetu sote na inaposhindikana tunakuwa tumeshindwa wote kama Taifa. Taifa letu likipata hasara, Taifa letu likipata aibu tunakuwa tumepata aibu wote. *United we stand divided we fall*, twende pamoja tuweze kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika mambo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Nawashukuru Mawaziri wote kwa michango yenu na sasa tunaendelea kuhitimisha hoja na tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ili aweze kuja kuhitimisha hoja yake. Karibu Mwenyekiti, dakika 15.

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii niweze kuhitimisha hoja yangu, hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Niwashukuru sana waliochangia kwa kuongea humu Bungeni, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Aida Khenani. Pia kuna Waheshimiwa Wabunge wamechangia hoja hii kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Juma Othman Hija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kwa kifupi sana. Ukimuona nyani mzee porini ufahamu kwamba amekwepa mishale mingi sana. Kwa hiyo, ndugu zangu hii ndiyo hali ya maisha. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasilisha hoja hii, Waheshimiwa Wabunge mtakapopata fursa isomeni, hoja ya msingi hapa ni kwamba Sheria Ndogo ni sheria halali za nchi hii na zinawagusa wananchi wetu katika maisha yao ya siku hadi siku. Mimi nashukuru sana uamuzi wa Mheshimiwa Spika kwamba Kamati hii iwe inapewa fursa ya kuwasilisha taarifa yake mapema kabla ya taarifa zote. Kwa sababu tusipofanya hivyo kama mnavyoona sasa hivi wananchi wataendelea kuumizwa tu kwa sheria ambazo zina dosari na ambazo zingeweza kurekebisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu amesema ziko kodi, ada na tozo nyingi sana kwenye mazao hasa ya biashara, hilo ni agizo, tunategemea kwamba Wizara zenye sekta hizo watafanya haraka ndani ya uwezo wao kuzipitia zile sheria na kanuni, kama msingi wake uko kwenye sheria mama basi wafanye marekebisho kupitia sheria mama kuleta Muswada wa Marekebisho hapa Bungeni. Kama ni kwenye Sheria Ndogo ndiyo unachukua nafasi ya Kamati hii kuyaleta mapema ili tuweze kuyapitia tuyanyooshe twende mbele. Hivyo hivyo kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, maelekezo mazuri sana ameyatoa alipokuwa katika ziara Mikoa ya Kusini. Maana tukiacha hizi zitaendelea kutumika, ni sheria. Kwa hiyo, nimeona hilo niliseme kwa sababu linatuhusu sote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hija ameshauri tu kwamba labda Kamati ya Sheria Ndogo itusaidie hii migogoro ya wafugaji na wakulima, mtoe mchango wenu kwa hilo. Napenda sana hiyo lakini hali halisi sio hivyo. Kamati hii inafanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ambazo zimewasilishwa hapa Bungeni na Serikali. Ombi langu kwenu kama viongozi, kwa sababu tatizo hili ni kubwa, tukianza chini kwenye maeneo yetu katika kutunga au kupendekeza maoni yetu ya kutunga Sheria Ndogo ambazo zitasimamia matumizi bora ya ardhi, Sheria Ndogo hizo ndiyo zitaweza sasa kufanikisha hilo ambalo Mheshimiwa Juma Othman Hija anapendekeza lakini sisi hatuwezi kwenda tukafanya kazi ambayo siyo sehemu ya majukumu ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la elimu, kuwawezesha wanasheria, kwanza wanasheria kwenye Serikali za Mitaa au Halmashauri zetu tumelisema kwenye taarifa, hiyo ndiyo inachangia dosari nyingi ambazo zinaonekana katika Sheria Ndogo hizi. Hata hivyo, mimi najua uandishi wa sheria ni taaluma ya kipekee na ndiyo maana hata kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni wachache na wale wazuri,

hii siyo *feature* ya Tanzania tu, nenda kokote ndani ya Nchi za Jumuiya ya Madola tatizo hili lipo, kwa sababu hawa *is a special breed*, wanafunzwa namna ya kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili uweze kufika ile *grade* tunayoitaka lazima uwe una uzoefu mpana sana wa sheria lakini pia na masuala ya kijamii sasa kuwapata hao itatuchukua muda. Hata hivyo, tukasema tunapendekeza angalau kwa wanasheria waliopo katika Halmashauri zetu wakinolewa kila baada ya muda kama walivyofanya juzi hapa Dodoma, wamefanya semina ya wanasheria wote hawa waliletwa hapa, ya siku tatu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetoa *inputs* zake, wanasheria wa TAMISEMI wametoa *inputs*, ndivyo inavyotakiwa, labda itatusaidia sana katika kuimarisha uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema vizuri, jamani Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali, ofisi kwanza yenyewe ni hatari. Serikali imetoa ahadi na sisi tunaamini kabisa kwamba ahadi ni deni tunategemea tuone ndani ya muda mfupi ofisi hiyo inaboreshwa kiutendaji lakini kwa vifaa vya kisasa. Maana haya tunayoyasema ya kuwasilisha Sheria Ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 37(2) na kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri yanategemea ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Kama hajafanya utakuwa unaonea Serikali kwamba kwa nini hamjaleta mawasilisho yenu Bungeni, lakini acha tuone. Kuna mchango mzuri tu wa Mheshimiwa Kuchauka, yeye anasema hawa wananchi wanaokaa karibu na hifadhi ndiyo wanasaidia kutunza hifadhi hizi lakini tunapata mapato kiduchu asilimia 25. Sasa yeye anapendekeza waongezewe, hayo ni ya kwenu huko, sisi tunasimamia Sheria Ndogo kama itakuja na mapendekezo hayo na yamekubalika kule itakuwa ni uamuzi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme moja, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kupitia Bunge la bajeti mwaka wa fedha 2011/2012 wote mliokuwa Bungeni mnakumbuka, yaliletwa marekebisho ya kuongeza cess ya mazao ili watoze kwa kuangalia hali halisi ya Halmashauri yako, kati ya asilimia tatu mpaka asilimia tano. Hata hivyo, ukweli wa mambo, hakuna Halmashauri nchini ambayo imetoza chini ya asilimia tano, zote zimepiga ile *ceiling*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati, ingawa siyo la kwetu lakini tunayaona, tumemwambia na Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba kama malalamiko ni haya hebu tujitahidi basi tukaweka ifahamike. Maana sasa hivi mmewapa ile *leeway* wanapiga mpaka kwenye *ceiling*, ni afadhali ikafahamika kama ni asilimia tano iwe asilimia tano, kama ni mbili au tatu iwe tatu, tutakuwa tumeiweka sheria katika msingi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nipigiwe kengele ya pili, kazi hii tumeianza, tunaomba Kamati hii iendeleo kuungwa mkono kwa kuwezesha. Hawa wajumbe wa Kamati hii kazi yao ni kusoma *documents*. Wenyewe pia ili waweze kuifanya kazi hii vizuri lazima wawezeshe vizuri. Tofauti na baadhi ya wajumbe ambao ni wanasheria kama akina Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Ngeleja na wanasheria wengine lakini wengine hawa siyo wanasheria na siyo lazima uwe mwanasheria kuweza kuzifanya kazi hizi lakini ukisaidiwa ukawasikia wale ambao wamebobeza katika masuala haya mtakuwa mmeisaidia sana Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisichukue muda wako mwingi, tuna mambo mengi sana leo, lakini niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotuunga mkono. Nami nimalizie kwa kusema maoni na mapendekezo yote ambayo yamo kwenye taarifa ya Kamati sasa Bunge lako iyakubali kama Maazimio yaliyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Haya hoja hii imekubaliwa. Kwa hiyo, taarifa hii imekuwa ni maazimio rasmi ya Bunge.

Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge aje kutoa hitimisho la hoja yake.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena. Sitamaliza hiyo robo saa kwa sababu Kamati yangu wamechangia watu watatu; hapakuwa na maneno mengi sana. Nadhani hiyo ni kuonesha alama wanazoipa Kamati, nadhani zaidi ya asilimia 90 hawakuwa na mambo ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wawili wamechangia humu ndani, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Dkt. Semesi. Mheshimiwa Juma Othman Hija alichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, yeye ametoa rai kwamba kila Mbunge ajiheshimu mwenyewe kwanza. Sisi tunakubaliana naye na ndiyo msimamo wa Kamati yangu kwamba kama hapa ndani kila mmoja atajiheshimu, nafikiri hata kazi ya Kamati hii itakuwa rahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Semesi amependekeza Kamati iwe na Wajumbe 50 kwa 50. Nataka nimweleze kwamba Kamati hizi hapa ndani zinaundwa kulingana na uwiano wa Wabunge kwenye Vyama. Kamati zote zilizomo humu ndani kile Chama ambacho kina Wabunge wengi ndicho kina Wajumbe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati zote zinategemea hiyo. Ukichambua hizi Kamati, ni yale yale ninayoyakemea kwamba kwa utaratibu wa humu ndani, kama mmoja anaongea, wewe unanyamaza. Nadhani ndiyo mnaona umuhimu wa Kamati yangu, kwamba wako watu ambao lazima tushughulike nao ili hapa ndani pawe shwari. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukitoka hapa, nenda kachambue Kamati yote, *in reality*, ratio iko 7:3 nenda Kamati zote. Kwa hiyo, siyo kwamba hii Kamati ya Maadili *isan exception*, hapana. Ndivyo ilivyo kwa muundo wa Kamati zote. La mwisho, niseme tu kwamba anayeunda hizi Kamati, sio Wajumbe wa Kamati, ni Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watatu, ndugu yangu hapa, Mheshimiwa Juma Abdallah Juma, yeye amechangia kwa maandishi, anaipongeza kazi ya Kamati na anapendekeza kanuni ziangaliwe upya ili kuwabana wanaofanya fujo ndani ya Bunge. Ninachotaka kusema ni kwamba, Kamati ya Kanuni ndiyo inayotengeneza kanuni, sisi tunafanya kazi kwa kutumia kanuni zilizotengenezwa na Kamati ya Kanuni na kupitishwa na Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimalizie tu kusema kwamba sisi kama Kamati ya Maadili, tunatoa rai na kama tulivyosema pale mwanzo, hapa ndani kuna maendeleo makubwa sana. Ukilinganisha vurugu zilizokuwepo mwanzoni wakati Bunge linaanza na tulivyo leo, yapo mabadiliko makubwa. Kwa mtu yeyote ambaye akili yake haina matatizo, anaelewa kwamba tumepiga hatua. Yule ambaye hataki kuelewa, mwache aendele kutokutaka kuelewa kwa sababu ndiyo watu wengine walivyo, lakini hali ya hapa katika Bunge nadhani kwamba tumeanza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie...

Mheshimiwa Mwenyekiti, si ndiyo haya haya ninayokemea? Mimi si ndiyo nimepewa nafasi hapa kusema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema hivi, tukiwa hapa ndani, naomba tuendeleo kuheshimiana, kuvumiliana, kuzingatia kanuni, kuheshimu kiti na nimalizie kusema tu kwamba ukizomea wakati mwingine wanasema, haujajenga hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka leo tuondoke wote na msembo huu ambao katufundisha Baba yetu Mwalimu Nyerere. Alitufundisha hivi, *argue, don't shout*. Tuondoke na *spirit* hiyo, Baba yetu katufundisha, "*argue don't shout*." Kama mwenzio anaongea, kapewa nafasi, nawe ghafla bin vup, unabonyeza unasema 'nini wewe?' "Mambo gani hayo?" *You are shouting. Argue, don't shout*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuipokea taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge pamoja na mapendekezo yake ili yakubaliwe na kupitishwa na kuwa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, maoni na mapendekezo ya Kamati yamepitishwa kuwa azimio la Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia na Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, aje ahitimishe hoja yake.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB - MWENYEKITI KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kumaliza hii hoja. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 29. Waheshimiwa Wabunge 23 wamepata nafasi ya kuzungumza na sita wameweza kuleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge michango yao yote tutaichukua na kuboresha kwenye maazimio yetu. Nawashukuru pia Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri kwa michango yao ambayo ni muhimu sana kwenye Kamati hii ambayo inajumuisha karibu Wizara tatu na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia wana Kamati wenzangu, wamefanyakazi nzuri sana na wengine kwa kweli wamekuwa na roho ngumu; hata tulipoingia kwenye Magereza na kuwaona wafungwa na mahabusu jinsi walivyo, wengine machozi yaliwatoka. Nawashukuru sana kwa kuwa wavumilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani na utulivu katika nchi yoyote ile ni jambo la msingi sana. Tukichezea amani na utulivu, naamini hatuwezi kukaa. Kuna mifano mingi sana ambayo ipo kwenye ulimwengu huu. Nchi ambazo zimechezea amani na matokeo yake wanayaona na wasingeweza kukaa hata kwenye ukumbi wa Bunge kama hivi. Sisi kama Kamati yetu tutajaribu kwa kadri tunavyoweza kushauri Serikali namna ya amani na utulivu umuhimu wake unavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ambayo yote yapo kwenye Wizara hizi; za Mambo ya Ndani na Mambo ya Ulinzi na Usalama yanahitaji fedha; lakini kwenye Wizara zote hizi tatu ambazo tumezungumza zote zimeonekana kuna upungufu wa fedha. Fedha ambazo zimepitishwa na Bunge lako Tukufu hili, zimeshindwa kuwafikia wahusika ili waweze kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetembea kwenye baadhi ya Magereza na baadhi ya Magereza mengine tumekuta wafungwa wanadai vyombo, zana za kufanyia kazi ya kilimo. Wanasema tunaomba matrekta, tuna ardhi iko hapo imejaa na tuna hela zetu. Ni Gereza la Songwe wanasema tuna hela zetu shilingi milioni 40 ziko kwenye akaunti, tupeni tununue matrekta. Sijui kwa nini, nafikiri Waziri wa Fedha na Waziri wa Mambo ya Ndani, atakuwa analisikia. Toeni hizo hela na kuacha huo urasimu, wapeni wafungwa walime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa mahabusu kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Kama nilivyosema kwenye taarifa yetu, kuna watu wamekaa Magerezani kwa miaka mine mpaka mitano kwa makosa ya mauaji na madawa ya kulevya; kitu ninachongojewa ni kitu kinaitwa *High Court Session*. Polisi na Mahakama zimefanya kazi nyingi sana za kesi ndogo ndogo, bado hizi kesi kubwa. Mahakama Kuu kuna nini? Kwa nini hambadilishi taratibu za kuangalia kubadilisha huu mfumo wa *High Court Session* ambao unawaweka mahabusu muda mrefu ndani ya Magereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhusu, msongamano wa mahabusu ambao unaambatana na hiyo kwa kweli ni suala ambalo linatakiwa lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza na tumetoa mapendekezo na maoni ambayo tunaona ni muhimu yaweze kuchukuliwa, isipokuwa cha msingi ni fedha ziende kwenye Balozi nje ya nchi. Mabalozzi kule hawana hela. Hela tumepitisha lakini haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa mabalozzi watatumika sana kwenye diplomasia ya uchumi. Wao wana uwezo mkubwa sana wa kuleta Wawekezaji hapa na watalii. Tuwapelekee fedha, tuwawezeshe waweze kufanya hayo mambo. Hii ni pamoja na Mabalozzi ambao wako hapa nje; nyumba nyingi tu; mfano huo wa Sweden ni mmoja, lakini nyumba nyingi za Mabalozzi ziko kwenye hali mbaya na zinahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata mchango wa Mheshimiwa Bilago. Warundi wamejaa kwenye Gereza la Kibondo, kwa sababu pale ni mpakani, huwa kuna utaratibu wa mikutano ya ujirani mwema. Waburundi wanakuja na sisi tunakwenda, tunanunua vitu na wao wanunua vitu. Sasa wanapokuja wale, unawakamata kwamba wameingia nchini isivyo halali, unawajaza kwenye Magereza, kwa kweli siyo haki. Waziri wa Mambo ya Ndani na Serikali ilianganalie hilo ikafanye mikutano ya ujirani mwema kuondoa hilo tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wanafanya kazi nzuri sana na mpaka sasa hivi wamepunguza uhalifu kwa kiwango kikubwa sana, tukichukulia uhalifu *in totality*; lakini hawana nyenzo. Bajeti ambayo tumeipitisha hapa kuwapa fedha, hawajapata hizo hela, au kama wamepata, zote zimekwisha. Sasa tusiwafanye Polisi wawe ombaomba, isipokuwa naitaka Serikali ianganalie hilo suala na kuhakikisha fedha ambazo tumepitisha hapa, basi Polisi wale wanapewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madawa ya kulevya ni tatizo kubwa, watoto wetu wameharibika, Watanzania wanakamatwa sana huko nje. Sisi tunaweza kuwafuatia Nigeria sasa hivi. Kwa hiyo, wamejaa kwenye Magereza ya nje, ni vita. Nami naomba tutakaporudi kwenye Majimbo yetu tuwasaidie kutoa taarifa ya wote wanaohusika na madawa ya kulevya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, Makamanda wa Mikoani wa Polisi na Makamanda wa Wilaya, wana jukumu kubwa sana la kuwasaidia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Ni lazima wafuate taratibu za upelelezi. Taratibu za upelelezi zipo wazi. Upelelezi ni *profession* jamani. Kuna *doctorate* ya *investigation* inachukuliwa. Upelelezi hauendi hivi hivi. Huwezi ukatoa upelelezi kwa kutaja watu majina, hakuna! Mimi sijawahi kuona kitu kama hicho. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba Makamanda wa Polisi na wa Wilaya, waanganalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo *Police General Orders*, *Police Force Ordinance* na *Criminal Procedure Act* ambazo zinaeleza kabisa namna ya Polisi kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kukaa pamoja na hao Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwasaidia. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati Mheshimiwa Lyatonga Mrema alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, mimi nilikuwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Dar es Salaam na alifanya kazi kubwa sana, lakini kulikuwa na kazi nyingine anakwenda nje, kinyume. Nikasema tukimwacha Mheshimiwa Lyatonga aende hivi, ataharibu kesi Mahakamani. Ikabidi Wakuu wakae na Mheshimiwa Mrema, wakaelekezana taratibu za kufanya na Polisi walimpa *support* na mambo yakawa yanakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wilaya wakae na Wakuu wa Mikoa wao na Wakuu wa Wilaya zao, waangalie na kuwashauri namna ya kugawanya hizi kazi. Hawa Makamanda wamesomea, wanaelewa. Wamekwenda kwenye vyuo mbalimbali, wanaelewa taratibu. Hatutaki waharibu hizi kesi nzuri au hii *operation* nzuri ambayo imeanza ili kesi hizi ziende kufa kule Mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba yote ambayo mmeyaongea na kushauri tutayachukua na tutaweka kwenye maazimio yetu na ninawahakikishia kwamba tutaunda Kamati Maalum ya kufuatilia yote ambayo tumeyasema ili kuhakikisha kwamba kabla hatujatoa *report* nyingine mwaka kesho, basi tutatoa utekelezaji wa maazimio haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, napenda kuwasilisha taarifa yangu na naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana. hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitalihoji Bunge.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Hoja hiyo imepita na sasa taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imepitishwa kuwa Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana na niwapongeze sana Kamati zote tatu ambazo tumezijiadili leo kwa umahiri mkubwa na sasa zimekuwa ni taarifa rasmi ama maazimio rasmi ya Bunge. Kwa hiyo, Mungu awabariki sana wote ambao mmeshiriki kwa njia moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nampisha Mheshimiwa Spika ili aweze kuendelea na shughuli zinazofuata. (Makofi)

Hapa Spika (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

SPIKA: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli kwa ajili ya kufanyiwa kazi katika Mkutano huu wa Sita, zimemalizika.

SPIKA: Ahsante. Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH - KATIBU WA BUNGE: Hoja ya Kuahirisha Bunge.

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Sasa naomba kwa heshima zote nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kutoa hotuba yake ya kuahirisha Mkutano huu wa Sita wa Bunge.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali. (Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutufikisha siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Sita wa Bunge lako Tukufu tuliloanza siku ya tarehe 31 Januari, 2017. Mwenyezi Mungu ameendelea kuitikia dua ya kuliombea Bunge lako Tukufu kwa kutuongezea hekima na maono kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Tunamshukuru kwa Baraka hiyo.

Mheshimiwa Spika, wakati mkutano huu ukiendelea, wapo Watanzania wenzetu waliokutwa na masahibu mbalimbali kama vile mafuriko yaliyotokea Wilayani Mpwapwa; kimbunga huko Njombe, Ileje na Nyamagana; na ajali ya treni eneo la Ruvu mkoani Pwani. Aidha, zimekuwepo ajali mbalimbali za barabarani. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kutuma salamu zangu za pole kwa wale wote waliopoteza wapendwa wao na kuwaombea uponaji wa haraka kwa wale waliopata majeraha kwa ajali hizo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, itakumbukwa kuwa tarehe 26 Januari, 2017 ilitokea ajali ya kuporomoka kwa kifusi katika machimbo ya dhahabu kwenye Mgodhi wa Mawe Meru, ya kule Nyarugusu, mkoani Geita ambapo vijana wetu 15 waliofukiwa na kifusi kwenye machimbo hayo waliokolewa wakiwa hai. Nawashukuru na kuwapongeza kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu waliofanikisha uokoaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi tunayoweza kujifunza kutokana na hali hiyo na hususan hatua za kuchukua kuzuia ajali kama hizo pindi zinapojitokeza siku zijazo na jinsi ya kuokoa watu wetu jambo kama hilo linapojitokeza. Natoa rai kwa kila taasisi inayohusika, ifanyie kazi funzo tulilolipata kwenye zoezi hili ili kuepuka ajali za migodini na endapo zitatokea, kuwepo na utayari katika uokoaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa pongezi za teule mbalimbali kwenye Mkutano huu. Bunge lako Tukufu limepokea na kuwaapisha Wabunge wapya wanne, ambao ni Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mheshimiwa Juma Ali Juma na Mheshimiwa Profesa Paramagamba John Aidan Mwaluko Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wapya kwa heshima waliyoipata ya kujumuika nasi kwenye Bunge lako Tukufu. Kama ilivyo ada, naamini wote tutatoa ushirikiano unaotarajiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wapya ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na tija ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Kaimu Jaji Mkuu wa Tanzania. Sina mashaka Mheshimiwa Jaji Profesa Juma ataendeleza uhusiano mzuri uliopo kati ya mhimili wa Mahakama na mihimili mingine ya dola, kama ambavyo alifanya mtangulizi wake, Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mohammed Chande Othman. Serikali inaahidi kumpa ushirikiano unaostahili ili aendeleze maboresho kwenye mhimili huo yaliyoanzishwa na mtangulizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 2 Februari, 2017, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, alimteua Jenerali Venance S. Mabeyo kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Jenerali Davis Mwamunyange ambaye amestaafu. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Jenerali Mabeyo kwa uteuzi huo na kumshukuru Jenerali Mwamunyange kwa kulitumikia Taifa letu kwa uzalendo na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge. Tunapohitimisha Mkutano huu leo, tumeweza pia kukamilisha mjadala wa Miswada miwili; kupokea Kauli za Mawaziri mbili na taarifa 14 za Kamati za Kudumu za Bunge. Itakumbukwa kuwa, awali Serikali ilipanga kuwasilisha Miswada mitatu ikiwemo Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016)*, lakini tukaomba kuuondoa ili twende kujipanga vizuri zaidi. Hivyo, Miswada iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwenye Mkutano huu ni hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016 (*The Legal Aid Bill, 2016*) na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2016 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (Na.4) Bill, 2016*].

Mheshimiwa Spika, Miswada hii ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu, hivyo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri kwa maslahi ya Taifa letu. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Miswada hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawasihi Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na Miswada iliyopitishwa, wasimamie utayarishaji wa kanuni za sheria hizo zilizopitishwa pindi Mheshimiwa Rais atakaporidhia ili utekelezaji wake uanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali ya msingi, ya nyongeza na ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu pia ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge na kutolewa kauli mbili za Mawaziri kuhusu Hali ya Chakula Nchini; Deni la Taifa na Hali ya Uchumi. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuwasilisha kwa umakini na umahiri mkubwa taarifa za Kamati zao pamoja na kuzihitimisha. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango, maoni na ushauri wao mzuri walioutoa wakati wa mijadala yote ya taarifa hizo nilizozitaja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Wataalam wetu wote kwa kufanikisha kazi zote zilizokuwa zimepangwa kwenye Mkutano huu tena kwa ufanisi mkubwa sana. Nawashukuru na kuwapongeza sana nyote; na ninawasihi mwendelee na umahiri huo mlionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa maelezo mazuri ya ufafanuzi waliyoyotoa katika kujibu baadhi ya hoja za Kamati za Kudumu za Bunge na zile zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge binafsi au kwa ujumla wao. Napenda kuahidi kuwa Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge mlioutoa, pamoja na mapendekezo yote yaliyotolewa katika Kamati husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja za Kamati za Kudumu za Bunge, naomba nami uniruhusu nitumie fursa hii kutoa maelezo mafupi ya msisitizo kuhusu baadhi ya hoja zilizojitokeza katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni Vita Dhidi ya Dawaa za Kulevya. Moja ya eneo lililojadiliwa na kuibua hisia kali, ni kuhusu vita inayoendelea nchini dhidi ya dawaa za kulevya. Watanzania wote ni mashahidi kwamba vijana wetu wengi wameendelea kudhoofisha afya zao kutokana na matumizi ya dawaa za kulevya. Dawaa za kulevya ni hatari sana kwa usalama na ustawi wa Taifa letu. Vita hii inayopiganwa sasa dhidi ya uagizaji, uzalishaji, usambazaji na matumizi ya dawaa za kulevya ni kubwa. Sote tunapaswa kuunga mkono jitihada hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitaalam, madhara ya kiafya yanayosababishwa na matumizi ya dawaa za kulevya ni mengi; ni pamoja na kuathirika kwa mfumo wa fahamu kwa mtumiaji ikiwemo kuchanganyikiwa, kuwa na ulevi usioponyeka kirahisi na kusababisha kifo kama mtumiaji atazidisha matumizi ya dawaa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kiuchumi ni pamoja na gharama kubwa za kuwatibu waathirika wa dawaa za kulevya; gharama kubwa za uchunguzi wa kimaabara kwenye Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na watumiaji wa dawaa hizi za kulevya kushindwa kujisimamia na kuendesha maisha yao wao wenyewe. Aidha, takwimu za jumla za Watanzania waliokamatwa na kufungwa gereza katika nchi mbalimbali kutoka hapa nchini Tanzania juu ya makosa yanayohusiana na biashara ya madawa ya kulevya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna Watanzania 200 nchini China, waliofungwa kwenye Magereza, tuna wafungwa 12 nchini Brazil, tuna Watanzania 63 walioko nchini Iran, tuna Watanzania saba walioko Ethiopia na tuna Watanzania 296, wako kwenye Magereza mbalimbali za Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kulevya hapa nchini, huingia zaidi kutumia njia za bandari bubu kupitia Bahari ya Hindi na mipaka yetu kwa njia ya magari binafsi na mabasi kupitia nchi za Kenya, Uganda na mpaka wa Tunduma.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuwasaidia walioathirika na dawa za kulevya na kuwachukulia hatua kali wale waliowaathiri kwa maana ya wauzaji na wasambazaji. Tunashukuru kwamba Watanzania wengi na Waheshimiwa Wabunge pia mmetoa mchango wenu mkubwa na ushauri wa namna nzuri zaidi ya kupambana na janga hili. Dhamira ya Serikali ni kupambana na janga hili kwa dhahiri na kwa dhati bila kumwonea mtu yeyote na kwa kuzingatia misingi ya sheria na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyovuta sana hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi ni kuhusu utaratibu na utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu. Suala hili ni pana na linagusa familia nyingi za Watanzania na hususan walio maskini. Hivyo, Serikali imeunda Kamati ya Wataalam ambao wanaupitia upya utaratibu wa sasa kwa lengo la kupendekeza vigezo muafaka kwa kuzingatia changamoto zilizopo. Azma ya Serikali ni kuanza utekelezaji wa vigezo vilivyoboreshwa katika upangaji na utoaji wa mikopo kuanzia mwaka wa masomo wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuimarisha urejeshwaji mikopo hii kwa wakopaji ili kuongeza fedha kwa ajili ya kugharamia wanufaika wapya wa mikopo ya Elimu ya Juu ili kupunguza utegemezi kutoka katika bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja kuhusu uhakiki wa watumishi na madai ya watumishi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, zoezi la uhakiki wa watumishi hewa limekamilika, kinachoendelea sasa ni uhakiki wa vyeti vya kitaaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni, Mkaguzi wa Ndani wa Serikali amefanya uhakiki wa madai mbalimbali ya Watumishi wa Umma ya hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imeanza kulipa madeni hayo ambapo hadi sasa Serikali imelipa shilingi bilioni 42.35 kwa watumishi wasiokuwa Walimu. Aidha, kwa upande wa Walimu, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 23.458 kwa Walimu 63,955 kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na mwaka 2016/2017. Serikali itaendelea kulipa madeni yote ya Watumishi wa Umma yaliyohakikiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine muhimu iliyojadiliwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu utawala bora hususan mipaka ya kimadaraka kati ya mihimili mikuu ya nchi, yaani Serikali, Bunge na Mahakama. Dhana ya mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili ya dola imewekwa wazi kwa mujibu wa Katiba kwa Ibaraya 4 (1).

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya mihimili hiyo unategemea sana viongozi na watendaji wake kuheshimiana, kuvumiliana na kufanya kazi zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Shabaha kuu hapa ni kuwaletea wananchi maendeleo, hivyo tuepuke misugvano isiyokuwa na lazima, isiyokuwa na tija ambayo itatuondoa katika lengo la kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya. Hali ya upatikanaji wa dawa nchini imeendelea kuimarika kufuatia kutolewa kwa wakati fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Mathalan, kiasi cha shilingi bilioni 91 kimeshatolewa kati ya shilingi bilioni 251 zilizotengwa, sawa na wastani wa shilingi bilioni 20 kila mwezi. Haya ni mafanikio makubwa na ni dhamira njema ya Serikali katika kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Haya ni mafanikio makubwa ukilinganisha na mwaka wa fedha 2015/2016. Katika kipindi hiki tulikuwa tumepeleka fedha chini ya shilingi bilioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekuwa tukieleza kuhusu dhamira ya Serikali ya kununua madawa na vifaa tiba moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya mawakala, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu huo umeanza na tayari Serikali

imekamilisha taratibu za kimkataba na Wazalishaji watano wakubwa wa ndani ya nchi kwa ajili ya kununua baadhi ya dawa kutoka ndani ya nchi, wakati mikataba mingine 76 ya wazalishaji wa nje iko katika hatua za mwisho. Matarajio yetu ni kwamba utekelezaji wa mikataba ya nje utaanza katika mwaka wa fedha 2017/2018. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya kusambaza dawa kwa wakati kwenye Halmashauri zetu haitafanikiwa endapo Halmashauri zitachelewa kuwasilisha maoteo ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Hivyo, Halmashauri zote nchini, zinaagizwa kufanya maoteo na kuyawasilisha Bohari Kuu ya Dawa kabla au ifikapo tarehe 5 Machi, 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kutoa rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge, kupata wasaa wa kufuatilia mchanganuo wa usambazaji dawa katika Halmashauri zetu ambao hutolewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Jitihada za Serikali za usambazaji wa dawa pia zinafanywa na maduka ya dawa yanayoendelea kujengwa sehemu mbalimbali nchini. Shabaha yetu hapa ni kwamba, ifikapo mwezi Juni, 2017 usambazaji wa dawa muhimu nchini kote kwenye hospitali zetu uwe umefikia asilimia 85.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maboresho kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), ambayo yatawezesha wanachama kupata huduma kutoka ngazi ya Zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Katika maboresho hayo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) utabaki na jukumu la kununua dawa wakati Halmashauri zitakuwa na jukumu la kutoa huduma tofauti na ilivyo sasa. Kwa kuanzia, Mpango huu utatekelezwa katika Halmashauri 50 katika Mikoa ya Ruvuma, Kagera, Mwanza, Mara, Singida, Tabora na Pwani ambapo Mpango huu utazinduliwa rasmi mwishoni mwa mwezi Februari, 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwelekeo huo wa Serikali, ni vema sasa Waheshimiwa Wabunge kupitia Halmashauri zetu mkaanza kuwaandaa wananchi kupokea mpango huu wa Bima ya Afya kwa kila mwananchi. Aidha, anzeni kutafakari namna bora zaidi ya kutekeleza mpango huo katika muktadha na mazingira ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi wa Sekta ya Afya ilikuwa ni sehemu mojawapo iliyoleta mjadala. Kuna kilio kikubwa cha uhaba wa watumishi kwenye Sekta ya Afya. Jambo hili tunalifahamu na kwa hakika linatugusa sote. Kama ambavyo tumeanza kwa kutangaza ajira 4,348 za Walimu wa Masomo ya Sayansi, pia tutaajiri watumishi wa kada ya afya na kada nyingine vile vile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo wa mwaka 2017, tunayo matarajio ya uandikishaji wa wanafunzi wa awali, msingi na pia kwa Sekondari, Kidato cha Kwanza. Zoezi la uandikishaji katika Kidato cha Kwanza linaendelea na linatarajiwa kufungwa tarehe 28 Februari, 2017. Naomba nitumie fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kuongeza kasi ya uandikishaji kwa Elimu ya Msingi, pia usajili kwa Kidato cha Kwanza pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa ili wanafunzi wote wanaostahili kuandikishwa au kuendelea na ngazi inayofuata katika shule wasipoteze fursa hiyo kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa elimu bora kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule. Kutokuwepo kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum imekuwa ni changamoto kwao katika kujifunza kwa ufanisi. Ili kuboresha upatikanaji, ushiriki na usawa katika elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali imenunua vifaa vya kielimu na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na wenye ulemavu wa akili (mtindio wa ubongo). Vifaa hivyo vinajumuisha mashine 932 za maandishi ya nukta nundu, rimu za karatasi za breli zipatazo 2,548 na shime sikio (*hearing aids*) 1,150.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza dhana ya elimu jumuishi, Serikali imenunua pia vifaa kwa ajili ya upimaji ili kubaini mahitaji maalum ya ujifunzaji kabla na baada ya usajili wa watoto katika Shule za Msingi. Vifaa hivyo vinajumuisha pia vifaa vya upimaji kwa ajili masikio, macho na ulemavu wa mtindio wa ubongo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum ambavyo vimegharimu kiasi cha Shilingi bilioni 3.6 vimekwishapokelewa na vitasambazwa katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji hayo kuanzia tarehe 1 Machi, 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Maafisa Elimu na Walimu wote wanaofundisha wanafunzi wetu wenye mahitaji maalum kutumia ipasavyo vifaa hivyo. Aidha, wazazi wa watoto wenye mahitaji maalum, wawapeleke watoto wao shule, badala ya kuwaficha majumbani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu upatikanaji wa vitabu vya Elimu ya Msingi na Sekondari. Serikali inaendelea na jitihada zake za kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Hadi sasa Serikali imefanikiwa kusambaza nakala 6,862,800 kwa vitabu vya Kiada kwa Darasa la Kwanza vya Mtaala ulioboreshwa kwa Shule zote za Msingi Tanzania Bara. Aidha, uchapaji wa vitabu vya Darasa la Pili nakala 6,862,800 unaendelea na uchapishaji wa nakala 6,818,181 za Darasa la Tatu umekamilika. Nakala hizo za Darasa la Tatu zitasambazwa sambamba na vifaa vya Darasa la Pili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shule za Sekondari, ziko nakala 2,109,683 zimechapishwa na usambazaji umeanza tarehe 7 Februari, 2017. Natoa wito kwa Walimu wote nchini na wanafunzi wetu wote kutunza vizuri vitabu hivyo ili viweze kutumika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango maalum wa kukuza na kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi nchini. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali ilihamasisha ujenzi wa madarasa, maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeagiza vifaa vya maabara kwa ajili ya Shule 1,625 za Sekondari nchini. Hadi sasa asilimia 70 ya vifaa hivyo imekwishawasilili nchini na usambazaji wake umeanza hivi karibuni katika Kanda ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Wakuu wa Shule kuweka utaratibu mzuri wa kutunza vifaa hivyo ili viweze kudumu. Aidha, ni matumaini yangu kwamba vifaa hivyo vitakuwa ni chachu ya wanafunzi kuchangamkia masomo ya sayansi na hivyo kulifanya Taifa letu kutengeneza wanasayansi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu; mwishoni mwa mwaka 2016, Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu, ilifanya uhakiki wa ubora wa elimu ya juu kwa Vyuo Vikuu vyote nchini. Matokeo ya uhakiki huo yatatumika katika kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha elimu ya juu ili kupandisha viwango vya taaluma ya wahitimu. Uhakiki huo utakuwa unafanyika kila baada ya miaka mitatu ili kuhakikisha ubora wa elimu inayotolewa unalingana kote nchini.

Mheshimiwa Spika, sanjari na jitihada hizo, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaweka Viwango vya Ulingalifu (*Benchmark Standards*) vya kuainisha kozi zinazotakiwa kusomwa katika nyanja za Ualimu, Udaktari wa Binadamu, Sheria na Biashara. Matarajio yetu ni kwamba jitihada hizi na nyingine zitakazokuwa zinaendelea kufanyika, zitasaidia kuboresha Elimu ya Juu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika Kauli ya Serikali kuhusu Hali ya Chakula na Lishe Hapa Nchini kwa Mwaka 2016/2017, baadhi ya maeneo katika Halmashauri 55 yana upungufu wa chakula na bei za vyakula hasa nafaka kwenye masoko ya Halmashauri hizo imeendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, leo sikusudii kurudia maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Sekta ya Kilimo bali kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwahamasisha wananchi kulima mazao yanayokomaa mapema kwa kutumia mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi hapa nchini. (Makofi)

Pili, kuwashauri wananchi kutumia vizuri chakula walichonacho na kuwasihi wafanyabishara wasifiche chakula, bali wasaidie kuchukua chakula kutoka kwenye maeneo yenye chakula cha ziada na kwenda kuuza kwenye maeneo yenye chakula pungufu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, Serikali inahimiza wananchi kuondokana na mazoea ya uchungaji na kujikita zaidi katika ufugaji wa kisasa ambao utawawezesha kuwa na mifugo michache yenye ubora ambayo itawaongezea tija katika uzalishaji wa nyama na maziwa mengi zaidi kwa ng'ombe mmoja. Hivyo, Serikali kupitia mashamba ya mifugo na Vituo vya Taasisi za Serikali vilivyoko katika maeneo mbalimbali ya nchini kote, itaendelea kuhakikisha kuwa mbegu bora za mifugo zinazalishwa kwa ajili ya uhamilishaji na mitamba na madume bora yanazalishwa kwa wingi na kusambazwa ili kukidhi mahitaji ya wafugaji wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha Taasisi zinazoagiza mbegu za mifugo kutoka nje ya nchi kama vile *Heifer Project International (HPI)* na *SAGCOT* na kwa kushirikiana na mashamba makubwa ya kisasa ya sekta binafsi ili wafugaji wawe na wigo mpana wa kuchagua aina bora zaidi za mifugo. Hivyo, natoa rai kwa wananchi kuchangamkia fursa hiyo kwa kushiriki vizuri zaidi katika ufugaji wa kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna uhusiano mkubwa sana kati ya ufugaji bora na upatikanaji wa malisho bora. Hivyo, Serikali inaendelea kuboresha na kuendeleza mashamba ya mbegu za malisho ya mifugo yaliyo chini ya Serikali katika maeneo mbalimbali nchini kote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwaagiza Maafisa Ugani wa Mifugo katika Halmashauri zote nchini, kufungua mashamba darasa ya kuzalisha mbegu hizo na kuhamasisha wafugaji kupanda malisho katika maeneo yao na kutoa stadi za ufugaji bora na wa kisasa. Baada ya miaka mitatu, Wizara husika ifanye tathmini ya utekelezaji wa agizo hili na kuwasilisha taarifa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza juhudi za kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi inayojitokeza katika maeneo mbalimbali nchini, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi imeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 50 katika Wilaya 19 na kuandaa hatimiliki za Kimila 1,361. Katika Wilaya ya Mvomero hatimiliki 2,943; katika Wilaya za Mkuranga hatimiliki 297; Ikungi hatimiliki 957; Karagwe hatimiliki 1,099 na Nachingwea hatimiliki 590.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeandaa hatimiliki za kimila 44 za nyanda za malisho za Wilaya za Monduli, Ngorongoro, Hanang, Simanjiro na Karatu. Hadi sasa jumla ya vijiji 1,690 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ambayo imeainisha pia matumizi ya kilimo na ufugaji ikilinganishwa na vijiji 12,545 vilivyopo nchini. Vilevile, upimaji wa mipaka ya vijiji 53 umefanyika katika Wilaya ya Kilombero, vijiji saba na Ulanga vijiji vitano.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda maeneo ya umma, ikiwemo sehemu za huduma kama vile Shule, Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali, Vyuu, Ofisi za Serikali, Vituo vya Polisi, Mahakama, Maeneo ya Majeshi, Mashamba ya Serikali, Hifadhi za Misitu na Wanyamapori, Maeneo ya Makumbusho na kadhalika dhidi ya uvamizi, Serikali inaendelea na upimaji wa maeneo hayo na kuyapatia hatimiliki. Aidha, Wizara zote Tanzania Bara zinaagizwa kuhakikisha kuwa maeneo wanayoyamiliki na yale yaliyoko chini ya taasisi zao yanapimwa na kuandaliwa hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha zoezi la upimaji, upangaji na utoaji wa hatimiliki za maeneo ya umma, Serikali imeelekeza Wizara na Taasisi za Umma kutumia Wapima wa Serikali au Wapima Binafsi waliosajiliwa na Bodi ya Wapima Ardhi Nchini, kupima maeneo yao kwa kugharimia upimaji wa maeneo hayo. Nitumie fursa hii kuzipongeza baadhi ya taasisi ambazo zimeanza kutekeleza kazi hiyo kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mahakama Kuu ya Tanzania na baadhi ya Sekretarieti za Mikoa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa kulinda usalama wa maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba kwa kuweka mawe ya mipaka yanayoonekana kwa mbali, yaani *Pillars* ili kuzuia uvamizi na uharibifu wa maeneo hayo kwa kushirikisha wadau na mipaka hiyo. Pia malengo yetu ni kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaoishi mipakani mwa mapori haya waweze kutambua mipaka ya mapori hayo kuondoa migogoro na miingiliano isiyokuwa ya muhimu. Wizara ya Ardhi,

Nyumba na Maendeleo ya Makazi inashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba mipaka yote ya maeneo hayo inawekwa alama hizo za mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushughulikia migogoro ya mipaka ya vijiji, wakulima na wafugaji, wanavijiji na hifadhi na mapori ya akiba inayoibuka hapa nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeunda Kamati Maalum ya Kisekta ya kushughulikia migogoro ikijumuisha Watendaji wa Sekta mbalimbali zinazohusika kwa njia moja au nyingine kwenye masuala ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo tayari imepokea na kuchambua migogoro yote iliyowasilishwa kutoka Halmashauri mbalimbali nchini na kutembelea Wilaya zenye viashiria vya migogoro, ambazo baada ya zoezi hilo kukamilika, Serikali itawasilisha taarifa ya hali ya migogoro na hatua itakayofikiwa ya utatuzi wa migogoro hiyo nchini ili kuondokana kabisa na migogoro miongoni mwa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshatoa maelekezo mahsusi kwa Halmashauri mbalimbali na naomba kutumia Bunge hili kurejea maelekezo yangu kuhusu migogoro ya mipaka kati ya kijiji na kijiji; vijiji na hifadhi; au wilaya na wilaya. Kwa migogoro ya mpaka kati ya kijiji na kijiji, maelekezo ya Serikali ni kwamba, migogoro hiyo imalizwe kupitia vikao vya vijiji husika na wataalam wa Halmashauri wasaidie katika kumaliza migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro kati ya vijiji na hifadhi, au wilaya na wilaya, itatuliwe kwa kuangalia mipaka halali inayotambuliwa kwa kutumia GN na Wataalam wa Upimaji na Ramani wa Halmashauri au wale wa Wizara ya Ardhi, wasaidie kubainisha mipaka hiyo iliyowekwa na Serikali miaka iliyopita na kuhakikisha kwamba wanasuluhisha pande zote mbili. Nasihii Halmashauri zote nchini zizingatie mwongozo huo ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara zangu mbalimbali ninazofanya mikoani, nimebaini uwepo wa malalamiko mengi ya wananchi ambayo hayashughulikiwi kwa wakati katika ngazi za vijiji, mitaa na kata. Aidha, nimebaini kuwa Mikutano ya Vijiji, Kata na Mitaa imekuwa haifanyiki kama inavyotakiwa kisheria na hivyo kufanya kero nyingi kutopatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kutotatua kero za wananchi katika ngazi ya Serikali za Mitaa ni kinyume na dhamira ya Serikali ya kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi. Aidha, ni kinyume na msimamo wa Ibara ya 146 (1) ya Katiba ya yetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotamka kama ifuatavyo, naomba kunukuu:

“Madhumuni ya kuwapo Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Na vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki kuwashirikisha wananchi katika mpango wa shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika Serikali zao na nchi kwa ujumla.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa inaelekeza kuitishwa kwa Mikutano Mkuu ya Vijiji kila baada ya miezi mitatu. Sheria pia inatoa fursa ya kuitishwa kwa mikutano ya dharura, endapo ipo haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msimamo huo wa kisheria na kutokana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kutatua kero za wananchi, suala la utatuzi wa kero za wananchi halitakiwi kuendelea kusubiri ziara za viongozi wakuu, badala yake, kero hizo zitatuliwe kwenye ngazi zinazohusika na zitatuliwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, naomba kutumia Bunge lako Tukufu kusisitiza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa wanakumbushwa kuitisha Mikutano ya kisheria ya Vijiji, Kata na Mitaa na kusoma taarifa za mapato na matumizi ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Wakurugenzi wa Halmashauri nao wanaagizwa kusimamia kikamilifu uitishaji wa Mikutano Mikuu ya Vijiji na Mitaa kwa mujibu wa sheria na kuchukua hatua dhidi ya viongozi wote watakaoshindwa kutekeleza sharti hilo la kisheria. Tembeleeni vijiji kusikiliza kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; Viongozi na Watendaji katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri wajenge utamaduni wa kuwatembelea wananchi vijijini kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi wa papo kwa papo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama nchini ni ya kuridhisha. Vyombo vya Ulinzi na Usalama viko imara na katika hali ya utayari katika kulinda amani na utulivu. Operesheni za kupambana na uhalifu kama vile unyang'anyi wa kutumia silaha/nguvu, kuteka magari na matishio mengine ya kiusalama vimefanyika katika jitihada za kupambana na uhalifu nchini. Mathalan, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Desemba, 2016, Operesheni Kamata Magendo ilifanyika katika mikoa mbalimbali na kufanikiwa kukamata watuhumiwa 109 na mali zenye thamani ya zaidi ya sh. 388,271,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Usalama Barabarani kinaendelea na kusimamia usalama barabarani. Pamoja na operesheni hizo, bado kuna ripoti za vifo vinavyotokana na ajali. Licha ya takwimu kuonesha vifo vinavyotokana na ajali kupungua, bado jitihada za makusudi pamoja na umakini katika matumizi ya vyombo vya moto inabidi viongezoke. Kila mtumia chombo cha moto, aendeshe kwa uangalifu na Askari wa Usalama Barabarani waendeleo kuchukua hatua stahiki kwa wanaovunja Sheria za Usalama Barabarani ili kuokoa maisha yetu na ya watumiaji wengine wa barabara.

Mheshimiwa Spika, misako na doria zilizofanyika kati ya Julai, 2016 na Desemba, 2016 ziliwezesha kukamatwa kwa Watanzania na wageni 6,916 kwa makosa mbalimbali ya kiuhamiaji ikilinganishwa na Watanzania na wageni 3,119 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2015. Hili ni ongezeko la asilimia 55. Takwimu hizi zinaonesha ama kuongezeka kwa jitihada za kuwasaka wahamiaji haramu na kuwachukulia hatua za kisheria au changamoto hii imeongezeka duniani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, lazima idara iendeleo kujizatiti. Haiingii akilini kundi la wahamiaji linapita kwenye mikoa zaidi ya mitatu bila kukamatwa. Ni lazima Idara ya Uhamiaji iendeleo kujitathmini na kujipanga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwakamata wahalifu wanaojihusisha na uhalifu wa kutumia silaha haramu. Aidha, imeweka utaratibu wa kuteketeza silaha zote zinazokamatwa ili zisiweze kurudi tena kutumika katika uhalifu. Hivi karibuni jumla ya silaha 5,608 ziliharibiwa huko mkoani Kigoma. Kwa upande mwingine, katika juhudi za kudhibiti uzagaaji holela wa silaha haramu, Serikali inaendelea kufuatilia mipaka ya Mkoa wa Kigoma na Kagera ili kudhibiti uhamiaji holela wa nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia mipaka hiyo ili kudhibiti uingiaji huo pamoja na uingizaji wa silaha kiholela kwenye Mikoa hiyo ya Kigoma na Kagera. Pia, Serikali ilifanya zoezi la kuhakiki silaha zote zinazomilikiwa kihalali, ambapo asilimia 65 ya wamiliki wa silaha walihakikiwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wamiliki wote wa silaha nchini, ambao bado hawajahakiki silaha zao, wafanye hivyo kabla na ifikapo tarehe 30/06/2017 vinginevyo watapoteza leseni ya umiliki kwa kukiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jukumu la ulinzi na usalama wa nchi yetu, ni la kila mwananchi. Hivyo, natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutekeleza jukumu hili kwa kuepuka kushiriki hujuma dhidi ya nchi yetu na kwa kutoa taarifa za watu wenye nia mbaya ya kuhatarisha amani na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, niruhusu nibainishe masuala matano ya msisitizo, ambayo nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa jumla wayazingatie na wahamasishane katika kuyatekeleza. Masuala haya ni haya yafuatayo:-

Moja, usalama wa chakula unanza katika ngazi ya kaya. Kila kaya inatakiwa iwe na utaratibu wa kuwa na chakula cha akiba. Wakati Serikali inaendelea na wajibu wake wa kuhakikisha kwamba pale kwenye upungufu tunaweka utaratibu mzuri wa kuongeza chakula, kwa kuwa na hifadhi ya chakula. Kila mwananchi anao wajibu wa kujiwekea akiba ya chakula kwa ajili ya kaya yake. (Makofi)

Pili, dhamira ya kuwa na Bajeti ya kujitegemea kwa asilimia 100 inategemea jitihada zetu za makusanyo ya kodi. Hivyo, kila mwananchi ana wajibu wa kulipa kodi stahiki bila kushurutishwa; na kila mnunuzi anao wajibu wa kudai stakabadhi kwa kila bidhaa anayonunua. Aidha, kila mwananchi anao wajibu wa kufichua vitendo vya ukwepaji kodi pale anapoona kwamba pana dalili za vitendo vya hujuma za uibijaji kodi. Tulipe kodi kwa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Tatu, tunapoendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda na kuvutia mitaji kwa ajili ya biashara mbalimbali hapa nchini, atakayefanya viwanda na biashara hizi ziwe endelevu ni sisi Watanzania. Hivyo, pamoja na kusisitiza uzalishaji bora, tunalo jukumu la kulinda viwanda na biashara za Tanzania kwa kununua bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Unaponunua bidhaa zilizozalishwa hapa nchini, siyo tu unasaidia viwanda hivyo viendeleo kuongeza ubora wa bidhaa zao, bali pia unavifanya vizidi kuimarika na kutoa ajira nyingi kwa vijana wa Kitanzania. (Makofi)

Nne, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kumtumikia kila Mtanzania popote pale alipo. Kama nilivyoeleza awali, nimebaini baadhi ya kero za wananchi ambazo zingeweza kutatuliwa katika ngazi za Wilaya, zinaletwa kwenye Ofisi za Viongozi wa Kitaifa, au zinasubiri ziara za viongozi hao.

Mheshimiwa Spika, nawasihaji Viongozi wa Mikoa na Halmashauri tena, tembeleeni vijijini na mtatue kero za wananchi huko vijijini. Aidha, hakikisheni Mikutano ya Vijiji iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria inasimamiwa ufanyakaji wake na maazimio yanayopatikana kwenye vikao hivyo yafike kwenye vikao halali vya maamuzi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninyi ni sehemu ya Halmashauri zenu, nawasihaji sana mwendeleo kutoa msukumo wa uwepo wa vikao kwenye ngazi zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho, mipango ya maendeleo nchini na jitihada za wananchi kujikwamua na umaskini vitafanikiwa iwapo tutaendelea kuwa na umoja na kudumisha amani na utulivu. Hivyo, kila mmoja wetu aendeleo kuwa mlinzi wa amani na kuhamasisha, ufanyaji kazi kwa bidii na maarifa.

Mheshimiwa Spika, tunaahirisha Bunge lako Tukufu tukiwa na habari njema kwenye tasnia ya michezo ambazo zinatupa nguvu na hamasa ya kuendelea kufuatilia na kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za michezo na burudani kama moja ya maeneo ya kutengeneza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, mwezi Januari, 2017, Mtanzania mwenzetu Alphonse Felix Simbu, aliibuka mshindi kwa kunyakua medali ya dhahabu kwenye mashindano ya riadha ya Dunia ya Mumbai *Marathon*. (Makofi)

Pili, Mtanzania mwenzetu, Nassib Abdul, maarufu kama *DiamondPlatinumz*, alipata heshima ya kutumbuiza kwenye ufunguzi wa Fainali za Kombe la Afrika lililomalizika hivi karibuni nchini Gabon. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, Timu ya Taifa ya Vijana walio chini ya umri wa miaka 17 (*Serengeti Boys*) imefuzu kwenye Fainali za Kombe la Afrika kwa vijana walio chini ya umri wa Miaka 17 zitakazofanyika nchini Gabon tarehe 2 – 16 Aprili, 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia, nitambue jitihada za Timu ya *Bunge Sports Club* iliyoshiriki nchini Kenya, kwani miongoni mwa matukio muhimu yaliyojitokeza katika mwaka uliopita, tunawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushiriki wenu na kwa makombe mliyoyaleta. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu 2017, Tanzania au Bunge letu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwenyeji wa Mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki. Tunayo nafasi ya kujiandaa

vizuri na tunaomba Wabunge wote tushiriki kwenye mazoezi ili tuweze kubaini vipaji vyenu na hatimaye tuunde timu za Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwapongeza wachezaji, Benchi la Ufundi la Timu ya Bunge, lakini Benchi la Ufundi la TFF na wengine wote waliofanikisha timu zetu zote hizi; ile ya Bunge na *Serengeti Boys* kufikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wa *Serengeti Boys* wametimiza wajibu wao na kwa hakika wametutoa kimasomaso kwa kufikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Watanzania wote kote ulimwenguni kuiunga mkono timu yetu ili iweze kushindana kikamilifu. Nalishauri Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) liwe na maandalizi mazuri na ya mapema ili Timu yetu ya *Serengeti Boys* isiwe mshiriki tu, bali itoe ushindani wa kweli na kuchukua kombe hilo. Aidha, TFF itumie mashindano hayo kama chachu ya kuongeza msukumo katika soka nchini. Binafsi sifurahishwi sana kuona Taifa letu lenye vipaji lukuki vya michezo ikiwemo soka na riadha pia, ikiwemo, likiwa nyuma hapa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu, kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge muwe na safari njema mnaporejea Majimboni kwenu. Mwenyezi Mungu awajaalie na siha njema katika kipindi chote mtakachokuwa Majimboni ili muweze kuchukua maoni ya wananchi mnaowawakilisha kwa lengo la kufikisha maoni yao kwenye Mkutano ujao ambao utakuwa ni mahsus kwa ajili ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 4 Aprili, mwaka huu 2017, siku ya Jumanne, Saa 3.00 asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Dodoma, Makao Makuu ya Serikali, nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi kweli kweli. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niwahoji kuhusu hoja iliyowekwa Mezani hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja ya kuahirisha Bunge hadi tarehe 4 mwezi wa Nne.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Nadhani walioafiki wameshinda. Wale wengine wanaotaka kubaki na sisi Dodoma hapa wanakaribishwa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo mmetenda kazi katika Mkutano huu wa Sita wa Bunge. Mmefanya kazi nyingi kwa weledi mkubwa, nasema hongereni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wenzangu na wasaidizi wangu, Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Najma Giga. Kwa hakika wamefanya kazi nzuri sana hapa Mezani. Nawashukuru sana kwa ushirikiano huu ambao tumekuwanao hapa Mezani. Nami nilikuwa Kochoa Mchezaji, nilikuwa siko mbali, nilikuwa niko karibu tu hapa. Kwa hiyo, nawapongeza sana wenzangu. *(Makofi)*

Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukumbuke kwamba *Bunge Sports Club* mwezi Aprili wakati wa Pasaka hivi ukikaribia, wenzetu Wawakilishi kutoka Zanzibar watakuja hapa kwa ajili ya michezo kadhaa ikiwemo ya mpira wa pete na mpira wa miguu, hapa hapa Dodoma. Kwa hiyo, tutakaporudi mara moja tuendeleo na mazoezi, maana taarifa walizonipa ni kwamba, *Bunge Sports*

Club itakuwa kwenye hali ngumu kweli kweli wakati wa michezo hiyo. Nami nikawahakikishia kwamba *Bunge Sports Club* ni wembe ambao siyo wa kuchezewa hata kidogo. (Makofi)

Kwa hiyo, Wawakilishi watakuja kwa mwaka huu wakiamini kwamba mwaka utakaofuata na *Bunge Sports Club* nanyi mtaenda Zanzibar ili tuweze kuimarisha Muungano wetu katika namna hiyo pia, katika ngazi ya Mabunge au ngazi ya Wawakilishi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Mkutano huu palijitokeza baadhi ya wenzetu wakawa wanasema hadhi ya Bunge hili la Kumi na Moja imeshuka.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwahakikishieni, kama Kiongozi wa Bunge hili la Kumi na Moja, Hadhi ya Bunge hili iko pale pale kama siyo kwamba imepanda zaidi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mhimili huu hauna ugomvi wowote na Serikali, wala hatuna ugomvi wowote na Mahakama, wala hatufikiri kuwa na hali ya namna hiyo. Mambo haya ya Afisa mmojawapo hapa na pale kusahau mipaka ya kazi zao na kuvuka kidogo ni mambo ya kawaida ambayo mahali panapohusika watachukua hatua za kuweka sawasawa tu. Haya ni mambo ya kujisahausahau hivi.

Eeh, maana mimi naweza nikawa nawahitaji Wabunge hapa, kuna mambo inatakiwa tufanye ambayo ni ya Kitaifa; nimewaita Waheshimiwa Wabunge mko hapa, labda mko kwenye Kamati na tunahitaji *quorum*, wakati mwingine hata akikosekana Mbunge mmoja, inawezekana jambo hilo kwenye Kamati lisipite. Kwa hiyo, kama kuna *junior officer* huko anamhitaji Mbunge, lazima aniambie kwanza, hatuwezi kwenda hivyo. (Makofi)

Kwa hakika tukienda tu kibabebabe namna hii, tutavuruga nchi. Haiwezekani, hatuwezi kwenda hivyo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba tusimame ili tumbe wimbo wa Taifa.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba
Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Wheshimiwa Wabunge, sasa noamba hapo hapo mkiwa mmesimama niahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe 4 mwezi wa Nne, Siku ya Jumanne, mwaka huu 2017, saa 3.00 asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 4 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)